

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Tisa – Tarehe 21 Mei, 2015

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 33(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013; tarehe 15 Mei, 2015 nilitoa taarifa kwamba Miswada tisa ya Sheria ya Serikali iliyopitishwa katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge ilikwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria za nchi. Kwa taarifa hii ya leo, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba Miswada mitano iliyokuwa imebaki nayo imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa sheria zilitazwo:-

Ya kwanza, Sheria ya Udhhibiti na Usimamizi wa Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015 (*The Drug Control and Enforcement Act, 2015*) Na. 5 ya Mwaka 2015.

Ya pili, Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2015, (*The Disaster Management Act, 2015*) Na. 7 ya Mwaka 2015.

Ya tatu, Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji ya Mwaka 2015 (*The Immigration Amendment Act, 2015*) Na. 8 ya Mwaka 2015.

Ya nne, Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya Mwaka 2015, (*The Tax Administration Act, 2015*) Na. 10 ya Mwaka 2015 na;

Ya Tano, Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 (*The Budget Act*) Na. 11 ya Mwaka 2015.

Kwa hiyo, Waheshimiwa sasa hii ni Miswada ya kisheria. (Makofi)

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa na:-

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hati za kuwasilisha mezani, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi! Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwamwaka wa fedha 2015/2016.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA (MHE. JASSON S. RWEIKIZA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA (MHE. TUNDU A. M. LISSU):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

SPIKA: Kutokana na matatizo ya umeme leo, Msemaji wa Upinzani ameleta hotuba yake sasa hivi. Lakini siyo utaratibu.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Leo ni siku ya Alhamisi, tunaanza na Maswali na Waziri Mkuu. Kwa kawaida yetu Kiongozi Mkuu Kambi ya Upinzani huwa anaanza, lakini leo naona amepata dharura. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya ndiyo atauliza swali kwanza.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kumuuliza swali dogo Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, dini zote kuanzia Zaburi, Taurati, Injili na Qurani na hata zilizokuwa na wafuasi wengi *buddhism* na *hinduism* zinakataza kabisa kitu unyanyasaji. Vilevile zinahubiri amani na watu kuwa kitu kimoja. Watanzania tunajulikana kwa utamaduni wetu wa kupendana na kutokufanyiana mabaya.

Mheshimiwa Spika, linapotokea jambo la dharura likatolewa taarifa katika vyombo vya habari, Bunge hili limeshuhudia mara mbili kuweza kutoa tamko au kupinga taarifa ambazo zinaharibia nchi yetu jina lake, likiwepo la mapanki kule Mwanza na la juzi juzi la kusema kwamba Rais wa China alipofanya ziara, ndege yake iliondoka na pembe za ndovu, likakanushwa *only second or third day* katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, ndugu zetu ambao wako jela kwa tuhuma na kesi yao inaendelea, taarifa zao zimetoka katika vyombo vya habari, siyo mara moja wala mara mbili kutokana na unyanyasaji wanaofanyiwa. Unyanyasaji huo unapelekea watu kutokuwa na imani na vyombo vya sheria na vya dola vinavyofanya kazi katika Magereza hayo na hata kunyimwa matibabu ambayo ni haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama wewe ndiyo Mtendaji Mkuu wa Serikali, mbali ya kulitolea tamko suala hili, huoni kwamba sasa kuna haja ili Serikali ijikoshe, kuunda Tume ya Bunge itakayokuwa na Wabunge wa pande zote mbili za Muungano, vyama vyote vya siasa ikiwashirikisha Maaskofu mmoja wa Zanzibar na mmoja wa Bara na Mashehe wawili ili kwenda kufanya uchunguzi kwa kipindi kifupi hiki na Serikali kutoa tamko ili Serikali yetu ijikoshe? Iwapo kama ni kweli waliofanya vitendo hivyo siyo kwa amri ya Serikali wachukuliwe hatua kwa mujibu wa Serikali; na kama hakujafanyika kitu, Serikali itoe tamko.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, unatuambia nini kuhusu hilo? (*Makofi*)

SPIKA: Nani hao walioko Magerezani wakafanyiwe uchunguzi?

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, ni Mashehe wa Uamsho ambao wanahusishwa na kesi ya kigaidi, ambao wamedai kwenye

vyombo vya habari na magazeti tunayo kwamba wanafanyiwa vitendo ambavyo mimi siwezi kuvitamka ndani ya Bunge hili kwa sababu siyo vizuri kuvitamka mara kwa mara. Ni mambo ambayo yana heshima zake na taadhima. Kama mnataka ushahidi huo, hayo magazeti yapo, yachukuliwe na yafanyiwe uchunguzi ili Serikali yetu isiwe inapakwa matope. Kama ni kweli, wanaohusika waweze kuchukuliwa sheria ili jambo hili likome na waendesheve mashitaka yao kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri na sheria ya nchi ili wasidhalilishwe kwa sababu wana haki zao za msingi na haki zao za kibinadamu katika maabusu hiyo. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya tu kwamba swali haliko wazi sana ili tuweze kujua hasa kinachotafutwa ni nini. Ningeshukuru sana kama ningejua Mashehe hawa ni akina nani? Wanatuhumiwa kwa makosa yapi? Pengine kwa sasa wako katika hatua ya upelelezi au wameshafikishwa mahakamani? Ili niweze kuwa na uhakika kwamba kinachotafutwa hapa ni katika *stage* gani ya mchakato kwa ajili ya suala hilo ambalo linawakabili.

Mheshimiwa Spika, naungama tu kwamba bahati mbaya maswali ya papo kwa papo yanakuja hapo hapo. Nina hakika ningekuwa nimepata maelezo kutoka kwa rafiki yangu Sanya mapema, tungeweza kulifanyia kazi vizuri tu kwa nia njema ili tuweze kuona hili jambo likoje.

Mheshimiwa Spika, naweza kumuahidi Mheshimiwa Sanya, yeye ameshauri tuunde timu ndogo, Wabunge wawemo ili kuweza kulichunguza hilo jambo. Sina tatizo na hilo kwa sababu nchi hii tunaheshimu sana uhuru, haki za binadamu na mambo yote ya msingi. Lakini ningefurahi sana kama pengine angenipa muda kwanza na mimi nilifanyie kazi baadaye nije nitoe taarifa hapa kwa Mheshimiwa Spika nilichokiona na utaratibu ambao anapendekeza tuone unaweza ukafanywa namna gani. Nadhani itakuwa ni nzuri zaidi kwa sababu itakuwa imenisaidia na mimi kupata picha ya jambo lenyewe lilivyo.

SPIKA: Kwa hiyo, tunategemea utapata taarifa nyingine. Naomba Mheshimiwa Sanya tungoje tupate taarifa nyingine.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Nina swali lingine dogo tu.

SPIKA: Tofauti?

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Nataka nielezee kidogo kumsaidia Mheshimiwa Waziri alielewe vizuri.

SPIKA: Ehe!

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimefarijika sana namna ulivyojibu. Kutokana na uwezo wako na nafasi yako, nina hakika utafanya kama matamshi yako yalivyotoka katika Bunge hili. Ila nakuomba, hili suala liko katika Wizara husika ambayo unaiielewa, ilifanyie kazi haraka. Isipokuwa kati ya hao watuhumiwa, wengine ni wagonjwa, hali zao siyo nzuri na siyo za kuridhisha. Hata kwenye Mahakama ya Kisutu hawawezi kwenda, wako Segerea wanasota. Ichukuliwe hatua ya haraka kupelekwa katika hospitali kufanyiwa uchunguzi na kupata matibabu ili waridhike na wao waone kwamba ni sehemu ya jamii kabla ya hukumu yao, kwani wana haki zote za msingi za kuangaliwa kama raia wengine.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema kinachohitajika ni kupata undani wa jambo lenyewe, kwa sababu watuhumiwa hata wale wanaokuwa rumande, kama wana dalili zozote za maradhi wanahudumiwa. Nadhani siyo mara moja tumewaona watu wako Muhimbili tumewapeleka kwa ajili ya matibabu, endapo huduma katika Vituo vyao Afya katika Magereza pengine haviwezi kukidhi tatizo la mgonjwa. Ndiyo maana nadhani katika jambo hili kwa uzito wake nafikiri njia rahisi ni hiyo tu. Bahati nzuri watu wa Mambo ya Ndani wananisikia, tukitoka hapa tutawapa maagizo specific ili tuweze kupata hadithi yote vizuri na baadaye tuweze sasa ama kulitolea tamko hapa Bungeni kauli ya Serikali, lakini lijulikane hasa ni kitu gani kinachozungumzwa.

SPIKA: Naomba tuendele na Mheshimiwa Dkt. Goodluck Ole-Medeye.

MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano inampa mamlaka ya kugawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo ya kiutawala ikiwemo Mikoa, Wilaya, Tarafa na mengineyo. Hata hivyo, hakuna kigezo ama vigezo ambavyo vimewekwa wazi juu ya sifa ambazo mikoa, wilaya au maeneo yanayotakiwa yafikie kuwa Mikoa au Tarafa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba utufafanulie juu ya vigezo vinavyotumika kugawa maeneo ya utawala katika nchi hii?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nadhani Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba katika maombi yote ambayo tumewahi kuyapata kuhusu mgao wa maeneo ya kiutawala ngazi ya Kitongoji, Kijiji, Kata,

Tarafa, Wilaya, Mkoa na kila kimoja kina maeneo yake ambayo lazima yazingatiwe. Sasa kwa upande wa hili ambalo Mheshimiwa Ole-Medeye anaulizia, vigezo muhimu sana mara nyingi sana inakuwa kwanza ni idadi ya watu ambalo ni jambo la msingi sana ili tuweze kujua kwamba katika mgao utakaofanyika, unaacha kila upande na idadi ya watu kiasi gani?

Ukubwa wa eneo. Tuweze kuona je, eneo lile litakuwa na uwiano unaoweza kuacha vile vigezo vya msingi bado viweze kuwepo au hapana? Wakati mwingine kunaweza kuwa na sababu tu za kijamii, kwa sababu nchi yetu ina mazingira mengine ambayo kidogo ni lazima ukubali kuyazingatia. Nne, ni hali ya kijiografia ya eneo linahusika. Wakati mwingine tunalazimika kukubali eneo moja kugawanywa.

Kama nilivyosema mara ya mwisho, nilipata bahati ya kwenda kwa mfano Kilolo. Kilolo ni milimani lakini kuna sehemu ya bondeni ambayo ina maeneo kama Ilula yale, nalo ni eneo kubwa sana. Nilipokuwa nimefanya ziara katika eneo lile na kwa kuzingatia ukubwa na ugumu wa kiongozi au hata Mtendaji ambaye yuko juu Kilolo kwamba atakuwa na fursa ya kuhudumia eneo hili lililo kwenye kanda tambarare, nikawapendekezea pale kwamba hebu kaeni chini tazameni tuone kama vigezo vinaweza vikakaribiana ili tutenganishe maeneo haya mawili angalau kwa *level* ya Halmashauri mbili.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Ole-Medeye, vigezo vipo, lakini kama una suala mahsusi labda eneo lako hivi, ingenisaidia sana kujua kama je, lina sifa au hapana.

SPIKA: Mheshimiwa Ole-Medeye kwa kifupi!

MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Arumeru ambayo ilianzishwa mwaka 1973 iliomba igawanywe, karibu miaka kumi hivi sasa imeshapita. Mwaka 2007 Mheshimiwa Rais akakubali, akagawa kuwa Halmashauri mbili. Lakini umuhimu wa kugawa kuwa na maeneo mawili ya kiutawala kwa maana ya kuwa na Wilaya mbili, bado wananchi wameendelea kuliona na amewasilisha mapendekezo kupitia ngazi mbalimbali zinazohusika kuja ofisini kwako.

Hata hivyo, pamoja na ahadi ya Serikali ambayo ilitolewa mwaka 2012 wakati wa mazishi ya Marehemu Jerry Sumari kwamba Wilaya hiyo ingegawanywa kichama na Kiserikali, Chama kimeshatekeleza ahadi yake; Serikali mpaka leo haijatekeleza. Wilaya hii ina takribani wakazi 900,000.

Kwa mazingira ya Wilaya ile na hususan Jimbo hili la Arumeru Magharibi ambapo zamani Makao Makuu ya Wilaya yalikuwa katikati ya Wilaya, pale kwenye Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, lakini baadaye

kwa sababu ambazo hatujui, yakahamishwa kwenda Usa, pembezoni kule na hivyo, kuwaacha wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha wakiteseka. Wanakamatwa na polisi kutoka kwa mfano Nangugu mpakani mwa Monduli wanapelekwa mpaka Usa; wanachukuliwa kutoka kule bwawani wanapelekwa Usa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba utuambie, ni lini Wilaya ya Arumeru itagawanywa kuwa Wilaya mbili?

SPIKA: Yaani mfano wake, ni kama Wilaya hiyo. Maana yake hapa ni kuuliza swali moja tu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni lini, siwezi nikaitamka hiyo tarehe hapa. Lakini kwa kawaida likishatoka katika eneo linalohusika kwa maana ya Wilaya husika au Halmashauri husika, mmekubaliana mtakuja Mkoani, mtakwenda kwenye RCC au Kamati ya Mashauriano ya Mkoa; ikitoka pale itakwenda Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao ndiyo wanaoifanyia uchambuzi kuangalia vigezo; kurejea kwenu, kutazama mipaka ambayo mmependekeza kwamba itatumika, hatimaye wanarudi ofisini wanajiridhisha, wanaandaa maelezo kuniletea.

Sasa moja ambalo naweza kumtamkia Mheshimiwa Mbunge hapa ni kwamba, bado mimi kama Waziri Mkuu sijapokea mapendekezo hayo. Ninachoweza kumwahidi tu ni kwamba kwa sababu wataalam wangu wote wako hapa, Mawaziri wote wako hapa, siyo suala gumu sana. Ni suala tu ambalo tukiwauliza TAMISEMI kwamba kwa nini jambo hili? Mmekwama wapi? Tunaweza tukapata majibu. Kwa hiyo, nimwahidi Mheshimiwa Ole-Medeye kwamba majibu tutayapata tena leo hii hii kutoka TAMISEMI ili tuweze kujua hasa liko katika hatua gani na kwa nini limechukua muda mrefu, ili kama haiwezekani tukwambie haiwezekani na kama inawezekana tuseme inawezekana, ila tulichelewa kwa sababu moja, mbili ,tatu.

SPIKA: Mheshimiwa Paul Lwanji!

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nalo ni kwamba wiki iliyopita tulipitisha Bajeti ya Ofisi yako na katika maeneo mengi uliyoinisha mojawapo ni suala la maeneo mapya ya utawala. Sasa katika ule ukurasa wa 77 mpaka 78 tukivyoangalia na hasa mimi niliona maeneo hayo yaliyoainishwa ni yale yaliyotangazwa mwaka 2010 na ni kwamba ni maeneo ambayo yanafanyiwa kazi na Serikali hivi sasa kwa maana ya miundombinu na mambo mengine.

Sasa sisi baadhi yetu ambao tuna maombi yetu ya muda mrefu, ni mwaka wa kumi sasa hivi, tulitarajia kwamba maeneo ambayo yako tayari

yamefuata utaratibu na vigezo na hasa ule utaratibu ulioutaja sasa hivi wa kupitia vikao vyote, kwamba safari hii basi wananchi wangetangaziwa ili waweze kujua hayo maeneo mapya hasa, maana ni kama sasa umekuwa utaratibu kila baada ya miaka mitano tunatarajia kwamba Serikali ingetangaza maeneo mengine mapya yajayo. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri Mkuu utatangaza lini? (Makofi)

SPIKA: Linafanana na hili la kwanza. Mheshimiwa Waziri Mkuu! Maswali leo yanaulizwa kwa kirefu, kwa hiyo, muda hautoshi.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Lwanji amekuwa na maombi kuhusu eneo lake, nami nakiri kwamba ni ya muda mrefu. Kimsingi nilimkatalia kumpa Wilaya kwa sababu idadi ya watu ilikuwa kwa kweli haitoshelezi kwa kiasi kikubwa, lakini nilikubali kwamba tunaweza tukaanza na hatua ya awali kwa maana ya kuigawa Halmashauri yake katika Halmashauri mbili ili tuweze kupata chombo cha kusukuma maendeleo katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, msingi wa uamuzi huo niliufanya kabla sijaufikisha TAMISEMI ni ukubwa wa eneo lake. Bahati mbaya eneo lake ni kubwa sana ingawa sehemu kubwa ni msitu, lakini linao wananchi ambao wanastahili kuhudumiwa kwa karibu zaidi kuliko ilivyo sasa.

Hata juzi hapa tulizungumza naye wakati wa Bajeti ya Waziri Mkuu, nikamwahidi kwamba basi ngoja watu wa TAMISEMI wakamilishe, wanalitee. Kwa hiyo, ninachoweza kumwahidi tu Mheshimiwa Lwanji, kwa sababu ni jambo nalifahamu na bahati nzuri nimeenda kutembelea na nimefanya ziara Manyoni, najua tatizo hili la kijografia lililopo pale, nimwambie tu kwamba nimeshawaagiza watu wa TAMISEMI wakamilishe ule mchakato wa kuigawa Halmashauri ile katika Halmashauri mbili ili uweze kuwa na chombo kitakachosaidia katika kusukuma maendeleo. Kwa hiyo, nafikiri pengine kabla Bunge hatujamaliza, tunaweza kuwa tumeshamaliza mchakato huu. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Lwanji, si unasema haya, utasubiri! (Kicheko)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na majibu mazuri lakini mara nyingi tunaelewa kwamba Serikali haiishii kwa kutoa ahadi za mdomo, Serikali hufanya kazi kwa maandishi; na wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu unajua jinsi nilivyosumbuka, ni miaka mingi! Sasa msinipe hisia kwamba viongozi wa Wizara hiyo, wakiwemo Mawaziri na watu wengine wamezidiwa nguvu na watendaji, kwamba mnapoagiza, yanaishia kuagizwa lakini haitekelezeki, tukifika ofisini...

SPIKA: Naona maswali yamekuwa marefu mpaka leo inakuwa *boring* sasa!

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, samahani.

Kwa kifupi ni kwamba, juzi nimefuatilia hili suala kama tulivyozungumza, lakini inaonekana sasa wanaanza kuitisha takwimu pamoja na mihutasari kutoka huko Wilayani, kitu ambacho kilikwishafanywa. Sasa mchakato huu unapoanza sasa hivi wakati kuna mchakato mwingine uliokwishafanyika katika ngazi hiyo ya kuomba Wilaya na ngazi ya kuomba Halmashauri.

Mimi nilikuja katika *fallback position* uliyoisema kwamba mtanipa Halmashauri. Sasa nilitarajia kingefanyika kitu kidogo tu cha kuweza kuhakikisha kwamba sisi tunatangaziwa eneo...

SPIKA: Mheshimiwa, unafanya kama uko ofisini kwa Waziri Mkuu? Tuko Bungeni, kitu gani unataka? Naomba tafadhali! (*Kicheko*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nirejee nilichosema. Tutalimaliza kabla ya Bunge hili. Ni jambo la siku nyingi, lakini alikuwa na sababu zake nzuri sana. Nafikiri baada ya kuwa nimelielewa, ndiyo maana nimesema bwana tutalimaliza. Hatuhitaji barua! Najua sasa hivi nazungumza hapa, watu wake Manyoni waniangalia, nami nisingependa kesho wakaniuliza swali hili nikiwa kwenye ziara.

Mheshimiwa Spika, jambo linaeleweka, sababu ya kutosha ipo, kutakuwa na changamoto za hapa na pale katika utekelezaji wako huko baada ya kupata lile eneo, lakini mengine haya huwa tunayakabili tunapokuwa kwenye utekelezaji wenyewe.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa David Kafulila!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu; unafahamu kwamba mpaka sasa bajeti nyingi kwenye miradi ya maendeleo imekwama kwa kiasi kikubwa ukichukua kwa mfano Wizara ya Viwanda, pesa ya kutoka kwa Wahisani ni asilimia 15; Wizara ya Maji, asilimia 23. Kwa ujumla bajeti imekwama na sababu moja kubwa kabisa ni namna ambavyo Serikali imeshindwa kuchukua hatua za kutosha katika sakata la ufisadi wa *Escrow*.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali mahususi kabisa; mwaka jana hapa Bungeni nilizungumza kuhusuana na kukwama kwa fedha za kutoka Marekani zaidi ya dola milioni 700 ambazo msingi wake ni ufisadi huu kwamba hawana imani na Serikali hii kwa namna

ambavyo inashughulikia utawala bora. Waziri wa Fedha akishirikiana na aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, wakasema huo ni uongo na kwamba taratibu ziko vizuri na Desemba mwaka 2014 Tanzania ingesaini Mkataba wa MCC II.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa wiki chache baadaye Bodi ya MCC ya Marekani ilithibitisha kutokusaini hizo fedha na sababu mojawapo ni hiyo; na kwa kuwa mpaka sasa nchi wenzetu mpaka Ghana walishapata; je, nini msimamo wa Serikali kuhusiana na uongo huu wa Waziri wa Fedha ndani ya Bunge kwamba Marekani haijazuia fedha lakini baadaye imethibitika kwamba imezuia, kwamba Desemba tungesaini, lakini mpaka sasa hatujasaini; na badala ya Desemba mpaka sasa ni takriban ni miezi sita imepita. Kwa hiyo, naomba msimamo wa Serikali, inachukua hatua gani kuhusiana na suala hili kwa sababu nchi inaumia kwa bajeti kuzidi kukwama? *(Makofi)*

SPIKA: Kama nilivyosema, mtakula maswali ya wenzenu, mengine hayatafikiwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza ametaka kwa uongo wa Waziri wangu ndani ya Bunge nitoe msimamo. Hilo siyo la kwangu, hilo ni la Bunge sasa. Kwa hiyo, kama alisema uongo hapa Bungeni, ziko taratibu ambazo unaweza ukazitumia kumtaka sasa atoe maelezo juu ya uongo wake na kadhalika. Nadhani hili siyo la kwangu hasa kwa maana hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa hapa, mimi naongoza Serikali hii. Tatizo hili la bajeti ya maendeleo toka kwa wadau, ukiamua kwamba utang'ang'ania katika kipindi kwenye eneo moja, siyo sahihi sana. Wewe mwenyewe unajua, miaka yote karibu mitatu, minne mfululizo, wadau hawa wa maendeleo wamekuwa hawatoi fedha kwa kiasi chote, huo ndiyo ukweli!

Kwa hiyo, hili lingine linalokuja kujitokeza, siyo kwamba ni jambo jipya, ni kitu *unique* sana. Sababu iliyotufanya Serikali tukachukua uamuzi wa kusema, basi bora tufunge mikanda sisi wenyewe tuwe na bajeti ambayo inatokana na vyanzo vyetu kwa sehemu kubwa, siyo kwa sababu hiyo unayoisema ambayo wewe umechukua tukio moja unalihusisha kana kwamba ndiyo msingi wa hoja yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema jambo hili limekuwepo kwa kipindi kirefu, ndiyo maana tukafika mahali kama Serikali tukasema, kama Serikali lazima sasa tuondokane na utaratibu wa kutegemea mno watu hawa halafu wanakaa wanawafikisha mahali ambapo kama Serikali mnashindwa hata kutekeleza majukumu yenu ya shughuli za maendeleo.

Sasa hilo unalolisema kwa sababu liliibuka katika mfumo ulioueleza, njia rahisi ni kumtaka Waziri wa Fedha atoe kauli ya Serikali juu ya jambo hilo ili Bunge liweze kujua kilichotokea ni nini na maelezo ya kina juu ya mtiririko mzima wa suala hili na namna lilivyoshughulikiwa.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kafulila, kwa kifupi sana. Nitawakata watu wawili hapa!

MHE. DAVID J. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwa mujibu wa taarifa ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ambaye ndiye Msemaji Mkuu katika masuala ya fedha nchi hii, ameshasema wazi kwamba sakata la Escrow ndiyo lilisababisha hali hii itokee mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali mahsusi kabisa; miongoni mwa maazimio ambayo tuliyafanya katika Bunge hili ilikuwa ni kwamba mmiliki wa sasa wa IPTL Singh Seth kwa mujibu wa *report* ya CAG alimiliki kwa kutumia nyaraka za kugushi, lakini mpaka sasa mmiliki huyo ukiachilia mbali *report* ya CAG lakini pia hukumu ICSID ya terehe 12 Februari, 2014 imethibitisha kwamba Serikali ya Tanzania inapunjwa kwenye malipo ya *capacity charge* ya dola milioni 2.6 ambazo ni takribani bilioni tano kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na hukumu ile ya ICSID ya Februari 12, 2014 pamoja na Maazimio ya Bunge, bado mmiliki huyo wa IPTL anaendelea kulipwa dola milioni 2.6 kila mwezi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kupata msimamo wa Serikali; inakuwaje inaendelea kumlipa mtu shilingi bilioni tano kila mwezi wakati umiliki wake ni wa *document* za kugushi kwa mujibu wa *report* ya CAG, lakini pia hukumu ya ICSID imeshasema kwamba Serikali inapunjwa. Ni kwa nini Serikali inaendelea kulipa shilingi bilioni tano kila mwezi katika mazingira kama haya? (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Kafulila, ungekaa mezani kama hapa, hili swali huoni kama jipya kabisa? Ndiyo, huwezi kunionyesha kidole, ni jipya na Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba usijibu. (Makofi)

Ni jipya! Sasa namwita Mheshimiwa Mnayaa! Msianze kupinga, ni jipya kabisa! La kwanza lilikuwa kodi. Mheshimiwa Kafulila, sipendi ubishi!

Mheshimiwa Mnyaa, tena kwa kifupi, una dakika tano!

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNAYAA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sheria Namba 5 ya Vyama Vingi ya mwaka 1992 ilikataza vyombo vyetu vya ulinzi kujihusisha na mambo ya siasa. Mfumo wetu wa siasa utasikia

kuna Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, kuna Naibu Katibu Mkuu Bara, yanatokea katika Chama cha CCM, Chama cha CUF, lakini bahati nzuri nchi hii hatujasikia kwamba CDF wawili au Naibu. CDF ni mmoja na vilevile IGP ni mmoja.

Mheshimiwa Spika, ujio wa Rais wa Mozambique hapa ulikuza mahusiano. Alisisitiza kukuza mahusiano ya kibiashara na ya kinchi na tunaelewa kwamba kuna mahusiano ya muda mrefu na vilevile tunaelewa kwamba tuna mahusiano ya FRELIMO na CCM. Swali langu liko hapo, hivi sasa kuna taarifa vyombo vya usalama vinajihusisha na uandikishaji wa ZAN ID kule Zanzibar katika Kambi za Chukwani na Misaili Masingini.

Pia huko nyuma ulishalalamikiwa ndani ya Bunge hili kwamba kuna watu wa kigeni wanapiga kura Tanzania. Je, uhusiano huu ambao umekuzwa na Rais wa Mozambique ambaye kalihutubia Taifa kupitia Bunge, Serikali itafanya mipango gani ya kuhakikisha raia wa kigeni wa Tanzania hawatapiga kura Mozambique; lakini na wa Mozambique walioko hapa hawatapiga kura katika Uchaguzi Mkuu ujao kwa Tanzania kama ambavyo imelalamikiwa hapa Bungeni na mimi mwenyewe na Mheshimiwa Genzabuke katika Bunge lililopita kuhusu raia wa kigeni wanaopiga kura Tanzania?

SPIKA: CDF! Haya Waziri Mkuu! (Kicheko)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, raia wa Msumbiji ni raia wa Msumbiji kama ilivyo raia wa Kenya ni raia wa Kenya; raia wa Uganda ni raia wa Uganda; na Burundi hivyo hivyo na Rwanda hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunayo matatizo mipakani kutokana na mwingiliano wa jamii ambazo ziko pande zote mbili na wakati mwingine zinazungumza lugha zilezile kuweza kupambanua juu ya uraia wa wakazi hao, lakini mkiwa makini, hili siyo tatizo hata kidogo! Ndiyo maana nilizungumza hapa mara ya mwisho, nikasema kinachohitajika, kwanza ni wakati wa uandikishaji kuhakikisha kwamba wale wanaokwenda kujandikisha, maeneo yale ambako wanatoka; vyombo, jamii kwa ujumla wake wanakuwa na uhakika kwamba hawa wanaokwenda kujandikisha ni raia kweli wanaotoka katika eneo hilo. (Makofi)

Pili, kutakuwepo na utaratibu vilevile ambao nilisema hapa wakati wa bajeti ya Waziri Mkuu. Tume walichofanya kwamba kila watakapokuwa wanamaliza uandikishaji, tusingoje mpaka tuje hatua za baadaye. Ile orodha ya majina ambayo yametokana na uandikishaji katika eneo husika, mapema kwa kadri itakavyowezezana iwekwe katika maeneo husika ili watu waweze kupata nafasi ya kuyapitia kujiridhisha kama kweli Bwana Pinda huyo anayesomeka hapa ni raia kweli wa hapa? Mbona najua huyu anatoka Malawi na siyo raia wa hapa?

Kwa hiyo, sisi tunachofanya kama Serikali, tunafanya kazi kwa karibu sana na Tume lakini tumewambia vilevile kwamba mara orodha ile itakapokuwa imekamilika, basi tutawaagiza viongozi katika maeneo husika wawaombe watu sasa wapitie ile orodha kwa umakini mkubwa kujiridhisha tu kwa sababu wanajuana katika ngazi nyingi za vijiji na kwa hiyo, kupunguza uwezekano wa mtu kutumia haki hiyo wakati sio raia. Hili utaliona litakuwa jambo la msingi hasa maeneo ya Karagwe na Kigoma ambapo mwingiliano ni mkubwa zaidi.

SPIKA: Kwa kifupi. Mheshimwia Mnyaa kuna mtu mmoja nitamruhusu.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, Mheshimwia Waziri Mkuu umakini unaozungumzia, nasikitika kwamba niseme labda haupo au una kusudi linalofanywa, kwa sababu wewe mwenyewe uliponiambia nishirikiane na Waziri wa Mambo ya Ndani wakati ule Mheshimiwa Masha, ulipatikana ushahidi wa watu wengi Dar es Salaam ambao wamepiga kura ambao sio Watanzania lakini wanaishi Dar es Salaam, ulipatikana ushahidi wa watu kutoka Mozambique ambao wanapiga kura Zanzibar na Mozambique.

Mheshimiwa Spika, ushahidi huo wanao Wizara ya Mambo ya Ndani, ushahidi huo mezani kwa Spika uliletwa hapa Ofisi ya Spika. Hivi sasa umakini huo utapatikanaje ikiwa kuna watu wanaandikishwa ndani ya Kambi za Jeshi au unataka mpaka ushahidi huo nao mwingine tukulettee? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nafikiri tusaidiane tu, kwa sababu hili jambo hili ni letu wote. Kwa hiyo, kama una maelezo mahususi ya uandikishaji unatokea katika makambi ya Jeshi, Kambi gani? Nani umeona ameandikishwa pale kinyume cha utaratibu? Jukumu letu kwa hatua hii tuliyonayo ni kutoa hiyo orodha mapema, kwa sababu mchakato bado unaendelea ili hawa wanaosadikiwa kwamba sio Watanzania, hatua stahiki kupitia Tume ziweze kuchukuliwa, maana hili ni jambo ambalo umelieleza vizuri, unaonekana una *facts* za kutosha.

Mheshimiwa Spika, nasema inawezekana kabisa kukawa na *oversights* hapa na pale ikapitiwa kabisa kwa sababu watu ni wengi na wanakwenda kujiandikisha kwa wakati tofauti. Lakini hili la kwako ambalo unasema ni ndani ya makambi ya Jeshi, hili ni rahisi. Ndiyo maana nasema ukitusaidia maelezo vizuri, tunaweza kabisa tukawabaini hao, wakaondolewa kwenye daftari na tukawa tumepunguza uwezekano wa watu kujitokeza wa aina hiyo.

SPIKA: Naongeza muda kwa sababu kulikuwa na matangazo pale mwanzoni. Mheshimiwa Selasini!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nipate kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika nchi yetu wananchi wetu wana pombe nyingi sana za kienyeji ambazo kwa namna moja ama nyingine zinawasaidia kuongeza kipato katika familia, kusomesha watoto na vilevile kuchangia shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, askari wetu hasa Jeshi la Polisi, wamekuwa wakiwabugudhi sana hawa wananchi, kuwapiga, kuwakamata na kuwanyang'anya vyombo vyao ambavyo wanatumia kwa ajili ya shughuli hii.

Napenda kujua Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama Serikali yetu ina sheria mahususi au kwa kutumia vyombo vyake kama *TBS* au *TFDA* kuweza kuwasaidia wananchi hawa kufanya hizi shughuli zao kitaalam zaidi na kwa sababu hii ni kama viwanda vidogo vidogo, shughuli hizi ziweze kuongeza ajira kwa Watanzania ambao wanazunguka maeneo mbalimbali ambayo pombe hizi zinatengenezwa!

SPIKA: Sijui kama unazijua pombe zenyewe! Mheshimiwa Waziri Mkuu! *(Kicheko)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Selasini amefichaficha jambo pale, hakutaka kulisema. Ni kweli zipo pombe za aina mbalimbali ambazo Watanzania wanazitumia katika mazingira yetu ya vijijini. Ukienda uchagani kule mnayo pombe tunajua vizuri, lakini kwa maelezo yake inaonekana pombe anayoizungumza itakuwa ni gongo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gongo ni pombe ambayo ni kweli kabisa kwa maana ya usimamizi wa utendaji wa Serikali, Serikali imekataza utengenezaji wa hiyo pombe; na kwa hiyo, unywaji wa hiyo pombe na msingi wake ni rahisi tu, ni kwa sababu viwango vyake havipimiki kwa kiwango ambacho unasema hiki ndiyo kiwango, wastani ambacho binadamu anaweza akakitumia. Ndiyo maana Serikali imekuwa makini kuhakikisha kwamba pombe hii lazima tuipege vita kwa sababu hiyo.

Sasa umenipa changamoto, kwamba lakini badala ya kuipiga vita, kwa nini msitafute utaratibu wa namna ya kuwawezesha Watanzania hawa; pombe hiyo hiyo, basi ikatengenezwa kwa viwango vinavyotakiwa, halafu muendele kuitumia kwa maana hiyo.

Sasa hilo ni jambo jema, lakini mimi sio mtalaam sana wa jambo hili. Ndiyo maana sisi tunachojua tu ni kwamba Konyagi ni aina nyingine ya gongo vilevile,

lakini Konyagi imepita kwenye mchakato, imethibitika, ikawekewa viwango ndiyo maana inanyweka kwa namna ambayo tunaamini haina madhara makubwa sana kwa binadamu.

Kwa hiyo, nakubali kuchukua hiyo changamoto. Sasa sina hakika, labda tuwape watu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, labda walitazame waone kama kuna uwezekano gani. Inaweza ikawa vilevile pengine ni *product* ambayo unaweza ukaipeleka kwenye kiwanda chetu cha Konyagi, ikafanyiwa kazi ya ziada kidogo kuweza kuiboresha na ikawa ni kinywaji kizuri. Sijui, lakini kwa sasa ni lazima tuendelee kusema, jamani Watanzania, pombe hii ni hatari, kwa sababu madhara yake yanajulikana.

Maeneo mengi yanayotumia pombe hii, mara nyingi ndiyo kwenye mauaji mengi na matatizo mengi sana. Ndiyo maana siyo vizuri kuiendekeza pombe ya kiwango kile.

SPIKA: Mheshimiwa Selasini, kwa kifupi sana, muda umepita!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, juzi Mkuu wa Wilaya ya Rombo alitoa taarifa kwamba wananchi wa Wilaya ya Rombo kutokana na kunywa kwa wingi pombe za aina mbalimbali, wanaume wamekosa uwezo wa kuwahudumia wake zao kindoa na kusababisha akina mama kwenda nchi jirani ya Kenya kutafuta huduma hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo hili limeleta tafrani kubwa katika Wilaya ya Rombo, akina mama wamekasirika; akina baba wamekasirika; na kwa sababu hiyo, kumetokea hali ya sintofahamu katika familia nyingi, hata ya kwangu; pale ambapo akina mama wanahisi kwamba hatuwezi kufanya kitu hicho na kwamba na sisi wanaume tunahisi wake zetu wanakwenda nchi jirani ya Kenya kukodisha wanaume! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, huu ni udhalilishaji wa hali ya juu na hiki ni kinyume kabisa cha haki za binadamu. Nakuomba; je, uko tayari kuwaomba radhi au kusema chochote kwa wananchi wa Rombo ili kuleta utulivu ambao umepotea kutokana na hali hii na tamko hili la Mkuu wa Wilaya?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya jambo lenyewe silijui. Sikupata nafasi ya kulipata. Tungeweza tukasema tuwaombe radhi. Lakini kuomba radhi kwa jambo usilolijua nayo ina tatizo lake vilevile. Hebu nipe muda nilifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, nipe nafasi kidogo nilichunguze kidogo, tuweze kuona kilichotokea hasa ni kitu gani na kauli ilitoka katika mazingira gani? Halafu tutaona ni hatua gani stahiki zinazopaswa kuchukuliwa. Kwa sababu kama ni

radhi, mwombaji ambaye anatakiwa ni huyo huyo aliyotoa hiyo kauli na katika maeneo yale alikoweza kutumia sentensi ambayo pengine imewaudhi Watanzania katika eneo husika.

Kwa hiyo, TAMISEMI tutawaagiza hapa walifanyie kazi haraka sana, baadaye tuweze kuona ni hatua gani sasa tuchuke dhidi ya huyo Mtendaji wetu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumechukua muda mwingi sana na sababu kubwa ni kwamba waulizaji walikuwa wanapiga hotuba kwetu. Lakini tumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maswali ya ajabu ajabu ya siku ya leo na umefanikiwa kuyajibu na mengineyo. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tukiuliza maswali *precisely*, wengi wanapata nafasi. Vinginevyo wanabakia wale wachache tu ndiyo wanapata muda wa kuuliza maswali. Kwa hiyo, tunaedelea. Katibu!

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali ya kawaida, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Atakayeuliza swali la kwenza ni Mheshimiwa David Kafulila!

Na. 64

Ubinafsishaji wa Shamba la Uvinza

MHE. DAVID Z. KAFULILA aliuliza:-

Mchakato wa ubinafsishaji wa shamba la Uvinza kwa mwekezaji *Aggrosoil* ulifanyika bila ridhaa ya wanavijiji na kwa shinikizo kutoka juu:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhusu uwekezaji huo ambapo mwekezaji kapewa ardhi kuzunguka Makao Makuu ya Wilaya?

NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Uvinza ni shamba la Serikali Namba 206 lenye ukubwa wa hekta 15,000 na siyo shamba la vijiji. Shamba hilo lilikuwa Ranchi ya mifugo chini ya Wizara ya Mendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Mwaka

1994 eneo hilo lilitolewa ili litumike kwa wakimbizi waliotoka nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo.

Baada ya wakimbizi hao kurudi nchini kwao, Mkoa wa Kigoma uliomba Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi shamba hilo ili litumike kwa shughuli za maendeleo kama vile kujenga Makao Makuu ya Wilaya ya Uvinza na Uwekezaji katika kilimo na mifugo, kwa barua yenye Kumbu. Na. CD 131/133/01 ya tarehe 27 Februari, 2010.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ilikubali kulitoa shamba hilo kwa Mkoa wa Kigoma kwa barua yenye Kumb. Na. BA 252/433/01 ya tarehe 2 Februari, 2011 kwa ajili ya malengo yaliyobainishwa likiwemo suala la uwekezaji katika Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2011 shamba hilo lilipimwa na kutengenezewa mpango wa matumizi bora ya ardhi, yaani *land use plan*. Hekta 10,000 za shamba hilo zilitengwa kwa ajili ya kilimo na kumilikishwa Kituo cha Uwekezaji (TIC) kwa madhumuni ya uwekezaji.

Hekta 5,000 zilizobaki zilitengwa kwa ajili ya Makao Makuu ya Wilaya ya Uvinza na makazi kwa watu watakaoshi jirani na Makao Makuu ya Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kampuni ya *Aggrosoil* kuwasilisha TIC maombi ya kuliendeleza shamba la hekta 10,000, mwaka 2012 TIC iliipa kampuni hiyo mkataba wa upangishaji (*derivative right*) kwa ajili ya uwekezaji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa upangishaji ulitaka *Aggrosoil* kuanza uwekezaji ndani ya miaka mitatu na pia kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kila baada ya miezi sita.

Kwa kuwa Kampuni ya *Aggrosoil* haijatumia masharti haya, Serikali ipo katika taratibu za kufuta mkataba wa upangishaji na baadaye kutafuta mwekezaji mwenye uwezo wa kutekeleza uwekezaji uliopangwa.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kuna tatizo la Serikali kualika wawekezaji bila kufanya uchunguzi kuhusu uwezo wao; na hii ipo katika sekta zote, ndiyo maana unaona kwamba hata kwenye *scandal* ya mabehewa, moja ya sababu ni kualika mwekezaji ambaye hana uwezo, matokeo yake tunaharibu nchi. (*Makofi*)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mwekezaji huyu Aggrosoil, tangu mwaka juzi, tuliambia Serikali hapa Bungeni kwamba huo uwezo hana na hata *consultant* wake wa Marekani alithibitisha hilo na akaachana naye.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata kauli ya Serikali, ni kwa nini inaalika wawekezaji matapeli kiasi cha kwamba baadaye wanathibitisha kushindwa kama ambavyo ameshindwa huyu mwekezaji na Serikali kukataa kuchukua ushauri wa Bunge inapoambiwa ukweli? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, hili shamba la hekta 10,000, linazunguka Makao Makuu ya Wilaya; kwa maneno mengine, lile eneo la hekta 5,000 Serikali ililolitoa itakuwa kwamba ili raia aende Makao Makuu ya Wilaya, inabidi apite shamba la mzungu kwanza ndiyo aingie Makao Makuu ya Wilaya!

Mheshimiwa Spika, naomba msimamo wa Serikali, ile Wilaya imeanzishwa pale katikati ya hekta 5,000, inazungukwa na hekta 10,000 za shamba la mwekezaji huyo, ile Wilaya kimantiki inatakiwa itanuke.

Mheshimiwa Spika, naomba msimamo wa Serikali, ni kwa nini isitamke hapa kwamba inaachana kabisa na mpango wa kutafuta mwekezaji wa aina yoyote katika eneo hilo kutokana na mazingira hayo ya Wilaya kuhitaji kupanuka; lakini pia mazingira ya kwamba mtu anakwenda kwenye Ofisi ya Serikali yake, anapita kwenye shamba la mzungu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, hili suala la kwamba Serikali inatafuta wawekezaji tapeli, mimi sina hakika nalo, nami nina hakika Serikali kwa vyovyote vile haiwezi kutafuta mwekezaji ambaye ni tapeli. Hilo nina hakika hivyo. Lakini kunaweza kukawa pengine habari ambazo labda hazikujulikana vizuri, inawezekana hilo, inawezekana watu wakaleta taarifa ambazo zinapopitiwa na Taasisi yetu ya Uwekezaji (*TIC*) zikaonekana za kweli.

Kwa mfano, suala la uwezo; wanaweza wakaleta *statements* zao za Benki wakaonekana wana uwezo huo na inawezekana pia wakaonyesha taarifa kwamba wamefanya kazi hizi maeneo mengine, kwa maana hiyo, wakapewa shamba kwa taarifa zile ambazo walikuwa wamewasiliha kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Kituo chetu cha *TIC* kabla hakijatoa shamba au shughuli nyingine yoyote ya uwekezaji kwa mtu yeyote mwekezaji, huwa inafanya *due diligence* ili kujua kwamba huyu anastahili kupewa au hastahili. Lakini pale inapobainika kwamba hawezi tena kufanya kazi ambayo aliomba; na kama nilivyojibu kwenye maswali ya nyongeza, Serikali inachukua hatua za kunyang'anya uwekezaji huo na mpango tulio nao

Nakala ya Mtandao (Online Document)

sasa hivi ni kupitia taarifa hiyo na kunyang'anya eneo hilo ili kuweza kutangaza kwa wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba mtu anapotaka kwenda Makao Makuu lazima apite katika eneo hilo ambalo linazunguka Makao Makuu na kwamba inawezekana wananchi pia hawana ardhi ya kutosha katika maeneo yao:-

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hivi, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama kweli bado wananchi wa Wilaya ya Uvinza wanahitaji eneo hilo, ni vizuri pia wakaomba kwa Serikali, na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ninayojua ni Serikali sikivu, itapitia hayo maombi itayafikiria.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba haya mambo yanapitia kwenye DCC, yatakwenda RCC na baadaye yatakwenda Serikali Kuu na TIC tutakaa pamoja, tutaangalia kama kuna uwezekano huo au namna gani. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Mheshimiwa Pauline Gekul, kwa niaba yake, Mheshimiwa Selasini.

Na. 65

X-Ray Katika Hospitali za Wilaya

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. PAULINE P. GEKUL) aliuliza:-

X-Ray zinazotumika katika Hospitali za Wilaya nchini ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Babati (Hospitali ya Mara) zimekuwa zikiharibika mara kwa mara na Serikali imekuwa ikitumia Wakala mmoja (*Phillips*) katika kutengeneza:-

(a) Kwa nini Serikali inatumia Wakala huyu mmoja wakati hatengenezi kwa wakati?

(b) Je, ni kwa nini X-Ray hizi zinakuwa zinaharibika mara kwa mara hata pale zinapotengenezwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selasini kama ifuatavyo:-

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, unajibu swali la Mheshimiwa Gekul, siyo la Mheshimiwa Selasini.

NAIBU WAZIRI W AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gekul, Mbunge wa Babati, kama ifuatavyo:-

WABUNGE FULANI: Siyo Mbunge wa Babati!

NAIBU WAZIRI W AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mbunge wa Viti Maalum. Swali hili limeelekezwa kule *Babati Urban*, Hospitali ya Mara, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitumia Wakala mmoja yaani *Phillips* kwa kuwa ndiye mtengenezaji, msambazaji na ndiye kupitia taratibu za ununuzi anayefanya matengenezo na matengenezo kinga kwa hospitali zote za Wilaya, Mkoa, Kanda na Taifa. Mashine hizi pia ni aina ya *Phillips*.

(b) Mheshimiwa Spika, mashine hizi kuharibika kwake hutokana na kutumika, kwa kuwa zimeendelea kutumika tangu mwaka 1999 hadi sasa. Kwa sasa Serikali ina mpango maalumu wa kuzibadili na tayari mashine nne za X-Ray na *Ultrasound* 14 mpya ziko bandarini kwa utaratibu wa ugomboaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupita Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Fedha na Wizara ya Uchukuzi, imekamilisha utaratibu wa mashine zilizopo bandarini na vipuri vilivyopo uwanja wa ndege na wakati wowote kuanzia sasa vitapelekwa katika Wilaya husika.

SPIKA: Mheshimiwa Selasini, maswali la nyongeza!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kutokana na ajali nyingi za barabarani zinazotokea hivi sasa, hasa vijijini, naomba kujua kama Serikali inafikiria au ina mpango wowote wa kununua *mobile X-Rays* za kuziweka katika Vituo vya Afya ili kuweza kusaidia wananchi wanaopata ajali mbalimbali vijijini na sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Hospitali nyingi Teule ambazo zinamilikiwa na mashirika ya dini, zinanunua na kutengeneza vifaa hivi zenyewe na inakuwa ni gharama kubwa sana. Je, Serikali haioni kwamba ili kuwasaidia wananchi wake umefika wakati sasa wa kusaidia hospitali hizi kupata vifaa hivi ili kuwahudumia wananchi wetu vizuri?

SPIKA: Ahsante. Sasa ni maswali ya Mheshimiwa Selasini hayo. Umjibu sasa! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI W AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, juu ya suala la kuwa na hizi *mobile X-Rays*, yaani zile za kutembeza, suala hili linawezekana na ninatoa rai kwa hospitali zote nchini zikiwemo za wenzetu za Mashirika ya Dini mbalimbali, waweze kutumia fursa ambayo tunayo pale

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii chini ya Bima ya Afya ya Taifa. Mwaka huu tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kukopesha maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa nchi nzima kwamba fursa hii ichangamkiwe. Imelazimu pale Ofisini tutoe timu yetu kuzunguka Mikoani kwa ajili ya kuhamasisha ukopaji wa vifaa hivi. Kwa hiyo, ni pamoja na *mobile x-rays* hizi, siyo tu katika maeneo yale ya ziada, hata katika hospitali kubwa. Siyo lazima kumwondoa mgongwa ambaye amezidiwa, yuko kitandani, kumpeleka Idara ya Mionzi, hapana.

Mheshimiwa Spika, *mobile x-rays* hizi hata kwenye hospitali kubwa zinatumiwa kwa wagonjwa ambao wako vitandani. Kwa hiyo, natoa rai, fursa hii itumike vizuri.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, suala la hizi Hospitali ambazo ni za Mashirika ya Dini, za binafsi kupewa *x-ray*, kupitia fursa hii ambayo nimeeleza, tunahimiza na fursa hii inawezekana na hospitali nyingine za wadau ambazo ziko kwenye maeneo kama hospitali teule; *x-rays* hizi tunazitoa, ndiyo sababu katika orodha tuliyonayo sasa hivi ya kupewa *x-ray*, tunazo hospitali 23 na nyingine za Mashirika ya Dini zimo, ziko katika mpango wa kupewa *x-ray*.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya!

Na. 66

Uharibifu Utokanao na Wanyamapori – Morogoro Vijijini

MHE. DKT. LUCY S. NKYA aliuliza:-

Kumekuwepo na matukio ya wanyamapori kuharibu mashamba, kuua mifugo na hata kuwajeruhi pamoja na kuwaua binadamu katika Kata za Kidugalo, Tonunguo, Ngerengere, Tegetero, Mkuyuni na Mkambarani katika Wilaya ya Morogoro Vijijini:-

(a) Je, ni lini Serikali italipa fidia ya mazao yaliyoharibiwa kwani ni muda mrefu tangu makadirio yapelekwe Wizarani?

(b) Je, ni kwa nini Serikali haijalipa kifuta jasho kwa familia zilizopoteza mifugo na ndugu zao kutokana na mashambulizi ya simba na mamba?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na kifungu Na. 68 kifungu kidogo cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, Serikali hulipa kifuta jasho na siyo fidia. Aidha, kifungu cha (3) cha Kanuni ya Malipo ya Kifuta Machozi/Kifuta Jasho ya Mwaka 2011, kinaainisha kuwa malipo yatafanyika tu endapo wananchi waliojeruhiwa au kuuawa au kuharibiwa mazao na mifugo. Malipo ya kifuta jasho au machozi huandaliwa baada ya tathmini kufanyika kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa kwenye kanuni.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014 Wizara yangu ilipokea maombi ya malipo ya kifuta machozi ya wananchi 65 kutoka katika kijiji cha Kidugo, Kolambili, Kisemo, Bonye, Ngerengere ambao mashamba yao yenye ukubwa wa hekari 68.3 yaliharibiwa na wanyamapori. Mazao yaliyoharibiwa ni mpunga, mahindi na matikiti maji.

Mheshimiwa Spika, wananchi walilipwa jumla ya shilingi 5,368,000/=. Aidha, kuanzia Septemba, 2014 hadi sasa, Wizara yangu imepokea maombi ya malipo ya kifuta machozi kutoka kwa ndugu wa wananchi watatu waliouawa na mamba katika Kijiji cha Mkono wa Mara. Wizara yangu imejiridhisha na maombi hayo ya malipo ya kifuta machozi na malipo yanaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, tumepokea kwa njia ya simu kutoka kwa Afisa wa Wanyamapori wa Wilaya ya Morogoro taarifa ya matukio manne; mawili ya watu kujeruhiwa na mamba katika Kijiji cha Bwakila Chini na wawili walioripotiwa, mtu mmoja kuuawa na mwingine kujeruhiwa na kukatwa vidole na fisi katika Kijiji cha Bwakila Juu. Malipo yatalipwa mara tu baada ya kupokea maombi rasmi na kuhakiki taarifa kwa mujibu wa kanuni za kifuta machozi.

Mheshimiwa Spika, hatujapokea tathmini inayohusu kuuawa kwa mifugo katika Kata ya Kichigula, Tonunguo, Ngerengere, Tegetero, Mkuyuni na Mkambarani. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa mara tutakapopokea tathmini kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini, Wizara yangu itaifanyia kazi na kuwalipa wahanga wa tatizo hilo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Nkya, swali la nyongeza!

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa kuwa hii Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 inahalalisha Serikali kulipa kifuta machozi na kifuta jasho na siyo fidia ambayo inaonekana kwamba wananchi wanaolipwa, madhara wanayokuwa wamepata ni makubwa sana; napenda kuuliza; je, Serikali haioni kwamba kwa kutumia dhana ya kifuta jasho na kifuta machozi wanawanyima wananchi haki yao? Kwa mantiki hiyo basi, kuwepo na haja ya kurekebisha hii sheria ili wananchi walipwe fidia kulingana na madhara waliyopata kutokana na hawa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba anasema maombi yaliyopelekwa ni ya wananchi 65. Maombi yaliyopelekwa ni zaidi ya wananchi 200 na zaidi na hela iliyolipwa inaonekana ni kwa wananchi 65 na inaelekea kwamba hata hao wananchi hawajapata hizo hela. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kunipa orodha ya wale ambao wamelipwa na wale ambao hawajalipwa na wanatarajia kulipwa kiasi gani ikilinganishwa na madhara waliyopata kutokana na huo uharibifu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, amekuwa anafuatilia sana matatizo ya watu wake katika Jimbo lake la Morogoro Kusini Mashariki. Ameshakuja ofisini kwetu zaidi ya mara tatu.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie tu kwamba tarehe 1 Julai, 2015 Mamlaka ya Wanyamapori itaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tumejipanga kupitia Mamlaka ya Wanyamapori kuangalia Sheria Na. 5 ya mwaka 2009 kama ina ukakasi wowote tuifanyie marekebisha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa; alifika Ofisini kwetu akazungumzia habari ya watu waliouawa na samba na tulilipokea. Lakini nataka nimwambie tu kwamba madai yanayohusiana na matatizo ya wanyamapori yako mengi. Kwa hiyo, tunayashughulikia awamu kwa awamu. Kwa hiyo, wale 65 tuliowashughulikia ni wale ambao tayari tumeshawalipa. Hata juzi Mheshimiwa Mzee Wassira alikuja Ofisini kwangu kuzungumzia madai kama hayo, kwa hiyo, tunalipa awamu kwa awamu, kwa sababu madai yako mengi. Nataka nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kulipa kadiri uwezo wetu wa kulipa tutakaporuhusu.

SPIKA: Ahsante. Tuendeleo na Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Jasson Rweikiza atauliza swali.

Na. 67

Ukosefu wa Mitandao ya Simu Vijiji vya Bukoba Vijijini

MHE. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza:-

Maeneo ya Bukoba Vijijini kama vijiji vya Ibosa, Butainamwa, Nsheshe na kadhalika, yanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa mitandao ya simu:-

Je, kwa nini wananchi wa vijiji hivi wamekuwa wakipewa ahadi hewa ya kupatiwa minara ya simu bila kutekelezwa?

SPIKA: Ahsante. Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia! Nani anajibu sasa swali hili la Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia? Mnatakiwa muwe *ready*, siyo kupoteza muda.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote uliainisha maeneo yenye uhitaji wa mawasiliano nchi nzima, ikiwa ni pamoja na maeneo yaliyo Wilayani Bukoba Vijijini. Baada ya zoezi la kuainisha maeneo kukamilika, kazi ya kupeleka mawasiliano maeneo yenye uhitaji ilianza kwa kutegemea upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bukoba Vijijini, upelekaji wa mawasiliano unafanyika katika Kijiji cha Bushagara (*phase II*), Igombe (*phase II*), TTCL na Rubale (*phase II B*) kwa Kampuni ya Vodacom. Sambamba na hilo, mkataba baina ya Serikali kupitia mfuko na watoa huduma na mawasiliano kwa lengo la kupeleka mawasiliano katika vijiji hivi na vijiji vingine vilivyoko kwenye awamu hii (*phase II B*) utasainiwa tarehe 23 Mei, 2015.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Mawasiliano ya *Viattel* itapeleka mawasiliano katika vijiji vya Kyaitoke, Lugaze, Omubwea na Rubale katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wake.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Ibosa, Butainamwa na Nsheshe katika Wilaya ya Bukoba Vijijini Mkoani Kagera vitajumuishwa katika miradi ijayo ya mfuko kwa kadiri fedha itakavyokuwa inapatikana.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Rwikiza, swali la nyongeza!

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kweli kwamba kazi alizosema zinafanyika, na mimi ni shahidi. Lakini nina swali moja la nyongeza. Vijiji hivi vya Ibosa, Butainamwa na Nsheshe havina mawasiliano kama alivyosema, kama nilivyouliza; na nimeuliza swali hili nafikiri leo ni mara ya tatu.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano haya ni muhimu sana kwa sababu licha ya mawasiliano tu ya simu, vile vile ndiyo njia pekee nzuri iliyopo sasa hivi ya kusafirisha fedha na huduma nyingine.

Mheshimiwa Spika, nilipojibiwa huko nyuma nilikuwa nimembiwa kwamba tayari fedha zipo kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na kazi hii itaanza mara moja, leo naambiwa kwamba hela hiyo inatafutwa. Sasa wananchi hawa waeleweje? Kwamba hiyo hela imekwenda wapi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Spika, vijiji hivi ambavyo nimevitaja ambavyo Mheshimiwa Mbunge anasema huko nyuma tuliwahi kusema kwamba vitapewa mawasiliano, inawezekana kweli tulishatoa tamko hilo, lakini kazi zote ambazo Wizara inafanya zinategemea na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo tumeahidi kwamba kazi zitafanyika, lakini zitafanyika pale ambapo fedha zitakuwepo; na pale ambapo fedha zinakosekana, tuna-reschedule hiyo kazi au tunaisogeza mbele.

Mheshimiwa Spika, lakini lazima niseme kwamba Wilaya ya Bukoba Vijijini ambayo bahati nzuri naifahamu, nimetembea eneo kubwa, kwa sehemu kubwa ina mawasiliano.

Sasa namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira. Wakati tunapeleka mawasiliano katika maeneo mengine ya Jimbo lake, basi pia maeneo haya mengine ambayo yanabaki na yenyewe tunasema kwamba hali ya fedha itakapokuwa nzuri, tutapeleka mawasiliano, basi Mheshimiwa Mbunge aridhie kwa sababu nchi yetu ni kubwa na mahitaji kila upande ni makubwa. Lakini tutapeleka mawasiliano katika maeneo haya kadiri ya upatikanaji wa fedha kwa kutumia Mfuko wa UCSAF, lakini pia na makampuni ya simu pale ambapo bajeti yake ya fedha haitakuwa sawa sawa.

SPIKA: Tuna Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Eugen Mwaiposa atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Betty Machangu!

Na. 68

TBC kuonesha Mashindani ya Kombe la Nchi za Afrika

MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MHE. EUGEN E. MWAIPOSA) aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Televisheni ya Taifa (TBC) ilishindwa kuonesha mashindano ya Kombe la Nchi Huru za Afrika yaliyofanyika Afrika Kusini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inawanyima Watanzania wapenda michezo hasa wa kipato cha chini fursa ya kuangalia na kujifunza kwa kuzingatia kuwa hawana uwezo wa kulipia king'amuzi cha *DSTV* na *Super Sport*?

(c) Je, Serikali inajipangaje kuonesha mashindano kama hayo katika siku zijazo katika Televisheni ya Taifa (TBC)?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Elishilinga Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), hurusha matangazo ya mashindano mbalimbali ikiwemo ya mpira wa miguu baada ya kununua haki ya matangazo hayo. Gharama ya kununua haki ya kuonyesha mashindano ni kati ya shilingi 800,000,000/= hadi shilingi 1, 200,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, haki ya kupata matangazo ya michezo katika televisheni inapatikana kwa kushindanisha vituo mbalimbali vya televisheni. TBC ilishindwa kuonyesha Mashindano ya Kombe la Nchi Huru za Afrika yaliyofanyika Afrika Kusini baada ya kushindwa kupata haki ya kurusha mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwapatia haki wananchi wake ya kuangalia mashindano ya michezo mbalimbali, Serikali ilinunua haki ya kuonyesha mashindano ya fainali ya Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Brazil mwaka 2014. Aidha, Serikali kupitia TBC ilinunua haki ya kuonyesha fainali za Mashindano ya Kombe la Nchi za Afrika (AFCON) mwaka 2015 yaliyofanyika Equatorial Guinea na mashindano hayo yote yaliainishwa kwenye vituo vya televisheni vya TBC na radio.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha TBC kuonyesha mashindano kama hayo, Serikali itaendelea kuliwezesha Shirika kununua haki za kuonesha mashindano

mbalimbali ya michezo na kuyatangaza kwenye vyombo vyake vya televisheni na redio.

SPIKA: Mheshimiwa Betty Machangu, swali la nyongeza!

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, wakati wa awamu ya kwanza ya Mwalimu Nyerere, kulikuwa na utaratibu wa kuonyesha sinema katika maeneo ya wazi kwa ajili ya kuwasaidia watu wasiokuwa na kipato kikubwa kuweza kupata burudani. Je, kwa nini Serikali isirudishe mpango huo, ikaweka screen kubwa kwenye maeneo ya wazi kwa ajili ya kuwasaidia hawa watu wenye kipato cha chini na hususan wakati wa michezo ya Kimataifa kama anavyosema Mheshimiwa Waziri kwamba wamenunua haki hiyo? Kwa kuweka hizo screen kwenye maeneo ya wazi, watu wa kipato cha chini wataweza ujifunza, lakini pia itaondoa utata wa watoto na vijana kwenda kwenye maeneo ya uchochoroni kuangalia video za picha chafu ambazo zinaoneshwa na watu binafsi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali itafanya lini *operation* ya kuondoa au kuzuia hao watu wanaofanya video za uchochoroni kuonyesha picha chafu? Kwa sababu mahudhurio ya wanafunzi wa shule za msingi katika maeneo mengine na hata mimba za utotoni zinatokana na kwenda kuangalia hizo sinema?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Betty Machangu ni kweli kwamba katika Serikali ya awamu ya kwanza ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kulikuwa na utaratibu huo wa kuonyesha picha katika maeneo ya wazi, lakini hii pia ilikuwa inachangiwa kutokana na mazingira yaliyokuwepo wakati huo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari ikishirikiana na Wizara ya Sayansi na Teknolojia, tumekuwa tukionyesha na picha na sinema mbalimbali katika baadhi ya maeneo kwa magari yanayozunguka nchini. Lakini uwezo wa magari yale hayawezi kuenea sehemu zote za Tanzania, lakini tutalichukua pia tuangalie namna gani tulifanyie kazi ili kuboresha hali hiyo ili maeneo mengi ya Tanzania yaweze kupata picha kama hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kwamba Serikali itafanya lini *operation* ya kuzuia picha chafu zinazooneshwa katika vituo mbalimbali na kuharibu utamaduni na mila za vijana wetu wanaosoma? Hili ni jambo ambalo kwa namna moja ama nyingine limeenea sana hasa katika maeneo ya Dar es Salaam na baadhi ya miji mikubwa.

Mheshimiwa Spika, nami naomba kutumia fursa hii kuziomba Halmashauri za Wilaya na Polisi kuchukua hatua za dhati kabisa dhidi ya vibanda ambavyo vinaonesha picha za sinema ambazo ni chafu na mara nyingi wamekuwa wakionesha baada ya saa 8.00 mchana wakijua fika kwamba wazazi wa wanafunzi wako makazini na ndipo wanafunzi wanapokimbia nyumbani na kwenda kuangalia picha hizi. Nirudie tena kuziomba mamlaka zinazosimamia maeneo yao kuchukua hatua za haraka ili kudhibiti hali hii.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Rage, swali la nyongeza!

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Sasa hivi ving'amuzi vya *DSTV* ni vya gharama kubwa sana. Je, ni lini Serikali itafanya mpango wa kuweza ku-control au kupata bei nafuu kama wanavyopata wenzetu wa Uganda na nchi nyingine za Afrika?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, biashara ya ving'amuzi ni biashara ya ushindani. Makampuni mbalimbali yanashindana kuonyesha ama kufanya biashara zao, lakini sisi kwa upande wa Serikali tumeliona hilo na tutalifanyia kazi.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Mnisamehe leo hayakuwepo maswali ya nyongeza, tulikuwa tunafidia pale tulipopoteza kwenye Maswali ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, naomba niwatambue baadhi ya wageni walioko hapa.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni Watendaji Wakuu kutoka Wizara ya Katiba na Sheria wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bi Maimuna Tarishi. Naomba asimame alipo; ahsante, yuko pale. Yupo pia Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu, Mheshimiwa Jaji Shaban Lila; karibu sana, ahsante sana. Tuna Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Ndugu Hussein Katanga; ahsante sana. Tuna Msajili Mkuu wa Mahakama, Ndugu Ignus Kitusi; ahsante sana. Tuna Kaimu Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndugu Sara Mwaipopo; ahsante sana. Tuna Mkurugenzi wa Uendeshaji Mashitaka Tanzania (*DPP*) Bwana Biswalo Mganga, ahsante, karibu sana. Tunao Waheshimiwa Majaji, naomba walipo hapo wasimame kama wapo. Karibuni sana Waheshimiwa Majaji, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna Watendaji Wakuu wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara pamoja na Watumishi kutoka Wizara ya Katiba na Sheria; tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu ambao ni Makatibu kutoka Kata ya Gidhababieg Wilaya ya Hanang wakiongozwa na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ndugu Michael Sumaye; na hilo jina tena limenishinda kabisa! Naomba msimame mlipo; ahsante sana, karibuni sana. *(Kicheko)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, hao ni Ndugu Evans Saul kutoka *Marire Secondary School*, asimame alipo huyu! Yupo Ndugu Ramadhan Khalifa kutoka *DCT Secondary School*; yuko Asha Jafari kutoka *DCT Secondary School*, yuko Frank Joshua kutoka *Azania Secondary School*; na Ndugu Aboubakar Mohamed kutoka *Kiwanja cha Ndege Secondary School*. Naomba wasimame mahali walipo kama wapo, labda wamekosa nafasi, watakuja baadaye.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Tundu Lissu ambao ni Ndugu William Jansen kutoka Kampuni ya *Focus Design and Photography* ya Dar es Salaam. Yuko wapi huyo? Yuko pale nyuma, ahsante.

Vilevile wapo Wenyeviti 47 kati ya vijiji 50 vya Jimbo la Singida Mashariki pamoja na viongozi wa CHADEMA wa Jimbo wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jimbo, Ndugu Jumanne Mussa Rajab. Hawa wote wasimame walipo! Amehamisha Mkoa wote huko. Haya, karibuni sana! *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Waziri wa Nchi, Ofisi Makamu wa Makamu wa Rais, Mazingira ambao ni Ndugu Emmanuel Sanga, mpigakura wake. Emmanuel Sanga yuko wapi sijui! Karibuni sana!

Halafu tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Naibu Waziri wa Maji kutoka Mvomero ambao ni Kamati ya Wakulima wa Bonde la Mgongola wakiongozwa na Ndugu Patrick Longomez, Mwenyekiti wa Mkindo Bungoma. Naomba wasimame walipo kama wameingia. Ahsante na karibuni sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami ambao ni Ndugu Joel Makwaia, Katibu wa UVCCM Manispaa ya Moshi na Ndugu Abdallah Thabit, Mwenyekiti wa UVCCM Manispaa ya Moshi. Naomba wasimame walipo kama wapo. Ah, wako hapo, karibuni. Halafu tunao wageni wa Mheshimiwa Joshua Nassari ambao ni Ndugu Nicodemus Minde kutoka Taasisi ya Utafiti na Ushauri Arusha. Naye yuko wapi sijui! Ahsante, yuko hapa, karibu.

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, wakiongozwa na Baba Askofu Julio Raphael Usukwa wa Jimbo la Mufindi. Naomba hawa wageni pia wasimame walipo, ahsanteni na karibuni sana. Tuna wageni wa John Paul Lwanji, wakiongozwa na Ndugu Boniface Abraham. Naomba wasimame hawa wageni wa Mheshimiwa Lwanji. Ahsante, karibuni sana!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Nawashukuru wageni wote na wale ambao hatukuwataja hapa. Karibuni sana!

Waheshimiwa Wabunge, shughuli za kazi; Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii - Mheshimiwa Mustapha Mkullo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 21 watakuwa na kikao saa 8.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa 'B'.

Halafu nimeombwa na Ofisi kutangaza kwamba Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Madhehebu ya Kiprotestanti kwamba leo Alhamisi tarehe 21 watakuwa na Ibada katika Ukumbi wa Msekwa Ghorofa ya Pili; nafikiri na wengine wanaotaka kwenda huko, kwa hiyo kutakuwa na ibada hiyo.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Kwa kawaida tuna muda hafifu kwelikweli wa dakika, kwa hiyo, sitapokea miongozi mingi zaidi ya miwili tu.

Mheshimiwa Kayombo atafuatiwa na Mheshimiwa Kafulila, basi!

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nasimama kwa kanuni ya 68(7). Nchi yetu ilipokea utawala wa vyama vingi ikiamini kabisa kwamba ndiyo utakaoleta maendeleo, amani na kukomaza demokrasia.

Mheshimiwa Spika, jana katika Wilaya ya Mbinga, Kijiji cha Luanda kulikuwa na Mkutano wa chama cha CHADEMA na katika Mkutano ule kulikuwa na matusi mengi wakimtukana Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge na Madiwani. Mtendaji wa Kijiji kwa sababu alikuwa hana taarifa ya mkutano huo, alikwenda kwa wale waliokuwa kwenye mkutano na kuwaomba kama wana kibali chochote. Waliokuwa wanaendesha mkutano huo, walimwambia wewe ni kijana mdogo, ni takataka; wakampiga, akatoka damu sana na akakimbizwa hospitali na wasamaria wema.

Mheshimiwa Spika, Mtendaji wa Kijiji ni mlinzi wa amani katika kijiji. Kama huyu mlinzi wa amani anadhaliishwa namna hii na mlinzi huyu anapaswa kuwalinda hata hao wanaofanya mkutano, uko wapi usalama wa wananchi? Serikali inasema nini juu ya jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante!

SPIKA: Ahsante! Mheshimiwa Kafulila!

MHE. DAVID Z. KAFULILA Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako kuhusiana na maazimio ambayo tuliyafanya mwaka jana kuhusiana na sakata zima la ufisadi wa *Escrow* na katika maazimio hayo, tulikubaliana...

WABUNGE FULANI: Aaah!

MJUMBE FULANI: Si mtulie!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, nayazungumza haya kwa sababu yanatafuna nchi na bajeti zinakwama hapa!

SPIKA: Endelea! Nimekupa nafasi, endelea kuzungumza.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, tulikubaliana kwamba kabla ya mwisho wa uhai wa Bunge hili Serikali itatoa taarifa ya utekelezaji wa maazimio tuliyoyafanya kuhusiana na ufisadi huu wa *Escrow*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeipitia ratiba hii, hakuna mahali ambapo inaonyesha kwamba kuna siku Serikali itatoa taarifa kuhusiana na utekelezaji huo ili kusudi Waheshimiwa Wabunge tuchangie na tufikie maamuzi kwa sababu hali ya sasa; mara umesikia Ikulu imesafisha watu na kadhalika; kuna mambo ya msingi ambayo bado hayajapatikana. Kuna watu wamechukua fedha *Stanbic*, bado majina yao hayafahamiki!

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwamba ni lini suala hili litaingizwa kwenye ratiba ili tujue ni lini tunajadili utekelezaji wa maazimio hayo kama tulivyoazimia? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Opolukwa!

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita wakati nachangia kuhusu bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu niliongea kuhusu matatizo ya Walimu wa Wilaya ya Meatu; na kati ya mambo ambayo niliyaongelea ikiwa ni pamoja na maslahi yao ambayo hayajapatikana kuhusu mwalimu ambaye alifariki kwa uzembe wa madaktari ikiwa ni pamoja na mwalimu mwingine ambaye alipata ajali akaumia, akaomba kusogezwa kituo cha karibu na Hospitali ya Wilaya na ikawa imeshindikana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine mengi niliyoongea na walimu hawa, cha kushangaza, juzi tarehe 18, walimu hawa ambao niliwaita

kwa ajili ya kuongea nao na kujua matatizo yao na kuyaleta katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuyafanyia kazi, wamesimamishwa kazi eti kwa sababu waliongea na Mbunge na kwamba wameidhalilisha Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwamba ni kweli na hii ni sahihi kwamba wananchi wanapokwenda kuongea na mwakilishi wao na hasa Mbunge ili aweze kufikisha matatizo yao kwenye mamlaka inayohusika, wanasimamishwa kazi na kutishiwa kufukuzwa kazi tu kwa sababu wameongea na Mbunge wao kwa ajili ya uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa suala hili. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana kwa miongozo yote, Spika atajibu kwa wakati muafaka.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016 – Wizara ya Katiba na Sheria

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango wa Matumizi ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, hotuba nitakayoisoma ni muhtasari tu wa hotuba kamili ambayo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa. Naomba hotuba yote kama ilivyogawiwa iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2015/2016.

Kwa namna ya pekee napenda kutoa ahsante nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunipa fursa ya kuendelea kulitumikia Taifa letu katika ngazi hii ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa salamu za pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi kwa kuondokewa na Mbunge wao, Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba aliyefariki tarehe 28/2/2015. Hakika mchango wake utakuwa na nafasi ya pekee katika historia

ya Jimbo lake. Halikadhalika, Watanzania wengi tutamkumbuka kama askari wa mstari wa mbele na mhamasishaji wa aina yake. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu nikupongeze wewe kwa kuliongoza Bunge letu kwa umahiri, ushupavu na weledi mkubwa. Uongozi wako umeliweka Bunge letu katika ramani ya dunia na kufanya wewe Mheshimiwa ukabidhiwe nafasi mbalimbali za uongozi ndani na nje ya Bara letu.

Vilevile nampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wao mahiri kila wanapokalia Kiti cha Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati nimpongeze Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa dira na mwelekeo wa shughuli wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Wizara yetu ina imani kubwa kwake binafsi na kwa Kamati anayoiongoza. Wizara yetu inatoa shukrani nyingi kwa Kamati yake kwa ushauri mzuri na mapendekezo ambayo yamesaidia sana kuboresha mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Tutaendelea kushirikiana na Kamati hii ili tuweze kufikia Dira ya Wizara ya Haki Sawa kwa Wote na kwa Wakati na Dira ya Taifa Kuelekea mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kuwapongeza Waheshimiwa Dkt. Grace Puja na Innocent Sebba kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge. Nawatakia kheri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inazo Taasisi, Ofisi na Idara ambazo zinafanya kazi chini ya mwamvuli wake. Hizi ni Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Taasisi ya Mafunzo ya Wanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kwa kuongozwa na dira ya Wizara ya Haki Sawa kwa Wote na kwa Wakati, Wizara imejipanga vema kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake makuu ambayo ni pamoja na masuala ya Katiba, kusimamia Sheria na utoaji haki, kuandaa Miswada ya Sheria, kuendesha mashitaka, kutoa

ushauri wa kisheria na kuendesha mashauri ya madai, kukuza na kuhifadhi haki za binadamu, kushughulikia usajili, ufilisi na udhamini, kushirikiana Kimataifa katika kubadilisha Wahalifu, kutoa mafunzo ya Wanasheria na kusimamia ustawi na maendeleo ya watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nifanye mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Katika kipindi hiki Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishwa jumla ya shilingi 234,246,819,000/=. Hadi kufikia Aprili, 2015 ilipokea jumla ya shilingi 108,903, 900,746/= sawa na 46.5% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mpango kazi wa mwaka 2014/2015 Wizara ilitumia fedha zilizopokelewa kutekeleza vipaumbele vyake kama ilivyoielezwa katika aya ya 11 ya hotuba yangu. Naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba tumetekeleza vipaumbele hivyo kwa kuongozwa na kaulimbiu isemayo, “haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyopokonywa.” Katika utekelezaji wa vipaumbele hivyo, masuala yafuatayo yalizingatiwa:-

Mheshimiwa Spika, Bunge Maalum la Katiba lilihitimisha jukumu lake tarehe 4 Oktoba, 2014 na kukabidhi Katiba Inayopendekezwa kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tarehe 8 Oktoba, 2014 Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kufuatia tukio hilo la kihistoria, Wizara ilichapisha nakala 2,000,400 za Katiba Inayopendekezwa. Kati ya hizo, nakala 2,000,000 zilichapishwa katika mfumo wa maandishi ya kawaida, nakala 200 zilichapishwa katika maandishi ya nukta nundu kwa ajili ya watu wasioona na nakala nyingine 200 zilichapishwa katika maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya watu wenye ualbino. Nakala 1,141,300 zilizo katika maandishi ya kawaida zilisambazwa kwa wananchi Tanzania Bara ambapo kila Kata ilipata nakala 300 na nakala 200,000 zilipelekwa Zanzibar; nakala 658,700 zilisambazwa kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, Vyama vya Siasa, Jumuiya za Kidini, Taasisi za Elimu ya Juu na Asasi za Kiraia Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kusambazwa kwa Katiba Inayopendekezwa kumesaidia sana kujenga uelewa wa maudhui ya Katiba inayopendekezwa ili kuwawezesha wananchi kujiandaa kwa kura ya maoni wakati utakapofika.

Napenda kutoa rai kwa viongozi wa Serikali, Vyama vya Siasa, Jumuiya za Kidini, asasi za kiraia na wanajamii kwa ujumla kuwahamasisha wananchi kuisoma Katiba Inayopendekezwa na kuielewa vizuri kwa manufaa ya Taifa letu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mfumo wa sheria na utoaji haki. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliimarisha usikilizaji wa mashauri yaliyosajiliwa Mahakamani na kupunguza idadi ya mashauri ya muda mrefu katika ngazi zote za mahakama. Katika kipindi hicho kulikuwa na mashauri 247,267 ambapo mashauri 70,484 ni ya kutoka mwaka 2013/2014 na mashauri 176,783 ni yaliyosajiliwa mwaka 2014/2015. Kati ya hayo, mashauri 179,469 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati za Kusukuma Uendeshaji Mashauri ambazo zipo katika ngazi za Wilaya, Mkoa, Kanda na Taifa zimekuwa nyenzo muhimu katika kupunguza idadi ya mashauri ya muda mrefu na msongamano wa mahabusu. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliratibu vikao vya Kamati hizi katika ngazi mbalimbali pamoja na kuyatembembelea maeneo wanamoshikiliwa watuhumiwa wa uhalifu ili kusikiliza kero zao. Wizara itaendelea kuimarisha Kamati hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha unaokwisha, Wizara ilisimamia utekelezaji wa mpango wa kutengenisha mashtaka na upelelezi. Madhumuni ya mpango huo ni kudhibiti, kusimamia uendeshaji wa mashitaka na kuratibu shughuli za upelelezi kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki inatendeka. Aidha, madhumuni mengine ya kuanzishwa kwa mpango huu ni kuhakikisha kuwa huduma za uendeshaji mashitaka zinasogezwa karibu na jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imekamilisha kufungua Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Aidha, tunakusudia kufikisha huduma hizo kwenye ngazi ya Wilaya nchini kote kwa kuanzia na Wilaya za Monduli na Temeke.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilisimamia uendeshaji wa mashauri ya jinai 8,025 katika ngazi za Mahakama za Rufani, Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya. Kati ya hayo, mashauri 5,772 yalihitimishwa na mengine 2,253 yanaendelea kusikilizwa. Aidha, Wizara iliratibu uendeshaji wa jukwaa la Taifa la Haki Jinai na kushirikiana na vyombo mbalimbali vinavyohusika na masuala ya sheria ili kuimarisha utekeleza wa majulimu ya Wizara katika Sekta hii ya Haki Jinai.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya rushwa na udanganyifu, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya vimekuwa tishio katika jamii. Kadhalika, vitendo vya mauaji na ukatili kwa watu wenye ualbino, vimelifedhehesha Taifa na kuchafu taswira ya nchi yetu.

Wakati Bunge lako Tukufu likiendelea, tarehe 13 Mei, 2015, mwanamke mmoja katika Wilaya ya Mlele Mkoa wa Katavi, alikatwa kiganja cha mkono

kwa imani za kishirikina. Wizara yetu imejizatiti katika kukabiliana na matuko haya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Sheria na waliomo ndani ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa mnasaba huo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilisimamia uendeshaji wa mashauri 14 ya mauaji na ukatili kwa watu wenye ualbino. Kati ya hayo, shauri moja lilihitimishwa ambapo watuhumiwa wanne walipatikana na hatia ya mauaji na kuhukumiwa adhabu ya kifo. Mashauri sita yako katika hatua mbalimbali za usikilizaji Mahakamani na mashauri saba yako katika hatua ya upelelezi.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitumie fursa hii kutoa wito maalum kwa Watanzania wote kuchukua hatua za dhati kukomesha vitendo hivi vya kikatili, vya kijinai, vinavyokiuka haki za binadamu na vinavyochafua jina zuri la nchi yetu. Ni sharti tutambue kwamba maisha ya watu wenye ualbino ni maisha yetu, tuyalinde.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa dawa za kulevya, katika mwaka wa fedha 2014/2015 kulikuwa na jumla ya mashauri 79 yaliyohusu dawa za kulevya. Kati ya hayo, mashauri 58 ni ya zamani na 21 ni mapya. Mashauri yote haya yapo katika hatua mbalimbali za kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mashauri yanayohusu rushwa na udanganyifu, kulikuwa na majalada 250 yaliyopokelewa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Baada ya kufanyiwa uchambuzi, majalada 131 yaliandaliwa hati za mashtaka na 72 yalirejeshwa TAKUKURU kwa uchunguzi zaidi. Majalada 47 yaliyobaki yanaendelea kufanyiwa uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliwakilisha Serikali Mahakamani katika mashauri 839 yanayohusu ndani na nje ya nchi. Mashauri hayo ni ya kikatiba, madai na yale yanayohusu ukiukwaji wa haki za binadamu. Kati ya hayo, mashauri 37 yalihitimishwa na 802 yako katika hatua mbalimbali za kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashauri ya kikatiba, Wizara iliwakilisha Serikali katika mashauri 93 ambapo mashauri matano yalihitimishwa na mengine 88 yanaendelea kusikilizwa. Mashauri ya madai yalikuwa 51 na yote yanaendelea kusikilizwa. Vilevile Wizara iliwakilisha Serikali katika mashauri sita ya ukiukwaji wa haki za binadamu yanayoendelea kusikilizwa katika Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliyoko Banjul, Gambia.

Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua za mara kwa mara kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mfumo imara wa sheria unaokidhi mahitaji

ya jamii kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ili kufanikisha hilo, Wizara iliendesha tafiti mbalimbali ambazo zimekuwa msingi wa marekebisho ya baadhi ya sheria na kutungwa kwa sheria mpya.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya tafiti hizo ni pamoja na kuwepo kwa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa, Sheria ya Msaada wa Kisheria na Sheria ya Kulinda Watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi. Muswada wa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa umesomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge lako Tukufu. Mapendekezo ya kutunga sheria za Msaada wa Kisheria na Sheria ya Kulinda Watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi yapo katika ngazi za maamuzi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, uandishi na uwasilishaji wa Miswada ya Sheria Bungeni ni moja ya hatua muhimu katika kuimarisha utawala wa sheria nchini. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliandaa jumla ya Miswada 21 iliyosomwa mbele ya Bunge lako ambapo Miswada 14 kati ya hiyo ilijadiliwa na kupitishwa na Bunge. Miswada yote iliwasilishwa Bungeni kwa Kiingereza na Kiswahili ili kuzifanya sheria hizi zieleweke kwa urahisi na wananchi. Vilevile Wizara ilihakiki Sheria Ndogo 286 na kuzitangaza katika Gazeti la Serikali. Sheria 128 zilifanyiwa urekebu katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuhakikisha kuwa Miswada yote ya sheria inaandikwa kwa Kiingereza na Kiswahili, Wizara ilitafsiri sheria nyingine za nchi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Sheria zilizotafsiriwa zimetajwa katika aya ya 30 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, uhakika na ubora wa huduma za kisheria zinazotolewa na Wizara unategemea sana kuwepo kwa miundombinu imara kama vile majengo, vitendea kazi vya kisasa na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilitekeleza miradi mbalimbali ili kuimarisha upatikanaji wa majengo ya ofisi, nyumba za watumishi na matumizi ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilitumia TEHAMA katika usikilizaji wa mashauri, upokeaji na uchambuzi wa malalamiko yaliyohusu kuvunjwa kwa haki za binadamu na kukiukwa kwa misingi ya utawala bora; na ufuatiliaji wa majalada ya mashauri ya jinai.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara inakamilisha maandalizi ya kuanzisha mfumo wa malipo ya ada za usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini kwa njia ya kielektroniki. Mifumo hii itasaidia kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali za Umma na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilikuwa na miradi ya ujenzi wa jengo la Mahakama ya Tanzania, Dar es Salaam; ujenzi wa nyumba 12 za Majaji katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Dodoma, Iringa, Tanga, Arusha, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mtwara na Kilimanjaro; ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Shinyanga Kigoma, Lindi, Manyara, Mara, Morogoro na Singida; ujenzi wa Mahakama tisa za Wilaya za Bagamoyo, Baridadi, Bunda, Bukombe, Hanang, Kasulu, Kilindi, Nkasi, Makete; na ujenzi wa Mahakama 26 za Mwanzo nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara ilikuwa na miradi ya ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Tabora, Mwanza, Ruvuma na Mbeya; Mahakama nane za Hakimu Mkazi katika Mikoa ya Singida, Mara, Ruvuma, Tabora, Kigoma, Rukwa, Kagera na Morogoro.

Vilevile Wizara ilikuwa na miradi ya ukarabati wa majengo ya Mahakama nne za Wilaya za Monduli, Kiteto, Newala na Muleba; na Mahakama tisa za Mwanzo za Magugu, Vwawa, Lindi Mjini, Kiteto, Bereko, Robanda, Gairo, Rusumo na Makambako. Miradi yote ya ujenzi na ukarabati iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji kazi wa Mahakama ya Tanzania, Rais alifanya uteuzi wa Majaji wawili wa Mahakama ya Rufani, Jaji Kiongozi na Majaji 20 wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Pia Rais alifanya uteuzi wa Msajili wa Mahakama ya Rufani na Msajili wa Mahakama Kuu. Katika kipindi hicho walijajiriwa Mahakimu Wakazi 57 na Wasimamizi wa Mahakama 24.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha nidhamu kwa watumishi wa Mahakama, Wizara iliendesha programu za mafunzo kwa Kamati za Maadili za Mikoa za Mikoa ya Dodoma, Katavi, Rukwa na Singida. Kamati hizi zimekuwa vyombo muhimu vya kusimamia maadili na nidhamu za watumishi wa Mahakama.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliziwezesha Kamati saba za Mikoa na 36 za Wilaya kuendesha vikao vya kuchunguza na kujadili malalamiko ya ukiukwaji wa maadili ya Mahakimu. Pia Tume ya Utumishi wa Mahakama ilishughulikia mashauri 27 ya nidhamu na kuyatolea maamuzi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa elimu kwa umma ni mkakati muhimu wa Wizara wa kuhakikisha watu wanafahamu na kudai haki zao; na wanajua wajibu wao kwa mamlaka za nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango huo, Wizara ilirusha hewani vipindi 25 vya redio na televisheni na kusambaza machapisho 15,500 ya aina

mbalimbali kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara, maonesho ya Kitaifa, Idara na Taasisi za Serikali.

Vilevile Wizara ilifanya mikutano na viongozi wa kijamii na watendaji wa Serikali katika Wilaya za Chato na Tabora ili kuongeza uelewa wa wajibu wao wa kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu. Aidha, Wizara ilitoa elimu kwa wafanyakazi wa viwanda vilivyo chini ya mradi wa Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuuza Nje (EPZA) na kuratibu maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Ulimwenguni kama ilivyoelezwa katika aya ya 38 ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, usajili wa matukio muhimu ya binadamu una manufaa kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa takwimu zinazohitajika katika mipango ya maendeleo na kuweka mazingira mazuri ya kuimarisha haki mbalimbali za raia.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilitekeleza mikakati ya jumla na mahsusi ya kuimarisha usajili wa matukio yanayomhusu binadamu kama vile hali ya ndoa, talaka, vizazi na vifo. Idadi ya matukio yaliyosajiliwa imeelezwa katika aya ya 40 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliandaa programu mahsusi ya usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano iliyotekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Chini ya programu hii Wizara ilisajili jumla ya watoto 59,463 na kutoa vyeti vya kuzaliwa bila malipo. Mkakati mwingine mahsusi ulikuwa ni usajili wa watoto waliopo mashuleni waliokuwa na umri wa kati ya miaka sita na 18 ambapo Wizara ilisajili jumla ya watoto 18,800.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweza kuongeza kiwango cha usajili kutoka wastani wa chini ya asilimia 10 mwaka 2012 hadi asilimia 16 ilipofika Aprili, 2015. Hata hivyo, kiwango hiki bado ni cha chini ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2020. Sanjari na shughuli za usajili, Wizara ilitoa hati 203 kwa wadhamini wa taasisi na asasi za kijamii na kuwapa elimu juu ya haki na wajibu wao wa kisheria kulingana na Katiba za Asasi wanazozisimamia. Aidha, Wizara ilitoa elimu kwa umma kuhusu mirathi, namna ya kuandika na kuhifadhi wosia kupitia redio, televisheni na mabaraza ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ilitoa ushauri wa kisheria katika maeneo mbalimbali. Wizara ilihakiki na kuchambua mikataba 2,993 ya kibiashara, ununuzi wa umma na uwekezaji. Pia Wizara ilitoa ushauri wa kisheria kwa masuala anuwai yaliyowasilishwa kwake na Wizara, Idara, Wakala na Taasisi nyingine za umma.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuiwakilisha Serikali katika masuala ya kisheria, Wizara ilitoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi wasio na uwezo wa kupata huduma za Uwakili kupitia mfumo wa kawaida uliopo. Huduma zilizotolewa zilihusu elimu na ushauri wa kisheria; na kuandaa nyaraka za kupeleka mashauri Mahakamani. Aidha, Wizara ilikamilisha maandalizi ya mapendekezo ya kutunga Sheria ya Msaada wa Kisheria ili kuiwezesha Serikali kusimamia ubora na upatikanaji wa huduma za kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za uwakili nchini.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko kubwa la mahitaji ya huduma zinazotolewa na Wizara linalokwenda sanjari na mahitaji zaidi ya Watumishi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kukidhi mahitaji ya watumishi kila yanapojitokeza ambapo katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilipewa kibali cha kuajiri watumishi wapya 460.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali katika mwaka wa fedha 2014/2015 ni shilingi 8,571,209,121/=. Katika kipindi hicho Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 8,581,417,819/= ikiwa ni asilimia 0.12 juu ya makadirio ya awali. Ongezeko hilo linatokana na kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji ada za huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ni nyenzo muhimu ya kupata watumishi wenye sifa na kudhibiti ubora wa huduma zinazotolewa. Wizara ilichukua hatua mbalimbali kuiwezesha Taasisi hii kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwa mwaka. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza bajeti ya taasisi kwa asilimia 20 na kuajiri watumishi wapya.

Mheshimiwa Spika, sanjari na jitihada hizo, Wizara ilishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuanzisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuruhusu wanafunzi wa taasisi kupata mikopo inayotolewa na Bodi hiyo. Katika kipindi hicho Taasisi ilidahili wanafunzi wapya 1,049 na wanafunzi 446 walihitimu masomo yao na kuwa na sifa za kusajiliwa kuwa Mawakili.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Chuo cha Uongozi wa Mahakama ikiwemo Kampasi ya Mwanza kilidahili jumla ya wanafunzi 834. Kati yao, wanafunzi 354 walikuwa katika ngazi ya Cheti cha Sheria na 480 wa Stashahada ya Sheria. Pia wanafunzi 649 walihitimu masomo yao wakiwemo wanafunzi 386 wa Stashahada na 263 wa Cheti cha Sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio tuliyoyaeleza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2014/2015, changamoto zilizojitokeza ni upungufu wa watumishi, ufinyu wa Bajeti ya Serikali, uhaba wa majengo na vitendea kazi. Licha ya changamoto hizi, Wizara imefanya jitihada za kuongeza watumishi na kuchagua maeneo machache ya kipaumbele ili kuhakikisha tija zaidi kwa fedha kidogo zinazopatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itaimarisha huduma zake ili kwenda sambamba na Dhima ya Wizara ya kukuza utawala wa sheria, haki na usawa kwa kutoa huduma bora na kwa wakati. Ili kufikia azma hiyo, Wizara itaelekeza rasilimali zake katika maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni mabadiliko ya Katiba; mfumo wa sheria na utoaji haki; hifadhi ya haki za binadamu na utawala bora; usajili wa matukio muhimu ya binadamu; ushauri wa kisheria na kuiwakilisha Serikali katika masuala ya kisheria; na kuimarisha mfumo wa kitaasisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itasimamia mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Hali kadhalika, Wizara itaratibu hatua za kuundwa kwa Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Masharti yatokanayo na Masharti ya Mpito.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaimarisha mfumo wa Sheria na utoaji haki kwa kukamilisha utungwaji wa Sera ya Sekta ya Sheria; Sheria ya Mawakili na Sheria ya Ufilisi. Aidha, Wizara itafanya mapitio na utafiti wa sheria zinazoratibu utoaji wa huduma kwa wazee; sheria zinazolinda haki za watumiaji wa bidhaa na huduma; na sheria zinazosimamia mfumo wa haki jinai. Pia Wizara itasimamia uandishi na urekebu wa sheria mbalimbali, kutayarisha Miswada ya Sheria kwa Kiingereza na Kiswahili, kupitia sheria mbalimbali ili kuziwianisha na misingi iliyoainishwa na Katiba na kuridhia Maazimio na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa. Vilevile Wizara itasimamia uendeshaji wa mashauri ya jinai katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kuhifadhiwa, Wizara itakuza uwezo wa kushughulikia malalamiko yanayotokana na uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora; na pia itatoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha shughuli za usajili wa matukio muhimu ya binadamu, Wizara itasimamia utekelezaji wa mpango wa usajili wa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa; kuhuisha viwango vya ada za usajili, ufilisi na udhamini; na kuanzisha mfumo wa malipo ya huduma hizo kwa njia ya kielektroniki.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itashiriki kikamilifu katika masuala ya kuleta utangamano wa kikanda; kufanya majadiliano yanayohusu mikataba ya kibiashara; na mikataba ya uhusiano wa Kimataifa na kushiriki katika Mikutano ya Kamati za Uanachama wa Mamlaka mbalimbali. Aidha, Wizara itawasilisha Bungeni Miswada ya Sheria tunayoitaja katika aya ya 57 ya hotuba yangu. Vilevile, Wizara itaimarisha mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za malalamiko.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaziimarisha taasisi za mafunzo zilizo chini yake ili ziweze kutoa huduma bora zaidi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara itakamilisha miradi ya ujenzi wa majengo ya Mahakama, Ofisi na nyumba za watumishi; kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma na kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itaratibu kazi za Kamati ya Kitaifa ya kuzuia mauaji ya Kimbari; itawajengea uwezo waendesha mashtaka, Mahakimu na Maafisa Ustawi wa Jamii ili kusimamia vema mfumo wa utoaji haki kwa watoto. Pamoja na hatua nyingine zinazolenga kuweka mazingira mazuri ya utumishi, Wizara itaandaa mpango mahsusi wa kuwahudumia Watumishi wanaoishi na Virusi vya Ukimwi na UKIMWI na wale wenye magonjwa sugu yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuwashukuru wale wote waliochangia mafanikio ya utekelezaji wa majukumu yetu. Natoa shukrani za dhati kwa viongozi na watendaji wote wa Wizara kwa ushauri wao wa mara kwa mara toka nilipokabidhiwa dhamana ya kuiongoza Wizara hii na kwa usimamizi makini wa majukumu ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu - Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Mohamed Chande Othman - Jaji Mkuu wa Tanzania; Mheshimiwa George Masaju - Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Shaaban Lila - Jaji Kiongozi; Bibi Maimuna Tarishi - Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria; Bwana Hussein Kattanga - Mtendaji Mkuu wa Mahakama; Mheshimiwa Ignus Kitusi - Msajili Mkuu wa Mahakama; Bibi Sarah Mwaipopo - Kaimu Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Jaji Aloysius Mujulizi, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Bwana Bahame Tom Nyanduga - Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru wakuu wote wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu kama tunavyowataja katika aya ya 62 ya hotuba yangu. Vilevile napenda kuwashukuru wafanyakazi wote na wa ngazi zote kwa ushirikiano na kwa kujituma katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nitoe shukurani nyingi kwa Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, kwa miongozo na ushauri mbalimbali waliutoa kwetu wakati wote wa maandalizi ya makadirio ya bajeti ambayo leo hii naona fahari kuyawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wadau wa maendeleo ambao wameendelea kufanya kazi bega kwa bega na Serikali yetu katika kuimarisha Sekta ya Sheria kama tunavyowataja katika aya ya 64 ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2015/2016, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni mia mbili ishirini na tatu mia nane sitini na tisa milioni tisini na tisa elfu (Sh. 223,869,099,000/=) kwa ajili ya Wizara na Taasisi zake.

Kati ya hizo shilingi bilioni mia moja tisini na saba mia nane na sita milioni mia saba sabini na tatu elfu (Sh. 197,806,773,000/=) ni kwa matumizi ya kawaida zikiwemo shilingi bilioni sitini na nane mia nane kumi na tisa milioni mia moja ishirini na sita elfu (Sh. 68,819,126,000) kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni mia moja ishirini na nane mia tisa themanini na saba milioni mia sita arobaini na saba elfu (Sh. 128,987,647,000) kwa matumizi mengineyo.

Fedha za Maendeleo ni shilingi bilioni ishirini na sita milioni sitini na mbili mia tatu ishirini na sita elfu (Sh. 26,062,326,000/=) kati ya hizo Shilingi bilioni ishirini na nne (Sh. 24,000,000,000/=) ni fedha za ndani na shilingi bilioni mbili sitini na mbili milioni mia tatu ishirini na sita elfu (Sh. 2,062,326,000) ni fedha za nje. Makadirio ya matumizi hayo kwa mafungu saba ya Wizara ni huu ifuatavyo:-

Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama, shilingi bilioni nne milioni tatu mia nne hamsini na sita elfu (Sh.4,003,456,000).

Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, shilingi bilioni kumi na tatu arobaini milioni mia nane themanini na tatu elfu (Sh. 13,040,883,000/=).

Fungu 35 - Divisheni ya Mashtaka, shilingi bilioni ishirini na moja mia tano arobaini na tano milioni mia tano na tano elfu (Sh. 21,545,505,000/=).

Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama, shilingi bilioni mia moja hamsini na nane mia nne themanini na saba milioni mia tano kumi na tatu elfu (Sh. 158,487,513,000/=).

Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria, shilingi bilioni kumi na sita mia moja arobaini na moja milioni mia nane ishirini na tano elfu (Sh.16,141,825,000).

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, shilingi bilioni sita mia tano kumi na saba milioni mia sita hamsini na sita elfu (Sh. 6,517,656,000/=).

Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, shilingi bilioni nne mia moja thelathini na mbili milioni mia mbili sitini na moja elfu (Sh. 4,132,261,000/=). Jumla shilingi bilioni mia mbili ishirini na tatu mia nane sitini na tisa milioni tisini na tisa elfu (Sh. 223,869,099,000/=).

Mheshimiwa Spika, muhtasari wa matumizi; sasa naomba nitoe mchanganyo wa makadirio haya kwa kila mafungu kama ifuatavyo:-

Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama, Matumizi ya mishahara ni shilingi 668,916,000/=; Matumizi mengineyo shilingi 3,334,540,00/=, matumizi ya maendeleo fedha za ndani ni sifuri (0) , matumizi ya maendeleo fedha za nje ni sifuri (0). Jumla ni Sh. 4,003,456,00/=.

Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali matumizi ya mishahara Sh. 3,832,615,000/=; matumizi mengineyo ni Sh. 7,908,268,000/=, matumizi ya maendeleo fedha za ndani ni Sh. 1,000,000,000/=, matumizi ya maendeleo fedha za nje ni Sh. 300,000,000/= . Jumla ni shilingi 13,040,883,000/=.

Fungu 35 - Divisheni ya Mahakama, matumizi ya mishahara ni Sh. 9,365,978,000/=; matumizi mengineyo ni Sh. 11,836,643,000/=, matumizi ya maendeleo fedha za ndani ni sifuri (0), matumizi ya maendeleo fedha za nje ni Sh. 342,884,000/= . Jumla ni shilingi 21,545, 505,000/=.

Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama, matumizi ya mishahara ni Sh. 48,998,032,000/=; matumizi mengineyo Sh. 89,087,667,000/=, matumizi ya maendeleo fedha za ndani ni Sh. 20,000,000,000/=, matumizi ya maendeleo fedha nje ni Sh. 401,814,000/= . Jumla ni Sh. 158,487,513,000/=.

Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria, matumizi ya mishahara Sh. 1,944,187,000/=; matumizi mengineyo Sh. 10,237,919,000/=; matumizi ya maendeleo fedha za ndani ni Sh.3,000,000,000/=; matumizi ya maendeleo fedha za nje Sh. 959,719,000/= . Jumla ni shilingi 16,141,825,000/=.

Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora matumizi ya mishahara ni Sh. 2,779,581,000/=; matumizi mengineyo ni Sh. 3,680,166,000/=; Matumizi ya maendeleo fedha za ndani ni sifuri (0); matumizi ya maendeleo fedha za nje Sh. 57,909,000. Jumla Sh. 6, 517,656,000/=.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria, Matumizi ya mishahara ni Sh. 1,229,817,000/=; matumizi mengineyo ni Sh. 2,902,444,000/=; matumizi ya maendeleo fedha za ndani sifuri (0), matumizi ya maendeleo fedha za nje sifuri (0). Jumla ni Sh. 4,132,261,000/=.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli ya Serikali; katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha sh. 17,023,993,750 ikiwa ni maduhuli ya Serikali kama inavyoonekana kwenye jedwali.

- Fungu 12	-	Sh.	0
- Fungu 16	-	Sh.	1,002,000
- Fungu 35	-	Sh.	13,002,000
- Fungu 40	-	Sh.	5,203,298,750
- Fungu 41	-	Sh.	11,801,400,000
- Fungu 55	-	Sh.	5,131,000
- Fungu 59	-	Sh.	100,000

JUMLA Sh. 17,023,993,750

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante. Hoja hiyo imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA MHESHIMIWA
DKT. ASHA-ROSE MIGIRO, (MB), KUHUSU MPANGO NA MAKADIRIO YA BAJETI
KWA MWAKA WA FEDHA
2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Kwa namna ya pekee napenda kutoa asante

nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniadini na kunipa fursa ya kuendelea kulitumikia taifa letu katika ngazi hii ya uongozi.

3. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kutoa salamu za pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi kwa kuondokewa na Mbunge wao Kapteni John Damiano Komba, aliyefariki tarehe 28.02.2015. Hakika mchango wake utakuwa na nafasi ya pekee katika historia ya jimbo lake. Hali kadhalika Watanzania wengi tutaendelea kumkumbuka kama askari shupavu wa mstari wa mbele na mhamasishaji wa aina yake katika kukuza umoja na utangamano wa taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Kapteni John Damiano Komba mahali pema peponi, amina.

4. Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu nikupongeze wewe, Mheshimiwa, kwa kuliongoza Bunge letu kwa umahiri, ushupavu na weledi mkubwa. Uongozi wako umeliweka Bunge letu katika ramani ya dunia na kufanya wewe, Mheshimiwa, ukabidhiwe nafasi mbali mbali za uongozi ndani na nje ya bara letu, na hivi karibuni kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC). Vile vile nimpongeze Naibu Spika, Mhe. Job Ndugai, mbunge wa Kongwa na wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wao mahiri kila wanapokalia kiti cha Spika.

5. Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati nimpongeze Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki, na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa dira na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

6. Mheshimiwa Spika, napenda hali kadhalika, kumpongeza Mheshimiwa Jason Samson Rweikiza, mbunge wa Bukoba Vijijini, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Wizara yetu inayo imani kubwa kwake binafsi na kwa Kamati anayoiongoza. Katika muktadha huo, Wizara yetu inatoa shukrani nyingi kwa Kamati yake, kwa ushauri mzuri na mapendekezo ambayo yamesaidia sana kuboresha Mpango na Makadirio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Ninaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana na Kamati hii ili kutuwezesha kufikia dira ya Wizara ya *Haki Sawa kwa Wote na kwa Wakati*, pamoja na Dira ya Taifa kuelekea mwaka 2025.

7. Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kuwapongeza Waheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja, na Innocent Rwabushaija Sebba, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, kuwa wabunge. Ninawatakiya kheri na mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

8. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inazo taasisi, ofisi na idara ambazo zinafanya kazi chini ya mwamvuli wake. Hizi ni Mahakama ya Tanzania; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Tume ya Kurekebisha Sheria; Tume ya Utumishi wa Mahakama; Wakala wa Usajili, Ufilisi, na Udhamini; Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; na Chuo cha Uongozi wa Mahakama.

9. Mheshimiwa Spika, kwa kuongozwa na Dira ya Wizara ya Haki Sawa kwa Wote na kwa Wakati, Wizara imejipanga vema kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake makuu ambayo ni pamoja na masuala ya Katiba; kusimamia sheria na utoaji haki; kuandaa miswada ya Sheria; kuendesha mashtaka; kutoa ushauri wa kisheria na kuendesha mashauri ya madai; kukuza na kuhifadhi haki za binadamu; kushughulikia usajili, ufilisi na udhamini; kushirikiana kimataifa katika kubadilishana wahalifu; kutoa mafunzo ya uanasheria na kusimamia ustawi na maendeleo ya watumishi wake.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

10. Mheshimiwa Spika, naomba sasa nifanye mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Katika kipindi hiki, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 234,246,819,000. Kati ya hizo, shilingi 48,804,234,000 ni mishahara, shilingi 131,880,015,000 ni kwa matumizi mengineyo na shilingi 53,562,570,000 ni fedha za maendeleo. Kufikia Aprili, 2015 fedha zilizopokelewa ni jumla ya shilingi 108,903,009,746 ambapo kati ya hizo shilingi 42,898,115,751 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 64,852,164,777 ni matumizi mengineyo na shilingi 1,152,729,218 zikiwa ni fedha za maendeleo za nje. Fedha zote zilizopokelewa ni sawa na asilimia 46.5 ya bajeti iliyoidhinishwa.

11. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mpango kazi wa mwaka 2014/2015, Wizara ilitumia fedha zilizopokelewa kutekeleza vipaumbele vyake kama ifuatavyo: kusimamia mchakato wa mabadiliko ya Katiba; kuimarisha mfumo wa sheria na misingi ya utoaji haki; kusimamia na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora; kuimarisha usajili wa matukio muhimu ya binadamu; kutoa ushauri na huduma za kisheria; na kuimarisha uwezo wake wa kitaasisi. Vipaumbele vya Wizara vinatokana na dhima ya Wizara ya kukuza utawala wa sheria, haki na usawa kwa kutoa huduma bora za kisheria. Naomba kulieleza Bunge lako tukufu kwamba tumeweza kufanya yote haya tukiongozwa na kauli mbiu isemayo: *haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyopokonywa.*

MCHAKATO WA MABADILIKO YA KATIBA

12. Mheshimiwa Spika, Bunge Maalum la Katiba lilihitimisha jukumu lake tarehe 4 Oktoba, 2014 na kukabidhi Katiba Inayopendekezwa kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, tarehe 8 Oktoba, 2014 mjini Dodoma. Kufuatia tukio hilo la kihistoria, Wizara ilichapisha nakala 2,000,400 za Katiba Inayopendekezwa. Kati ya hizo, nakala 2,000,000 zilichapishwa katika mfumo wa maandishi ya kawaida, nakala 200 zilichapishwa katika maandishi ya nukta nundu kwa ajili ya watu wasioona, na nakala nyingine 200 zilichapishwa katika maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya watu wenye ualbino. Nakala 1,141,300 zilizo katika maandishi ya kawaida zilisambazwa kwa wananchi Tanzania Bara ambapo kila kata ilipata nakala 300; na nakala 200,000 zilipelekwa Zanzibar. Nakala 658,700 zilisambazwa kwa Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali, vyama vya siasa, jumuiya za kidini, taasisi za elimu ya juu na asasi za kiraia Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

13. Mheshimiwa Spika, kusambazwa kwa Katiba Inayopendekezwa kumesaidia sana kujenga uelewa wa maudhui ya Katiba Inayopendekezwa ili kuwawezesha wananchi kujiandaa kwa kura ya maoni wakati utakapofika. Napenda kutoa rai kwa viongozi wa Serikali, vyama vya siasa, jumuiya za kidini, asasi za kiraia na wanajamii kwa ujumla kuwahamasisha wananchi kuisoma Katiba Inayopendekezwa na kuelewa vizuri kwa manufaa ya taifa letu.

MFUMO WA SHERIA NA UTOAJI HAKI

Uendeshaji wa Mashauri na Utoaji Haki

14. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliimarisha usikilizaji wa mashauri yaliyosajiliwa mahakamani na kupunguza idadi ya mashauri ya muda mrefu katika ngazi zote za mahakama. Katika kipindi hicho kulikuwa na jumla ya mashauri 247,267 ambapo mashauri 70,484 ni ya kutoka mwaka 2013/2014; na mashauri 176,783 ni yaliyosajiliwa mwaka 2014/2015. Kati ya yote hayo, jumla ya mashauri 179,469 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi.

15. Mheshimiwa Spika, Kamati za Kusukuma Uendeshaji Mashauri (*case-flow management committees*) ambazo zipo katika ngazi za wilaya, mkoa, kanda na taifa, zimekuwa nyenzo muhimu katika kupunguza idadi ya mashauri ya muda mrefu na msongamano na mahabusu. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliratibu vikao vya Kamati hizi katika ngazi mbalimbali pamoja na kuyatembelea maeneo wanamoshikiliwa watuhumiwa wa uhalifu ili kusikiliza kero zao. Wizara itaendelea kuziimarisha Kamati hizi ili ziweze kutekeleza

majukumu yake kwa ufanisi zaidi kwa kuzingatia ratiba za vikao, kanuni na taratibu nyingine zilizowekwa.

16. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka unaokwisha wa fedha, Wizara ilisimamia utekelezaji wa Mpango wa Kutenganisha Mashtaka na Upelelezi (**civilianization of prosecutions**). Madhumuni ya mpango huu ni kudhibiti, kusimamia uendeshaji wa mashtaka na kuratibu shughuli za upelelezi kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa kuzingatia misingi ya sheria. Kupitia mpango huu mashauri ya jinai katika mahakama za wilaya na mahakama za hakimu mkazi yanaendeshwa na mawakili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mpango huu umekuwa ni kiungo muhimu kati ya Wizara na vyombo vya upelelezi wa makosa ya jinai katika kuharakisha upatikanaji haki na kuongeza ufanisi.

17. Mheshimiwa Spika, madhumuni mengine ya kuanzishwa kwa mpango wa kutenganisha mashtaka na upelelelezi ni kuhakikisha huduma za uendeshaji mashtaka zinapatikana karibu na jamii. Hivyo, Wizara imefanikiwa kufungua ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mikoa yote ya Tanzania Bara na inakusudia kufikisha huduma hizo kwenye ngazi ya wilaya nchini kote kwa kuanzia na wilaya za Monduli na Temeke.

18. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha, 2014/2015 Wizara ilisimamia uendeshaji wa mashauri ya jinai 8,025 katika ngazi za mahakama ya rufani, mahakama kuu: mahakama za hakimu mkazi; na mahakama za wilaya. Kati ya hayo, mashauri 5,772 yalhitimishwa, na mengine 2,253 yanaendelea kusikilizwa.. Aidha, Wizara iliratibu uendeshaji wa Jukwaa la Taifa la Haki Jinai na kushirikiana na vyombo mbali mbali vinavyohusika na masuala ya sheria ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika sekta hii ya haki jinai. Jukwaa hili liliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka, na. 27 ya mwaka 2008, na linashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wakuu wa taasisi zinazohusika na uchunguzi wa makosa, uendeshaji na usimamizi wa makosa ya jinai.

19. Mheshimiwa Spika, vitendo vya rushwa na udanganyifu, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya vimekuwa fishio katika jamii. Kadhalika, vitendo vya mauaji na ukatili kwa watu wenye ualbino vimelifedhehesha sana taifa na kuchafua taswira ya nchi yetu. Wakati Bunge lako tukufu likiendelea, tarehe 13 Mei, 2015 mwanamke mmoja katika wilaya ya Mlele, mkoa wa Katavi, alikatwa kiganja cha mkono kwa imani za kishirikina. Wizara yetu imejizatiti kukabiliana na matukio haya kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa sekta ya sheria na waliomo ndani ya jamii.

20. Mheshimiwa Spika, kwa mnasaba huo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilisimamia uendeshaji wa mashauri 14 ya mauaji na ukatili kwa

watu wenye ualbino. Kati ya hayo, shauri moja lilihitimishwa ambapo watuhumiwa wanne walipatikana na hatia ya mauaji na kupewa adhabu ya kifo; mashauri sita yako katika hatua mbalimbali za usikilizaji mahakamani, na mashauri saba yako katika hatua ya upelelezi.

21. Mheshimiwa Spika, 'niruhusu nitumie fursa hii kutoa mwito maalum kwa Watanzania wote kuchukua hatua za dhati kukomesha vitendo hivi vya kikatili, vya kijinai, vinavyokiuka haki za binadamu na vinavyochafua jina zuri la nchi yetu. Ni sharti tutambue kwamba **maisha ya watu wenye ualbino ni maisha yetu – tuyalinde!**

22. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa dawa za kulevya, katika mwaka wa fedha 2014/2015 kulikuwa na jumla ya mashauri 79 yaliyohusu dawa za kulevya aina ya *heroine, cocaine na cannabis*. Kati ya hayo, mashauri 58 ni ya zamani na 21 ni mapya. Mashauri yote haya yapo katika hatua mbalimbali ya kusikilizwa. **(Kiambatisho A)**

23. Mheshimiwa Spika, Wizara, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kufuatilia na kuchukua hatua za kisheria kwa watu watakaobainika kujihusisha na dawa za kulevya. Katika kukabiliana na tatizo hili Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali katika vita hivi wakiwemo wananchi wenyewe, viongozi wa kisiasa, wa kidini na wa kijamii.

24. Mheshimiwa Spika, kwa mashauri yanayohusu rushwa na udanganyifu, kulikuwa na majalada 250 yaliyopokelewa na Mkurugenzi wa Mashtaka kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Baada ya kufanyiwa uchambuzi, majalada 131 yaliandaliwa hati za mashtaka na 72 yalirejeshwa TAKUKURU kwa uchunguzi zaidi. Majalada 47 yaliyobaki yanaendelea kufanyiwa uchambuzi.

25. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliiwakilisha Serikali mahakamani katika mashauri 839 yanayoihusu, ndani na nje ya nchi. Mashauri hayo ni ya kikatiba, madai, na yale yanayohusu ukiukwaji wa haki za binadamu. Kati ya hayo, mashauri 37 yalihitimishwa na 802 yako katika hatua mbalimbali za kusikilizwa.

26. Mheshimiwa Spika, kuhusu mashauri ya kikatiba, Wizara iliiwakilisha Serikali katika mashauri 93 ambapo mashauri matano yalihitimishwa na mengine 88 yanaendelea kusikilizwa. Mashauri ya madai yalikuwa 51 na yote yanaendelea kusikilizwa. Vilevile, Wizara iliiwakilisha Serikali katika mashauri sita ya ukiukwaji wa haki za binadamu yanayoendelea kusikilizwa katika Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliyoko Banjul, Gambia.

Utafiti, Urekebu na Uandishi wa Sheria

27. Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua za mara kwa mara kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mfumo imara wa sheria unaokidhi mahitaji ya jamii kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ili kufanikisha hilo, Wizara iliendesha tafiti mbalimbali ambazo zimekuwa msingi wa marekebisho ya baadhi ya sheria na kutungwa kwa sheria mpya. Tafiti hizo zinahusu sheria za huduma za kijamii kwa wazee; sheria zinazolinda haki za watumiaji wa bidhaa na huduma; na sheria zinazosimamia haki jinai. Vile vile, Wizara ilichambua hukumu 70 za Mahakama ya Rufani kwa lengo la kupata misingi ya kisheria iliyotumika katika hukumu hizo ili kusaidia marekebisho ya sheria mbalimbali. Wizara pia ilishirikiana na wadau wengine katika kuwianisha sheria za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo.

28. Mheshimiwa Spika, matokeo ya tafiti zilizofanyika ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa wa mwaka 2015 ambao umesomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika mkutano wa 19 wa Bunge, mapendekezo ya kutunga Sheria ya Msaada wa Kisheria na mapendekezo ya kutunga Sheria ya Kulinda Watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi. Hivi sasa mapendekezo hayo yapo katika mchakato wa kiserikali wa kuyafanyia uamuzi.

29. Mheshimiwa Spika, uandishi na uwasilishaji wa miswada ya sheria Bungeni ni moja ya hatua muhimu katika kuimarisha utawala wa sheria nchini. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliandaa jumla ya miswada 21 iliyosomwa mbele ya Bunge lako ambapo miswada 14 kati ya hiyo ilijadiliwa na kupitishwa na Bunge. Miswada yote iliwasilishwa Bungeni kwa Kiingereza na Kiswahili ili kuzifanya sheria hizi zieleweke kwa urahisi na wananchi. Vile vile, Wizara ilihakiki sheria ndogo 286 na kuzitangaza katika Gazeti la Serikali. Sheria 128 zilifanyiwa urekebu katika kipindi hichi.

30. Mheshimiwa Spika, sambamba na kuhakikisha kuwa miswada yote ya sheria inaandikwa kwa Kiingereza na Kiswahili, Wizara ilitafsiri sheria nyingine za nchi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Sheria zilizotafsiriwa ni Sheria ya Ushirikiano wa Pamoja wa Kimataifa Katika Masuala ya Jinai, Sura ya 254; Sheria ya Silaha na Risasi, Sura ya 223; Sheria ya Kuhamisha Wafungwa ya mwaka 2004; Sheria ya Uangalizi wa Wahalifu, Sura ya 247; na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Serikali, Sura ya 5.

MIFUMO YA UTOAJI HUDUMA

31. Mheshimiwa Spika, uhakika na ubora wa huduma za kisheria zinazotolewa na Wizara unategemea sana kuwepo kwa miundombinu imara kama vile majengo, vitendea kazi vya kisasa na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Hivyo, katika mwaka wa fedha 2014/2015

Wizara ilitekeleza miradi mbalimbali ili kuimarisha upatikanaji wa majengo ya ofisi, nyumba za watumishi na matumizi ya TEHAMA.

32. Mheshimiwa Spika, Wizara ilitumia TEHAMA katika usikilizaji wa mashauri, upokeaji na uchambuzi wa malalamiko yaliyohusu kuvunjwa kwa haki za binadamu na kukiukwa kwa misingi ya utawala bora; na ufuatiliaji wa majalada ya mashauri ya jinai. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara inaendelea kukamilisha maandalizi ya kuanzisha mfumo wa malipo ya ada za usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini kwa njia ya kielektroniki. Mifumo hii itasaidia kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

33. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilikuwa na miradi ya ujenzi wa jengo la Mahakama ya Tanzania, Dar es Salaam; ujenzi wa nyumba 12 za majaji katika mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Dodoma, Iringa, Tanga, Arusha, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mtwara na Kilimanjaro; ujenzi wa Mahakama Kuu katika mikoa ya Shinyanga Kigoma, Lindi, Manyara, Mara, Morogoro, na Singida; ujenzi wa Mahakama 9 za wilaya za Bagamoyo, Baridadi, Bunda, Bukombe, Hanang, Kasulu, Kilindi, Nkasi, Makete; na ujenzi wa Mahakama 26 za Mwanzo nchini.

34. Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara ilikuwa na miradi ya ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Tabora, Mwanza, Ruvuma na Mbeya; Mahakama 8 za Hakimu Mkazi katika Mikoa ya Singida, Mara, Ruvuma, Tabora, Kigoma, Rukwa, Kagera na Morogoro. Vile vile ilikuwa na miradi ya ukarabati wa majengo ya Mahakama 4 za wilaya za Monduli, Kiteto, Newala na Muleba; na mahakama tisa za mwanzo za Magugu (Babati), Vwawa (Mbozi), Lindi Mjini, Kiteto, Bereko (Kondoa), Robanda (Serengeti), Gairo, Rusumo (Ngara), na Makambako. Miradi yote ya ujenzi na ukarabati iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji, **(Kiambatisho B)**.

35. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji kazi wa Mahakama ya Tanzania, Rais alifanya uteuzi wa majaji wawili wa Mahakama ya Rufani, Jaji Kiongozi na majaji 20 wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Kati ya majaji walioteuliwa tisa ni wanawake na 13 ni wanaume. Pia, Rais alifanya uteuzi wa Msajili wa Mahakama ya Rufani na Msajili wa Mahakama Kuu. Katika kipindi hicho walijiririwa mahakimu wakaazi 57 na wasimamizi wa mahakama (court administrators) 24. Pia, Wizara iliendesha programu za mafunzo kwa Kamati za Maadili za mikoa na wilaya ili kuimarisha nidhamu kwa watumishi wa mahakama.

36. Mheshimiwa Spika, Kamati hizi za mikoa na wilaya zimekuwa vyombo muhimu vya kusimamia maadili na nidhamu za watumishi wa mahakama. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilizivezesha Kamati saba za

mikoa na 36 za wilaya kuendesha vikao vya kuchunguza na kujadili malalamiko ya ukiukwaji wa maadili ya mahakimu. Pia, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilishughulikia mashauri 27 ya nidhamu na kuyatolea uamuzi. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa Kamati za Maadili za mikoa ya Dodoma, Katavi, Rukwa na Singida ili ziweze kutekeleza majukumu yake vizuri.

HAKI ZA BINADAMU NA ELIMU KWA UMMA

37. Mheshimiwa Spika, mpango wa elimu kwa umma ni mkakati muhimu wa Wizara wa kuhakikisha watu wanafahamu na kudai haki zao; na wanajua wajibu wao kwa mamlaka za nchi. Katika kutekeleza mpango huo, Wizara ilirusha hewani vipindi 25 vya redio na televisheni na kusambaza machapisho 15, 500 ya aina mbalimbali kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara, maonesho ya kitaifa, idara na taasisi za serikali. Vile vile, Wizara ilifanya mikutano na viongozi wa kijamii na watendaji wa Serikali katika wilaya za Chato na Tabora ili kuongeza uelewa wa wajibu wao wa kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu.

38. Mheshimiwa Spika, katika kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu, Wizara ilitoa elimu kwa wafanyakazi wa viwanda vilivyo chini ya mradi wa Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuuza Nje (EPZA) katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga. Jumla ya wafanyakazi 884 kutoka viwanda 14 walishiriki mafunzo hayo, kati yao wanawake walikuwa 389 na wanaume 495. Vile vile, Wizara iliratibu na kusimamia maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Ulimwenguni yaliyofanyika tarehe 10 Desemba, 2014 na ilitumia fursa hiyo kueleza juhudi zinazofanywa na Serikali katika kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu chini ya mfumo wa Umoja wa Mataifa wa mapitio kwa kipindi maalum (*universal periodic review mechanism*).

39. Mheshimiwa Spika, Wizara iliiwakilisha Serikali kwenye mikutano mbali mbali nje ya nchi ambayo ilisaidia kubadilishana uzoefu na mataifa mengine, kuimarisha utendaji na kuongeza ufanisi kazini. Mikutano hiyo ni pamoja na mkutano wa Umoja wa Afrika kuhusu haki za kijamii na kiuchumi uliofanyika Ghana; na mkutano uliojadili Demokrasia, Utawala Bora na Uchaguzi uliofanyika nchini Ethiopia.

USAJILI, UFILISI NA UDHAMINI

40. Mheshimiwa Spika, usajili wa matukio muhimu ya binadamu una manufaa kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa takwimu zinahotijika katika mipango ya maendeleo; na kuweka mazingira mazuri ya kuimarisha haki mbalimbali za raia. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilitekeleza mikakati ya jumla na mahsus ya kuimarisha usajili wa matukio yanayomhusu binadamu kama vile hali ya ndoa, talaka, vizazi na vifo. Kupitia

mikakati ya jumla Wizara ilisajili vizazi 349,440; vifo 49,168; ndoa 11,351 talaka 118 na watoto 34 walioasiliwa.

41. Mheshimiwa Spika, Wizara iliandaa programu mahsusi ya usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano iliyotekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Chini ya programu hii, Wizara ilisajili jumla ya watoto 59,463 na kutoa vyeti vya kuzaliwa bila malipo. Mkakati mwingine mahsusi ulikuwa ni usajili wa watoto waliopo mashuleni waliokuwa na umri wa kati ya miaka 6 na 18 ambapo Wizara ilisajili jumla ya watoto 18,800.

42. Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada zinazochukuliwa, Wizara imeweza kuongeza kiwango cha usajili kutoka wastani wa chini ya asilimia 10 mwaka 2012 hadi asilimia 16 ilipofika Aprili 2015. Hata hivyo, kiwango hiki bado ni cha chini ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2020. Hivyo, Wizara ilifanya tathmini ya mfumo uliopo wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu na kuandaa Mkakati wa Taifa ili kuimarisha shughuli za usajili.

43. Mheshimiwa Spika, sanjari na shughuli za usajili Wizara ilitoa hati 203 kwa wadhamini wa taasisi na asasi za kijamii na kuwapa elimu juu ya haki na wajibu wao wa kisheria kulingana na Katiba za asasi wanazosisimamia. Aidha, Wizara ilitoa elimu kwa umma kuhusu mirathi, namna ya kuandika na kuhifadhi wosia kupitia redio, televisheni na mabaraza ya wafanyakazi.

USHAURI NA HUDUMA ZA KISHERIA

Ushauri na Majadiliano ya Mikataba

44. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ilitoa ushauri wa kisheria katika maeneo mbalimbali. Wizara ilihakiki na kuchambua mikataba 2,993 ya kibiashara, ununuzi wa umma na uwekezaji. Pia, Wizara ilitoa ushauri wa kisheria kwa masuala anuwai yaliyowasilishwa kwake na wizara, idara, wakala na taasisi nyingine za umma.

Huduma ya Msaada wa Kisheria

45. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuiwakilisha Serikali katika masuala ya kisheria, Wizara ilitoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi wasio na uwezo wa kupata huduma za uwakili kupitia mfumo wa kawaida uliopo. Huduma zilizotolewa zilihusu elimu na ushauri wa kisheria; na kuandaa nyaraka za kupeleka mashauri mahakamani. Aidha, Wizara ilikamilisha maandalizi ya mapendekezo ya kutunga Sheria ya Msaada wa Kisheria ili kuiwezesha Serikali kusimamia ubora na upatikanaji wa huduma za kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za uwakili nchini.

UWEZO WA KITAASISI

Hali ya Watumishi

46. Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la mahitaji ya huduma zinazotolewa na Wizara linaloenda sanjari na mahitaji zaidi ya watumishi. Hivyo, Wizara imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kukidhi mahitaji ya watumishi kila yanapojitokeza ambapo katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilipewa kibali cha kuajiri watumishi wapya 460. Pia, katika kipindi hicho watumishi 1,048 walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji wakiwemo 442 wa mafunzo ya muda mfupi, na 606 wa mafunzo ya muda mrefu.

Maduhuli ya Serikali

47. Mheshimiwa Spika, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali katika mwaka wa fedha 2014/2015 ni Shilingi 8,571,209,121. Katika kipindi hicho Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi 8,581,417,819 ikiwa ni asilimia 0.12 juu ya makadirio ya awali. Ongezeko hilo linatokana na kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji ada za huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi za Wizara. Kuimarika kwa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali ni chachu kwa Wizara na taasisi zake katika kuboresha huduma zinazotolewa, **(Kiambatisho C)**.

URATIBU WA TAASISI ZA MAFUNZO

48. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ni nyenzo muhimu ya kupata watumishi wenye sifa na kudhibiti ubora wa huduma zinazotolewa. Kwa hiyo Wizara ilichukua hatua mbalimbali kuiwezesha Taasisi hii kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwa mwaka. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza bajeti ya taasisi kwa asilimia 20 na kuajiri watumishi wapya. Sanjari na jitihada hizo Wizara ilishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuanzisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuruhusu wanafunzi wa Taasisi kupata mikopo inayotolewa na Bodi hiyo. Katika kipindi hicho Taasisi ilidahili wanafunzi wapya 1,049; na wanafunzi 446 walihitimu masomo yao na kuwa na sifa za kusajiliwa kuwa mawakili, **(Kiambatisho D)**.

49. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Chuo cha Uongozi wa Mahakama (ikiwemo Kampasi ya Mwanza), kilidahili jumla ya wanafunzi 834 kati yao wanafunzi 354 walikuwa katika ngazi ya Cheti cha Sheria na 480 wa Stashahada ya Sheria. Pia, wanafunzi 649 walihitimu masomo yao wakiwemo wanafunzi 386 wa Stashahada na 263 wa Cheti cha Sheria. Udahili na kuhitimu kwa wanafuzi katika Chuo hiki ni hatua muhimu za kukidhi mahitaji ya wataalam wa sheria katika taifa letu, hatua ambazo zitaimarishwa kwa mwaka 2015/16.

C. CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA

NAZO

50. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio tuliyoyaeleza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2014/15, changamoto zilizojitokeza ni upungufu wa watumishi, ufinyu wa bajeti ya Serikali, uhaba wa majengo na vitendea kazi. Licha ya changamoto hizi Wizara imefanya jitihada za kuongeza watumishi kila fursa ya kufanya hivyo ilipojitokeza na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo. Aidha, Wizara imeanza kufanya mawasiliano na wawekezaji wa sekta binafsi ili waweze kushiriki katika miradi ya mbalimbali ya maendeleo.

51. Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine wa kukabiliana na changamoto za kibajeti ni Wizara kuchagua maeneo machache ya kipaumbele na kuhakikisha tija zaidi kwa fedha kidogo zinazopatikana.

D. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016

52. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itaimarisha huduma zake ili kwenda sambamba na Dhima ya Wizara ya kukuza utawala wa sheria, haki na usawa kwa kutoa huduma bora na kwa wakati. Ili kufikia azma hiyo Wizara itaelekeza rasilimali zake katika maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni mabadiliko ya Katiba; mfumo wa sheria na utoaji haki; hifadhi ya haki za binadamu na utawala bora; usajili wa matukio muhimu ya binadamu; ushauri wa kisheria na kuiwakilisha Serikali katika masuala ya kisheria; na kuimarisha mifumo ya kitaasisi.

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itasimamia mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Hali kadhalika Wizara itaratibu hatua za kuundwa kwa Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Masharti Yatokanayo na Masharti ya Mpito.

54. Mheshimiwa Spika, Wizara itachukua hatua madhubuti za kuimarisha mfumo wa Sheria na utoaji haki kwa kukamilisha utungwaji wa sera ya sekta ya sheria; Sheria ya Mawakili na Sheria ya Ufilisi. Aidha, Wizara itafanya mapitio na utafiti wa sheria zinazoratibu utoaji wa huduma kwa wazee; sheria zinazolinda haki za watumiaji wa bidhaa na huduma; na sheria zinazosimamia mfumo wa haki jina. Pia, Wizara itasimamia uandishi na urekebu wa sheria mbalimbali, kutayarisha miswada ya sheria kwa Kiingereza na Kiswahili, kupitia sheria mbalimbali ili kuziwianisha na misingi iliyoainishwa na Katiba, na kuridhia maazimio na mikataba mbalimbali ya kimataifa. Vile vile, Wizara itasimamia uendeshaji wa mashauri ya jina katika ngazi zote.

55. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kuhifadhiwa, Wizara itakuza uwezo wake wa kushughulikia malalamiko

yanayotokana na kukiukwa kwa haki za binadamu na misingi ya utawala bora; na pia itatoa elimu kwa wananchi. Hali kadhalika, Wizara itafanya utafiti utakaochangia kuimarishwa kwa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

56. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha shughuli za usajili wa matukio muhimu ya binadamu, Wizara itasimamia utekelezaji wa mpango wa usajili wa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano katika mikoa ya Kanda ya Ziwa; kuhuisha viwango vya ada za usajili, udhamini na ufilisi; na kuanzisha mfumo wa malipo ya huduma hizo kwa njia ya kielektroniki.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itashiriki kikamilifu katika masuala ya kuleta utangamano wa kikanda; kufanya majadiliano yanayohusu mikataba ya kibiashara; na mikataba ya uhusiano wa kimataifa na kushiriki katika mikutano ya Kamati za uanachama wa mamlaka mbalimbali. Aidha, Wizara itawasilisha Bungeni miswada ya Sheria ya Msaada wa Kisheria; Sheria ya Kulinda Watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi. Vile vile, Wizara itaimarisha mfumo wa kielektroniki wa kupokea, kuchambua na kuhifadhi kumbukumbu za malalamiko.

58. Mheshimiwa Spika, Wizara itaziimarisha taasisi za mafunzo zilizo chini yake, ambazo ni Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto ili ziweze kutoa huduma bora zaidi. Aidha katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara inakusudia kukamilisha miradi ya ujenzi wa majengo ya mahakama, ofisi na nyumba za watumishi; kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma na kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

59. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itasimamia na kuratibu kazi za Kamati ya Kitaifa ya kuzuia mauaji ya kimbari; itawajengea uwezo waendesha mashtaka, mahakimu na maafisa ustawi wa jamii ili kusimamia vema mfumo wa utoaji haki kwa watoto kwa kuzingatia Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

60. Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua nyingine zinazolenga kuweka mazingira mazuri ya utumishi, Wizara itaandaa mpango mahsus wa kuwahudumia watumishi wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI na wale wenye magonjwa sugu yasiyoambukiza. Mpango huu unakusudia kuhakikisha kwamba watumishi wana ufahamu kuhusu afya zao na jinsi ya kujilinda.

E. SHUKRANI

61. Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia jitihada na mafanikio ya utekelezaji wa majukumu yetu. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa viongozi na watendaji wote wa Wizara

kwa ushauri wao wa mara kwa mara toka nilipokabidhiwa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Katiba na Sheria; na kwa usimamizi makini wa majukumu ya Wizara yetu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, Jaji Mkuu wa Tanzania; Mheshimiwa George M. Masaju, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Shaaban A. Lila, Jaji Kiongozi; Bibi Maimuna K. Tarishi, Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria; Bwana Hussein A. Kattanga, Mtendaji Mkuu wa Mahakama; Mheshimiwa Ignus P. Kitusi, Msajili Mkuu wa Mahakama; Bibi Sarah D. Mwaipopo, Kaimu Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Jaji Aloysius K. Mujulizi, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; na Bwana Bahame Tom Nyanduga, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

62. Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru Bwana Biswalo E. K. Mganga, Mkurugenzi wa Mashtaka; Mheshimiwa Jaji Dkt. Gerald A. M. Ndika, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; Mheshimiwa Jaji Ferdinand L. K. Wambali, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto; Bibi Mary Massay, Katibu Mtendaji, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Bibi Agnes Mgeyekwa, Kaimu Katibu Mtendaji, Tume ya Kurekebisha Sheria; Bibi Emmy Hudson, Kaimu Mtendaji Mkuu, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhhamini na Bibi Enzel W. Mtei, Katibu Msaidizi, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Wakurugenzi, watendaji na watumishi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria.

63. Mheshimiwa Spika, nitoe shukurani nyingi kwa Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, kwa miongozo na ushauri mbalimbali walioutoa kwetu wakati wote wa maandalizi ya makadirio ya bajeti ambayo leo hii ninaona fahari kuyawasilisha mbele ya Bunge lako tukufu.

64. Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wadau wa maendeleo ambao wameendelea kufanya kazi bega kwa bega na Serikali yetu kwa kutupatia ushauri na rasilimali fedha katika kuimarisha Sekta ya Sheria. Kwa namna ya pekee niwashukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la UN-WOMEN, Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA) na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Uingereza, (DfID).

F. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

Muhtasari wa Maombi ya Fedha

65. Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi 223,869,099,000 kwa ajili ya wizara na taasisi zake. Kati ya hizo Shilingi 197,806,773,000 ni kwa matumizi ya kawaida zikiwemo Shilingi 68,819,126,000

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa ajili ya mishahara na Shilingi 128,987,647,000 kwa matumizi mengineyo. Fedha za Maendeleo ni Shilingi 26,062,326,000 kati ya hizo Shilingi 24,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 2,062,326,000 ni fedha za nje. Makadirio ya matumizi hayo kwa mafungu saba ya Wizara ni haya yafuatayo:-

Fungu 12	- Tume ya Utumishi wa Mahakama	4,003,456,000
Fungu 16	- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	13,040,883,000
Fungu 35	- Divisheni ya Mashtaka	21,545,505,000
Fungu 40	- Mfuko wa Mahakama	158,487,513,000
Fungu 41	- Wizara ya Katiba na Sheria	16,141,825,000
Fungu 55	- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	6,517,656,000
Fungu 59	- Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania	4,132,261,000
JUMLA		223,869,099,000

Muhtasari wa Matumizi

66. Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mchanganuo wa makadirio haya kwa kila fungu kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama

Matumizi ya Mishahara	Sh.	668,916,000
Matumizi Mengineyo	Sh.	
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	Sh.	0
Jumla	Sh.	4,003,456,000

(ii) Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Matumizi ya Mishahara	Sh.	3,832,615,000
Matumizi Mengineyo	Sh.	7,908,268,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	Sh.	1,000,000,000
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	Sh.	300,000,000
Jumla	Sh.	13,040,883,000

(iii) Fungu 35: Divisheni ya Mashtaka

Matumizi ya Mishahara	Sh.	9,365,978,000
Matumizi Mengineyo	Sh.	11,836,643,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	Sh.	342,884,000
Jumla	Sh.	21,545,505,000

(iv) Fungu 40: Mfuko wa Mahakama

Matumizi ya Mishahara	Sh.	
48,998,032,000		
Matumizi Mengineyo	Sh.	
89,087,667,000		
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	Sh.	
20,000,000,000		
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	Sh.	401,814,000
Jumla	Sh.	158,487,513,000

(v) Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria

Matumizi ya Mishahara	Sh.	1,944,187,000
Matumizi Mengineyo	Sh.	10,237,919,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	Sh.	3,000,000,000
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	Sh.	959,719,000
Jumla	Sh.	16,141,825,000

(vi) Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Matumizi ya Mishahara	Sh.	2,779,581,000
Matumizi Mengineyo	Sh.	3,680,166,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	Sh.	57,909,000
Jumla	Sh.	6,517,656,000

(vii) Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria

Matumizi ya Mishahara	Sh.	1,229,817,000
Matumizi Mengineyo	Sh.	2,902,444,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	Sh.	0
Jumla	Sh.	4,132,261,000

Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 17,023,933,750 ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

Fungu 12	-	Sh.	0
Fungu 16	-	Sh.	1,002,000
Fungu 35	-	Sh.	13,002,000
Fungu 40	-	Sh.	5,203,298,750
Fungu 41	-	Sh.	11,801,400,000
Fungu 55	-	Sh.	5,131,000
Fungu 59	-	Sh.	100,000

68. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Sasa nitamwita Mwenyekiti aliyeshughulikia hoja hiyo Mheshimiwa Rweikiza!

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA
KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA
MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO
KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA
ILIVYOSOMWA BUNGENI**

MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 99(5), (9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kusoma taarifa yote ya Kamati, hivyo basi, naomba taarifa yote iingizzwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inahusisha mafungu saba kama ifuatavyo:-

- (i) Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama;
- (ii) Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- (iii) Fungu 35 - Mkurugenzi wa Mashtaka;
- (iv) Fungu 40 - Mahakama;
- (v) Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria;
- (vi) Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na
- (vii) Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 4 Mei, 2015, Kamati yangu ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro, Waziri wa Katiba na Sheria akishirikiana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummu Mwalimu, pamoja na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

watendaji wa Wizara. Katika maelezo yake Waziri aliieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa kipindi cha mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015; taarifa ilionesha kuwa hadi kufikia 30 Machi, 2015, Wizara ilipokea jumla ya Sh. 118,411,286,386/= za bajeti, sawa na asilimia 52.5 zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi iliyokuwa na asilimia kidogo ya Bajeti iliyoidhinishwa ikilinganishwa na Taasisi zingine ni Fungu 41 Wizara ya Katiba na Sheria. Kiasi cha fedha zilizopatikana kwa Fungu hili ni asilimia 36.7, wakati taasisi nyingine zilipata zaidi ya asilimia hiyo ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni ya ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2014/2015, wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali. Kamati ilitaka kujiridhisha ni kwa kiasi gani maoni na ushauri wake ulizingatiwa na Serikali. Kamati ilibaini kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri wa Kamati ulizingatiwa. Hata hivyo, baadhi ya maoni na ushauri upo katika hatua za utekelezaji na mwingine haukuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati uliotekelezwa na Serikali:-

- (i) Ushauri kuhusu Tume ya Utumishi wa Mahakama kujengewa uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuthibiti kuongezeka kwa vitendo vya rushwa miongoni mwa watumishi wa mahakama.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu umetekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya ili kuziimarisha ambapo Mikoa nane pamoja na Wilaya zake ambayo ni Tabora, Shinyanga, Mbeya, Njombe, Iringa, Pwani, Morogoro na Dodoma tayari zimekwishapewa mafunzo hadi sasa. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016, jumla ya Sh. 184,220,000.00/= zimetengwa kwa ajili ya kuendelea kutoa mafunzo kwa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara.

- (ii) Kamati inashauri Wizara kufanya utaratibu wa kuhamishia kiasi cha Sh. 1,400,000,000/= kutoka Mfuko wa Mahakama mapema kwenda Tume ya Utumishi wa Mahakama ili kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Wizara imetekeleza agizo hili na kufuatiwa na uhamisho wa kiasi hicho cha fedha kutoka Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama kwenda Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama.
- (iii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ijengewe uwezo katika kitengo cha mikataba kwa kuwapatia mafunzo Mawakili wa Serikali katika

Nakala ya Mtandao (Online Document)

masuala ya mikataba ya mafuta na gesi ili kuhakikisha kuwa watendaji hao wanatumika ipasavyo kuishauri Serikali katika kuingia mikataba yenye tija kwa taifa kuhusu sekta hizo na nyingine.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa sasa eneo hili la mikataba limepewa hadhi ya kuwa Divisheni na siyo Kitengo. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Wizara ya Nishati na Madini iliandaa mafunzo ya kushughulikia Mikataba ya Gesi na Mafuta (LING) kwa ajili ya kujenga uwezo wa Mwakili wa Serikali kuchambua na kujadili mikataba ya rasilimali gesi ili kulinda maslahi ya nchi.

- (iv) Elimu kuhusu uwepo wa Tume pamoja na majukumu yake iendelee kutolewa hasa vijijini ili kuwawezesha wananchi kuitumia kwa kupeleka malalamiko wakiona kuna ukiukwaji wa maadili. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 jumla ya Sh. 110,000,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu kuwepo kwa Kamati za Maadili za Mahakimu za Mikoa na Wilaya.
- (v) Kamati ilishauri kwamba maboresho ya Mahakama yaende sambamba na maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza ushauri huu. Katika kutekeleza ushauri huu, Serikali kwa mwaka 2014/2015 ilitoa kibali cha ajira kwa watumishi 429 wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hadi machi, 2015 tayari watumishi 321 wamesharipoti ofisini. Pia ofisi kwa mwaka 2014/2015 ilitengewa Sh. 5,000,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali Makao Makuu na Mikoani.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati unaoendelea kutekelezwa:-

- (i) Mahakama ipewe kibali cha kuajiri watumishi wengine wakiwemo Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi sambamba na kuboresha maslahi ya Watumishi hao. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mahakama ya Tanzania imepata vibali vya ajira kwa watumishi 1,010 wakiwemo Mahakimu. Hadi sasa nafasi 750 wameajiriwa na mchakato unaendelea kuwapata watumishi hao.
- (ii) Kamati inashauri Serikali itenge fedha za ndani za kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili iweze kujenga ofisi na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Taasisi hii.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Divisheni ya Mashtaka ijengewe uwezo kwa kupewa kibali cha kuajiri watumishi 489 na kuwapatia mafunzo ili waweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyokusudiwa. Katika kujenga uwezo wa Divisheni ya Mashtaka, Serikali imetoa kibali cha kuajiri watumishi 429 katika bajeti ya mwaka 2014/2015. Hadi Machi, 2015 tayari watumishi 289 walikuwa wameripoti kwenye vituo vyao vya kazi na 140 zilizobaki zimetangazwa tena.

- (iii) Kamati ilishauri kwamba kibali cha kuajiri watumishi 22 kilichokuwa kimeombwa kwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kitolewe ili kujengea uwezo Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imeomba kibali cha kuajiri watumishi 15 ambapo nafasi mbili kati ya hizo zimejazwa, bado nafasi 13 kibali zinafuatiliwa Utumishi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati ambao haujatekelezwa:-

- (i) Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan Mawakili wa Serikali ili kuwapa motisha watumishi hao kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu unaotakiwa.

Serikali ilipokea ushauri wa Kamati, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitengewa kiasi cha Sh. 5,000,000,000/= za fedha za ndani za maendeleo ili kuanza ujenzi wa Ofisi na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi. Hadi mwezi Machi kiasi hicho cha fedha hakijatolewa kutoka Hazina.

- (ii) Kamati inashauri hatua za makusudi na za haraka zichukuliwe ili kujenga majengo ya Mahakama na kuweka vitendea kazi bora na vya kisasa ili kuamsha ari ya utendaji kazi miongoni mwa watumishi wa Mahakama.

Mahakama imekamilisha michoro (*model courts*) kwa ajili ya Mahakama Kuu, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kubwa kuhusu upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo na hivyo kusababisha kukwama au kuchelewa kuanza kwa kazi zilizopangwa

- (iii) Kwa kuwa Wizara imekwishapelekewa na Tume ya Marekebisho ya Sheria, taarifa ya mapendekezo ya mfumo bora wa utatuzi wa migogoro ya ardhi, Kamati inashauri taarifa hiyo ifanyiwe kazi mapema ili mfumo bora wa utatuzi wa migogoro uanze kutumika kwa lengo la kumaliza migogoro ya ardhi inayoendelea hapa nchini.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zimeanza mashauriano kuhusu namna bora ya kuyafanyia kazi mapendekezo ya Taarifa ya Tume

- (iv) Serikali itoe kiasi cha fedha inachodaiwa na *RITA* ili kuiwezesha kutekeleza wajibu wake katika mkataba wa ubia wa jengo la *RITA Tower* ili kuepokana na uwezekano wa riba kubwa kutokea kwa kuchelewa kulipa kiasi inachodaiwa.

Wakala katika mwaka wa fedha 2014/2015 ilitenga kiasi cha Sh. 2,000,000,000/= kwa ajili ya kulipa deni lake katika mradi wa ujenzi wa jengo la *RITA Tower* kutokana na fedha inazodai kutoka Wizara ya Fedha, kiasi ambacho hakijatolewa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016; baada ya kuridhika na mpango wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii pamoja na Taasisi zake kwa mwaka 2015/2016, kamati ilichambua makadirio ya Mapato na Matumizi na kuhusianisha kiasi cha fedha inayoombwa na uzito pamoja na umuhimu wa malengo yanayowekwa kwa kila Fungu.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kuwa bajeti katika Fungu 35 - Divisheni ya Mashitaka na Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria zitaongezeka kwa kiasi wakati Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itakuwa na asilimia ya punguzo kubwa zaidi ya mafungu mengine ikilinganishwa na bajeti ya mafungu hayo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri; kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu 12; jukumu la kusimamia maadili na nidhamu kwa watumishi wa Tume ya Mahakama pamoja na kuboresha menejimenti ya watu ndani ya Tume na Utumishi wa Mahakama kutokana na umuhimu wa Taasisi hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- (i) Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha Kamati hizo kukaa na kuchunguza malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa maadili na nidhamu za watumishi wa Mahakama.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (ii) Tume ya Utumishi wa Mahakama iweke utaratibu madhubuti wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uwepo wa Tume hiyo na majukumu yake ili wananchi waweze kupeleka malalamiko pale wanapobaini ukiukwaji wa maadili na nidhamu ya watumishi wa Mahakama
- (iii) Serikali iendelee kujengea uwezo wa kifedha na kirasilimali watu Tume ya Utumishi wa Mahakama ili iweze kuwapatia mafunzo watumishi wake kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
- (iv) Tume ya Utumishi wa Mahakama iimarisha udhibiti wa nidhamu kwa Mahakimu na Majaji ili kuepusha watendaji wa taasisi hii muhimu ya Mahakama kuhusishwa na vitendo vya ukiukwaji wa maadili ikiwepo kuhusishwa na vitendo vya rushwa.
- (v) Tume iongeze juhudi za kuzijengea uwezo Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya zote nchini kwa kuzipatia mafunzo stahiki ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali – Fungu 16; wakati wa kupitia utekelezaji wa majukumu na makisio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoikabili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hivyo Kamati inashauri ifuatavyo ili kuboresha utendaji wake:-

- (i) Kutokana na ongezeko la kazi zilizosababishwa na kuongezeka kwa uhalifu nchini, watumishi wa ofisi hii hasa Mwakili wa Serikali hawawiani na ongezeko la uhalifu. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kupitia Menejimenti ya Utumishi wa Umma itoe kibali cha kuajiri watumishi wa kutosha ili kuwezesha ofisi hii kuhimili kasi ya ongezeko la uhalifu.
- (ii) Serikali iendeleo kuboresha maslahi ya watumishi wa ofisi hii ukizingatia uzito na unyeti wa kazi wanazofanya kwa kuweka mazingira stahiki yatakayoleta motisha kwa watumishi ili kuongeza ari ya ufanisi wa utendaji kazi.
- (iii) Serikali iongeze kasi ya kuimarisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuitengea bajeti ya kutosha, kuhakikisha fedha zinazotengwa zinatolewa kwa wakati na kuipa vitendea kazi vya kisasa vinavyotosheleza mahitaji pamoja na kujenga ofisi za kutosha kwa ajili watumishi wa ofisi hii ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Mashtaka (DPP) - Fungu 35. Divisheni ya Mashtaka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu muhimu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

katika Taifa letu la kuendesha mashtaka na kuratibu kazi zinazofanywa na vyombo vya uchunguzi.

Kutokana na umuhimu huo Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- (i) Kwa kuwa kumekuwa na upanuzi wa maeneo ya kiutawala kwa kuongeza mikoa na wilaya hali ambayo imelazimu Ofisi hii kufungua ofisi katika maeneo na hivyo kusababisha kupanuka kwa majukumu katika ngazi hizo, ni vema Serikali ikatenga bajeti ya kutosha inayolingana na mahitaji halisi ya ongezeko na upanuzi wa majukumu ya Ofisi na kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya ofisi hii zinatolewa kwa wakati.
- (ii) Kutokana na kuongezeka kwa wimbi la uhalifu wa makosa ya jinai kama vile utakatishaji fedha/mali haramu, matumizi ya vyombo vya usafiri vya umma ikiwa ni pamoja na kusafirisha dawa za kulevya, silaha, milipuko, nyara za Serikali na usafirishaji haramu wa binadamu, Kamati inashauri Serikali iongeze jitihada za kuwajengea uwezo Watumishi wa Ofisi hii hasa Mwakili wa Serikali ili waweze kukabiliana na wimbi hili la uhalifu.
- (iii) ili kuhakikisha usalama wa Mwakili wa Serikali kutokana na uhusika wao wa kushughulikia kesi zinazohusu wahalifu na mashauri ya mikataba, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwajengea nyumba katika eneo lenye usalama ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa haki na bila woga wowote kuhusiana na usalama wao.
- (iv) Serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iendelee kudhibiti nidhamu ya Mwakili wa Serikali ili kuhakikisha kuwa Mwakili wanafanya kazi zao kwa nidhamu ya hali ya juu na wanajiepusha na vitendo vya rushwa na kuhakikisha kuwa Mwakili wanaobainika kujihusisha na vitendo hivyo wanachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwepo kuwafukuza kazi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mahakama - Fungu 40. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 hadi kufikia Machi, 2015 Mahakama imesikiliza na kutolea uamuzi jumla ya mashauri 179,962. Hii ni hatua kubwa sana na ya kpongezwa kwa kila mwananchi mpenda haki.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na kasi hii na inaamini kwamba kama kasi hii ikiendelea Mahakama inaweza kabisa kumaliza kabisa tatizo la mlundikano wa mashauri Mahakamani. Pamoja na jitihada hizi, Kamati inashauri kama ifuatavyo ili kuboresha na kuimarisha utendaji wa Mhimili huu:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (i) Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama zinatolewa zote na kwa wakati.
- (ii) Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma itoe kibali cha ajira Mahakimu ili kuiwezesha Mahakama kukabiliana na upungufu wa watumishi wakiwemo Mahakimu.
- (iii) Serikali iboreshe maslahi na mazingira ya kufanyia kazi ya Watendaji wa Mahakama ili kuwapa motisha Watendaji hao na kuhakikisha kuwa wanajiepusha na vitendo vya rushwa kwani maslahi yasiyoridhisha ni kichocheo kikubwa cha rushwa.
- (iv) Viongozi wa Mahakama akiwemo Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi, Majaji Wafawidhi, Wasajili na Mahakimu Wafawidhi waongeze juhudi za kutembelea Mahakama za ngazi mbalimbali nchini ili kubaini changamoto zinazozikabili na kuzitatua kwa Wakati.
- (v) Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa katika kumaliza mrundikano wa mashauri, Kamati inashauri Mahakama kuongeza jitihada zaidi ili kumaliza kabisa tatizo na mlundikano wa Mashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria - Fungu 41; amani na utulivu uliopo nchini ni matunda ya usimamizi makini wa mfumo wa utawala wa sheria, hivyo, ni dhahiri kuwa Wizara hii ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Kwa umuhimu huo na ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kama ipasavyo, Kamati inashauri yafuatayo:-

- (i) Kwa kuwa kuna taasisi nyingi zinazotoa msaada wa sheria kwa wananchi wasiojiweza nchini, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, iandae Muswada wa Sheria utakaounda chombo mahsusi pamoja na mambo mengine kitakachokuwa na jukumu la kutoa msaada wa sheria na kuratibu utaratibu mzuri wa utoaji huduma ya msaada wa kisheria ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hii na kuwanufaika walengwa katika kulinda na kutetea haki zao.
- (ii) Kwa kuwa ufaulu wa wanafunzi wa Shule ya Sheria kwa Vitendo umekuwa si wa kuridhisha, Kamati inashauri Serikali kusimamia kikamilifu Taasisi hii kwa kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha tatizo hili na kulitafutia ufumbuzi wa kudumu.
- (iii) Kwa kuwa taasisi nyingi za Wizara ya Katiba na Sheria ofisi zake zipo katika majengo ya kupanga hali inayoisababishia Wizara kutumia gharama kubwa kwa ajili ya kulipa mapango, hivyo, Kamati inashauri Serikali itenge

Nakala ya Mtandao (Online Document)

bajeti ya kutosha kwa ajili ya kujenga majengo yake ili kuepuka gharama za upangaji wa ofisi hizo.

- (iv) Kwa kuwa Wizara inakabiliwa na malimbikizo ya madeni ya watumishi na wazabuni, Serikali ifanye uhakiki wa madeni hayo na kuyalipa kwa wakati kwa lengo la kuimarisha ari ya watumishi hao na wazabuni ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria, Fungu - 59. Ili kuboresha utendaji kazi za Tume, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- (i) Kwa kuwa Tume ya Kurekebisha Sheria hufanya utafiti wa sheria mbalimbali kwa kutumia muda, rasilimali watu na fedha kisha kuandaa mapendekezo na kuyawasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa ajili ya kufanyia kazi mapendekezo hayo, hata hivyo uzoefu unaonesha kuwa tafiti hizi hazifanyiwi kazi kwa wakati. Kamati inashauri Serikali kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Tume hii kwa kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa ili kuboresha sheria za nchi yetu ziweze kuendana na wakati.
- (ii) Kwa kuwa kazi ya kufanya utafiti kuhusu sheria mbalimbali hufanywa na Wizara/Taasisi nyingine nchini nje ya Tume ya kurekebisha Sheria, hivyo kusababisha kazi zinazofanana kwa kutumia rasilimali na muda, Serikali iweke mfumo thabiti wa namna ya Wizara na Taasisi zinazofanya tafiti kuhusu sheria mbalimbali kusimamiwa na Tume ya Kurekebisha Sheria kwani ndiyo yenye jukumu kisheria la kufanya tafiti huo.
- (iii) Serikali iendeleo kuijengea uwezo Tume ya kurekebisha Sheria kwa kuipatia fedha za kutosha na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Fungu 55. Jukumu kubwa la Tume hii ni kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu nchini. Ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inatoa ushauri ufuatao:-

- (i) Kwa kuwa fedha zinazotengwa kila mwaka wa fedha zimekuwa hazikidhi mahitaji halisi ya Tume ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Tume, Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti ya Tume ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia kiasi hiki kinachotengwa kitolewe kwa wakati.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (ii) Kutokana na umuhimu wa ofisi kwa ustawi wa Taifa letu, Kamati inashauri Serikali ichukue hatua madhubuti za kufungua Ofisi za Tume katika kila mkoa ili kusogeza huduma hii muhimu kwa wananchi na kuwaondolea adha ya kufuata huduma hii Dar es Salaam, Mwanza, Lindi na Zanzibar pekee.
- (iii) Kwa kuwa Tume inakabiliwa na upungufu wa vitendea kazi kama vile kompyuta, samani za ofisi na magari, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kujengea uwezo Tume hii kwa kutenga fedha za kununua vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *RITA* ni Idara ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria yenye jukumu la kusajili na kuweka kumbukumbuku muhimu za maisha ya binadamu nchini kwa maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu wa Idara hii Kamati inatoa ushauri:-

- (i) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wakala huu zitolewe kwa wakati ili iweze kutekeleza mipango iliyopangwa kwa mwaka husika.
- (ii) Kamati inashauri Serikali kupitia Wakala huu iongeze kasi ya utoaji elimu hasa vijijini ili kuwawezesha wananchi wengi kujisajili hivyo kuliwezesha Taifa kuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga na kutekeza mipango ya maendeleo kwa wanachi wote.
- (iii) Kwa kuwa Serikali imeanza mchakato wa kutunga Sheria ya Usajili na Sheria ya Ufilisi nchini, Kamati inashauri mchakato huo kuharakishwa na Muswada huo uletwe Bungeni kwa lengo la kutungwa sheria hizo ili utekelezaji wake uwanufaishe wananchi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt Asha-Rose Migiro; Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu; Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa George Mcheche Masaju kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

Vilevile nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zote kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu sekta ya sheria, haki za binadamu na utawala bora umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. *(Makofi)*

Kwa heshima na kwa sababu hii ndiyo taarifa yetu ya mwisho kwa kazi nzuri waliyoifanya, naomba ruhusa yako niwataje kwa majina. Wajumbe hawa ni Mheshimiwa Gosbert Blandes...

SPIKA: Hapana! Wapo kwenye *Hansard*. Ulisema iandikwe hivyo hivyo, imeshaandikwa, sisi tunawajua na Kanuni inakataza.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, sawa nashukuru basi sitawataja.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Dkt. Thomas Kashilillah, Katibu wa Bunge, Ndugu Charles Joseph Mloka, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati na Ndugu Athuman Brambath Hussein kwa msaada mkubwa waliotupatia katika kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA
KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA
MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI
HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 99 (5), (9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inahusisha mafungu saba kama ifuatavyo:-

- i) Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama;
- ii) Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- iii) Fungu 35 - Mkurugenzi wa Mashtaka;
- iv) Fungu 40 - Mahakama;
- v) Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria;
- vi) Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na
- vii) Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 4 Mei, 2015 Kamati yangu ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria akishirikiana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummu A. Mwalimu (Mb), pamoja na Watendaji wa Wizara. Katika maelezo yake Waziri aliieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, baadhi ya mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati ni kama ifuatavyo:-


- i) Uhusiano baina ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na mipango iliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015;
- ii) Uhusiano baina ya dhima na dhamira na namna malengo yalivyotekelezwa;
- iii) Uhusiano baina ya fedha zilizotengwa kwa mipango ya Wizara na taasisi zake pamoja na fedha zilizopatikana kutoka Hazina;
- iv) Uhusiano uliopo kati ya fedha zilizopatikana na malengo yalivyotekelezwa;
- v) Uwiano wa fedha zilizotumika ikilinganishwa na fedha zilizopatikana na kubaki hadi mwezi Machi, 2015; na
- vi) Azma ya Serikali katika usimamiaji wa haki na utawala wa sheria.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 30, 2015 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi (Tsh. **118,411,286,386**) za bajeti, sawa na asilimia 52.5 ya Shilingi **bilioni mia mbili ishirini na tano mia sita sitini na tisa milioni mia nne hamsini na sita elfu mia nane sabini na tisa** (Tsh. **225,669,456,879**) zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Shilingi **bilioni arobaini mia sita sabini na nane milioni mia sita na tano mia nane arobaini na sita** (Tsh. **40,678,605,846**) ni mishahara ya watumishi na Shilingi Tsh. **Bilioni themanini na nne mia nane thelathini na tisa elfu mia mbili themanini na saba** (Tsh. **84,890,939,287**) ni kwa Matumizi Mengineyo ambapo fedha za maendeleo ni Shilingi **milioni mia tisa na tatu mia saba thelathini na mbili mia na nane kumi na nane** (Tsh. **903,732,818**) zote zikiwa ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Ili kujiridhisha na mwenendo wa upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa taasisi zilizo chini ya wizara hii, Kamati ilichambua mwenendo huo kwa kila Fungu na kuwianisha upatikanaji huo na Bajeti iliyoidhinishwa. Uchambuzi wa Kamati ulibainisha kuwa uwiano wa upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge unatofautiana miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa Mfuko wa Mahakama, Fungu 40 umekuwa na uwiano mzuri kuliko taasisi nyingine. Mfuko huu hadi kufikia taraha 31 Machi, 2015 ulipokea asilimia 65.54 ya Bajeti yake iliyoidhinishwa, wakati taasisi nyingine zilipokea pungufu ya asilima hiyo ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi iliyokuwa na asilima kidogo ya bajeti iliyoidhinishwa ikilinganishwa na taasisi nyingine ni Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria. Kiasi cha fedha zilizopatikana kwa Fungu hili ni asilimia 36.7 wakati taasisi nyingine zilipata zaidi ya asilimia hiyo ya bajeti iliyoidhinishwa. Ili kuliwezesha Bunge hili kupata picha halisi, Kamati imeandaa Chati Na. 01 kwa madhumuni hayo.



Chanzo: *Randama na Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria yaliyowasilishwa kwenye Kamati*

Mheshimiwa Spika, kwa mchanganuo huu ni dhahiri kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya wizara hii hauridhishi hasa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Hali hii inahitaji kufanyiwa kazi ili isijirudie kwa mwaka wafedha 2015/2016.

2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali. Ushauri huo ulilenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa Majukumu katika Ofisi hii. Kamati ilitaka kujiridhisha ni kwa kiasi gani maoni na ushauri wake ulizingatiwa na Serikali. Kamati ilibaini kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri wa kamati ulizingatiwa. Hata hivyo baadhi ya maoni na ushauri upo katika hatua za utekelezaji na mwingine haukuzingatiwa.

2.1.1 Maoni na ushauri wa Kamati uliotekelzwa na Serikali

- i) Ushauri kuhusu Tume ya Utumishi wa Mahakama kujengewa uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuthibiti

kuongezeka kwa vitendo vya rushwa miongoni mwa watumishi wa mahakama.

Ushauri huu umetekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya ili kuzimarisha ambapo Mikoa 8 pamoja na Wilaya zake ambayo ni Tabora, Shinyanga, Mbeya, Njombe, Iringa, Pwani, Morogoro na Dodoma tayari zimekwishapewa mafunzo hadi sasa. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 jumla ya shs. 184,220,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea kutoa mafunzo kwa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara.

- ii) **Kutokana na uhaba wa fedha Serikalini na ukomo wa bajeti iliyopewa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Kamati inashauri Wizara kufanya utaratibu wa kuhamishia kiasi cha Shilingi Bilioni moja na Million mi nne (1,400,000,000/=) kutoka mfuko wa Mahakama mapema kwenda Tume ya Utumishi wa Mahakama ili kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo.**

Wizara imetekeleza agizo hili kwa barua Kumb. Na. AB 67/341/01 ya tarehe 06 Mei, 2014 kwenda kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, na kufuatiwa na uhamisho wa kiasi cha Shilingi 1,400,000,000 kutoka Fungu 40, Mfumko wa Mahakama, kwenda Fungu 12, Tume ya Utumishi wa Mahakama. Uhamisho huu uliongeza ukomo wa bajeti katika Fungu hili kutoka Shilingi 2,871,716,000 hadi 4,271,716,000.

- iii) **Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ijengewe uwezo katika kitengo cha mikataba kwa kuwapatia mafunzo Mawakili wa Serikali katika masuala ya mikataba ya mafuta na gesi ili kuhakikisha kuwa watendaji hao wanatumika ipasavyo kuishauri Serikali katika kuingia mikataba yenye tija kwa taifa kuhusu sekta hizo na nyingine.**

Kutokana na muundo wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa sasa eneo hili la mikataba limepewa hadhi ya kuwa Divisheni na siyo Kitengo, na liko chini ya uongozi wa Mkurugenzi akisaidiana na wakurugenzi wasaidizi wawili. Kila mwaka, Idadi ya mawakili wa serikali imekuwa ikiongezwa na sasa wapo mawakili 17. Ili kuboresha utendaji wa Divisheni ya Mikataba, Ofisi imekuwa ikiongezewa bajeti yake. Lengo likiwa ni kujenga uwezo wa kifedha na ujuzi kwa ajili ya eneo hili la mikataba.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na shirika la maendeleo la umoja wa Mataifa (UNDP) na Wizara ya nishati na Madini iliandaa mafunzo ya kushughulikia mikataba ya gesi na mafuta (LING) kwa ajili ya kujenga uwezo wa mawakili wa serikali kuchambua na kujadili

mikataba ya rasilimali gesi ili kulinda maslahi ya nchi. Mafunzo hayo yalishirikisha mawakili 32 kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Wizara ya nishati na Madini, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na Maji, Wizara ya fedha na wakala wa umeme Vijijini.

Chini ya Mradi Huu, Divisheni ya Mikataba ilitengewa bajeti ya shilingi 457,149,000 kwa ajili ya kupatiwa mafunzo watumishi waliopo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hadi Machi, 2015 kiasi cha shilingi 113,580,000 kimetolewa kuwapatia mafunzo ya kushughulikia mikataba ya gesi na mafuta

- iv) **Kwa kuwa bado hakuna uelewa wa kutosha kwa wananchi kuhusu uwepo wa Tume na Kamati za Maadili za Mahakama pamoja na Majukumu yake, Kamati inashauri kuwa Elimu kuhusu uwepo wa Tume pamoja na majukumu yake iendelee kutolewa hasa vijijini ili kuwawezesha wananchi kuitumia kwa kupeleka malalamiko wakiona kuna ukiukwaji wa maadili.**

Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 jumla ya shs. 110,000,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu kuwepo kwa Kamati za Maadili ya Mahakimu za Mikoa na Wilaya. Aidha, Tume inatumia njia nyingine ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na Wakuu wa Wilaya ambao ndiyo wenyeviti wa Kamati za Wilaya ili waweze kutoa elimu hii kwenye maeneo yao wakati wa mikutano na Wananchi. Pia yapo mawasiliano na Halmashauri yenye lengo la kuwaomba Madiwani kutoa elimu hii kwa wananchi katika maeneo yao. Hii itasaidia elimu hii kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa muda mfupi na kwa gharama kidogo.

- v) **Kwa kuwa Serikali imeendelea kujengea uwezo Mahakama ya Tanzania kupitia Mfuko wa Mahakama na kwa kuzingatia kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mdau mkubwa katika utekelezaji wa shughuli za Mahakama, Kamati inashauri kwamba maboresho ya Mahakama yaende sambamba na maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kuwa vyombo hivi vinafanya kazi kwa ufanisi katika kuhakikisha kuwa azma ya utoaji haki sawa na kwa wakati inafikiwa.**

Serikali inakubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati kuwa maboresho ya Mahakama yaende sambamba na maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika kutekeleza ushauri huu, Serikali kwa mwaka 2014/2015 ilitoa kibali cha ajira kwa

watumishi 429 wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hadi machi 2015 tayari watumishi 321 wamesharipoti ofisini. Pia ofisi kwa mwaka 2014/2015 imetengewa Shilingi Bilion 5 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali Makao Makuu na Mikoani.

2.1.2 Ushauri wa Kamati unaoendelea kutekelezwa

- i) Mahakama ipewe kibali cha kuajiri watumishi wengine wakiwemo mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi sambamba na kuboresha maslahi ya Watumishi hao.**

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mahakama ya Tanzania imepata vibali vya ajira kwa watuishi 1,010 wakiwemo Mahakimu hadi sasa nafasi 750 zimetangazwa na mchakato unaendelea kuwapata watumishi hao.

- ii) Kamati inashauri Serikali itenge fedha za ndani za kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili iweze kujenga ofisi na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Taasisi hii. Divisheni ya Mashtaka ijengewe uwezo kwa kupewa kibali cha kuajiri watumishi 489 na kuwapatia mafunzo ili waweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyokusudiwa.**

Katika kujenga uwezo wa Divisheni ya Mashtaka, Serikali imetoa kibali cha kuajiri watumishi 429 katika bajeti ya mwaka 2014/2015. Hadi Machi, 2015 tayari watumishi 289 walikuwa wameripoti kwenye vituo vyao vya kazi na 140 zilizobaki zimetangazwa tena. taratibu za kuwapatia mafunzo zinafanyika.

- iii) Kamati ilielezwa kwamba Wizara ina upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali. Katika kukabiliiana na changamoto hiyo Wizara iliomba kibali cha kuajiri watumishi 22 kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 lakini hakikutolewa. Hivyo Kamati inashauri kwamba vibali hivyo vitolewe ili kujengea uwezo Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.**

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imeomba kibali cha kuajiri watumishi 15 ambapo nafasi 2 kati ya hizo zimejazwa bado nafasi 13 kibali kinafuatiliwa Utumishi.

2.1.3 Ushauri wa Kamati ambao haujatekelezwa

- i) **Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan Mawakili wa Serikali ili kuwapa motisha watumishi hao kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu mkubwa.**

Serikali ilipokea ushauri wa Kamati, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, ofisi ya mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitengewa kiasi cha Shilingi bil.5 (5,000,000,000) za fedha za ndani za maendeleo ili kuanza ujenzi wa Ofisi na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi. Hadi mwezi machi kiasi hicho cha fedha hakijatolewa kutoka Hazina. Katika jitihada za kuboresha maslahi ya watumishi.

- ii) **Kutokana na upungufu na uduni wa Ofisi pamoja na vitendea kazi, Kamati inashauri hatua za makusudi na za haraka zichukuliwe ili kujenga majengo ya Mahakama na kuweka vitendea kazi bora na vya kisasa ili kuamsha ari ya utendaji kazi miongoni mwa watumishi wa Mahakama**

Mahakama imekamilisha michoro (model courts) kwa ajili ya Mahakama Kuu, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kubwa kuhusu upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo na hivyo kusababisha kukwama au kuchekewa kuanza kwa kazi zilizopangwa

- iii) **Kwa kuwa Wizara imekwishapelekewa na Tume ya Marekebisho ya Sheria, Taarifa ya Mapendekezo ya mfumo bora wa utatuzi wa migogoro ya ardhi, Kamati inashauri taarifa hiyo ifanyiwe kazi mapema ili mfumo bora wa utatuzi wa migogoro uanze kutumika kwa lengo la kumaliza migogoro ya ardhi inayoendelea hapa nchini.**

Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zimeanza mashauriano kuhusu namna bora ya kuyafanyia kazi mapendekezo ya Taarifa ya Tume

- iv) **Serikali itoe kiasi cha fedha inachodaiwa na RITA ili kuiwezesha kutekeleza wajibu wake katika mkataba wa ubia wa jengo la RITA Tower ili kuepukana na uwezekano wa riba kubwa kutokea kwa kuchelewa kulipa kiasi inachodaiwa**


Wakala katika mwaka wa fedha 2014/15 ilitenga kiasi cha Shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya kulipa deni lake katika Mradi wa ujenzi wa jengo la RITA Tower kutokana na fedha inazodai kutoka Wizara ya Fedha, kiasi ambacho hakijatolewa hadi sasa. Ili kuhakikisha kuwa deni hilo linalipwa RITA imetenga kiasi cha Shilingi 5,000,000,000 kutoka katika makusanyo ya ndani katika makadirio ya bajeti ya mwaka 2015/2016 sambamba na kufanya mazungumzo na NSSF kuhusu namna ya kushughulikia suala hilo.

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii na taasisi zilizo chini yake, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kila Fungu kwa mafungu yote saba. Kwa upande wa Malengo na majukumu yaliyowekwa, Kamati iliridhishwa mpango huo wa Wizara hii na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kama alivyowasilisha mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ulifanyika kwa kuhusianisha kiasi cha fedha inayoombwa na uzito pamoja na umuhimu wa malengo yanayowekwa kwa kila Fungu. Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kuwa bajeti katika Fungu 35 - Divisheni ya Mashitaka na Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria zitaongezeka kwa kiasi wakati Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali litakuwa na asilimia ya punguzo kubwa zaidi ya mafungu mengine ikilinganishwa na bajeti ya mafungu hayo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, sura nzima ya uwiano wa kupungua au kuongezeka kwa bajeti za Wizara na Taasisi zilizo chini yake inaonekana katika Chatii Na. 02 ya Taarifa hii.



Chanzo: Randama zilizowasilishwa mbele ya Kamati

4.0 MAONI NA USHAURI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake ili kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kuleta ufanisi kwa manufaa ya Taifa kama ifuatavyo:-

4.1 Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu 12

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 113 ya Katiba ya Jamhuri Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, ikisomwa pamoja na Sheria ya Utumishi wa Mahakama, Sura 237, ikiwa na jukumu la kusimamia maadili na nidhamu kwa watumishi wa Tume ya Mahakama pamoja na kuboresha menejimenti ya watu ndani ya Tume na Utumishi wa Mahakama Kutokana na umuhimu wa Taasisi hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- i) Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha Kamati hizo kukaa na kuchunguza malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa Maadili na nidhamu za Watumishi wa Mahakama.

- ii) Tume ya Utumishi wa Mahakama iweke utaratibu madhubuti wa kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu uwepo wa Tume hiyo na Majukumu yake ili wananchi waweze kupeleka malalamiko pale wanabaini ukiukwaji wa maadili na nidhamu ya Watumishi wa Mahakama kwani si wananchi wengi wanaofahamu uwepo wa Tume hii.
- iii) Serikali iendeele kujengea uwezo wa kifedha na kirasilimali watu Tume ya Utumishi wa Mahakama ili iweze kuwapatia Mafunzo watumishi watumishi wake kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
- iv) Tume ya Utumishi wa Mahakama iimarisha udhibiti wa nidhamu kwa Mahakimu na Majaji ili kuepusha watendaji wa taasisi Muhimu ya Mahakama kuhusishwa na vitendo vya ukiukwaji wa Maadili ikiwepo kuhusishwa na vitendo vya rushwa jambo linaloipunguzia heshima Taasisi ya Mahakama mbele ya Jamii.
- v) Tume iongeze juhudi za kuzijengea uwezo Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya zote nchini kwa kuzipatia mafunzo stahiki ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu.

4.2 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Fungu 16

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia utekelezaji wa majukumu na makisio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoikabili ofisi ya mwanasheria mkuu wa Serikali, hivyo Kamati inashauri ifuatavyo ili kuboresha utendaji wake:-

- i) Kutokana na ongezeko la kazi zilizosababishwa na kuongezeka kwa uhalifu nchini, watumishi wa ofisi hii hasa mawakili wa Serikali hawawiani na ongezeko la uhalifu, hivyo, Kamati inashauri Serikali kupitia Menejimenti ya Utumishi wa Umma itoe kibali cha kuajiri watumishi wa kutosha ili kuwezesha ofisi hii kuhimili kasi ya ongezeko la uhalifu.
- ii) Serikali iendeele kuboresha maslahi ya watumishi wa ofisi hii ukizingatia uzito na unyeti wa kazi wanazofanya kwa kuweka mazingira stahiki yatakayoleta motisha kwa watumishi ili kuongeza ari ya ufanisi wa utendaji kazi.
- iii) Serikali iongeze kasi ya kuimarisha ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuitengea bajeti ya kutosha, kuhakikisha fedha

zinazotengwa zinatolewa kwa wakati na kuipa vitendea kazi vya kisasa vinavyotosheleza mahitaji pamoja na kujenga ofisi za kutosha kwa ajili watumishi wa ofisi hii ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

- iv) Serikali itilie maanani suala la kuwajengea uwezo na ujuzi watumishi wa ofisi hii kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika Nyanja mbalimbali kulingana na taaluma zao hasa katika nyanja za makosa ya kimtandao ili kuwawezesha kutimiza majukumu yao kwa ufanisi.

4.3 Divisheni ya Mashitaka (DPP) - Fungu 35

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Mashitaka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzishwa kupitia Ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake kwa ajili ya kutekeleza jukumu muhimu katika Taifa letu la kuendesha Mashitaka na kuratibu kazi zinazofanywa na vyombo vya uchunguzi kama yalivyoainishwa na Katiba na sheria zingine. Kutokana na umuhimu huo, ili kuimarisha na kuboresha Divisheni hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- i) Kwa kuwa kumekuwana upanuzi wa maeneo ya kiutawala kwa kuongeza mikoa na wilaya hali ambayo imelazimu Ofisi hii kufungua ofisi katika maeneo na hivyo kusababisha kupanuka kwa majukumu katika ngazi hizo, ni vema Serikali ikatenga bajeti ya kutosha inayolingana na mahitaji halisi ya ongezeko na upanuzi wa majukumu ya Ofisi na kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya ofisi hii zinatolewa kwa wakati.
- ii) Kutokana na kuongezeka kwa wimbi la uhalifu wa makosa ya jinai kama vile utakatishaji fedha/mali haramu, matumizi ya vyombo vya usafiri vya umma ikiwa ni pamoja na kusafirisha dawa za kulevya, silaha, milipuko, nyara za Serikali na usafirishaji haramu wa binadamu, Kamati inashauri Serikali iongeze jitihada za kuwajengea uwezo Watumishi wa Ofisi hii hasa mawakili wa Serikali ili waweze kukabiliana na wimbi hili la uhalifu.
- iii) Ili kuhakikisha usalama wa Mawakili wa Serikali kutokana na uhusika wao wa kushughulikia kesi zinazohusu wahalifu na mashauri ya mikataba, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwajengea nyumba (quarters) katika eneo lenye usalama ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa haki na bila woga wowote kuhusiana na usalama wao.

- iv) Serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iendelee kudhibiti nidhamu ya Mawakili wa Serikali ili kuhakikisha kuwa Mawakili wanafanya kazi zao kwa nidhamu ya hali ya juu na wanajiepusha na vitendo vya rushwa na kuhakikisha kuwa Mawakili wanaobainika kujuhusisha na vitendo vya rushwa wanachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwepo kuwafukuza kazi.
- v) Serikali iimarisha Mfumo wa teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kuweka mfumo wa kisasa wa utunzaji wa kumbukumbu za kisheria utakaotumia TEKNOHAMA ili kuwezesha huduma za kisheria zinatolewa kwa ufanisi katika ngazi zote na kuimarisha mfumo wa matumizi ya kompyuta katika uendeshaji wa Mashauri nchini.

4.4 Mfuko wa Mahakama - Fungu 40

Mheshimiwa Spika, Mahakama ni mojawapo ya Mihimili mitatu ya Dola yenye jukumu kubwa la kutafsiri Sheria na Kutolea uamuzi mashauri mbalimbali yanayowasilishwa kwake na wananchi. Kwa mujibu wa Ibara ya 107 (A),(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Mahakama ndicho chombo cha mwisho cha kusimamia na kutoa uamuzi wa mwisho katika masuala ya utoaji Haki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kuthamini juhudi kubwa zinazofanywa na Mahakama ya Tanzania katika kupunguza mlundikano wa mashauri na hivyo kukuza imani kwa Wananchi na hivyo kuwawezesha kukitumia chombo hiki kikamilifu ili waweze kupata haki zao kwa mujibu wa Sheria. Katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 hadi kufikia machi 2015 Mahakama imesikiliza na kutolea uamuzi jumla ya mashauri 179,962. Hii ni hatua kubwa na ya kupongezwa na kila mwananchi anayependa haki.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na kasi hii na inaamini kwamba kama kasi hii ikiendelea Mahakama inaweza kumaliza kabisa tatizo la mlundikano wa mashauri mahakamani. Pamoja na jitihada hizi, Kamati inashauri kama ifuatavyo ili kuboresha na kuimarisha utendaji wa Mhimili huu:-

- i) Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama zinatolewa zote na kwa wakati ili kuhakikisha shughuli zinazopangwa na Mahakama zinatekelezwa kikamilifu.
- ii) Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma itoe kibali cha ajira kwa Mahakama ili kuiwezesha Mahakama kukabiliana na upungufu wa watumishi wakiwemo Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- iii) Kwa kuwa baadhi ya Makao Makuu ya Mikoa bado hayana Mahakama Kuu, na Mahakama nyingi zilizopo sasa hasa Mahakama za Mwanzo zimechakaa hivyo kuhitaji ukarabati mkubwa na wa haraka, Kamati inashauri Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 zitolewe zote na kwa Wakati ili kuwezesha Mahakama hizo kujengwa na kukarabatiwa kwa lengo la kujenga mazingira mazuri ya utoaji haki kwa watendaji wa Mahakama na Wananchi kwa ujumla.
- iv) Serikali iboreshe Maslahi na mazingira ya kufanyia kazi ya Watendaji wa Mahakama ili kuwapa motisha Watendaji hao na kuhakikisha kuwa wanajjepusha na vitendo vya rushwa kwani maslahi yasiyoridhisha ni kichocheo kimojawapo cha rushwa.
- v) Serikali ihakikishe inaboresha Mahakama za Mwanzo zote nchini kwa kuzipatia vitendea kazi kama kompyuta, meza, usafiri na mawasiliano. Kupatikana kwa vitendea kazi hivyo kutasaidia kuleta ufanisi katika utendaji wa Mahakama za Mwanzo.
- vi) Viongozi wa Mahakama akiwemo Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi ,Majaji Wafawidhi, Wasajili na Mahakimu Wafawidhi waongeze juhudi za kutembelea Mahakama za ngazi mbalimbali nchini ili kubaini changamoto zinazozikabili na kuzitatua kwa Wakati.
- vii) Pamoja na jitihada kubwa zilizofanyika katika kumaliza mrundikano wa Mashauri, Kamati inashauri Mahakama kuongeza jitihada zaidi ili kumaliza kabisa tatizo na mrundikano wa Mashauri nchini.
- viii) Mahakama iendeleo kuimarisha usafiri wa Umma kwa ajili ya Watumishi wa Mahakama ili kurahisisha usafiri wa Watendaji hao na kuongeza ufanisi wa utendaji wa Mahakama nchini.
- ix) Kwa kuwa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara ilianzishwa kwa lengo la kuharakisha mashauri ya kibiashara ili kuhakikisha kuwa shughuli za uwekezaji haziathiriwi na ucheleweshaji wa mashauri hayo, na kwa kuwa Sera ya Mahakama ni kuhakikisha kuwa Majaji hawakai katika kituo kimoja kwa zaidi ya miaka mitatu ni vyema Mahakama ikahakikisha kuwa utaratibu wa kuhamisha Majaji katika divisheni hiyo unafanyika vizuri pasipo kuathiri mashauri mbalimbali yanayoendelea kusikilizwa na kuhakikisha kuwa Majaji wa Divisheni hiyo hawahamishwi wote kwa wakati mmoja ili kuhakikisha uzoefu unaoendelezwa na kurithishwa kwa majaji

wageni. Aidha, Mahakama ihakikishe kuwa Majaji wa Divisheni hii wanaohamishwa wanapewa muda wa kutosha ili kukamilisha kuandika hukumu na kuzisoma kabla hawaripoti katika vituo vipya wanakohamishiwa.

4.5 Wizara ya Katiba Na Sheria – Fungu 41

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo chombo kikuu cha Serikali katika masuala yote ya kisheria katika nchi ikiwa na jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa kuna utawala wa sheria unaozingatia Katiba na kuwepo kwa mfumo wa sheria unaotoa fursa sawa kwa watu wote katika jamii ili kuweza kuendesha shughuli zao kwa ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu uliopo nchini ni matunda ya usimamizi makini wa mfumo wa utawala wa Sheria, hivyo, ni dhahiri kuwa Wizara hii ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Kwa kuzingatia unyeti wa Wizara hii na ili iendelee kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

- i) Kwa kuwa kuna taasisi nyingi zinazotoa msaada wa sheria kwa wananchi wasiojiweza nchini, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria iandae muswada wa Sheria utakaounda chombo mahsusi pamoja na mambo mengine kitakachokuwa na jukumu la kutoa msaada wa sheria na kuratibu utaratibu mzuri wa utoaji huduma ya Msaada wa Kisheria ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hii na kuwanufaika walengwa katika kulinda na kutetea haki zao.
- ii) Wizara ya Katiba na Sheria iendelee kuratibu na kusimamia kikamilifu utendaji wa taasisi zilizo chini yake ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza wajibu wao kikamilifu.
- iii) Kwa kuwa ufaulu wa wanafunzi wa shule ya sheria kwa vitendo umekuwa si wa kuridhisha, Kamati inashauri Serikali kusimamia kikamilifu Taasisi hii kwa kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha tatizo hili na kulitafutia ufumbufu wa kudumu.
- iv) Kwa kuzingatia majukumu muhimu ya wizara hii, Kamati inashauri Serikali iwezeshe wizara hii kwa kuitengea bajeti muafaka na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa zinatolewa kwa wakati, kuipa rasilimaliwatu na vitendea kazi vya kisasa ili kuimarisha wizara hii kwa lengo la kuimarisha mfumo wa sheria nchini na kufikia azma ya haki sawa na kwa wakati.

- v) Kwa kuwa taasisi nyingi za wizara ya Katiba na Sheria ofisi zake zipo katika majengo ya kupanga hali inayoisababishia wizara kutumia gharama kubwa kwa ajili hiyo, hivyo, Kamati inashauri Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya kujenga majengo yake ili kuepuka gharama za upangaji wa ofisi hizo
- vi) Kwa kuwa Kamati wakati wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, ilielezwa kuwa wizara inakabiliwa na malimbikizo ya madeni ya watumishi na wazabuni, Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye uhakiki wa madeni hayo na kuyalipa kwa wakati kwa lengo la kuimarisha ari ya watumishi hao na wazabuni ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

4.6 Tume ya Kurekebisha Sheria- Fungu 59

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria ni Taasisi ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyoanzishwa kwa mujibu Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura 171. Majukumu ya Tume ni kufanya mapitio ya Sheria Mbalimbali, kufanya utafiti na kuandaa mapendekezo kisha kuyawasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria. Waziri wa Katiba na Sheria baada ya kupokea mapendekezo hayo huyawasilisha Bungeni kwa ajili ya utunzi wa Sheria au kuzifanyia mabadiliko Sheria zinazokuwa zina mapungufu katika kuhakikisha kuwa Sheria za nchi zinaenda sanjari na mazingira ya sasa katika kudumisha utawala wa Sheria na usimamizi wa Haki nchini.

Ili kuboresha utendaji kazi wa Tume, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- i) Kwa kuwa Tume ya Kurekebisha sheria hufanya utafiti wa sheria mbalimbali kwa kutumia muda, rasilimali watu na fedha kisha kuandaa mapendekezo na kuwasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa ajili ya kufanyia kazi mapendekezo hayo, hata hivyo uzoefu unaonesha kuwa tafiti hizi hazifanyiwi kazi kwa wakati, Kamati inashauri Serikali kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Tume hii kwa kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa ili kuboresha sheria za nchi yetu ziweze kuendana na wakati.
- ii) Kwa kuwa kazi ya kufanya utafiti kuhusu sheria mbalimbali hufanywa na wizara/taasisi nyingine nchini nje ya Tume ya kurekebisha Sheria, hivyo kusababisha kazi zinazofanana (duplication of work) na kutumia rasilimali na muda, Kamati

inashauri Serikali iweke mfumo thabiti wa namna ya wizara na taasisi zinazofanya tafiti kuhusu sheria mbalimbali kusimamiwa na Tume ya Kurekebisha Sheria kwani ndiyo yenye jukumu kisheria la kufanya tafiti.

- iii) Tume iendelee kufanya tafiti kuhusu sheria mbalimbali ambazo kutokana na mabadiliko ya kujamii, kisiasa na kiuchumi zinahitaji kufanyiwa marekebisha ili ziweze kuendana na wakati.
- iv) Serikali iendelee kujengea uwezo Tume ya kurekebisha Sheria kwa kuipatia fedha za kutosha na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

4.7 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Fungu 55

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni idara huru ya Serikali ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 129 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisha yake ikisomwa pamoja na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura 391. Majukumu ya Tume yameainishwa katika Ibara ya 130 (1) ya Katiba. Jukumu kubwa la Tume hii ni kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu nchini. Ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inatoa ushauri ufuatao:-

- i) Kwa kuwa fedha zinazotengwa kila mwaka wa Fedha zimekuwa hazikidhi mahitaji halisi ya Tume ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Tume, Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti ya Tume ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
- ii) Kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala utolewaji wake kutoka Hazina umekuwa si wa kuridhisha hali inayokwamisha utekelezaji wa majukumu yake, matharani fedha iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Tume kwa mwaka wa 2014/ 2015 kiasi cha shilingi 6,734,370,800/= hadi kufikia May, 2015 ni shilingi 3,119,015,975 tu ndicho kilitolewa na Hazina sawa na asilimia 34. Kwa mazingira haya Kamati inashauri Serikali ihakikishe fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya Tume zinatolewa kwa wakati ili iweze kutimiza azma yake ya kujenga jamii ya watu wanaojali haki na utamaduni unaoaheshimu, kulinda, kutekeleza na kudumisha haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

- iii) Kutokana na umuhimu wa ofisi kwa ustawi wa Taifa letu, Kamati inashauri Serikali ichukue hatua madhubuti za kufungua ofisi za Tume katika kila mkoa ili kusogeza huduma hii muhimu kwa wananchi na kuwaondolea adha ya kufuata huduma hii Dar es salaam, Mwanza, Lindi na Zanzibar pekee.
- iv) Kwa kuwa Tume inakabiliwa na upungufu wa vitendea kazi kama vile kompyuta, samani za ofisi na magari, Kamati inaendelea kulisitiza Serikali kujengea uwezo Tume hii kwa kutenga fedha za kununua vitendea kazi vya kisasa.

4.8 Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Registration, Insolvency and Trusteeship Agency-RITA)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) ni idara ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria yenye jukumu la kusajili na kuweka kumbukumbuku muhimu za maisha ya binadamu nchini kwa maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu wa idara hii kamati inatoa ushauri ufuatao ili kuimarisha na kuboresha idara hii:-

- i) Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuiwezesha Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (**RITA**) ili kutekelezaji wa majukumu yake, hata hivyo Kamati inaendelea Kushauri Serikali kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya wakala huu zitolewe kwa wakati ili iweze kutekeleza mipango iliyopangwa kwa mwaka husika.
- ii) Pamoja na zoezi la utoaji elimu kwa wananchi kuhusu majukumu na umuhimu wa wakala huu kufanyika, Kamati imebaini kuwa bado elimu hiyo haijaeleweka kikamilifu kwa wananchi, hivyo Kamati inashauri Serikali kupitia wakala huu iongeze kasi ya utoaji elimu hasa vijijini ili kuwawezesha wananchi wengi kujisajili hivyo kuliwezesha Taifa kuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga na kutekeza mipango ya maendeleo kwa wananchi wote.
- iii) Kwa kuwa Serikali imeanza mchakato wa kutunga Sheria ya Usajili na Sheria Ufilisi nchini, Kamati inashauri mchakato huo kuharakishwa na mswada huo uletwe Bungeni kwa lengo la kutungwa sheria hizo ili utekelezaji wake uwanufaishe wananchi.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Pia, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt Asha- Rose

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Migiro, (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy A.Mwalimu (Mb), Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, George Mcheche Masaju, (Mb), na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George M. Masaju kwa ushirikiano wao mkubwa waliutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Vile vile nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu sekta ya sheria, Haki za Binadamu na Utawala Bora umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

- | | |
|--|---------------|
| 1) Mhe. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) | - Mwenyekiti |
| 2) Mhe. Gosbert Begumisa Blandes, (Mb) | -M/Mwenyekiti |
| 3) Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu,(Mb) | - Mjumbe |
| 4) Mhe. Nimrod Elirehema Mkono,(Mb) | - Mjumbe |
| 5) Mhe. Halima James Mdee, (Mb) | - Mjumbe |
| 6) Mhe. Fakharia Khamis Shomar,(Mb) | - Mjumbe |
| 7) Mhe. Nyambari C.M Nyangwine, (Mb) | - Mjumbe |
| 8) Mhe. Jaku Hashim Ayoub, (Mb) | - Mjumbe |
| 9) Mhe. Felix Francis Mkosamali, (Mb) | - Mjumbe |
| 10) Mhe. Rukia Khasim Ahmed, (Mb) | - Mjumbe |
| 11) Mhe. Mustapha Boay Akunaay,(Mb) | - Mjumbe |
| 12) Mhe. Ramadhan Haji Saleh, (Mb) | - Mjumbe |
| 13) Mhe. Tundu Antipas Mughwai Lissu,(Mb) | - Mjumbe |
| 14) Mhe. Deogratias Aloys Ntukamazina,(Mb) | - Mjumbe |
| 15) Mhe. William Mganga Ngeleja, (Mb) | - Mjumbe |
| 16) Mhe. Ali Khamis Seif,(Mb) | - Mjumbe |
| 17) Abdallah Sharia Ameir,(Mb) | - Mjumbe |
| 18) Mhe. Mariam R. Kasembe,(Mb) | - Mjumbe |
| 19) Mhe. Zahra Ali Hamad, (Mb) | - Mjumbe |
| 20) Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, (Mb) | - Mjumbe |

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, Ndugu Charles Joseph Mloka,Mkurugenzi wa Idara ya Kamati na Ndugu Athuman Brambath Hussein kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kipekee, nawashukuru ndugu Matamus Fungo, ndugu Maria Mdulugu na ndugu Abdallah Selemani kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Jasson Samson Rweikiza

MWENYEKITI

KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA

20 Mei, 2015

SPIKA: Sasa namwita msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MAONI YA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA TUNDU A.M. LISSU (MB.) KUHUSU MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA 2015/2016
(Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)
KAMA YALIVYOSOMWA BUNGENI**

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, naomba kuwasilisha maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, juu ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, naomba kufanya hivyo kwa mujibu wa kanuni 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa vile huu ni Mkutano wa Ishirini na wa mwisho katika maisha ya Bunge hili la Kumi, hii ni hotuba yangu ya mwisho kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu kwenye masuala ya Katiba na Sheria. Ni matumaini yangu kwamba katika miaka hii mitano, nimelitendea haki Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwa kutoa Maoni yaliyojengwa kwenye msingi imara wa utafiti.

Mheshimiwa Spika, katika maisha yake, Mwenyekiti Mao wa China alipendelea kusema *'no investigation, no right to speak'* yaani 'bila utafiti, hakuna haki ya kuzungumza.' Katika miaka hii mitano ya maisha ya Bunge lako Tukufu, nilitofautiana na Serikali hii ya CCM na Mawaziri wake watatu wa Katiba na Sheria na Wanasheria Wakuu wa Serikali wawili karibu kwa jambo lililoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mjadala.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sidhani kama yupo mmoja kati ya Mawaziri na Wanasheria Wakuu hao anayeweza kusema, kwa haki kabisa, kwamba msimamo wangu haukuwa *based on solid research and factual data*. Sina shaka kwamba watakaoandika historia ya Bunge la Tanzania ya kipindi hiki wataona tofauti kati ya Msemaji huyu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wasemaji waliomtangulia.

Mheshimiwa Spika, kwa vile hii ni hotuba yangu ya mwisho kama Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu kwa Wizara hii, naomba nichukue fursa hii kufanya mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, kwa kupitia Wenyeviti wa Vijiji 47 kati ya 50 wa Jimbo la Singida Mashariki ambao leo hii wako ndani ya Ukumbi huu wa Bunge lako Tukufu, niwashukuru wapiga kura na wananchi wangu kwa moyo wangu wote kwa kunipa heshima kubwa ya kuwatumikia wao na Watanzania wengine katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya heshima hii kubwa waliyonipatia, miaka hii mitano imekuwa ni miaka yenye maana kubwa sana katika maisha yangu binafsi na naamini, katika maisha ya wapiga kura na wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki. Kwa kiasi kikubwa tumekuwa huru.

Mheshimiwa Spika, hii, kwa maoni yangu binafsi, ndiyo tafsiri sahihi ya ushindi mkubwa tulioupata katika Uchaguzi wa Vijiji na Vitongoji wa Desemba ya mwaka jana ambako tuliachia CCM Wenyeviti wa Vijiji vitatu tu! Kabla ya Uchaguzi huo, CCM ilikuwa na Wenyeviti wa Vijiji arobaini na tano na sisi wa UKAWA tulikuwa na Wenyeviti wa Vijiji watano. Sasa tunawasubiri mahasimu wetu hawa mwezi Oktoba, mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni hoja iliyopo mezani. Kwa vile hotuba hii inahitimisha kazi yangu ya miaka mitano kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu katika Wizara hii, naomba kwa ruhusa yako nifanye rejea ya masuala muhimu ya Kikatiba na kisheria ambayo tumeyazungumzia katika kipindi hiki. Kwa maneno mengine, maoni haya ni *post mortem* ya Serikali hii ya CCM katika masuala ya Katiba na Sheria katika miaka mitano ya maisha ya Bunge la Kumi. Kwa sababu za wazi kabisa, napendelea kuanza na mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 31 Desemba, 2010, Rais wa nchi yetu, Mheshimiwa Profesa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliihutubia Taifa na kuwahidi Watanzania kwamba itakapofika tarehe 26 Aprili, 2014 wakati wa *Golden Jubilee* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu itapata Katiba Mpya. Miezi miwili na nusu baadaye yaani tarehe 11 Machi, 2011, Serikali hii ya CCM ilichapisha Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba katika Gazeti la Serikali. Tarehe 18 Novemba ya mwaka huo, Muswada huo ulipitishwa na Bunge lako Tukufu na kuwa sheria ambayo ndiyo iliweka msingi wa kisheria wa kutekeleza ahadi ya Rais Profesa Dkt. Kikwete kwa Watanzania.

Siku hiyo ya tarehe 18 Novemba, 2011, nilisema yafuatayo mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu mchakato wa Katiba Mpya uliokuwa unanza rasmi;

“Bunge hili Tukufu lina wajibu mbele ya historia na kwa vizazi vya sasa na vijavyo, kuhakikisha kwamba tunapata muafaka wa Kitaifa juu ya Tanzania tunayoitaka. Hukumu ya historia, endapo Bunge hili Tukufu litaendeleza ushabiki wa kisiasa na kufanya maamuzi ya mambo makubwa kama haya kwa kupiga kelele au kwa kuzomea au kwa kugonga meza kwa nguvu, itakuwa ni kali sana.”

Kwa ushahidi wa miaka minne iliyofuatia, ni wazi kwamba ushauri wetu juu ya haja ya kutafuta muafaka wa Kitaifa juu ya Katiba Mpya ulipuuzwa na hukumu ya historia imekuja haraka kuliko pengine tulivyotarajia, lakini imekuwa kali kama tulivyoitabiri.

Mheshimiwa Spika, *Golden Jubilee* ya Muungano wetu yaani tarehe 26 Aprili, 2014, ilipita bila ya nchi yetu kuwa na Katiba Mpya iliyoahidiwa na Profesa Dkt. Kikwete. Baadaye tarehe 2 Oktoba ya mwaka huo, ‘Bunge Maalum’ lenye Wajumbe wa Chama cha waliohusika na *EPA, Richmond, Tegeta Escrow*, Operesheni Tokomeza Wafugaji na Operesheni Kimbunga dhidi ya Watanzania waishio mipakani, ilipitisha Katiba inayopendekezwa, baada ya kura iliyopigwa na wafu waliokuwa wametangulia mbele ya haki, mahujaji waliokuwa wanampiga shetani mawe katika Mlima Ararat, Makka nchini Saudi Arabia, wagonjwa waliokuwa wamelazwa katika hospitali mbalimbali nchini India na wajumbe wengine wasiojulikana kwa majina wala walikokuwa wakati wa kura hiyo!

Mheshimiwa Spika, baada ya kukabidhiwa Katiba Inayopendekezwa katika sherehe iliyofanyika hapa Dodoma na kususiwa na viongozi wote wa taasisi kubwa za kidini hapa nchini yaani Baraza la Maaskofu Katoliki (*TEC*), Baraza la Kikristo Tanzania (*CCT*), Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (*CPCT*) na Masheikh na Maimamu wa Taasisi mbalimbali za Kiislamu, pamoja na vyama vyote vikuu vya kisiasa nchini (*UKAWA*) na Mashirika ya Kiraia na Wawakilishi wa Ofisi za Kibalozi zilizopo Tanzania, Rais Profesa Dkt. Kikwete

aliwaahidi Watanzania kwa mara nyingine tena kwamba Katiba Inayopendekezwa na chama chake itapigiwa kura ya maoni mnamo tarehe 30 Aprili, 2015.

Mheshimiwa Spika, ahadi hiyo ilirudiwa rudiwa na kila kiongozi wa CCM na Serikali yake ndani na nje ya Bunge hili Tukufu. Hata hivyo, tarehe 30 Aprili ilipita na kura ya maoni iliyoahidiwa na Profesa Dkt. Kikwete haikufanyika. Leo ni wiki ya tatu tangu tarehe ya kura ya maoni ipite bila kura hiyo kufanyika na watu wale wale, wa chama kile kile, kwa maneno yale yale, wanatuahidi kwamba kura ya maoni itafanyika katika tarehe ambayo hawaitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wahenga wetu walisema wajinga ndio waliwao. Kwa sababu hiyo, Mtanzania yeyote atakayeamini ahadi hewa za watu hawa na chama chao asije akashangaa wala kulalamika atakapoliwa tena. Kwa kifupi, hakuna uhakika wowote kwamba kutakuwa na kura ya maoni ili kuhalalisha Katiba Inayopendekezwa na CCM, badala yake uhakika pekee tulio nao ni kuwa Rais Profesa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ataondoka madarakani bila Katiba Mpya aliyowaahidi Watanzania takriban miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, ndiyo kusema kwamba, kwenye *signature issue* ya utawala wake, yaani Katiba Mpya, huyu ni Rais aliyeshindwa, hii ni Serikali iliyoshindwa na kwa vile imekuwa *fashionable* kwa upande wa pili kusema kwamba sisi wa UKAWA tuliweka mpira kwapani na kuondoka uwanjani, wale waliobaki uwanjani peke yao, yaani Wabunge wa CCM na washirika wao, CCM ni chama kilichoshindwa. Tunaomba kufafanua zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake mbele ya Kamati ya Katiba na Sheria wiki chache zilizopita, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria alizungumzia mchakato wa mabadiliko ya Katiba kwa aya tatu tu, kati ya aya hamsini na mbili za Taarifa yake! Mheshimiwa Waziri alisema yafuatayo kuhusu Katiba Inayopendekezwa:

"...Ni matumaini yangu kuwa wananchi watatumia muda uliopo kwa kuisoma na kuelewa Katiba Inayopendekezwa na hatimaye kutumia haki yao ya kidemokrasia kwa kushiriki katika kura ya maoni kuhusu Katiba hiyo." Ameyarudia maneno haya leo hii.

Mheshimiwa Spika, swali analotakiwa Mheshimiwa Waziri kulijibu ni lini kura hiyo ya maoni itafanyika na kwa sheria ipi? Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, hata kama Tume ya Uchaguzi itakamilisha jukumu lake la kuandikisha wapiga kura nchi nzima, bado hakuna na hakutakuwa na uhakika wa kufanyika kwa kura ya maoni kuhalalisha Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msingi hapa ni matakwa ya Sheria ya Kura ya Maoni, 2013. Sheria hiyo imeweka utaratibu mgumu wa uendeshaji wa kura ya maoni ambapo kila hatua inayotakiwa kuchukuliwa haiwezekani kuahirishwa wala kuongezewa muda. Kwa mfano, ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kupokea Katiba Inayopendekezwa, Rais anatakiwa kwa Amri iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali na baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar, kuelekeza Tume ya Uchaguzi kuendesha kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa. Amri hiyo ya kura ya maoni inatakiwa kufafanua kipindi cha kampeni na kipindi ambacho kura hiyo ya maoni inatakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Rais Kikwete alikwishatoa amri kwa mujibu wa kifungu cha (4) cha Sheria ya Kura ya Maoni. Rais hana mamlaka yoyote, kwa mujibu wa sheria hii wa kutengua amri yake au kutoa amri mpya ili kuwezesha kura ya maoni kufanyika kwa tarehe nyingine tofauti na tarehe iliyotangazwa kwenye amri ya kwanza.

Pili, ndani ya siku saba, baada ya kuchapishwa kwa Katiba Inayopendekezwa, Tume inatakiwa kuandaa swali la kura ya maoni na kulichapisha katika Gazeti la Serikali. Ndani ya siku kumi na nne baada ya kuchapishwa swali hilo, Tume inatakiwa kutoa Taarifa ya kufanyika kwa kura ya maoni, itakayoeleza kipindi cha kuhamasisha na kuelimisha umma juu ya kura hiyo na siku ya kura ya maoni.

Pia kila msimamizi wa kura ya maoni anatakiwa ndani ya siku 21 baada ya kuchapishwa kwa Taarifa ya Tume, kuwajulisha wananchi katika Jimbo lake la Uchaguzi kuhusu utaratibu wa kufanyika kwa kura ya maoni. Aidha, Tume inatakiwa kutoa elimu kwa umma juu ya Katiba Inayopendekezwa kwa muda wa siku 60 tangu Katiba Inayopendekezwa ilipochapishwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi ilikwishaandaa na kuchapisha swali la kura ya maoni na ilikwishatoa taarifa ya kura ya maoni na ratiba yake nzima. Tume haina mamlaka yoyote, kwa mujibu wa Sheria hii ya kutengua taarifa yake na kutoa taarifa nyingine au kuweka ratiba nyingine badala ya ratiba iliyokwishatolewa. Vilevile Tume haiwezi kujiongezea muda wa kutoa elimu kwa umma juu ya Katiba Inayopendekezwa au kujipa muda mwingine kwa vile muda uliowekwa na Sheria haukutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wao wasimamizi wa kura ya maoni hawana mamlaka yoyote kisheria ya kuongeza au kuongezewa muda wa kutoa taarifa kwa umma chini ya kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi haina mamlaka yoyote kisheria kuongeza muda kwa Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali kuendesha elimu kwa umma juu ya Katiba Inayopendekezwa baada ya muda wa awali uliowekwa

kwa ajili hiyo kupita. Kwa kifupi, hakuna uwezekano kisheria wa kurudia tena hatua zozote muhimu ambazo zilikwishachukuliwa kwa ajili ya kufanyika kwa kura ya maoni iliyokuwa imepangwa tarehe 30 Aprili, 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna uwezekano kisheria wa kuongeza muda kwa hatua zozote ambazo muda wake ulikwishapita lakini hazikutekenezwa. Kwa sababu hizi, hakuna uwezekano wa kufanyika kwa kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni kama ilivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi yenyewe imeshatangaza kwa maandishi kwamba kura ya maoni kuhusu Katiba Inayopendekezwa haiwezekani katika mazingira ya sasa ya kisheria. Katika Randama ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2015/2016 ya Tume ya Uchaguzi, Tume imesema kwamba na naomba kunukuu:

"Sheria ya Kura ya Maoni ina maeneo ambayo hayawezi kutekelezeka na baadhi yake kuwa na tafsiri zaidi ya moja. Eneo ambalo linaweza kuleta utata ni uhesabuji wa kura ya maoni na utangazaji wa matokeo."

Tume inasema kwamba suluhisho la changamoto hiyo naomba kunukuu tena ni: "Sheria ya Kura ya Maoni ifanyiwe marekebisho kwenye maeneo ambayo hayatekelezeki au kuwa na tafsiri zaidi ya moja." Hadi sasa Serikali hii ya CCM haijaleta Muswada wowote wa marekebisho ya sheria hiyo ili kuwezesha kufanyika kwa kura ya maoni siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa kwa ahadi hewa ya kupata Katiba Mpya ifikapo tarehe 26 Aprili, 2014; kama ilivyokuwa kwa ahadi hewa ya kufanyika kwa kura ya maoni ya tarehe 30 Aprili, 2015, Serikali hii ya CCM inadanganya Watanzania kuwa kutakuwa na kura ya maoni katika mazingira ya sasa ya kisheria. Kwa sababu hiyo, huyu ni Waziri aliyeshindwa vilevile! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuzungumzia fedha za Mahakama. Katika maoni yangu ya juu ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 nililiambia Bunge lako Tukufu kwamba, tatizo kubwa linalozikabili Mahakama zetu sio uhaba wa uwezo wa kusimamia fedha zinazotolewa kwa ajili yao, bali ni uhaba wa fedha zenyewe.

Mheshimiwa Spika, pili, tatizo la uhaba wa fedha lililosababishwa na ukosefu wa uelewa wa mahitaji halisi ya Mahakama. Tatu, tatizo la ukosefu wa uelewa wa mahitaji halisi ya Mahakama, linasababishwa na ukosefu wa watu wanaoelewa mahitaji hayo Serikalini au ukosefu wa wafanya maamuzi ya migawanyo ya fedha wanaofahamu mahitaji halisi ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, mwaka huo huo wa 2011, wakati nawasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama, nilirudia tena hoja hiyo kwa kusema kwamba moja ya matatizo makubwa yanayokabili Mahakama zetu nchini ni vipaumbele vyake kutozingatiwa katika migawanyo ya bajeti za Serikali za kila mwaka. Mwaka uliofuata nilirejea hoja hiyo kwa mara nyingine tena.

Mheshimiwa Spika, tishio kubwa kuliko mengine yote kwa uhuru wa Mahakama za Tanzania siyo tu kuingiliwa na wanasiasa na Watendaji Wakuu wa Serikali. Tishio kubwa zaidi ni lile la Serikali kutumia udhibiti wa Hazina ya Taifa kuinyima Mahakama rasilimali za kuiwezesha kutimiza wajibu wake Kikatiba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu haikuchoka kuzungumzia matatizo ya kibajeti ya Mahakama ya Tanzania. Mwaka 2013/2014 nilisema kwenye maoni ya Kambi kwamba Mahakama ya Tanzania imeshindwa kutekeleza wajibu wake huu wa Kikatiba kwa sababu ya kunyimwa fedha na vitendea kazi vingine na Serikali hii hii inayodai kwamba dira yake ni haki kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, niliyarudia maneno haya *verbatim* katika maoni yetu ya mwaka jana. Nilipendekeza, katika maoni hayo ya mwaka jana kama nilivyopendekeza katika mjadala wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama miaka mitatu kabla kwamba badala ya Mahakama kutegemea ukomo wa bajeti unaowekwa na Hazina, sheria ielekeze kama ilivyo kwa Bunge na Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni na kama ilivyo kwa nchi jirani ya Kenya kwamba bajeti ya Mahakama ya kila mwaka isiwe pungufu ya asilimia tatu ya bajeti ya kila mwaka ya Serikali ili kuiwezesha Mahakama kuwa na uhakika wa fedha zake na kuiwezesha kupanga mipango yake kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu lilitokana na ukweli kwamba utaratibu wa sasa wa kutegemea mgawo wa Hazina hauwezi kutatua matatizo ya fedha ya Mahakama ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano ya maisha ya Bunge lako Tukufu, Serikali hii ya CCM haijawahi kuipatia Mahakama ya Tanzania fedha za kukidhi mahitaji yake kwa mujibu wa vipaumbele vyake. Ukweli ni kwamba Serikali hii ya CCM haijawahi kukana jambo hili. Wimbo wake ni ule ule wa miaka yote, ufinyu wa bajeti. Hivyo, kwa mfano, kwenye taarifa yake ya mwaka huu Waziri amesema kwamba kumekuwepo na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2014/2015 na naomba kunukuu: "Upungufu wa watumishi; ufinyu wa bajeti na fedha kutokutolewa kwa wakati na uhaba wa majengo na vitendea kazi."

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya Wizara yake kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2013/2014, Waziri huyu huyu alilalamikia bajeti finyu isiyokidhi majukumu ya Mahakama na fedha kutokutolewa kadiri ya mpango wa kazi wa mwaka na kwa wakati. Aidha, Waziri alilalamikia upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, kompyuta, uduni wa mazingira ya kazi na nyumba za kuishi watumishi hususani Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wa umma.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Waziri alikiri mwaka jana, hali ya majengo ya Mahakama haijaridhisha kiasi cha kutosheleza mahitaji kwani kiasi cha fedha za maendeleo kinachotolewa na Serikali ni kidogo sana ukilinganisha na idadi na hali halisi ya majengo ya Mahakama hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hali ilikuwa hiyo hiyo katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2012/2013. Katika mwaka huo mtangulizi wa Mheshimiwa Waziri wa sasa, yaani Mheshimiwa Mathew Chikawe, alilalama kwamba Wizara yangu bado inakabiliwa na changamoto nyingi katika vyombo vyake vya utoaji haki nchini ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa Serikali kifedha na rasilimali watu katika vyombo vyake vya utoaji haki kwa wananchi wake na kusababisha kuendelea kuwepo kwa mlundikano wa mashauri ya jina na madai kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Chikawe alikiri kwamba licha ya idadi ya watumishi wa kada mbalimbali wa Mahakama kuongezeka, bado uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika utoaji wa haki hapa nchini. Pia Wizara yangu ina upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi kama magari, ofisi, samani na nyumba za watumishi. Changamoto hizi zinaathiri utekelezaji wa azma ya Serikali ya upatikanaji wa haki kwa wote mapema na kupunguza tija ya taasisi mbalimbali zilizoko chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya mtangulizi wa mtangulizi wa Mheshimiwa Dkt. Migiro, yaani Mheshimiwa Celina Kombani kuhusu ufinyu wa bajeti nayo yako *on official record* ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, athari za Serikali hii ya CCM kushindwa kutoa fedha kwa mujibu wa mahitaji na vipaumbele vya Mahakama ya Tanzania zimekuwa nyingi, kubwa na zimezungumzwa katika miaka yote mitano ya maisha ya Bunge lako Tukufu. Kwa mfano, kwa sababu ya kutopatiwa fedha za kukidhi mahitaji halisi ya utoaji wa haki, Mahakama ya Tanzania imeshindwa kabisa kutatua tatizo la mlundikano mkubwa wa kesi na mashauri katika ngazi zote za Mahakama. Kwa sababu hiyo hiyo, uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa bado unaendelea kuwa tatizo. Maslahi yasiyokidhi hali ya utendaji katika Mahakama inapelekea baadhi ya watumishi kuacha kazi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania imeendelea kufedheheka kwa kuwa mdeni mkubwa na sugu wa Majaji na watumishi wengine wa Mahakama, watoa huduma, wenye nyumba za kupangisha Majaji, wajenzi na wazabuni mbalimbali. Kama Jaji Mkuu Mstaafu Augustino Ramadhani alivyowahi kusema juu ya madeni ya majaji na naomba kunukuu:

“Ni vigumu sana kwa Jaji anayeishi katika nyumba inayodaiwa kodi kuweza kusikiliza na kutoa hukumu katika kesi za mwenye nyumba na mpangaji au kesi yoyote ya uvunjwaji mkataba. Lazima Jaji atoe boriti kwenye jicho lake ili aweze kuona kibanzi kwenye jicho la mwingine.” (Makofi)

Mheshimiwa Spika, haya yanatokea Bunge lako Tukufu lilikwishatunga Sheria ya Malipo na Mafao ya Majaji (*Judges Remuneration and Terminal Benefits, Act*) ya mwaka 2007. Sheria hiyo inaweka masharti kwamba Majaji wanastahili kulipiwa nje ya mishahara yao nyumba yenye samani ya Daraja A; gharama za matibabu kwa ajili yao wenyewe na familia zao; gari ya Serikali pamoja na dereva. Tumewahi kusema siku za nyuma kwamba fedheha hizi kwa Majaji wetu na watumishi wengine wa Mahakama ya Tanzania, zinaonyesha siyo tu ukiukwaji makusudi wa sheria tajwa bali zinathibitisha jinsi gani ambavyo mfumo wa utoaji haki na uhuru wa Mahakama haujawa kipaumbele cha Serikali hii ya CCM.

Mheshimiwa Spika, hali ya miundombinu ya Mahakama zetu imekuwa mbaya na ya kusikitisha katika miaka hii mitano ya maisha ya Bunge lako Tukufu. Randama ya Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 ya Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama, inataja mojawapo ya changamoto za Mahakama ya Tanzania kuwa ni hali mbaya ya miundombinu ya Mahakama kutokana na uchakavu na uhaba wa majengo ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumewahi kusema siku za nyuma, katika kipindi cha zaidi ya nusu karne ya uhuru wetu, Kanda nane kati ya kumi na tatu za Mahakama Kuu ya Tanzania zimeendelea kutumia majengo yaliyorithiwa kutoka dola ya kikoloni. Kanda nne kati ya tano zilizobaki na Divisheni tatu za Mahakama Kuu yaani Divisheni ya Biashara, ya Kazi na ya Ardhi, zinatumia majengo yaliyoazimwa au kuchukuliwa kutoka taasisi nyingine za umma. Ni Kanda moja tu ya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Bukoba ambayo imejengewa jengo jipya ya Mahakama katika kipindi cha miaka 50 ya Utaifa wetu na hata hilo moja halijakamilika hadi leo!

Mheshimiwa Spika, aidha, Mahakama ya Rufani ya Tanzania haijawahi kuwa na jengo lake yenyewe tangu kuanzishwa kwake mwaka 1979 na kwa miaka kumi iliyopita, imekuwa mpangaji wa iliyokuwa Hoteli ya Forodhani. Sasa, yapata miaka thelathini na sita tangu Mahakama ya Rufani kuanzishwa, Randama inasema kwamba zoezi la kusafisha kiwanja, katika Mtaa wa Chimala

limekamilika na kazi ya uchambuzi wa kumpata Mshauri Elekezi zimekamilika na Mshauri kapatikana. Mkataba wa Mshauri Elekezi umesainiwa na mshauri ameanza kazi na kuwasilisha *inception report* kwa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, tangu tupate Uhuru mwaka 1961, mikoa ya Kigoma, Mara, Singida, Lindi, Morogoro, Manyara, Geita, Njombe na Simiyu haijawahi kuwa na Masjala za Mahakama Kuu. Sasa kwa mujibu wa Randama ya Fungu 40, Mshauri Elekezi amekamilisha na kuwasilisha rasimu michoro yaani *architectural drawings* na makisio. Aidha, tunaambiwa kwamba michoro ya mwisho (*detailed architectural, structural and service drawings*) inakamilishwa sambamba na kuandaa makisio na rasimu ya makabrasha ya zabuni (*tender documents*).

Mheshimiwa Spika, kwa rekodi ya Serikali hii ya CCM, tutasubiri kwa nusu karne nyingine wakati mchakato wa ujenzi wa majengo hayo unaendelea! Kwa kifupi, sera za utoaji haki za Serikali hii ya CCM hazijawahi kutekelezeka na hazitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie haki za binadamu; sehemu hii ya maoni imechukuliwa, kwa kiasi kikubwa kutoka katika maoni yetu ya mwaka jana. Sababu ya kufanya hivyo ni moja tu, tuliyoyasema mwaka jana yameendelea kufanyika katika mwaka huu wa fedha. Ukweli ni kwamba kuna kila dalili za kuonyesha kwamba tuliyoyapigia kelele mwaka jana badala ya kupungua, yameongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi, hali ya haki za binadamu katika miaka mitano ya maisha ya Bunge lako Tukufu inatisha na imezidi kuwa mbaya. Mauaji na mashambulio dhidi ya viongozi wa kidini na waumini wao na sehemu zao za ibada yaliyotokea kati ya mwaka 2012 na 2013 hayajatatuliwa hadi leo. Hakuna mtu yeyote ambaye ameadhibiwa kwa mauaji ya Padri mmoja wa Kanisa Katoliki Zanzibar. Hakuna aliyeadhibiwa kwa shambulio la risasi na la tindikali dhidi ya Mapadri wengine wawili wa Kanisa hilo huko huko Zanzibar wala kwa shambulio la tindikali dhidi ya Msaidizi wa Mufti wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hakuna aliyetiwa hatiani wala kuadhibiwa kwa kuhusika na shambulio la bomu katika Kanisa Katoliki Olasiti Arusha lililoua watu watatu na kujeruhi wengine wengi. Serikali ya CCM haijataoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni juu ya wahusika wa mauaji na mashambulio hayo na sababu zake. Mauaji na mashambulio ya waandishi wa habari na wanaharakati wengine kama madaktari yaliyotokea kati ya 2012 na 2013 hayajatatuliwa pia. Maafisa wa Jeshi la Polisi walioamuru mauaji ya mwandishi wa habari Daudi Mwangosi hawajachukuliwa hatua yoyote. Badala yake aliyekuwa kamanda wa Polisi hao amepandishwa cheo na kuhamishiwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, huu ni ushahidi wa wazi kabisa kwamba mauaji hayo yalipangwa na yalifanywa kwa maelekezo ya Serikali hii. Maafisa wa Idara ya Usalama wa Taifa na wa Jeshi la Polisi waliohusika kumteka nyara na kumtesa Mwenyekiti wa Chama cha Madaktari Tanzania, Dkt. Ulimboka hawajakamatwa hadi leo licha ya majina yao kujulikana. Raia wa Kenya aliyebambikiziwa kesi ya kumteka Dkt. Ulimboka amekwishaachiliwa huru na Mahakama. Serikali ya CCM hajitoea taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni ushahidi wa kuhusika kwa Serikali hii ya CCM katika shambulio hilo. Hakuna aliyekamatwa wala kuadhibiwa kwa kumteka nyara na kumtesa aliyekuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Ndugu Absalom Kibanda. Serikali hii ya CCM hajitoea taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni kuhusu shambulio hilo linalofanana na shambulio dhidi ya Dkt. Ulimboka. Serikali hii ya CCM ina wajibu kisheria na kisiasa wa kulinda maisha ya Watanzania na mali zao. Imeshindwa kutekeleza wajibu huo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya CCM imeitua demokrasia kitanzini na inatishia kuinyonga na kuiua. Mikutano halali ya vyama vya siasa vya upinzani imeshambuliwa kwa mabomu na risasi za moto na Jeshi la Polisi. Watu wengi wameuawa katika mashambulizi hayo, wengine wengi wamejeruhiwa. Viongozi, wanachama na hata wapita njia tu wamepigwa, kukamatwa na kufunguliwa mashtaka ya jinai kwa kushiriki mikutano halali ya vyama vya siasa vya upinzani.

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza ni jana Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imetoa taarifa rasmi kwamba Jeshi la Polisi lilikiuka haki za binadamu na sheria za nchi yetu wakati wa kuwakamata viongozi waandamizi wa Chama cha Wananchi (CUF) mnamo tarehe 27 Januari, 2015.

Mheshimiwa Spika, jana hiyo hiyo, Jeshi la Polisi limeripotiwa kuuu raia mmoja aitwaye Basil Ngole na kujeruhi mwingine baada ya kudaiwa kukutwa wakinywa pombe baada ya saa nne usiku Mjini Njombe. Matokeo ya mauaji hayo, siku nzima ya jana Mji wa Njombe umefuka kwa moshi wa mabomu ya machozi na kurindima kwa milio ya risasi baada ya wananchi wa Njombe kupinga mauaji hayo kwa maandamano.

Mheshimiwa Spika, wakati sisi wa UKAWA ndani ya Bunge lako Tukufu tulipolazimisha mjadala wa dharura kuhusu vitendo hivi viovu dhidi ya viongozi na wanachama wa CUF tarehe 28 Januari, wapo Wabunge wa CCM pekee waliojaribu kuutetea au kuukosha udhalimu huu wa Jeshi la Polisi. Sasa Tume ya Haki za Binadamu iliyoteuliwa na Rais na Mwenyekiti wao, Profesa Dkt. Kikwete, imewaumbua. Sasa na wajitokeze hadharani na kulitetea Jeshi la Polisi kwa ujasiri ule ule waliouonesha tarehe 28 Januari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo viongozi na wanachama wa CUF peke yao ambao wamepata chungu ya *element* za kifashisti katika Jeshi la Polisi. Kwa kushirikiana na watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa na viongozi na makada wa CCM, Jeshi hilo limewabambikizia viongozi na wanachama wa CHADEMA kesi za uongo za ugaidi. Wengi wameteswa kwa ukatili mkubwa baada ya kukamatwa na kuhojiwa katika Vituo vya Polisi katika kesi hizi. Hadi sasa Serikali hii ya CCM haijasema chochote juu ya kufutwa kwa kesi za uongo za ugaidi walizofunguliwa viongozi na wanachama wa CHADEMA kama vile Wilfred Lwakatare na Henry Kileo; walioshiriki kutunga mashtaka hayo ya kidhalimu hawajachukuliwa hatua yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi, sisi wa UKAWA tumelalamika kwamba Jeshi la Polisi linatumiwa na CCM kukandamiza wapinzani wa kisiasa wa chama hicho kichovu. Ushahidi ni mwingi! Mwenyekiti wa CCM, Profesa Dkt. Kikwete mwenyewe aliwaambia wana CCM wenzake wafanye kazi ya siasa badala ya kutegemea nguvu za Jeshi la Polisi. Tume ya Haki za Binadamu, katika uchunguzi wake wa mauaji ya mwandishi wa habari Mwangosi, ililishauri Jeshi la Polisi waepuke kufanya maamuzi au matendo yanayoibua hisia za ubaguzi au upendeleo miongoni mwa jamii wakati wanapotekeleza majukumu yao kisheria.

Mheshimiwa Spika, mengine ambayo sijayasema, yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante.

**MAONI YA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA
KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA TUNDU A.M. LISSU (MB.) KUHUSU MPANGO NA
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA
KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA 2015/2016 (Kanuni
ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika,
Kwa vile huu ni Mkutano wa Ishirini na wa mwisho katika maisha ya Bunge hili la Kumi, hii ni hotuba yangu ya mwisho kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu kwenye masuala ya Katiba na Sheria. Ni matumaini yangu kwamba katika miaka hii mitano, nimelitendea haki Bunge lako tukufu na Watanzania kwa ujumla kwa kutoa Maoni yaliyojengwa kwenye msingi imara wa utafiti.

Katika maisha yake, Mwenyekiti Mao alipendelea kusema 'no investigation, no right to speak', yaani, 'bila utafiti, hakuna haki ya kuzungumza.' Katika miaka hii mitano ya maisha ya Bunge lako tukufu, nilitofautiana na Serikali hii ya CCM na Mawaziri wake watatu wa Katiba na Sheria na Wanasheria Wakuu wa Serikali wawili karibu kwa jambo lililoletwa mbele ya Bunge lako tukufu kwa mjadala. Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, sidhani kama yupo mmoja kati ya Mawaziri na Wanasheria Wakuu hao anayeweza kusema, kwa haki kabisa, kwamba msimamo wangu haukuwa based on solid research and factual data. Sina shaka kwamba watakaoandika historia ya Bunge la Tanzania ya kipindi hiki wataona tofauti kati ya Msemaji huyu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Wasemaji waliomtangulia.

Mheshimiwa Spika,

Kwa vile hii ni hotuba yangu ya mwisho kama Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu kwa Wizara hii, naomba nichukue fursa hii kufanya mambo mawili. Jambo la kwanza, kwa kupitia Wenyeviti wa Vijiji arobaini na saba kati ya hamsini wa Jimbo la Singida Mashariki ambao leo hii wako ndani ya Ukumbi huu wa Bunge lako tukufu, niwashukuru wapiga kura na wananchi wangu kwa moyo wangu wote kwa kunipa heshima kubwa ya kuwatumikia wao na Watanzania wengine katika Bunge lako tukufu.

Kwa sababu ya heshima hii kubwa waliyonipatia, miaka hii mitano imekuwa ni miaka yenye maana kubwa sana katika maisha yangu binafsi na, ninaamini, katika maisha ya wapiga kura na wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki. Kwa kiasi kikubwa, tumekuwa huru. Hii, kwa maoni yangu binafsi, ndio tafsiri sahihi ya ushindi mkubwa tulioupata katika Uchaguzi wa Vijiji na Vitongoji wa Desemba ya mwaka ambako tuliachia CCM Wenyeviti wa Vijiji vitatu tu! Kabla ya Uchaguzi huo, CCM ilikuwa na Wenyeviti wa Vijiji arobaini na tano na sisi wa UKAWA tulikuwa na Wenyeviti wa Vijiji watano. Sasa tunawasubiri mahasimu wetu hawa mwezi Oktoba ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika,

Jambo la pili ni hoja iliyopo mezani. Kwa vile hotuba hii inahitimisha kazi yangu ya miaka mitano kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu katika Wizara hii, naomba kwa ruhusa yako nifanye rejea ya masuala muhimu ya kikatiba na kisheria ambayo tumeyazungumzia katika kipindi hiki. Kwa maneno mengine, Mheshimiwa Spika, Maoni haya ni post mortem ya Serikali hii ya CCM katika masuala ya katiba na sheria katika mitano ya maisha ya Bunge la Kumi. Kwa sababu za wazi kabisa, napendekeza kuanza na mchakato wa Katiba Mpya.

KATIBA MPYA IMEKWAMA!!!

Mheshimiwa Spika,

Tarehe 31 Disemba, 2010, Rais wa nchi yetu, Mheshimiwa Profesa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete alilihutubia Taifa na kuwaahidi Watanzania kwamba itakapofika tarehe 26 Aprili, 2014 – wakati wa *Golden Jubilee* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – nchi yetu itapata Katiba Mpya. Miezi miwili na nusu baadae, yaani tarehe 11 Machi 2011, Serikali hii ya CCM ilichapisha Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba katika Gazeti la Serikali. Tarehe 18 Novemba ya mwaka huo, Muswada huo ulipitishwa na Bunge lako tukufu na kuwa Sheria, ambayo ndio iliweka msingi wa kisheria wa kutekeleza ahadi ya Rais Profesa Dokta Kikwete kwa Watanzania.

Siku hiyo ya tarehe 18 Novemba, 2011, nilisema yafuatayo mbele ya Bunge lako tukufu kuhusu mchakato wa Katiba Mpya uliokuwa unanza rasmi: *“Bunge hili tukufu lina wajibu mbele ya historia na kwa vizazi vya sasa na vijavyo, kuhakikisha kwamba tunapata muafaka wa kitaifa juu ya Tanzania tunayoitaka. Hukumu ya historia, endapo Bunge hili tukufu litaendekeza ushabiki wa kisiasa na kufanya maamuzi ya mambo makubwa kama haya kwa kupiga kelele au kwa kuzomea au kwa kugonga meza kwa nguvu, itakuwa ni kali sana.”* Kwa ushahidi wa miaka minne iliyofuatia, ni wazi kwamba ushauri wetu juu ya haja ya kutafuta muafaka wa kitaifa juu ya Katiba Mpya ulipuuzwa. Na hukumu ya historia imekuja haraka kuliko pengine tulivyotarajia, lakini imekuwa kali kama tulivyoitabiri.

Mheshimiwa Spika,

Golden Jubilee ya Muungano wetu, yaani tarehe 26 Aprili, 2014, ilipita bila ya nchi yetu kuwa na Katiba Mpya iliyoahidiwa na Profesa Dokta Kikwete. Baadaye tarehe 2 Oktoba ya mwaka huo, ‘Bunge Maalum’ lenye wajumbe wa chama cha waliohusika na EPA, Richmond/Dowans, Tegeta Escrow, Operesheni Tokomeza Wafugaji na Operesheni Kimbunga dhidi ya Watanzania waishio mipakani, kilipitisha Katiba Inayopendekezwa, baada ya kura iliyopigwa na wafu waliokuwa wametangulia mbele ya haki, mahujaji waliokuwa wanampiga shetani mawe katika Mlima Ararat, Makka nchini Saudi Arabia, wagonjwa waliokuwa wamelazwa katika hospitali mbali mbali nchini India na wajumbe wengine wasiojulikana kwa majina wala walikokuwa wakati wa kura hiyo!

Na baada ya kukabidhiwa Katiba Inayopendekezwa katika sherehe iliyofanyika hapa Dodoma na kususiwa na viongozi wote wa taasisi kubwa za kidini hapa nchini, yaani Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC), Baraza la Kikristo Tanzania (CCT), Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT) na Masheikh na Maimam wa taasisi mbali mbali za Kiislamu, pamoja na vyama vyote vikuu vya kisiasa nchini (UKAWA) na mashirika ya kiraia na wawakilishi wa ofisi za kibalozi zilizopo Tanzania, Rais Profesa Dokta Kikwete aliwaahidi Watanzania – kwa mara

nyingine tena – kwamba Katiba Inayopendekezwa na chama chake itapigiwa kura ya maoni mnamo tarehe 30 Aprili, 2015.

Ahadi hiyo ilirudiwa rudiwa na kila kiongozi wa CCM na Serikali yake ndani na nje ya Bunge hili tukufu. Hata hivyo, tarehe 30 Aprili ilipita na kura ya maoni iliyoahidiwa na Profesa Dokta Kikwete haikufanyika. Leo ni wiki ya tatu tangu tarehe ya kura ya maoni ipite bila kura hiyo kufanyika na watu wale wale wa chama kile kile kwa maneno yale yale wanatuahidi kwamba kura ya maoni itafanyika katika tarehe ambayo hawaitaji.

Mheshimiwa Spika,

Wahenga wetu walisema ‘wajinga ndio waliwao.’ Kwa sababu hiyo, Mtanzania yeyote atakayeamini ahadi hewa za watu hawa na chama chao asije akashangaa wala kulalamika atakapoliwa tena. Kwa kifupi, Mheshimiwa Spika, hakuna uhakika wowote kwamba kutakuwa na kura ya maoni ili kuhalalisha Katiba Inayopendekezwa na CCM. Badala yake, uhakika pekee tulio nao ni kuwa Rais Profesa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete ataondoka madarakani bila Katiba Mpya aliyowaahidi Watanzania takriban miaka mitano iliyopita. Ndio kusema kwamba, kwenye *signature issue* ya utawala wake, yaani Katiba Mpya, huyu ni Rais aliyeshindwa. Hii ni Serikali iliyoshindwa. Na kwa vile imekuwa *fashionable* kwa upande wa pili kusema kwamba sisi wa UKAWA ‘tuliweka mpika kwapani na kuondoka uwanjani’, wale waliobaki uwanjani peke yao, yaani CCM na washirika wao, CCM ni chama kilichoshindwa. Tunaomba kufafanua zaidi.

Katika Taarifa yake mbele ya Kamati ya Katiba na Sheria wiki chache zilizopita, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria alizungumzia ‘Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba’ kwa aya tatu tu, kati ya aya hamsini na mbili za Taarifa yake! Mheshimiwa Waziri alisema yafuatayo kuhusu Katiba Inayopendekezwa: “... [Ni matumaini yangu kuwa wananchi watatumia muda uliopo kwa kuisoma na kuielewa Katiba Inayopendekezwa na hatimaye kutumia haki yao ya kidemokrasia kwa kushiriki katika kura ya maoni kuhusu Katiba hiyo.”¹ Swali analotakiwa Mheshimiwa Waziri kulijibu ni lini kura hiyo ya maoni itafanyika na kwa Sheria ipi?

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, hata kama Tume ya Uchaguzi itakamilisha jukumu lake la kuandikisha wapiga kura nchi nzima, bado hakuna – na hakutakuwa na - uhakika wa kufanyika kwa kura ya maoni kuhalalisha Katiba Inayopendekezwa. Tatizo la msingi hapa ni matakwa ya Sheria ya Kura ya Maoni, 2013.² Sheria hiyo imeweka utaratibu mgumu wa uendeshaji wa kura ya maoni, ambapo kila hatua inayotakiwa kuchukuliwa haiwezekani kuahirishwa wala kuongezewa muda.

Kwa mfano, ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kupokea Katiba Inayopendekezwa, Rais anatakiwa – kwa Amri iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali na baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar – kuielekeza Tume ya Uchaguzi kuendesha kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa.³ Amri ya kura ya maoni inatakiwa kufafanua kipindi cha kampeni na kipindi ambacho kura hiyo ya maoni inatakiwa kufanyika.⁴ Rais Kikwete alikwishatoa Amri kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Kura ya Maoni. Rais hana mamlaka yoyote, kwa mujibu wa Sheria hii, wa kutengua Amri yake au kutoa Amri mpya ili kuwezesha kura ya maoni kufanyika kwa tarehe nyingine tofauti na tarehe iliyotangazwa kwenye Amri ya kwanza.

Pili, ndani ya siku saba baada ya kuchapishwa kwa Katiba Inayopendekezwa, Tume inatakiwa kuandaa swali la kura ya maoni na kulichapisha katika Gazeti la Serikali.⁵ Na ndani ya siku kumi na nne baada ya kuchapisha swali hilo, Tume inatakiwa kutoa Taarifa ya kufanyika kwa kura ya maoni, itakayoeleza kipindi cha kuhamasisha na kuelimisha umma juu ya kura hiyo na siku ya kura ya maoni.⁶ Na kila msimamizi wa kura ya maoni anatakiwa, ndani ya siku ishirini na moja baada ya kuchapishwa kwa Taarifa ya Tume, kuwajulisha wananchi katika Jimbo lake la Uchaguzi kuhusu utaratibu wa kufanyika kwa kura ya maoni.⁷ Aidha, Tume inatakiwa kutoa elimu kwa umma juu ya Katiba Inayopendekezwa kwa muda wa siku sitini tangu Katiba Inayopendekezwa ilipochapishwa.⁸

Tume ilikwishaandaa na kuchapisha swali la kura ya maoni na ilikwishatoa Taarifa ya kura ya maoni na ratiba yake nzima. Tume haina mamlaka yoyote, kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni, ya kutengua Taarifa yake na kutoa Taarifa nyingine, au kuweka ratiba nyingine badala ya ratiba iliyokwishatolewa. Vile vile, Tume haiwezi kujiongezea muda wa kutoa elimu kwa umma juu ya Katiba Inayopendekezwa; au kujipa muda mwingine kwa vile muda uliowekwa na Sheria haukutumika ipasavyo. Kwa upande wao, wasimamizi wa kura ya maoni hawana mamlaka yoyote kisheria ya kuongeza au kuongezewa muda wa kutoa taarifa kwa umma chini ya kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Kura ya Maoni.

¹ Taarifa ya Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro (MB), Waziri wa Katiba na Sheria, Akiwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara Kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, aya ya 13, ukurasa wa 5.

² Sheria Na. 11 ya 2013

³ Ibid., kifungu cha 4(1)

⁴ Ibid., kifungu cha 4(2)(b) na (c)

⁵ Ibid., kifungu cha 4(3)

⁶ Ibid., kifungu cha 5(1)

⁷ Ibid., kifungu cha 5(2)

⁸ Ibid., kifungu cha 5(3)

Mheshimiwa Spika,

Tume ya Uchaguzi haina mamlaka yoyote kisheria kuongeza muda kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kuendesha elimu kwa umma juu ya Katiba Inayopendekezwa baada ya muda wa awali uliowekwa kwa ajili hiyo kupita.⁹ Kwa kifupi, Mheshimiwa Spika, hakuna uwezekano kisheria wa kurudia tena hatua zozote muhimu ambazo zilikwishachukuliwa kwa ajili ya kufanyika kwa kura ya maoni iliyokuwa imepangwa tarehe 30 Aprili, 2015. Hakuna uwezekano kisheria wa kuongeza muda kwa hatua zozote ambazo muda wake ulikwishapita. Kwa sababu hizi, hakuna uwezekano wa kufanyika kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni kama ilivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika,

Tume ya Uchaguzi yenyewe imeshatangaza kwa maandishi kwamba kura ya maoni kuhusu Katiba Inayopendekezwa katika mazingira ya sasa ya kisheria. Katika *Randama ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2015/16*, Tume imesema kwamba “*Sheria ya Kura ya Maoni ina maeneo ambayo hayawezi kutekelezeka na baadhi yake kuwa na tafsiri zaidi ya moja. Eneo ambalo linaweza kuleta utata ni uhesabuji wa kura ya maoni na utangazaji wa matokeo.*”¹⁰ Tume inasema kwamba ‘Suluhisho la Changamoto’ hiyo ni “*Sheria ya Kura ya Maoni ifanyiwe marekebisho kwenye maeneo ambayo hayatekelezeki au kuwa na tafsiri zaidi ya moja.*”¹¹

Hadi sasa, Serikali hii ya CCM haijaleta Muswada wowote wa marekebisho ya Sheria hiyo ili kuwezesha kufanyika kwa kura ya maoni siku za usoni. Kama ilivyokuwa kwa ahadi ya kupata Katiba Mpya ifikapo tarehe 26 Aprili, 2014; kama ilivyokuwa kwa ahadi hewa ya kufanyika kwa kura ya maoni ya tarehe 30 Aprili, 2015, Serikali hii ya CCM inadanganya Watanzania kuwa kutakuwa na kura ya maoni katika mazingira ya sasa ya kisheria. Kwa sababu hiyo, huyu ni Waziri aliyeshindwa!

FEDHA ZA MAHAKAMA NA UHURU WA MAHAKAMA

Mheshimiwa Spika,

Katika Maoni yangu ya juu ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/12 nililiambia Bunge lako tukufu kwamba “... *tatizo kubwa linalozikabili mahakama zetu sio uhaba wa uwezo wa kusimamia fedha zinazotolewa kwa ajili yao, bali ni uhaba wa fedha zenyewe! Pili, tatizo la uhaba wa fedha ... linasababishwa ...*

⁹ Ibid., 5(4)

¹⁰ Aya ya 2.6 ukurasa wa 14.

¹¹ Ibid., aya ya 2.7 ukurasa wa 14.

na ukosefu wa uelewa wa mahitaji halisi ya Mahakama. Tatu, tatizo la ukosefu wa uelewa wa mahitaji halisi ya Mahakama ... linasababishwa na ukosefu wa watu wanaoelewa mahitaji hayo serikalini au ukosefu wa wafanya maamuzi ya migawanyo ya fedha wanaofahamu mahitaji halisi ya Mahakama.”

Mwaka huo huo wa 2011, wakati nawasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama, nilirudia tena hoja hiyo kwa kusema kwamba moja ya matatizo makubwa yanayokabili mahakama zetu nchini ni “... vipaumbele vyake kutozingatiwa katika migawanyo ya bajeti za Serikali za kila mwaka.” Mwaka uliofuata nilirejea hoja hiyo kwa mara nyingine tena: “... [T]ishio kubwa kuliko mengine yote kwa uhuru wa Mahakama za Tanzania ... sio tu kuingiliwa na wanasiasa na watendaji wakuu wa Serikali. Tishio kubwa zaidi ni lile la Serikali kutumia udhibiti wake wa hazina ya taifa kuinyima Mahakama rasilmali za kuiwezesha kutimiza wajibu wake kikatiba.”

Mheshimiwa Spika,

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu haikuchoka kuzungumzia matatizo ya kibajeti ya Mahakama ya Tanzania. Mwaka 2013/14 nilisema, kwenye Maoni ya Kambi, kwamba “... Mahakama ya Tanzania imeshindwa kutekeleza wajibu wake huu wa kikatiba kwa sababu ya kunyimwa fedha na vitendea kazi vingine na Serikali hii hii inayodai kwamba dira yake ni ‘haki kwa wote na kwa wakati!’” Niliyarudia maneno haya verbatim katika Maoni yetu ya mwaka jana.

Nilipendekeza, katika Maoni hayo ya mwaka jana – kama nilivyopendekeza katika mjadala wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama miaka mitatu kabla - kwamba “... badala ya Mahakama kutegemea ukomo wa bajeti unaowekwa na Hazina, sheria ielekeze – kama ilivyo kwa Bunge na vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni na nchi jirani ya Kenya - kwamba bajeti ya Mahakama ya kila mwaka isiwe pungufu ya asilimia 3 ya bajeti ya kila mwaka ya Serikali ili kuiwezesha Mahakama kuwa na uhakika wa fedha zake na kuiwezesha kupanga mipango yake kwa uhakika zaidi.” Pendekezo langu lilitokana na ukweli kwamba “utaratibu wa sasa wa kutegemea mgawo wa Hazina hauwezi kutatua matatizo ya fedha ya Mahakama ya Tanzania.”

Mheshimiwa Spika,

Katika miaka mitano ya maisha ya Bunge lako tukufu, Serikali hii ya CCM haijawahi kuipatia Mahakama ya Tanzania fedha za kukidhi mahitaji yake kwa mujibu wa vipaumbele vyake. Ukweli ni kwamba Serikali hii ya CCM haijawahi kukana jambo hili. Wimbo wake ni ule ule wa miaka yote: ‘ufinyu wa bajeti.’ Hivyo, kwa mfano, kwenye Taarifa yake ya mwaka huu Waziri amesema kwamba kumekuwepo na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2014/2015: “Upungufu wa watumishi; ufinyu wa

bajeti na fedha kutokutolewa kwa wakati; na uhaba wa majengo na vitendea kazi.”¹²

Mheshimiwa Spika,

Katika Maelezo ya Wizara yake kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2013/14, Waziri huyu huyu alilalamikia “*“bajeti finyu isiyokidhi majukumu ya Mahakama”*”, na “*“fedha kutokutolewa kadiri ya mpango wa kazi ... wa mwaka na kwa wakati.”*” Aidha, Waziri alilalamikia “*“upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, kompyuta, uduni wa mazingira ya kazi na nyumba za kuishi watumishi hususani majaji, mahakimu na watumishi wengine wa umma.”*” Vile vile, Waziri alikiri mwaka jana, “*“hali ya majengo ya Mahakama haijaridhisha kiasi cha kutosheleza mahitaji (kwani) kiasi cha fedha za maendeleo kinachotolewa na Serikali ni kidogo sana ukilinganisha na idadi na hali halisi ya majengo ya Mahakama hapa nchini.”*”

Mheshimiwa Spika,

Hali ilikuwa hiyo hiyo katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2012/2013. Katika mwaka huo, mtangulizi wa Mheshimiwa Waziri wa sasa, yaani Mheshimiwa Mathew Chikawe, alilalama kwamba: “*... Wizara yangu bado inakabiliwa na changamoto nyingi katika vyombo vyake vya utoaji haki nchini (ikiwa) ... ni pamoja na uwezo mdogo wa*

Aidha, Mh. Chikawe alikiri kwamba licha ya idadi ya watumishi wa kada mbali mbali wa Mahakama kuongezeka, “*... bado uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika utoaji wa haki hapa nchini. Pia Wizara yangu ina upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi kama magari, ofisi, samani, na nyumba za watumishi. Changamoto hizi zinaathiri utekelezaji wa azma ya Serikali ya upatikanaji wa haki kwa wote mapema na kupunguza tija ya Taasisi mbali mbali zilizoko chini ya Wizara.”* Malalamiko ya mtangulizi wa mtangulizi wa Mheshimiwa Dkt. Migiro, yaani Mheshimiwa Celina Kombani, kuhusu ‘ufinyu wa bajeti’ nayo yako *on official record* ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika,

Athari za Serikali hii ya CCM kushindwa kutoa fedha kwa mujibu wa mahitaji na vipaumbele vya Mahakama ya Tanzania zimekuwa nyingi, kubwa na zimezungumzwa katika miaka yote mitano ya maisha ya Bunge lako tukufu. Kwa mfano, kwa sababu ya kutopatiwa fedha za kukidhi mahitaji halisi ya utoaji wa haki, Mahakama ya Tanzania imeshindwa kabisa kutatua tatizo la mlundikano mkubwa wa kesi na mashauri katika ngazi zote za Mahakama. Kwa

¹² Taarifa ya Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro..., *ibid.*, aya ya 44, uk. 17

Serikali kifedha na rasilimali watu katika vyombo vyake vya utoaji haki kwa wananchi wake na kusababisha kuendelea kuwepo kwa mlundikano wa mashauri ya jinai na madai kwa kiwango kikubwa....”

sababu hiyo hiyo, “uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa bado unaendelea kuwa tatizo. Maslahi yasiyokidhi hali ya utendaji katika Mahakama inapelekea baadhi ya watumishi kuacha kazi.”

Mheshimiwa Spika,

Aidha, Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania imeendelea kufedheheka kwa kuwa mdeni mkubwa na sugu wa majaji na watumishi wengine wa Mahakama, watoa huduma, wenye nyumba za kupangisha majaji, wajenzi na wazabuni mbali mbali. Kama Jaji Mkuu Mstaafu Augustino S.L. Ramadhani alivyowahi kusema juu ya madeni ya majaji: “Ni vigumu sana kwa Jaji anayeishi katika nyumba inayodaiwa kodi kuweza kusikiliza na kutoa hukumu katika kesi za mwenye na mpangaji au kesi yoyote ya uvunjwaji mkataba. Lazima Jaji atoe boriti kwenye jicho lake ili aweze kutoa (sic!) kibanzi kwenye jicho la mwingine.”

Haya yanatokea Bunge lako tukufu lilikwishatunga Sheria ya Malipo na Mafao ya Majaji (*Judges (Remuneration and Terminal Benefits) Act*) ya mwaka 2007. Sheria hiyo inaweka masharti kwamba majaji wanastahili kulipiwa – nje ya mishahara yao – nyumba yenye samani ya Daraja A; gharama za matibabu kwa ajili yao wenyewe na familia zao; gari ya Serikali pamoja na dereva. Tumewahi kusema siku za nyuma kwamba “fedheha hizi kwa majaji wetu na watumishi wengine wa Mahakama ya Tanzania zinaonyesha sio tu ukiukwaji makusudi wa sheria tajwa bali zinathibitisha jinsi gani ambavyo mfumo wa utoaji haki na uhuru wa Mahakama haujawa kipaumbele cha Serikali hii ya CCM.”

Mheshimiwa Spika,

Hali ya miundombinu ya mahakama zetu imekuwa mbaya na ya kusikitisha katika miaka hii mitano ya maisha ya Bunge lako tukufu. *Randama ya Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/16, Fungu 40, Mfuko wa Mahakama*, inataja mojawapo ya ‘changamoto’ za Mahakama ya Tanzania kuwa ni “hali mbaya ya miundombinu ya Mahakama kutokana na uchakavu na uhaba wa majengo ya Mahakama.”¹³

Na kama ambavyo tumewahi kusema siku za nyuma, katika kipindi cha zaidi ya nusu karne ya uhuru wetu, “Kanda nane kati ya kumi na tatu za Mahakama Kuu ya Tanzania zimeendelea kutumia majengo yaliyorithiwa kutoka dola ya kikoloni. Kanda nne kati ya tano zilizobaki na Divisheni tatu za Mahakama Kuu, yaani Divisheni ya Biashara, ya Kazi na ya Ardhi zinatumia majengo yaliyoazimwa au kuchukuliwa kutoka taasisi nyingine za umma! Ni Kanda moja tu ya Mahakama Kuu ya Tanzania – Kanda ya Bukoba – ambayo imejengewa jengo jipya ya Mahakama katika kipindi cha miaka hamsini ya utafu wetu. Na hata hilo moja halijakamilika hadi leo!”

Aidha, Mahakama ya Rufani ya Tanzania haijawahi kuwa na jengo lake yenyewe tangu kuanzishwa kwake mwaka 1979 na kwa miaka kumi iliyopita, imekuwa mpangaji wa iliyokuwa Hoteli ya Forodhani. Sasa, yapata miaka thelathini na sita tangu Mahakama ya Rufani kuanzishwa, Randama inasema kwamba “zoezi la kusafisha kiwanja ... katika Mtaa wa Chimala limekamilika. Kazi ya uchambuzi wa kumpata Mshauri elekezi ... zimekamilika na Mshauri kapatikana. Mkataba wa mshauri elekezi umesainiwa na mshauri ameanza kazi na kuwasilisha **inception report** kwa majadiliano.”

Mheshimiwa Spika,

Tangu tupate uhuru mwaka 1961, Mikoa ya Kigoma, Mara, Singida, Lindi, Morogoro, Manyara, Geita, Njombe na Simiyu haijawahi kuwa na Masjala za Mahakama Kuu. Sasa, kwa mujibu wa Randama ya Fungu 40, “Mshauri elekezi ... amekamilisha na kuwasilisha rasimu michoro ya *Architectural Drawings, makisio cost estimates.*” Aidha, tunaambiwa kwamba “michoro ya mwisho (*detailed architectural, structural and service drawings*) inakamilishwa sambamba na kuandaa makisio (*cost estimates*) na rasimu ya makabrasha ya zabuni (*tender documents*).” Kwa rekodi ya Serikali hii ya CCM, tutasubiri kwa nusu karne nyingine wakati mchakato wa ujenzi wa majengo hayo unaendelea! Kwa kifupi, sera za utoaji haki za Serikali hii ya CCM hazijawahi kutekelezeka na hazitekelezeki.

HALI YA HAKI ZA BINADAMU

Mheshimiwa Spika,

Sehemu hii ya Maoni imechukuliwa, kwa kiasi kikubwa, kutoka katika Maoni yetu ya mwaka jana. Sababu ya kufanya hivyo ni moja tu: tuliyoyasema mwaka jana yameendelea kufanyika katika mwaka huu wa fedha. Ukweli ni kwamba kuna kila dalili za kuonyesha kwamba tuliyoyapigia kelele mwaka, badala ya kupungua, yameongezeka. Kwa kifupi, hali ya haki za binadamu katika miaka mitano ya maisha ya Bunge lako tukufu inatisha na imezidi kuwa mbaya. Mauaji na mashambulio dhidi ya viongozi wa kidini na waumini wao na sehemu zao za ibada yaliyotokea kati ya mwaka 2012 na 2013 hayajatatuliwa hadi leo. Hakuna mtu yeyote ambaye ameadhibiwa kwa mauaji ya padre mmoja wa Kanisa Katoliki Zanzibar. Hakuna aliyeadhibiwa kwa shambulio la risasi na la tindikali dhidi ya mapadre wengine wawili wa Kanisa hilo huko huko Zanzibar wala kwa shambulio la tindikali dhidi ya Msaidizi wa Mufiti wa Zanzibar.

Hakuna aliyetiwa hatiani wala kuadhibiwa kwa kuhusika na shambulio la bomu katika Kanisa Katoliki Olasiti Arusha lililoua watu watatu na kujeruhi wengine wengi. Serikali ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni juu ya wahusika wa mauaji na mashambulio hayo na sababu zake. Mauaji na mashambulio ya waandishi wa habari na wanaharakati wengine kama madaktari yaliyotokea kati ya 2012 na 2013 hayajatatuliwa pia. Maafisa wa

Jeshi la Polisi walioamuru mauaji ya mwandishi wa habari Daudi Mwangosi hawajachukuliwa hatua yoyote. Badala yake, aliyekuwa kamanda wa polisi hao amepandishwa vyeo na kuhamishiwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Huu ni ushahidi wa wazi kabisa kwamba mauaji hayo yalipangwa na/au yalifanywa kwa maelekezo ya Serikali hii ya CCM.

Maafisa wa Idara ya Usalama wa Taifa na wa Jeshi la Polisi waliohusika kumteka nyara na kumtesa Mwenyekiti wa Chama cha Madaktari Tanzania, Dk. Steven Ulimboka hawajakamatwa hadi leo licha ya majina yao kujulikana. Raia wa Kenya aliyebambikiziwa kesi ya kumteka Dk. Ulimboka amekwishaachiliwa huru na mahakama. Serikali ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni kuhusu jambo hili. Huu ni ushahidi wa kuhusika kwa Serikali hii ya CCM katika shambulio hilo.

Hakuna aliyekamatwa wala kuadhibiwa kwa kumteka nyara na kumtesa aliyekuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Absalom Kibanda. Serikali hii ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni kuhusu shambulio hilo linalofanana na shambulio dhidi ya Dk. Ulimboka. Serikali hii ya CCM ina wajibu kisheria na kisiasa wa kulinda maisha ya Watanzania na mali zao. Imeshindwa kutekeleza wajibu huo kwa Watanzania.

DEMOKRASIA KITANZINI!

Serikali hii ya CCM imeitia demokrasia kitanzini na inatishia kuinyonga na kuiua. Mikutano halali ya vyama vya siasa vya upinzani imeshambuliwa kwa mabomu na risasi za moto na Jeshi la Polisi. Watu wengi wameuawa katika mashambulizi hayo. Wengine wengi wamejeruhiwa. Viongozi, wanachama na hata wapita njia tu wamepigwa, kukamatwa na kufunguliwa mashtaka ya jinai kwa kushiriki mikutano halali ya vyama vya siasa vya upinzani.

Tunavyozungumza ni jana Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imetoa taarifa rasmi kwamba Jeshi la Polisi lilikiuka haki za binadamu na sheria za nchi yetu wakati wa kuwakamata viongozi waandamizi wa Chama cha Wananchi (CUF) mnamo tarehe 27 Januari, 2015. Na jana hiyo hiyo, Jeshi la Polisi limeripotiwa kuua raia mmoja na kujeruhi mwingine baada ya kudaiwa kukutwa wakinywa pombe baada ya saa nne usiku Mjini Njombe. Matokeo ya mauaji hayo, siku nzima ya jana Mji wa Njombe umefuka kwa moshi wa mabomu ya machozi na kurindima kwa milio ya risasi baada ya wananchi wa Njombe kupinga mauaji hayo kwa maandamano.

Wakati sisi wa UKAWA ndani ya Bunge lako tukufu tulipolazimisha mjadala wa dharura kuhusu vitendo viovu dhidi ya viongozi na wanachama wa CUF tarehe 28 Januari, wapo Wabunge – wa CCM pekee – waliojaribu kuutetea au kuukosha udhalimu huu wa Jeshi la Polisi. Sasa Tume ya Haki za Binadamu -

iliyoteuliwa na Rais na Mwenyekiti wao, Profesa Dakta Jakaya Kikwete – imewaumbua. Sasa na wajitokeze hadharani na kulitetea Jeshi la Polisi kwa ujasiri ule ule waliouonyesha tarehe 28 Januari.

Mheshimiwa Spika,

Sio viongozi na wanachama wa CUF peke yao ambao wamepata chungu ya 'element za kifashisti' katika Jeshi la Polisi. Kwa kushirikiana na watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa na viongozi na makada wa CCM, Jeshi hilo limewabambikizia viongozi na wanachama wa CHADEMA kesi za uongo za ugaidi. Wengi wameteswa kwa ukatili mkubwa baada ya kukamatwa na kuhojiwa katika vituo vya polisi katika kesi hizi. Hadi sasa Serikali hii ya CCM haijasema chochote juu ya kufutwa kwa kesi za uongo za ugaidi walizofunguliwa viongozi na wanchama wa CHADEMA kama vile Wilfred Lwakatare na Henry Kilewo. Walioshiriki kutunga mashtaka hayo ya kidhalimu hawajachukuliwa hatua yoyote.

Kwa miaka mingi, sisi wa UKAWA tumelalamika kwamba Jeshi la Polisi linatumiwa na CCM kukandamiza wapinzani wa kisiasa wa chama hicho kichovu. Ushahidi ni mwingi. Mwenyekiti wa CCM, Profesa Dakta Kikwete mwenyewe, aliwaambia wanaCCM wenzake wafanye kazi ya siasa badala ya kutegemea nguvu za Jeshi la Polisi. Tume ya Haki za Binadamu, katika uchunguzi wake wa mauaji ya mwandishi habari Daudi Mwangosi, ililishauri Jeshi la Polisi "... waepuke kufanya maamuzi au matendo yanayoibua hisia za ubaguzi au upendeleo miongoni mwa jamii wakati wanapotekeleza majukumu yao kisheria. Mfano, Jeshi la Polisi lilizuia mikutano ya CHADEMA kwa sababu ya sensa wakati huo huo ... CCM walikuwa wakifanya uzinduzi wa kampeni huko Zanzibar...."

Mheshimiwa Spika,

Licha ya Tume ya Haki za Binadamu kusisitiza katika Taarifa yake juu ya mauaji ya marehemu Mwangosi kwamba "*demokrasia ya mfumo wa vyama vingi iheshimiwe na kulindwa*", Jeshi la Polisi limebaki kiziwi. Halisikii. Jeshi la Polisi limeendelea kutumia visingizio vile vile dhaifu vya miaka yote, yaani kile kinachoitwa 'taarifa za kiintelijensia', kujaribu kuhalalisha vitendo vyake vya kihalifu dhidi ya haki za binadamu. Hivi, kwa mfano, ndivyo Naibu Kamishna wa Polisi S.N. Sirro wa Kanda Maalum ya Polisi Dar es Salaam alivyojaribu kuhalalisha kuzuia mkutano na maandamano halali ya CUF tarehe 28 Januari ya mwaka huu: "*Kutokana na taarifa za kiintelijensia zilizopo maandamano hayo/mkutano huo kama utafanyika kuna kila dalili za kuwepo vurugu na hatimaye uvunjifu wa amani.*"

Uongo kama huu uliofichuliwa jana na Tume ya Haki za Binadamu umerudiwa wiki iliyopita na Jeshi la Polisi Wilaya ya Iramba Mkoani Singida. Tarehe 14 Mei, 2014, CHADEMA Wilaya ya Iramba ilitoa taarifa ya mikutano ya hadhara katika

maeneo kadhaa ya Wilaya hiyo kwa lengo la 'ujenzi wa Chama.'¹⁴ Siku iliyofuata, yaani tarehe 15 Mei, Mkuu wa Polisi Wilaya Mrakibu Mwandamizi wa Polisi Juma W. Majula, alijulisha CHADEMA Wilaya kwamba 'taarifa (yao) imepokelewa kwa 'masharti' kwamba wazingatie tarehe, muda na maeneo ya mikutano yao; "... wajiepushe na kutoa maneno ya uongo na kukashifu vyama vingine", na kuzingatia Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa.¹⁵

SSP Majula aliwaonya CHADEMA Wilaya ya Iramba kwamba: *"Kinyume na kuendana na matakwa haya, mikutano yenu itasitishwa mara moja na wakati wowote."* OCD Majula alinakili barua yake kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Mkuu wa Wilaya ya Iramba na Mkuu wa Usalama wa Taifa Wilaya ya Iramba 'kwa taarifa tafadhali.' Aidha, Wakuu wa Vituo vya Polisi vya Kiomboi, Shelui, Kinampanda na Ndago walipewa maelekezo ya kusimamia usalama kwenye mikutano hiyo na *"hakikisheni Sheria za Nchi hazivunjwi na atakaevunja Sheria achukuliwe hatua za kisheria mara moja."*

Hata hivyo, kabla ya kufanyika mkutano hata mmoja na bila sheria yoyote kuvunjwa na CHADEMA au na mtu mwingine yeyote, kesho yake – tarehe 16 Mei, 2015 – SSP Majula aligeuka ghafla. Kwa maneno yake: *"Ninakujulisha kwamba kutokana na taarifa za kiintelijensia mkutano wa Kiomboi Stand hautakuwa salama. Hivyo ni rai yangu kuwa mkutano huo usitishwe ili kuwaweka wananchi salama ambao ndio tunategemea kuwaongoza. Hii ni kutokana na dhana iliyozoeleka kuwa machafuko yanapotokea wanaoathirika ni wananchi wa kawaida wa hali ya chini nasi viongozi tunabaki salama."*

Pengine bila kujua, SSP Majula alitoa sababu halisi za kuzuia mikutano ya CHADEMA wilayani Iramba: *"... Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya ya Iramba ameamuru kusitishwa kwa mikutano yote ya Vyama vya Siasa hapa wilayani ... kwa sababu za kiusalama."* Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, ni Mkuu wa Wilaya. Kwa sasa, nafasi hiyo katika Wilaya ya Iramba inashikiliwa na Bi. Lucy Mayenga, ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum anayewakilisha CCM ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika,
Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu imepigia kelele mara nyingi nafasi ya Wakuu wa Wilaya kama Mheshimiwa Mayenga katika mfumo wa ulinzi

¹⁴ Barua ya Katibu wa Wilaya kwa
'OCD Iramba Kumb. CH/IRA/ADM/VOL. 191 ya tarehe 14 Mei, 2015, YAH: TAARIFA YA KUFANYA MIKUTANO YA HADHARA.

¹⁵ Barua ya Mkuu wa Polisi Wilaya ya Iramba kwa Katibu wa Wilaya CHADEMA Kumb. KIO/SO.7/2/A/103 ya tarehe 15 Mei, 2015, YAH: TAARIFA YA KUFANYA MIKUTANO YA HADHARA KATIKA TARAFU ZA KISIRIRI, SHELUI, NDAGO NA KINAMPANDA WILAYA YA IRAMBA MKOA WA SINGIDA.

na usalama wa nchi yetu. Kwa mfano, katika Maoni yetu ya mwaka 2012/13, tuliliambia Bunge lako tukufu kwamba “... wengi wa Wakuu wa ... Wilaya wa Tanzania ya leo ni makada wa CCM. Mamlaka ya watu hawa hayatokani na wananchi kwani hawachaguliwi na mtu yeyote; na, kwa sababu hizo hizo, hawawajibiki kwa wananchi kwa utekelezaji wa kazi na majukumu yao.... Kwa vyovyote vile, lengo la uteuzi wa Wakuu hawa wa Wilaya ni kudhibiti wananchi – na katika zama hizi za vyama vingi vya siasa, vyama vya upinzani - kwa manufaa ya CCM.”

Katika Maoni yetu hayo, tulithibitisha – kwa kutumia Katiba ya CCM yenyewe – kwamba Wakuu wa Wilaya ni makada wa CCM: “Wakuu wa ... Wilaya wote ni, na wanatakiwa kuwa, wanachama wa CCM. Hii ni kwa sababu, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1977, Wakuu wa Wilaya wamekuwa ni wajumbe wa vikao vyote vikuu vya CCM katika ngazi ya Wilaya. Kwa mfano, kwa mujibu wa Katiba ya CCM ..., Mkuu wa Wilaya ni mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya ...; ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya ...; na ni mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya....”

Na kama utakumbuka, Mheshimiwa Spika, tulihoji kama Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wakuu wa Mikoa au Wilaya kama Mheshimiwa Mayenga bado wana sifa za kuendelea kuwa Wabunge, kwa vile ibara ya 67(2)(g) ya Katiba inamwondolea mtu sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge ““... ikiwa mtu huyo ameshika madaraka ya afisa mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano....”

Kwa vyovyote vile, Mheshimiwa Spika, vitendo vya Jeshi la Polisi kuzuia mikutano na maandamano halali ya vyama vya siasa kwa visingizio finyu na vya kijinga kama taarifa za kiintelijensia’ havikubaliki tena. Vyama vya siasa vilivyopata usajili wa kudumu vina haki, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa na Kanuni zake, ya kufanya mikutano na maandamano.

Kwa upande wake, Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama kama Idara ya Usalama wa Taifa, vimepewa wajibu na Sheria hiyo wa kutoa ulinzi katika mikutano na maandamano ya vyama vya siasa. Hivi ndivyo inavyofanyika katika mikutano yote ya CCM na kwenye ziara za viongozi wake mbali mbali; na ndivyo inavyopaswa kuwa kwa vyama vingine vyote. Aidha, Mkuu wa Wilaya na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kama Mheshimiwa Mayenga, hana mamlaka yoyote kisheria kukataza au kupiga marufuku mkutano wowote wa hadhara au maandamano ya vyama vya siasa. Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu itashangaa sana endapo, baada ya vitendo vyake vya uvunjaji wa sheria, Mheshimiwa Mayenga ataendelea kuwa Mkuu wa Wilaya ya Iramba au Wilaya nyingine yoyote katika nchi yetu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itamshangaa sana Inspekta Jenerali wa Polisi endapo SSP Majula ataendelea kuwa Mkuu wa Polisi wa

Wilaya ya Iramba au wilaya nyingine yoyote ya Tanzania, baada ya kuruhusu mamlaka yake kisheria kupokwa na Mkuu wa Wilaya Mayenga kwa namna tuliyoielezea hapa.

MATUMIZI HARAMU YA NGUVU ZA KIJESHI!

Mheshimiwa Spika,

Sehemu hii pia imechukuliwa, kwa sababu zile zile, kutoka kwenye Maoni yetu ya mwaka jana. *“Serikali ya CCM imewageuka Watanzania walioipigia kura na kuwaua, kuwatesa na kuwatia vilema vya maisha, kuwabaka, kuwafukuza kwenye maeneo yao na kuwafanya wakimbizi wa ndani au internally displaced persons (IDPs). Badala ya kulinda mali zao, Serikali ya CCM imekuwa mwizi wa mali za wananchi. Serikali ya CCM imeendesha Operesheni Kimbunga kwa kisingizio cha kuondoa wahamiaji haramu nchini. Matokeo ya Operesheni hiyo ni kwamba maelfu ya watu wasiokuwa na hatia wa mikoa ya Kagera na Kigoma – inayopakana na Burundi na Rwanda – walikamatwa, kuteswa na kuporwa mifugo, fedha na mali zao nyingine na makazi yao kuharibiwa.*

“Utaratibu wa kisheria wa kuwakamata watuhumiwa, kuwapeleka mahakamani, kuwapata na hatia na kuwaadhibu kwa mujibu wa sheria umepuuzwa. Cha kushangaza Operesheni Kimbunga haikuihusu mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mara, Mbeya, Mtwara, Rukwa na Ruvuma ambayo inapakana na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji na Zambia ambayo nayo pengine ina wahamiaji haramu. Katika mazingira haya, ni sahihi kuamini kwamba Operesheni Kimbunga ilikuwa ni lengo la kuwaadhibu watu wenye asili ya Rwanda kwa sababu ya mgogoro wa kidiplomasia kati ya Rais Jakaya Kikwete na Rais Paul Kagame wa Rwanda.

“Hata kabla vumbi lililotimuliwa na Operesheni Kimbunga halijatulia, Serikali ya CCM ilianzisha vita nyingine kubwa dhidi ya Watanzania. Hii ni Operesheni Tokomeza Ujangili. Licha ya jina lake, Operesheni hiyo imetokomeza maisha ya Watanzania wasiokuwa na hatia yoyote. Makumi ya watu wameuawa, mamia wamejeruhiwa, maelfu wamekamatwa na kuteswa, vijiji vizima vimechomwa moto na makazi ya wananchi kuharibiwa, mifugo imeuawa ama kuporwa kwa mtutu wa bunduki, mashamba na mazao yameharibiwa na maelfu ya wananchi wametiwa umaskini mkubwa na Serikali hii ya CCM.

“Hatimaye, baada ya kelele kubwa ndani na nje ya Bunge, Operesheni Tokomeza ilisitishwa na Mawaziri wa Ulinzi, Mambo ya Ndani, Maliasili na Utalii na Mifugo wakaondoshwa madarakani kwa sababu ya Operesheni hiyo. Walioua, kutesa na kulemaza Watanzania na kuwaibia au kuharibu mali zao hawajakamatwa wala kuchukuliwa hatua zozote za kisheria.

“Operesheni Kimbunga na Tokomeza zilikuwa Operesheni za Kijeshi. Zilianzishwa, kuongozwa na kutekelezwa na maafisa na askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na vikosi vingine vya ulinzi na usalama. Operesheni hizi za kijeshi zimefanyika wakati Tanzania haiko vitani na wala haiko katika hali ya vita. Rais Kikwete hakutangaza vita wala kuwepo kwa hali ya vita kwa mujibu wa Katiba ili kuweza kuamuru kutekelezwa kwa Operesheni hizi za kijeshi.

“Hakukuwa na maasi au vurugu zozote zozote za kijamii. Kwa sababu hiyo, hakuna Mkuu wa Mkoa yeyote aliyeomba msaada wa kijeshi ili kuwezesha matumizi ya Majeshi ya Ulinzi katika kusaidia mamlaka za kiraia kama inavyotakiwa na Sheria ya Ulinzi wa Taifa, 1970 na Kanuni zake. Kwa kila namna inavyoonekana, Operesheni Kimbunga na Operesheni Tokomeza zilikuwa ni matumizi haramu ya nguvu za kijeshi dhidi ya raia.

TUME YA UCHUNGUZI YA JAJI MSUMI

“... Tume ya Uchunguzi iliyoahidiwa Bungeni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuchunguza masuala yanayohusu ukiukwaji huu wa haki za binadamu imeundwa Rais kupitia Tangazo la Serikali Na. 131 la tarehe 2 Mei, 2014. Tume hiyo inaongozwa na Jaji Kiongozi mstaafu Hamisi Amir Msumi na Makamishna wenzake Majaji wastaafu Stephen Ihema na Vincent Kitubio Damian Lyimo.

“... Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu na kutambua utumishi uliotukuka wa Jaji Kiongozi Msumi. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina imani kabisa na uteuzi wa Makamishna Ihema na Lyimo. Itakumbukwa kwamba tarehe 13 Julai, 2012, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililalamikia uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu “... wakiwa wamekaribia muda wao wa kustaafu kwingineko katika utumishi wa umma (na) wanapewa ‘zawadi’ ya ujaji ili kuwawezesha kupata mafao ya Majaji wastaafu ambayo yameboreshwa sana katika miaka ya karibuni.”

“Ushahidi tuliowasilisha mbele ya Kamati ya Haki, Madaraka na Maadili ya Bunge baada ya Msemaji wa Kambi kushtakiwa kwenye Kamati hiyo kwa kile kilichoitwa ‘kuwadhalilisha’ majaji uliwahusisha Majaji wastaafu Ihema na Lyimo katika kundi la Majaji ambao uteuzi wao tuliupigia kelele. Sehemu ya ushahidi huo inaonyesha kwamba tarehe 16 Juni 2003, aliyekuwa Mwenyekiti CCM wa Mkoa wa Singida, Mzee Joram Allute alimwandikia Rais Benjamin Mkapa maombi ya kumwondoa Jaji Ihema kama Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania ‘kwa uzembe na kukosa maadili.’ Mzee Allute alikuwa na kesi kwa Jaji Ihema ambapo Jaji huyo ‘alikalilia’ uamuzi kwa zaidi ya miaka minne hadi aliponyang’anywa faili la kesi hiyo na kukabidhiwa Jaji mwingine aliyeandika uamuzi huo ndani ya wiki tatu! Mwezi mmoja kabla ya barua ya Mzee Allute kwa Rais Mkapa, mawakili wake walikuwa wamemwandikia Jaji Mkuu Barnabas Samatta kulalamikia ucheleweshaji wa uamuzi wa kesi hiyo. Mawakili hao

walidai: “Hadhi na heshima ya Mahakama inaporomoka vibaya kama inachukua zaidi ya miaka mitatu kwa Jaji kutafakari na kutoa uamuzi kwa jambo jepesi kama maombi ya pingamizi.”

“... Sio tu kwamba Jaji mstaafu Ihema ana rekodi mbaya ya kijaji, bali pia ana rekodi ya kutumiwa na Serikali hii ya CCM kuisafisha Serikali kwa matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na watendaji wa Serikali. Mwaka 2012, mara baada ya Jeshi la Polisi mkoani Iringa kumuua marehemu Daudi Mwangosi, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi alimteua Jaji Ihema kuongoza Kamati iliyoundwa na Waziri Nchimbi kuchunguza mauaji hayo.

“Taarifa ya Uchunguzi wa Kifo cha Mwandishi wa Habari wa Channel Ten Bw. Daudi Mwangosi, iliyoandaliwa na Kamati ya Jaji Ihema ni mfano wa namna ya kuisafisha Serikali kutoka kwenye lawama ya mauaji ya raia wake. Taarifa hiyo ilitofautiana kimsingi na Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Uchunguzi wa Tukio Lililopelekea Kifo cha Daudi Mwangosi Kilichotokea Septemba 2, 2012 Kijijini Nyololo, iliyoandaliwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Ripoti ya Timu Maalum ya Uchunguzi Iliyoteuliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) Kuchunguza Mazingira Yaliyopelekea Kuuawa kwa Mwandishi wa Habari Daudi Mwangosi Septemba 2, 2012 Katika Kijiji cha Nyololo, Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa, iliyotolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

“Kwa upande wake, Jaji Lyimo aliteuliwa tarehe 28 Machi 2007, mwaka mmoja kabla ya muda wake wa kustaafu kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, ilipofika tarehe 26 Oktoba, 2007 Katibu Mkuu Kiongozi wa wakati huo Phillemon Luhango alimtaarifu Jaji Mkuu kwamba Rais Kikwete “... ameamua kusogeza mbele muda wa kustaafu wa Mhe. Jaji Vincent Kitubio Damian Lyimo ... kwa miaka mitatu ... kuanzia tarehe 28 Machi 2008, siku ambayo angestaafu kwa lazima.”

“Uteuzi wa Majaji hawa na wengineo wenye sifa kama hizo ulilalamikiwa mno na majaji wengine kiasi kwamba ‘Kikundi Kazi kwa Ajili ya Kuchambua na Kushauri Kuhusu Ajira ya Majaji Baada ya Kustaafu’ chini ya Ofisi ya Rais, kilihitimisha, katika Taarifa yake tarehe 7 Machi 2008, “inaonekana wazi kuwa suala la ajira za mikataba kwa Majaji ambao wamekuwa wakifanya kazi za Jaji baada ya kufikia umri wa kustaafu ni kinyume cha Katiba.”

“Sasa Majaji hawa ndiyo wamepewa jukumu la kuchunguza matukio ya ukiukwaji haki za binadamu ambayo hayana mfano katika historia ya Tanzania tangu uhuru. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina imani yoyote na uteuzi wa Majaji Ihema na Lyimo na inapendekeza uteuzi wao ufutwe na majaji wenye sifa bora zaidi wateuliwe kwa ajili ya kazi hii muhimu. Vinginevyo matokeo ya Tume ya Msumi hayatakubaliwa na umma wa Watanzania.”

Mheshimiwa Spika,

Tuliyoyasema mwaka jana kuhusu Tume ya Jaji Msumi sasa yametimia. Licha ya Tume hiyo kukiri kwamba kulikuwa na mauaji, utesaji na vitendo vingine vya kinyama dhidi ya Watanzania wasiokuwa na hatia yoyote, Tume hiyo 'imewasafisha' Mawaziri na 'wakubwa' wengine waliowajibishwa na Bunge lako tukufu kwa kushindwa kusimamia idara au taasisi zao zilizohusika na mauaji na unyama huo. Watanzania waliuawa na kuteswa na mali zao kuharibiwa au kutwaliwa kwa nguvu lakini hakuna mkosaji na hakuna atakayewajibika kwa mauaji hayo. Hapa ndipo CCM ilipoifikisha nchi yetu baada ya zaidi ya nusu karne ya utawala wake. Wakati umewadia wa kuondoka na utawala wa aina hii. UKAWA, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, ndio tumaini pekee la Watanzania!!!

Tundu Antiphas Mughwai Lissu
**MSEMAJI & WAZIRI KIVULI, WIZARA
YA KATIBA NA SHERIA**

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawaita wafuatao wataendelea kuchangia hotuba hii. Atanza Mheshimiwa Aliko Kibona, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo.

Mheshimiwa Kibona!

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, nipende kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mtu wa kwanza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, mchana wa leo. Niwapongeze wote; Kamati mbalimbali zilizohusika na uandaaji wa hotuba hizi, lakini kusema kweli kwa mara ya kwanza kuna maeneo ambayo mbele ya safari tutakapofika kwenye vifungu nitaomba pia ku-consult Waheshimiwa kama Tundu Lissu ili wanisaidie. Kuna jambo ambalo linanikera, nataka kufahamu ni namna gani nitaweza kupata haki yangu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ileje imeanzishwa muda mrefu sasa umepita na mchakato wa uanzishwaji wa Wilaya, asubuhi ya leo kwa mfano, tumesikia jirani yangu mmoja akizungumza juu ya uanzishwaji wa Wilaya. Kuanzisha Wilaya kuna taratibu zake, mchakato ni mrefu wa kisheria, baada ya kukamilika vyombo mbalimbali vinahitajika kuwepo katika Wilaya ile.

Mheshimiwa Spika, kule Ileje nimezungumza kwa muda mrefu sana. Nimeanzia na Mheshimiwa Chikawe akiwa Waziri, kuomba Wilaya ya Ileje itendewe haki hasa upande wa Mahakama! Kuwepo kwa Hakimumu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, nashangaa nilijibiwa na Mheshimiwa Waziri kwamba Wilaya ya Ileje itapewa chombo cha usafiri, naanza na chombo cha usafiri (miundombinu). Baada ya kupewa taarifa hiyo nilifurahi, gari hili nimelitafuta kwa kupiga kelele mpaka mapovu yamenitoka hapa Bungeni, lakini nimekwenda kule Jimboni kwangu nimewauliza wahusika gari liko wapi? Nimeambiwa na Mheshimiwa Waziri kwamba gari limekwenda Ileje!

Mheshimiwa Spika, maajabu naambiwa kwamba, ni kweli gari limekuja, lakini halipo hapa liko Mbozi. Nimeuliza kwa nini liko Mbozi? Wameniambia eti Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Ileje hayupo. Aliyekuwepo amekwenda wapi? Alikimbia, alikataa kukaa Ileje!

Mheshimiwa Spika, hapa nadhani kuna ombwe la utawala bora katika Mahakama. *They are still in the box!* Wanatumia taratibu zile za zamani za Kijerumani au za Kiingereza ni za zamani.

Mheshimiwa Spika, kule Ileje kuna Idara ya Polisi, kuna Idara ya Magereza, kuna Idara ya TAKUKURU, kuna Idara ya TRA, Uhamiaji, Benki, Posta, TANESCO na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, je, iwapo mtu wa Magereza atasema anakataa kukaa Ileje eti kwa sababu, wafungwa ni wachache! Benki watasema tunafunga Ofisi ya benki eti kwa sababu, wateja ni wachache! Polisi wakasema wahalifu ni wachache! Inawezekana Mkuu wa Polisi akasema nahama Ileje kwa sababu, wahalifu ni wachache?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapo kwa kuokoa muda tutatoka hapa nitajaribu kuwa-consult wataalam, labda nitashika shilingi na sitakubali! Ni ngumu sana unapochangia hatua kama hii unakuwa na mtu ambaye anaongoza Taasisi au Wizara ambaye una mahusiano naye ya kiundugu!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kusema kweli ni mtu wa karibu katika mambo ya kifamilia, lakini kwa hili naomba ajiandae kunijibu sawasawa! Vinginevyo atakapokuja ku-wind up awe amewasiliana na wahusika na gari limekwenda Ileje.

SPIKA: Tunaomba mambo yenu ya familia huko huko! Hapa ni Waziri.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kuna mama mmoja kule Ileje peke yake Wilaya nzima wa Mahakama ya Mwanzo. Anapanda pikipiki umbali wa kilometa 90 kwenda kuhudumia Mahakama za Mwanzo! Eti Hakimu Mfawidhi amekumbatia magari mawili anakaa nayo Vwawa, Mbozi! Hii naomba na wewe ikuguse uanze

taratibu kunihurumia na kuwahurumia watu wa Ileje. Mheshimiwa Waziri na watendaji, hili nataka majibu gari liende Ileje.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwenye eneo moja tu, ingawa kwangu halijaguswa, naamini litakuja siku zijazo; ujenzi wa nyumba za Mahakama. Kwenye eneo hilo nawapongeza, lakini pia, nitahitaji kuwepo na nyumba kule Ileje maana sasa huyu Hakimu aliyekimbia mara ya kwanza moja ya vigezo aliorodhesha vigezo ni pamoja na nyumba. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo, najua sasa hivi haiwezekani, lakini liingizwe katika bajeti ili kuhakikisha kwamba Ileje tunapata jengo au nyumba ya kukaa Hakimu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Haki za Binadamu. Watu wapo kule Ileje Jimboni kwangu na maeneo mengine kwa kweli, wanatembea umbali mrefu kwenda Wilayani ambapo wakikutana na matatizo ya kesi zinazohusiana na kuonana na Hakimu wa Wilaya. Naomba kitendo cha wananchi kutembea umbali mrefu wa kilometa zaidi ya 100 au 90, hii si kuwatendea haki! Ni uvunjifu wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kwamba nililenga sana kulia kilio changu kwenye upande wa changamoto za usafiri au za huduma ya Mahakama ya Hakimu Mkazi kule Ileje.

Kwa hiyo, naishia hapa nikiamini kwamba, sasa hivi tunavyokwenda kukaa, Mheshimiwa Waziri au watendaji wake wataniandalia majibu sahihi juu ya jambo hili. Ahsante sana.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imejengeka katika Taasisi mbalimbali, kuna Idara ya Mahakama, kuna Mwanasheria Mkuu, kuna TAKUKURU na nyinginezo, lakini kwa kifupi zote hizi zinazungumzia kulinda na kutetea haki za wananchi wa Tanzania. Niseme kwamba wananchi wa Tanzania wamepoteza imani na vyombo hivi. Na imani kubwa ni kutokutendewa haki sawa kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba dira ya Mheshimiwa Waziri anasema ni haki sawa kwa wote na kwa wakati! Mimi nasema kwamba, anacheza shere, labda tafsiri ya neno hili kidogo haielewi!

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa sana mwezi uliopita nilikuwepo katika Mahakama ya Kisutu. Kule kuna kesi ile ya wanachama wa CUF ambayo inaongozwa na Mwenyekiti wetu, Profesa Lipumba. Profesa Lipumba aliondoka nyumbani kwake saa moja asubuhi akafika saa mbili na nusu pale

Mahakamani, tumekaa Mahakamani pale hadi saa tisa jioni bado washtakiwa hawajaitwa Mahakamani, wako nje wanazurura tu!

Mheshimiwa Spika, katika utawala bora huku ni kuwatesa wananchi. Ni kuwatesa wananchi na kuwadhalilisha na ni kitendo ambacho hakikubaliki. Ingekuwa labda vijana wale wamo katika ukumbi wa Mahakama na kesi zinaendelea kusikilizwa, hata kama ni saa mbili za usiku ningekuwa sina hoja yoyote! Watu wale wako nje hawajaitwa! Hakimu haonekani mpaka saa tisa za jioni na walipoitwa waliondoka saa moja usiku. Hii kwa kweli ni kukiukwa haki za binadamu. Mahakama ndiyo msimamizi Mkuu wa haki za wananchi na leo tunafikia hapa mwananchi wa kawaida atakimbilia wapi?

Mheshimiwa Spika, linapofikia suala hili ni hatari. Ni viashiria vya uvunjifu wa amani, wananchi hawatatahimili utaratibu kama huu ambao unachukuliwa na Mahakama. Wizara hii imepuuza misingi mikuu ya haki za binadamu; misingi ambayo ndiyo inayojenga haki na usawa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kumetajwa hapa katika ukurasa wa 12 wa hotuba hii kwamba kuna kesi 131 ambazo zimefanyiwa uchambuzi na zimefikishwa Mahakamani. lakini Mheshimiwa Waziri ameshindwa kutueleza ni kesi ngapi zimetolewa maamuzi!

Mheshimiwa Spika, rushwa ni adui kwa Taifa hili. Wananchi wote wanasikiliza ni hatua gani imechukuliwa, hukumu gani imechukuliwa? Hadi leo katika kitabu chake anasema kesi zimekwenda Mahakamani tu. Kesi ngapi zimehukumiwa, hakuna maelezo yoyote.

Mheshimiwa Spika, nirejee kusema kwamba kuna wananchi kutoka Zanzibar wamekamatwa kwa sababu ya kontena lile la pembe za ndovu. Wamewekwa ndani kwa muda wa mwaka mmoja na nusu, matokeo yake watu wale walifutiwa mashtaka halafu wamekamatwa tena. Hawa watu ni Watanzania, hata dhamana inashindikana! Walifutiwa shitaka lile, lakini walipotoka nje askari wamekwenda kuwakamata tena.

Mheshimiwa Spika, wale watu wana familia zao, wale watu wana shughuli zao za kiuchumi, ni watu *innocent* mpaka pale Mahakama itakapo-*prove* kwamba hawa ni *guilty*! Watu hawa wanapoteza heshima yao, watu hawa wanapoteza shughuli zao za maisha na familia zao, je, utawala bora uko wapi Tanzania? Tanzania imepoteza taswira ya haki za binadamu na imepoteza taswira ya utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba katika ukurasa wa nne katika dira ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, haki sawa kwa wote na kwa wakati; Wizara hii imeshindwa kutekeleza shughuli zote za uendeshaji wa kesi

mbalimbali. Kuna kesi zile za ufisadi, hakuna mtu ambaye mpaka sasa imeelezwa amefikishwa Mahakamani. Kuna utungaji wa sheria hizi za Katiba, Katiba Mpya hadi sasa hakuna taarifa zozote ambazo zimeelezwa kama ambavyo imeelezwa na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, mimi sielewi! Kuna huyu Mkurugenzi wa PCCB ambaye siku zote ana malalamiko makubwa, anasema kwamba yeye anapokamata kesi na anazipeleka kwa DPP zinafanyiwa uchambuzi, lakini inaonekana kwamba Mkurugenzi huyu haridhishwi na utekelezaji wa shughuli za kesi hizi kwa DPP! Siku zote anapiga kelele kwamba ni vyema angepewa nafasi Mkurugenzi huyu wa TAKUKURU aweze kusimamia kesi zake Mahakamani, lakini hili hakulizungumza Mheshimiwa Waziri na ameliacha huru!

Mheshimiwa Spika, hiki ni kitendo ambacho kinanyima uhuru wa chombo hiki. Kinalalamikiwa sana kwa kila kona kwamba hakifanyi kazi zake, lakini sio kwamba hakifanyi kazi zake. Kazi zake zinazuiwa na zinachujwa na kwa jinsi anavyotaka DPP na Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Waziri, nataka suala hili atakapokuja aweze kueleza ni kwa nini, TAKUKURU wameshindwa kupewa mamlaka haya ya kuweza kusimamia kesi zao ambazo wao wenyewe wamezipeleleza na wao wenyewe wana ushahidi wao na wanaweza kwenda mbele ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba niwasilishe. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa esther Matiko ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai ili leo nichangie japo kidogo kwenye Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze na matatizo yaliyopo Wilaya ya Rorya. Wilaya ya Rorya haina Mahakama ya Wilaya, wale ndugu zangu wa kule wanatoka Rorya wanatembea kuja kufuata huduma hiyo Tarime na kijiografia maeneo ya kule ni mbali sana, wanapata shida, hamna usafiri, wanatembea kwa baiskeli au kwa miguu, kama mtu anashitakiwa anatakiwa kuja Mahakama ya Wilaya ya Tarime na barabara zenyewe ndiyo hivyo tena, miundombinu mibovu.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine Wilaya ya Rorya Mahakama za Mwanzo mbili hazifanyi kazi. Kuna Mahakamaya Mwanzo ya Kinesi haifanyi kazi na ile Mahakama ya Riagoro nayo pia haifanyi kazi. Kwa hiyo, unakuta

wanahangaika kwenda kutafuta huduma hizi za Mahakama ya Mwanzo kwenye sehemu zingine ambapo ni shida sana.

Kwa hiyo, naomba Wizara ya Katiba na Sheria, kwenye bajeti ambayo mmepewa mwaka huu mhakikishe mnatusaidia Rorya, tunapata Mahakama ya Mwanzo kwenye hilo eneo la Kinesi na Riagoro, lakini pia Mahakama ya Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Spika, kingine nije kwenye suala zima la haki za binadamu. Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa, tunajua kabisa kwa mfano kwenye sakata hili la maabara, Waziri wa TAMISEMI alisema Serikali itajenga, lakini na wananchi wataelimishwa bila kulazimishwa! Ni dhahiri DC wa Rorya aliweza kulazimisha na kukamata wananchi wakaenda Mahakamani. Mahakama hizi hizi zikawahukumu miezi mitatu au faini ya 200,000/=! Sasa tukizungumzia kwenye muktadha mzima wa haki, ilhali unajua kabisa watu hawalazimishwi kuchangia maabara kwa mujibu wa majibu hata ya Waziri wa TAMISEMI, ni kwa nini sasa Mahakama inatumika kupoka haki hii au inakubali kutumika kisiasa?

Mheshimiwa Spika, kingine, kumekuwepo na ucheleweshaji wa kesi ambazo inakuwa ni unyimi wa haki za binadamu au za yule ambaye ameshitakiwa. Unakuta mathalani, mtu kakamatwa na kwa kiwango kikubwa kule kwetu Mara unabambikwa kesi, unakuta kesi inachukua zaidi ya miaka mitano, sita, saba. Mwisho wa siku anapatikana hana hatia, umeshampotezea muda wake mwingi tu, umemuathiri kisaikolojia, lakini pia, nguvu kazi ya Taifa na ukizingatia hao mahabusu unakuta hawafanyi kazi. Hata hivyo, kingine ni mapato, maana Serikali inagharimika kuwatunza wale, ilhali mwisho wa siku unakuta hawana hatia.

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi hao wananchi na tumekuwa tukilalamika, basi kama amekamatwa na kesi, kesi iende haraka haraka angalau mwaka mmoja, miwili mtu anajua hatima yake nini, siyo unamweka mtu miaka nane, tisa unakuja unamwachia kwamba hana hatia.

Mheshimiwa Spika, pia tulishawahi kushauri huku kwenye zile kesi za madai ambazo zinaweza kudhaminika, wapewe dhamana wale watu wakae nje kwa dhamana. Ukienda leo kwa mfano Gereza la Tarime limejaa yaani liko *over crowded* wafungwa, mahabusu ni wengi wa kesi zingine ambazo zinadhaminika, lakini wapelekwa kulundikwa kule ndani. Kwa hiyo, naomba Wizara husika iweze kulizingatia hili.

Mheshimiwa Spika, kingine kwenye kipengele hicho hicho cha haki za binadamu, nimeshaleta maswali mengi sana huku Bungeni mengine hadi ukaniambia nilete na ushahidi. Kuna askari mmoja alikuwa anaita afande Bahati wa Gereza la Tabora ambaye alimuua Mzee Daniel kwa kumpiga risasi

kisa ng'ombe wameingia kwenye Hifadhi ya Serengeti. Yule askari alichukuliwa hatua kwamba alikubali kweli ameua, badala ya kupelekwa kwenye magereza kama wengine wenye makosa ya jinai wanavyofanyiwa, yeye akakaa kwenye Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, niliuliza hilo swali humu ndani, aliyekuwa Mwanasheria Mkuu Ndugu Werema akadai watalifuatilia zaidi kuona kwa nini ilifanyika vile. Sasa nataka kujua kama kunakuwa na *double standard* yaani wale wanyonge wanatendewa visivyo wanakaa hata miaka tisa, kumi gerezani, lakini hili tabaka lingine linaua Watanzania wanawekwa kwenye kituo cha polisi miezi minne, mitano bila kuchukuliwa hatua kwenda gerezani kama wale wengine. Ndiyo maana tunaendelea kushuhudia polisi wanaua Watanzania bila hatia hawachukuliwi hatua yoyote ile na haya yamekithiri kwetu kule, mnayafahamu nimekuwa nikilalamika, Serengeti, Tarime, ni kwa nini sheria haifuati haki? Ni kwa nini kunakuwa kuna matabaka?

Kingine tumeendelea kushuhudia askari kwa maana ya Polisi pamoja na kwamba sheria inasema mwanamke au mwanamama au mdada atakwenda kukamatwa au kukaguliwa na askari wa kike, wakati wa sakata hata la viongozi wa CUF, ni dhahiri hata vyombo vya habari vilionesha, mapolisi wanaume walivyodhalilisha akinamama kwa kuwapiga na kuwatupa kwenye magari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa huu utawala wa sheria na haki za binadamu ulitembelea wapi na hao maaskari walikuwa wanaonekana, ningependa kujua wameweza kuchukuliwa hatua gani mpaka sasa hivi? Hata kipindi kile Mheshimiwa Halima Mdee amekamatwa tulishuhudia ni Polisi wakimpiga, lakini pia Mombo kuna maaskari wa kiume walimpiga mwanamama mpaka wakamharibia mimba ya miezi nane, sijui mpaka leo sijui amechukuliwa hatua ipi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea kuona kwamba hawa tabaka lingine wanaendelea kuwanyanyasa Watanzania, lakini Mtanzania mwingine anakamatwa tu hata kwa kutembea barabarani anabambikwa *murder case* na anakaa gerezani kwa zaidi ya miaka nane, sita, saba, lakini hawa wengine wanaendelea kuwaua, kuwanyanyasa na kuwalemaza Watanzania, wanaendelea kuachwa bila kuchukua hatua yoyote ile. Ningependa kujua ni nini kinafanyika na kwa nini hao wengine wanaendelea kuachwa kufanya wanayoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye sheria ambayo tumeipitisha na ambayo kwa kweli nikiwa mwanataaluma nilisikitika kwa sababu ni wingi wingi wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi mliweza kupitisha hii Sheria ya Takwimu. Kiuhalisia hii Sheria ya Takwimu haitekelezeki na inaminya uhuru wa

academicians. Leo mnasema watu wakienda kufanya tafiti hawatakiwi kutoa matokeo ya hiyo tafiti, hawatakiwa ku-*publish* mpaka wapeleke kwenye *Bureau of Statistics*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo najiuliza, juzi tu mnajisifu kwamba mna vyuo vingi, tumeweka wanafunzi wengi, leo wanafunzi mwisho wa siku wanatakiwa wafanye *research* zao, wakishafanya hizo *research* au haya Mashirika yasiyo ya Kiserikali, kwamba wasitoe mpaka nyie mje mzihakiki. Kwanza tukiangalia hii *Bureau of Statistics* ina *manpower* kiasi gani, lakini pia inapata wapi fedha za kuweza kuhakiki kwanza hiyo tafiti kama ni nzuri au imekidhi vigezo vyote ili waipe *go ahead*, kwanza hapo ukiangalia kuna muda utakuwa umepita, lakini pia hauwezi ukatekeleza kwa watafiti zote zinazofanyika nchini. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba kabisa, hiki kifungu kije kifanyiwe marekebisho...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ni wajibu wako wakati ukifika. Mheshimiwa Diana Chilolo, atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu Lissu!

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Naomba nianze kuchangia kwa kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Dkt. Asha-Rose Migiro. Ni ukweli usiofichika kwamba, hotuba hiyo ni mahiri, imejikita vizuri na ukweli usiofichika kwamba Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro ni mama mwenye uwezo, ni mama chapakazi, ni mama wa Kitaifa na wa Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitambue pia uwezo wa Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Naibu Waziri machachali, mwenye uwezo wa kujibu maswali vizuri na vilevile nitambue uwezo wa mtendaji Mkuu wa Mahakama Ndugu yangu na kaka yangu Hussein Katanga, alikuwa ni RAS wangu wa Mkoa wa Singida. Wakati anahamishwa tulitamani kuandama ili abaki Singida, lakini tuliheshimu kwa sababu alipanda cheo. Natambua kwamba hata mdogo wangu Tundu Lissu anatambua uwezo wa watendaji wa Wizara hii, lakini amekiri wazi kwamba wanakabiliwa na tatizo la fedha.

Sasa ndugu zangu Wabunge tuisadie Wizara hii, Wizara hii inatengewa fedha ndogo na hizo fedha ndogo zinazotengwa hazitolewi zote, inafika bajeti inamalizika fedha hazitoki. Ndugu zangu, Wizara hii imebeba mhimili, mhimili unaojitegemea ni vipi mhimili huu unakosa thamani, unakosa kuheshimiwa,

unakosa kuenziwa? Naiomba Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya Wizara hii ili mhimili huu upate heshima inayostahili.

Ndugu zangu Wabunge mwaka jana tulipambana hapa, tulitafuta fedha za maji, tulitafuta fedha za umeme vijijini ambazo hazikuwepo na zikapatikana, hebu tuwasaidie hawa wenzetu wapate fedha ambazo zitawawezesha kutimiza wajibu wao vizuri, mambo yote nitakayoainisha hapa yanakabiliwa na ukosefu wa fedha. Naomba sana Serikali itambue kwamba katika Wizara nyeti ni pamoja na hii.

Mheshimiwa Spika, hivi niwaulize Wabunge wenzangu unapokuwa na ndugu yako ana tatizo la kesi Mahakamani, kesi inaendeshwa miaka mitatu, mitano, hivi ndugu yako anakuwa ana hali gani? Akili yote ya uwajibikaji inapotea kwa sababu kila siku anawaza kesi. Naomba sana Wizara hii ipate fedha za kutosha ili hata Mahakama zetu ziweze kufanya kazi ipasavyo.

Naomba niongelee kuhusu Mahakama za Mwanzo, ni ukweli usiofichika kwamba sasa hivi Mahakama za Mwanzo zina vijana Mahakimu, wasomi, wachapakazi, vijana wenye taaluma iliyobobea lakini vijana wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Majengo hali zake ni duni, yamechakaa, majengo yana nyufa, majengo hayana kiwango chenye kufanana hata na hadhi za hao Mahakimu wala hadhi ya hizo kazi zinazofanywa kwenye majengo.

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali, hivi kweli mmetenga fedha za kuhakikisha kwamba Mahakama hizi za Mwanzo sasa zinakarabatiwa? Naomba sana Mahakama hizi zipatiwe fedha za kutosha ili ziweze kukarabatiwa, vijana hao wasomi waliokubali kufanya kazi katika Serikali yao mpaka vijijini pamoja na elimu walizokuwa nazo, waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri na yaliyoreshwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Mahakama hizi za Mwanzo, Mahakimu bado ni wachache, bado Mahakimu hawa, Hakimu mmoja anapewa Mahakama mbili au tatu, Hakimu huyu anayepewa Mahakama mbili au tatu hana hata usafiri, hivi unafikiri anafanyaje kazi mtu kama huyu?

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali yangu, Serikali naipenda, Serikali naithamini, naitambua, iangalie umuhimu wa maeneo kama haya, tuwasaidie vijana wetu ili waweze kuridhika kufanya kazi vijijini kwa sababu watakuwa wametengenezewa mazingira ya kazi. Nashukuru sana kama Serikali hii itakuwa imenisikia na itatoa majibu kwamba kila Hakimu atakuwa na Mahakama moja, siyo Hakimu kupewa Mahakama mbili au tatu.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu posho za Wazee wa Mahakama. Posho hizi tumeshaongea sana hapa ndani, lakini bado posho hizi ni ndogo na siyo udogo tu, bado zinatolewa kwa kuchelewa, unaniambia mpaka kesi iishe ndipo mtu apewe hiyo posho, hivi kweli tunawatendea haki hawa Wazee wa Mahakama? Naiomba Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kutoa hizi posho za Wazee wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ihakikishe inatoa posho hizi kila mwezi, badala ya kusubiri kesi iishe. Unakuta wazee wanakata tamaa, wengine sasa hivi hata kazini hawaendi kwa sababu ya posho. Hili linawezekana, kama mtu anafanya kazi analipwa mwisho wa mwezi kwa nini na hawa Wazee wa Mahakama wasilipwe mwisho wa mwezi? Naomba Serikali itengeneze utaratibu mzuri posho zianze kutolewa kila mwezi badala ya kusubiri kesi iishe. Mheshimiwa Waziri namwamini, Naibu Waziri namwamini, nina hakika hapo nitapata majibu ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu vitendea kazi vya Mahakimu. Mahakimu hawa ni kweli wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana, hawana usafiri, ukienda ofisini hakuna karatasi, hakuna faili, hakuna meza zenye kutunza kumbukumbu muhimu kama hizo.

Naomba Serikali itenge fedha kuhakikisha kwamba vifaa vinapatikana katika Mahakama zetu zote ziwe za Mwanzo, ziwe za Wilaya, ziwe za Mahakama za nini, sasa hivi hela zinaenda kwenye Mahakama Kuu na wapi, lakini twendeni mpaka chini kwa sababu wote hawa wanafanya kazi zenye umuhimu wa pekee.

Mheshimiwa Spika, niongelee Mahakama za Wilaya. Mahakama za Wilaya Mkoani Singida nilishaongea hapa kupitia maswali. Tuna Wilaya mbili mpya, Wilaya hizi mbili mpya hazina majengo, hazina Mahakimu, nilishaishauri Serikali kwamba basi kwa kuwa Wilaya ya Iramba tuna Mahakama ya Wilaya lakini inafanya kazi kwenye majengo ya Mahakama ya Mwanzo, basi hata Ikungi tutafute hata majengo ya Mahakama ya Mwanzo, tufanye Mahakama ya Wilaya ili tuwasaidie watu wa Ikungi, kuliko wanapopata rufaa kwenda Mahakama ya Wilaya wanaelekea mpaka Singida Mjini, wanatembea safari ndefu, mwendo mrefu, fedha hawana, hata Wilaya ya Mkarama, nao wapate basi Mahakama ya Wilaya. Hata kama watatafutiwa majengo ya Mahakama ya Mwanzo wakati wakisubiri Serikali yao inajenga majengo ya Mahakama ya Wilaya. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumesaidia Wilaya hizi kuendesha kesi zao za rufaa zinazotoka Mahakama za Mwanzo katika maeneo yao ya Wilaya, kuliko hivi wanavyosumbuka kwenda Singida Mjini, Iramba au kwenda mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu Mahakama Kuu. Niipongeze Serikali imetamka wazi hapa kwamba bajeti hii Mkoa wa Singida imetengewa fedha kwa ajili ya kujenga Mahakama Kuu. Ni jambo ambalo nimeshaliongelea hapa mara nyingi, jambo ambalo ni ahadi ya Serikali ya miaka mingi, nashukuru kwamba leo ahadi hii imeingia kwenye maandishi.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali kwa ahadi hii, maelezo haya aliyotoa Mheshimiwa Waziri anasoma yasiwe maneno basi, naomba maelezo haya yatekelezeke, kwa sababu tayari tuna kiwanja, tumejipanga vizuri na Singida ina uongozi mzuri, Mkuu wa Mkoa mzuri, tuna RAS mzuri, naamini tukipeleka fedha hizi hata Hakimu wa Mkoa ni mzuri, nina hakika kabisa usimamizi wa ujenzi wa Mahakama Kuu utakuwa ni mzuri sana. Naomba sana chonde chonde ahadi hiyo itekelezeke.

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu habari za Majaji. Majaji kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana, nina dada yangu ni Jaji Mahakama ya Arusha kule anaitwa Jaji Fatuma Massengi, anafanya kazi nzuri na akaniambia mdogo wangu mwaka huu nimefanya kazi nimemaliza kesi zote nilizopangiwa pamoja na uhaba wa pesa walizonao, lakini wanamaliza kesi zote.

Mheshimiwa Spika, naomba watu hawa tuwafikirie, tuwape heshima zao, tuwaunge mkono, tuwape fedha. Siyo hivyo tu, Majaji hawana ulinzi, wanapata ulinzi pale wanapokuwa na safari ndefu, anatoka Arusha anakwenda Singida, tuwape ulinzi wa kudumu kama wanavyopata Mawaziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Tundu Lissu atafuatiwa na Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Stella Manyanya!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii na naomba nianze mahali ambapo niliishia kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, masuala ya haki za binadamu na Wizara ya Katiba na Sheria ni Wizara muhimu sana katika nchi yoyote ile, mfumo wa utendaji wa haki ukivurugika, nchi haitawaliki, nchi haikaliki na moja ya dalili za mfumo wa utendaji haki kuharibika, ni pale ambapo vyombo ambavyo vimeundwa mahususi kwa ajili ya kusimamia mfumo wa utendaji haki vinapogeuka na kuwa vyombo vya kuhujumu haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili ni maslahi ya Taifa hili yanatutaka tupige kelele sana kuhusu utendaji wa vyombo vyetu vya ulinzi. Waheshimiwa Wabunge tunajisikiaje Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inaposema

kwa maandishi kwamba Jeshi la Polisi ambalo kauli yake ya miaka yote ni ulinzi wa raia na mali zao. Tume ya Haki za Binadamu inaposema Jeshi la Polisi linakiuka haki za binadamu tunajisikiaje? Tunajisikiaje Tume ya Haki za Binadamu inaposema kwamba Jeshi la Polisi linatumika na linaonekana kuwa na upendeleo wa vyama vya siasa. *(Makofi)*

Tume ya Haki za Binadamu ilizungumza mwaka 2012 kwenye uchunguzi wake wa mauaji ya Daudi Mwangosi kwamba Jeshi la Polisi lina upendeleo wa wazi, linapendelea CCM, linapiga marufuku mikutano ya vyama vya siasa vya upinzani, halina shida yoyote na mikutano ya Chama cha CCM. Sisi tunapigwa marufuku tunaambiwa sensa, CCM wanafanya mikutano wakati sensa inaendelea.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu inaposema kwamba Jeshi la Polisi, RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa) ameamuru Mwandishi wa Habari apigwe bomu, amepigwa bomu amekufa tunajisikiaje? Sasa matukio kama haya watu wakichoka hawataogopa Jeshi la Polisi, tukiwafikisha watu wakaamini kwamba hili Jeshi si Jeshi lao ni Jeshi la watesi wao, hii nchi haitakalika na yaliyotokea Njombe jana yanapaswa yafikiwiwe kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita tarehe 14 ya mwezi huu huu Wilaya ya Iramba, viongozi wa CHADEMA wa Wilaya ya Iramba wamepeleka taarifa ya kufanya mikutano ya hadhara ya kisiasa kama ambavyo Sheria ya Vyama vya Siasa inataka kumpeleka taarifa Mkuu wa Polisi wa Wilaya. Kesho yake Mkuu wa Polisi ya Wilaya akawajibu akawaambia endeleeni na mikutano ya hadhara, fuateni ratiba mliyoisema, muda mliousema, maeneo mliyosema msitukane watu, msivunje sheria za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barua hiyo ya OCD wa Iramba imenakiliwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Iramba, anaitwa Lucy Mayenga, ni Mbunge humu. Kesho yake tarehe 16 OCD huyo huyo aliyewaambia CHADEMA Wilaya waendeleo na mkutano, anawaandikia barua kuwaambia nimesitisha mikutano yenu yote kwa sababu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ameamuru kusitisha mikutano yote ya kisiasa Wilaya nzima. Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ni DC Lucy Mayenga, Mbunge humu, ana mamlaka gani Mheshimiwa Waziri unijibu leo, DC ana mamlaka gani kwenye masuala ya mikutano ya kisiasa? Ana mamlaka gani kada wa CCM ana mamlaka gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ambaye ana mamlaka kisheria ya kusimamia masuala ya mikutano ya kisiasa badala ya kutekeleza sheria anafuata maelekezo haramu ya kada wa CCM, anapiga marufuku mikutano, halafu anasambaza polisi na mabomu yao everywhere, ili

watakaotimiza haki yao ya Kikatiba ya kufanya mikutano wapigwe mabomu, wapigwe risasi. Tukisema Jeshi la Polisi limekuwa *armed wing* ya CCM hatukosei, nani atakayebisha?

Mheshimiwa Kikwete aliwaambieni, Mwenyekiti wenu aliwambieni fanyeni siasa msijjegemeze kwa mapolisi, hawa mapolisi hawa mnafikiria ni wa kwenu, kumbukeni yanayomtokea Nkurunziza. Acheni Jeshi la Polisi lifanye kazi ya Polisi, ninyi wanasiasa tukae, tukabiliane kwenye majukwaa, tufanye kazi ya siasa. Sidhani, Mheshimiwa Waziri utanisamehe sana mwalimu wangu, sidhani unaona fahari gani Tume ya Taifa ya Haki za Binadamu inapotoa taarifa kama hii. Ni aibu, aibu kwa wote ninyi. (Makofi)

Sasa haya masuala yaangaliwe, sisi tunaoyapigia kelele siyo kwamba tunafurahi sana, sisi ni wahanga wa Jeshi la Polisi, tumeumizwa na Jeshi la Polisi, hatutaki kuumizwa, tunataka tufanye siasa kama ninyi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa sababu ya muda nizungumze hii habari ya mapesa. Natoka Ikungi, Mahakama ya Mwanzo ya Ikungi ilijengwa 1951, Marehemu Baba yangu alikuwa Karani wa Kwanza wa Mahakama ile, bado iko vilevile. Katika Wilaya nzima ile hakuna Mahakama yoyote ambayo imejengwa tangu mwaka 1961 tulipopata Uhuru, hakuna, Mahakama Wilaya nzima. Sasa vipaumbele vyetu ni nini?

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Wilaya iliyojengwa mwaka 1964 ni hiyo hiyo ihudumie Wilaya ya Singida Vijijini, Singida Mjini, Ikungi, wakati tumejenga maboma ya ma-DC kila tunapoanzisha Wilaya mwaka unaofuata tunaanza kutenga mafungu ya ma-DC. Tumewekeza kwenye *Executive*, tumewekeza katika Utawala, *Judiciary Rule of Law has never been our priority*. Sasa haya masuala tuyajadili kwa utaratibu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa William Ngeleja atafuatiwa na Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed na Mheshimiwa Mohamed Chomboh na Mheshimiwa Assumpter ajiandae!

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam na watendaji katika Wizara hii. Naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu nzuri tu ambazo zimeelezwa katika hotuba yao pia na taarifa ya Kamati kwa kadri ambavyo tumeiwasilisha hapa kupitia kwa Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Rweikiza.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze na nukuu na naomba nianze na nukuu ya msanii mmoja kutoka Marekani. Mwezi wa Pili mwaka 2012 msanii maarufu wa Marekani anayeitwa William Henry Cosby maarufu kama Bill aliwahi kusema katika mojawapo ya maonyesho yake kwamba ili uweze kufanikiwa shauku yako ya kupata mafanikio yapaswa kuwa kubwa kuliko hofu yako ya kushindwa. Nasema haya kwa sababu tumesikia hapa taarifa kutoka kwa wenzetu. Kuna malalamiko mengi lakini kikubwa ni kwamba ukisoma hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri pamoja na taarifa ya Kamati unaona kabisa yale ambayo sisi kama Mbunge tumekuwa tukiishauri Serikali na Serikali imekuwa ikiyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, ukisoma ukurasa wa 6 mpaka wa 13 wa Taarifa ya Kamati utaona, tumesema pale mambo mengi ambayo si Serikali, Serikali imeyatekeleza kutokana na ushauri wa Bunge hili Tukufu. Sasa ni maajabu sana kuona kwamba wapo baadhi ya watu wanasema hapa na wanasimama na kuikosoa Serikali. Kukosoa si vibaya, lakini wanapoisema kwa kusema hii ni Serikali chovu isiyosikia na kuzingatia maelekezo ya Bunge hili Tukufu inashangaza sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema tu kwamba Watanzania waendeleo kutafakari vizuri, siasa ni vita lakini isiyokuwa ya kumwaga damu. Ukumbi huu unatumika kueneza siasa, kuzungumzia siasa, lakini watu kujinadi, lakini Watanzania waendeleo kuchukua uamuzi sahihi kama ambavyo walichukua mwezi Desemba, mwaka jana wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kwa sababu ilikuwa pia ni kipindi cha kujipima na kutathimini uwezo wa vyama vya siasa ambavyo vinakwenda kujinadi kwa wananchi, ushindi wa Chama cha Mapinduzi wa asilimia 81 haukuwa ni wa bahati mbaya ni kwa sababu Watanzania wametafakari.

Mheshimiwa Spika, Wanasengerema wamechangia katika ushindi huo kwa asilimia 83, ni jambo kubwa na tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoendelea kutafakari hii hotuba pia naomba niwakumbushe hawa wenzangu na nanukuu tena kwa mara nyingine, mwanaharakati Marcus Garvey ambaye wanamfahamu sana huyu alikuwa ni Mjamaika, aliwahi kusema: “Kama hujiamini wewe mwenyewe, basi tayari umeshashindwa mara mbili katika mbio za maisha, lakini ukijiamini wewe mwenyewe tayari utakuwa umeshashinda mbio za maisha hata kabla ya kuzianza.”

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi kimekuwa kikijiamini, kinajiamini kwa sababu ya sera zake na kwa sababu ya dhamira yake kwa Watanzania, lakini tunafahamu katika maisha kwa vyovyote vile maisha hayakosi changamoto. Haya yanayosemwa ni changamoto za maisha katika

hali ya kawaida. Taarifa za Tume ya Haki ya Binadamu na mambo mengine na sisi kama wanadamu, Serikali hii ambayo inaongozwa na wanadamu, wakiwa miongoni mwa Watanzania wanadamu katika jamii hii, haiwezekani Serikali hii ikawa na mambo ambayo yanafanywa na watu kama malaika.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ni ya wanadamu haiwezi kuwa timilifu lakini kwa hakika ni Serikali ambayo imedhamiria kuondoa madhila kwa Watanzania. Ndiyo maana tunasema, Chama cha Mapinduzi kwa mabadiliko kinayoendelea kuyafanya, maana yake ni kwamba kiko tayari kutimiza ile kanuni ya maisha, kwamba mabadiliko ni kanuni ya maisha, huwezi kuyakwepa, lakini tunaendelea kwa nia njema kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema haya pia nikiambuka maneno ya Rais wa 35 wa Marekani, Rais John Kennedy mnamfahamu, aliyekuwa anasisitiza sana huo na kuwakumbusha Wamarekani siku zile kwamba, katika maisha hutegemei kuyafanya yote kwa kadiri ambavyo wewe unakusudia. Yapo mambo utakwazika kwa sababu ya mipango ya kibinadamu, lakini zipo changamoto utakutana nazo katika kutekeleza mipango yako uliyokusudia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naendelea kuwasihi Watanzania kwamba tunapojadili na kutafakari maisha yetu katika kipindi hiki ambacho ni kigumu, kina mambo mengi, Watanzania wawe makini sana, tusiamue mambo kwa mihemuko, kwa sababu zipo kauli hapa za mihemuko zinatolewa zinaweza kulifikisha Taifa hili pabaya. Kwa hiyo, tuendeleo kuwakumbusha Watanzania waendeleo kujipanga vizuri na kujiandaa na hasa uchaguzi unaokuja kwa sababu nchi hii tumechagua njia ya kuendesha maisha yetu. Njia hii ni ya kidemokrasia, lakini pia njia hii ni ya kuheshimu utawala wa sheria. Katika kuheshimu utawala wa sheria, kuna sheria ambazo Watanzania wote kwa pamoja tunawajibika kuziheshimu, lakini pia tuna wajibu wa kutekeleza yale ambayo yanatoa haki kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nakusudia kusisitiza kwamba katika kipindi hiki kwa Taifa hili kuna mambo mengi yanajitokeza kati ya sasa na mwezi Oktoba, Watanzania waendeleo kutafakari sana. Pamoja na kuyatafakari yote yaliyoko mbele yetu, tusije tukatoka kwenye msingi mkuu wa kuheshimu utawala bora, misingi ya utawala ambayo inaheshimu sheria. Watanzania tuendeleo kujipa nafasi, tuzisikilize kauli zote zinazotoka kwa kila mmoja wetu, lakini hatma ya yote tusije tukamhukumu mtu yoyote, awe mtu mdogo, awe mkubwa, lazima tumhukumu kutokana na misingi ya kisheria ambazo zinaongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nasema hayo kwa sababu jana nilikuwa nasoma magazeti na kwa sababu ni rahisi sana, tusipozingatia na tusipojikumbusha katika jambo hili, mihemuko inaweza kutuyumbisha Watanzania na hatimaye

Watanzania wakachukua maamuzi ambayo siyo sahihi. Jana kuna taarifa zimeandika kuhusu taarifa ya CAG iliyotolewa. Yapo mambo mengi yamesemwa, lakini naamini katika hatua hii na ndiyo hilo ambalo nalisitiza, Watanzania wajiepuche na mihemuko.

Mheshimiwa Spika, haya yaliyoandikwa hapa hizi ni taarifa ambazo ambazo baadaye zitakuja kujadiliwa katika taratibu zilizokubalika kisheria. Haya yaliyosemwa hapa dhidi ya Serikali kwamba ufisadi huu wa kukithiri katika Serikali, tushukumu Serikali, Serikali hii imetokana na mikono ya watu, tuna taratibu zetu za kuisikiliza Serikali kwanza itakuja ieleze na kujibu haya ambayo yamesemwa na Mkaguzi na Mhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuwakumbusha Watanzania mahali tulipo, Bunge hili Tukufu ni sehemu kubwa sana ya kuwakumbusha Watanzania kwa sababu ni chombo ambacho kimetokana na mikono ya Watanzania, kwamba yote yanayosemwa iwe ni changamoto au ukosoaji zipo taratibu za kufuata, lakini kikubwa ni kwamba, chochote kinachosemwa kama haijafikiwa hatua ya kumshirikisha anayetuhumiwa ikiwemo Serikali yetu ambayo sasa imetuhumiwa kuwa imefuja mabilioni ya fedha, mpaka tutakapokuwa tunawasikia Serikali wakitoa ufafanuzi kwa haya yaliyosemwa, hakuna tuhuma na hakuna kosa lilofanywa na tushukumu Serikali kwamba inafanya ufisadi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalisema hili nikijenga msingi wa kila hatua ambayo itachukuliwa na chombo chochote ama mwenye mamlaka yoyote katika kuamua. Tukiamua nje ya utaratibu wa misingi ya haki, misingi ya kuwapa fursa wanaotuhumiwa kusikilizwa, tusipoipa fursa Serikali yetu, leo kwa tuhuma hizi, tutasema Serikali iwajibike, haiwezi kuwajibika sasa kwa sababu upo utaratibu, muda utafika, Serikali itatoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, sisi hapa tulipo katika chombo hiki, sisi ndiyo tunaogaliwa kwa mfano, waamuzi katika Vitongoji, waamuzi katika Serikali za Vijiji, wenye mamlaka katika ngazi za Wilaya na Mikoa wataangalia sisi tunaamua nini. Sisi tutakaposisitiza kubaki katika misingi ya haki, misingi inayozingatia utawala ya kisheria, msingi wa utawala bora, Taifa litafuata njia hiyo na hatimaye Taifa hili halitagawanyika.

Mheshimiwa Spika, wakati wowote kama kutakuwa na uamuzi ambao utafanywa bila kuzingatia haki, Bunge hili ni wawakilishi wa wananchi, ndiyo hayo yatakayoibua hisia za ukabila, hayo ndiyo yatakayoibua hisia za ukanda, hayo ndiyo yatakayoibua hisia za udini. Naamini kwamba chombo hiki ni chombo sahihi kusisitiza na kutoa mustakabali wa Taifa hili kwamba taratibu zote zinazohitajika zinazongoza mustakabali wa maisha yetu ya kila siku uzingatie sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naendelea tena kusisitiza kwamba naunga mkono hoja hii kwa sababu ina mambo yaliyosheheni, mambo mazuri ambayo ni kwa manufaa kwa Taifa hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ahsante Rais.

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Selasini!

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, lakini pia Mheshimiwa Jaji Mkuu na Viongozi wote bila kumsahau Mbunge wa Heshima wa Wilaya ya Mbinga, Mheshimiwa Katibu Mkuu ambaye ni Ndugu Hussein Katanga.

Mheshimiwa Spika, ninayo kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada na maamuzi ya makusudi ya kuona kwamba taasisi hii nyeti inahitaji kupewa Mtendaji Mkuu na kuwawezesha sasa Majaji pamoja na Mahakimu ku-*concentrate* katika shughuli zao za kisheria za kihakimu, lakini pia masuala ya kiutendaji kuwaachia watumishi wa utendaji na hivyo kuiwezesha sasa kuwa na uwezo mkubwa wa kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimesema hayo kwa sababu nimeona mabadiliko makubwa katika kipindi kifupi cha miaka hii minne. Kwanza kabisa naongea kwa *facts*, kwa *data*, kwa mfano, katika Mkoa wangu wa Rukwa Kamati za Nidhamu na Maadili ya Mahakama, kweli zilikuwepo, zinafanya kazi ya kuangalia matatizo yaliyojitokeza, lakini zilikuwa hazina uwezo wa kutosha kiutendaji, kimaamuzi, lakini tumewezeshwa, tumepewa mafunzo kiasi kwamba sasa tunaweza tukaona ni namna gani tuweze kushughulikia maadili na nidhamu juu ya watumishi wa Mahakama, wakati huo huo kuona kwamba si lazima tu kungojea wakati matatizo yanapojitokeza ni vema kukaa mara kwa mara kufuatilia na kujua wapi hapaendi vizuri na kuweza kufanya marekebisho mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala lililofanyika la kujenga mazingira bora ya kiutendaji. Kwa mfano, hali ya maboresho ya Mahakama, lakini vilevile kuwapa vitendea kazi kama magari watumishi wa Mahakama, naona hilo ni jambo zuri na linatia moyo kwa wale watendaji wa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naona kwamba pamoja na jitihada zinazofanywa na Mahakama, inawezekana taasisi nyingine zikawa ni kikwazo kwa Mahakama hasa katika utoaji wa haki kwa wakati. Mfano, sisi tulikuwa

tumedhamiria kuona kwamba haki za kisheria zipatikane katika maeneo husika kwa wakati, lakini unakuta kuna maeneo magereza hakuna.

Kwa hiyo, unakuta hata wale Mahabusu hawawezi kupelekwa Mahakamani kwa wakati, kwa sababu wanakosa wakati mwingine usafiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inabidi mpaka siku ambapo magereza inapata mafuta, yaani inapata hela za kutosha kuwapeleka hao Mahabusu kwa ajili ya Mahakama. Kwa hiyo, nadhani pamoja na kuiangalia Mahakama, iko haja pia ya kuangalia vikwazo vinavyosababisha Mahakama isiweze kufanya kazi zake vizuri kutokana na maeneo mengine ya Wizara nyingine ambazo zinashirikiana katika kutoa haki.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nizungumzie Mabaraza ya Ardhi. Namshukuru sana na kumpongeza pia Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi. Katika malalamiko mengi ya wananchi wa kawaida eneo la ardhi ni eneo nyeti sana kwao kwa sababu linahusu maisha yao ya kila siku, linahusu uhalisia wa rasilimali zao na utajiri wao. Sasa unakuta haya Mabaraza ya Ardhi kwa mfumo uliopo yanakuwa hayana uwezo sana kiutendaji lakini pia kirasilimali.

Napenda kujua kuna uwezekano gani wa kufananisha au kushirikisha Mabaraza haya ya Ardhi yakawa na mfumo sasa unaofanana na hizi Mahakama nyingine ili kuwe na mtiririko wa moja kwa moja kuanzia ngazi za chini mpaka ngazi za juu katika utoaji wa haki za ardhi.

Mheshimiwa Spika, vile vile haki itatolewa mpaka ngazi fulani ya Baraza la Ardhi, baada ya hapo kwama mteja hajaridhika inabidi akate rufaa katika Mahakama ya kawaida. Gharama za kumwezesha huyu mwananchi kukata rufaa zimekuwa ni kubwa.

Kwa hiyo, naona kwamba mwananchi wanakosa haki zao kutokana na mazingira hayo. Naona niaseme hayo kwa sababu na mimi nikiwa ni sehemu ya wananchi, lakini pia nikiwa sehemu ya Serikali ni vyema kushauri ili kuona tunapata muafaka mzuri katika kusaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naomba elimu pia wawezeshwe hawa wa Mabaraza ya Ardhi kwa kupewa elimu, lakini pia hata vitendea kazi kwa sababu nao wako katika utoaji wa haki. Ikibidi si lazima ingojewe labda Wizara fulani, washirikiane na kuweza kuona hayo yanawezekana.

Vilevile hawa watoa huduma wa msaada wa kisheria katika maeneo ya vijiji watu haki zao wakati mwingine zinapotea hivi hivi kwa ujanja ujanja tu. Kwa hiyo, ningeomba hao wasaidiwe ili kuweza kutoa msaada hasa katika maeneo ya vijijini.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi katika suala ambalo amelizungumzia sana Mheshimiwa Tundu Lissu juu ya Tume ya Haki za Binadamu kuzungumzia isivyoridhishwa na Jeshi la Polisi. Nilifikiri leo yeye ndiyo angesema kwamba vyombo vyetu vinatenda haki, yaani kama Tume inaweza ikaongea waziwazi kwamba haijaridhishwa na Polisi katika hili, basi ina maana Tanzania iko salama, kwa sababu inasema ukweli na inaangalia hapa hatujafanya vizuri, hapa tumefanya vizuri. Kinachotakiwa ni kurekebisha yale mapungufu yanayojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kama Polisi mmoja ametenda vibaya, huwezi kusema Jeshi lote la Polisi liko vibaya, lakini hatuwezi kufumbia macho pale ambapo chombo cha Polisi sehemu moja hakijafanya vizuri, eti tunaogopa kwamba Kambi ya Upinzani au bwana Tundu Lissu atalalamika kwa sababu kwa nini tumesema ukweli, si sawa hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, tuko hapa kwa ajili ya kulinda maslahi ya wananchi wetu, ukweli lazima uwe unasemwa na kuweza kurekebishwa popote pale.

Mheshimiwa Spika, nasema hajaona yanayotokea katika hizo nchi anazozitaja, hajayaona, angeyaona asingediriki kusema hivyo. Tuna kila sababu ya kuvitia moyo vyombo vyetu vya ulinzi kwa sababu havijaajiri Miungu, vimeajiri binadamu wanaotokana na sisi, wengine wanatoka kwenye familia zetu ambazo asubuhi unakuwa, kwa mfano, familia inayotoka kwangu mimi Manyanya mwana-CCM na yenyewe itakuwa kidogo ina kale ka-DNA ka-CCM, lakini inayotoka kwa Tundu Lissu itakuwa ina ka-DNA ka-Tundu Lissu kale ka-CHADEMA, siyo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inawezekana kwa ubinadamu wao wakajikuta nao wanateleza kidogo, lakini tunachotakiwa ni kuwaweka vizuri, tuendeleo kuwafahamisha, kuwaelimisha na kuona kwamba wanatekeleza wajibu wao pasipo kuingiliwa na matakwa ya vyama au watu wengine wengine kutoka maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize sana juu ya amani ya nchi yetu. Kunatokea hii hali ya kuibukaibuka makundi ya hapa na pale, tunayahamasisha sisi. Haya leo bwana mnataka nini, karatasi za kupigia kura zimechelewa, choma jengo moto. Kule Sumbawanga makundi ambayo mimi nina imani yako *affiliated* na chama cha upinzani, CHADEMA, sijui lakini ila mimi nilivyoona ule mtindo wake ulivyokujakuja ulikuwa wa chama hicho, ila sitaki kusema kama ushahidi wa moja kwa moja. Matokeo yake katika zile vurugu vurugu, wakachoma jengo la Afisa Mtendaji, lenye *documents!* Sasa mimi najiuliza, vurugu zetu sisi za kisiasa, tunapoamua kuchoma majengo kama hayo, mle kuna *documents* za watu mbalimbali, makaratasi ya kisheria yako mle, unategemea hawa watu watapata wapi haki zao? Kwa nini tunafikia mahali eti

kwa sababu zangu za kisiasa kuharibu hata ile miundombinu ambayo tayari tumeipata. Kwa hiyo, mimi nadhani pamoja na hamasa tunazozifanya, jamani, sisi Taifa la Tanzania lina tabia zake, Mungu ameliumba yaani ukimuona Mtanzania unajua huyu ni Mtanzania. Kwa hiyo, tuone kwamba hata kama siasa zetu, ziendeshe katika sura hiyo.

Mheshimiwa Spika, juzi tumeenda kule DRC, tumepewa ng'ombe na NGOs za DRC kutushukuru kwa uzalendo wa watu wetu waliokwenda kule kuwasaidia. Sasa kama nchi zingine zinaweza zikaonyesha hivyo, siyo walitupa sisi tuchukue tule, lakini walisema wafikishiwe wale watoto wa marehemu ili kutambua msada na mchango wao, waendeleo kunyonya lakini ni kuonyesha jinsi ambavyo Taifa hili limelelewa na linavyoweza kusaidia na kuona kwamba amani na utulivu vina umuhimu wake katika Taifa. Ninyi leo mnataka kila wakati tufundishane matusi hapa, kila wakati tuchambane tu, tuongee maneno ya ajabu ajabu, hapana, siyo sawa hata kidogo na hiyo siyo kwamba tunaongea katika misingi ya kisheria, sheria inasema lazima tuheshimiane, kila mtu atambue utu wa mwenzake, ndiyo tulivyolelewa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimeona nilisitize sana hilo hasa ikizingatiwa tunakwenda kwenye uchaguzi, ni vyema sana Mtanzania akaendelea kujiona ni Mtanzania bila kujali chama anachotoka na ndiyo maana hata sisi tukitoka humu ndani tunaongea hata tunashauriana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, juzi nilivyoona Mheshimiwa Mnyaa rafiki yangu ameachwa kwenye ile orodha yao nilihuzunika sana, nikasema hawa CUF vipi hawajui kama Mnyaa ni kichwa kabisa wanamuacha lakini upande mwingine nikasema afadhali, wakimtoa Mnyaa, CCM inaendelea kupeta. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, mimi nizidi kuwashukuru na kwapongeza wote na kusema kwamba wote tuchangie kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Lakini wote mwogopeni Mungu siyo kufanya mambo kama hakuna Mungu.

Mheshimiwa Rukia ameomba udhuru, atachangia jioni. Sasa nitamuita Mheshimiwa Joseph Selasini, atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter na baadaye Mheshimiwa Nyambari.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi kuchangia hoja hii. Binafsi sina shida na watumishi wa Wizara wala

watumishi wa Mahakama, ninawapa pole tu kwa kufanya kazi katika mazingira magumu, mazingira ambayo yanawafanya wafanye kazi zao kwa shida kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naposikiliza hoja zinazojengwa na Waheshimiwa Wabunge, kweli naridhika kwamba sasa tunaelekea kwenye uchaguzi, kwa sababu mengi yanayozungumzwa siyo kwa kusaidia kupata mwelekeo wa kusonga mbele lakini kwa kujenga hoja za kutuwezesha kufanya vizuri kwenye uchaguzi ujao. Kusema kwamba kesi ya Daudi Mwangosi imechelewa, siyo kuihukumu Mahakama. Kusema kwamba Jeshi la Polisi baadhi ya watendaji wake wamefanya kazi vibaya, wakawaua Watanzania, siyo kulidharau Jeshi la Polisi. Kusema kwamba kuna Mapadri waliuawa Zanzibar na ni ukweli waliuawa Zanzibar na mpaka sasa hivi hukumu haijatoka, siyo kuidhalilisha Mahakama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge, mambo haya ambayo ni ya muhimu na *serious* kabisa katika Taifa hili tusiyachukulie kisiasa. Kwa sababu Watanzania wanatusikia na wanapotusikia wakati mwingine wanajenga usugu katika mambo ambayo baadaye yanaweza yakaliletea Taifa hili madhara.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba katika suala la haki za binadamu yapo mambo mengi ambayo tunaweza tukazungumza. Kesi zinacheleweshwa Mahakamani na mimi ninachokisema siyo kwa sababu ya Majaji, Mahakimu wala siyo kwa sababu ya Mahakama yenyewe kwa ujumla wake, sote tumezungumza hapa, Mahakama haitengewi fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, mimi mawazo yangu yangechukuliwa, kazi za Serikali nadhani zingepaswa kuwa tatu tu, utawala, ulinzi na usalama na kutoa haki. Kwa sababu mengine yote ujenzi wa barabara, elimu, kilimo, ni mambo ambayo yanaweza yakafanywa kwa kushirikiana na *private sectors* lakini suala la kutoa haki hatuwezi kuliweka rehani. Wako watu wako Mahakamani miaka tisa, nane, mitatu, bila kesi zao kusikilizwa na sababu ni kwamba Mahakimu, Majaji, hawapati fedha za kutosha katika kutimiza wajibu wao. Sasa kusema hivyo, siyo kuitukana Serikali, siyo kuishambulia Serikali, huu ni ukweli, Idara ya Mahakama haitengewi fedha za kutosha ili kutoa na kusimamia haki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini wakati huo, naomba Mahakama za nchi hii ziangalie uwezekano wa kuepuka kutumiwa kisiasa. Kwa sababu zipo kesi Mahakamani kwa muda mrefu tu, Polisi wanawachukua wanasiasa wanawapeleka Mahakamani, halafu unasikia kila siku upelelezi haujakamilika, mtu umemkamata kafanya mkutano mnadai hauna kibali, hivi upelelezi unachukua miaka mitano kukamilika?

Mimi ni mmojawapo wa hao, nina kesi pale Arusha, tangu mwaka 2011 kesi haijakamilika mpaka leo. Ninachokiona Mahakama zetu zinatumiwa na wanasiasa kwa sababu zao. Hili likiendelea, Mahakama zitadharauliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano Jimboni kwangu, nilieleza hapa Bungeni, tulifanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwezi Desemba na Chama cha Demokrasia na Maendeleo tulishinda vijiji 38. Wenyeviti wale wa Vijiji kwa sababu ambazo watawala pale Rombo wanazijua, wamekataa kuwaruhusu wale viongozi kuingia katika Ofisi za Serikali wakidai kwamba ni Ofisi za Chama cha Mapinduzi. Jambo la ajabu ni kwamba baadhi ya viongozi walipoingia katika zile ofisi wamekamatwa, wamepelekwa Mahakamani sasa wanashtakiwa kwa kuvamia ofisi za wananchi. Mahakama badala ya kufanya kazi nyingine za wananchi, sasa zinafanya kazi ya kukiridhisha Chama cha Mapinduzi kwa matakwa ambayo kinayajua.

Mheshimiwa Spika, mimi sina mgogoro wowote na watawala lakini nataka niambie Serikali, baadhi ya Wakuu wa Wilaya katika nchi hii ni kero na baadhi yao ndiyo wanaosababisha hata Serikali kupigiwa kelele ambazo hazistahili. Asubuhi nilitoa mfano hapa wa kilichotokea kwenye Jimbo langu. Mkuu wa Wilaya anasimama, anasema wanaume wa Rombo hawana uwezo, wanashindwa kuhudumia familia zao, wanawake wa Rombo wanakwenda Kenya kutafuta huduma ya ndoa na anaona hili ni jambo la kawaida tu. Jambo hili nataka niwaambie limeleta hasira na sintofahamu kwa watu wa Rombo.

Mheshimiwa Spika, niwaambie ndugu zangu wa Rombo kwamba sisi watu wa Rombo tunajulikana katika mambo mengi ya maendeleo. Nadhani ni Jimbo la kwanza kuwa na shule nyingi za sekondari katika nchi hii, nadhani ni Jimbo la kwanza lenye wafanyabiashara wengi katika nchi hii, nadhani ni Jimbo la kwanza ambalo wananchi wake wanajibidiisha katika kazi katika nchi hii, lakini leo anasimama mtu tu anaamua kutukana Jimbo zima, hata kama kulikuwa na mtu mmoja ambaye amesimama akahojiwa akasema yeye ana matatizo na mke wake au yeye ana matatizo na mume wake lakini siyo Warombo wote, pamoja na Warombo ambao ni viongozi katika nchi hii, pamoja na Warombo ambao wana heshima katika nchi hii. *(Makofi)*

Mimi nataka niseme kwamba wananchi wa Rombo tulieni, jambo hili mimi nitalipigia kelele kwa nguvu zangu zote kwa sababu hii ni kashfa, huu ni udhalilishaji, ni kinyume cha haki za binadamu, sisi Warombo ni watu wazima. Nimepata meseji nyingi sana kutoka kwa vijana, wanasema sasa wataonyesha kwamba kweli wana afya, kwa kwenda kuvamia maeneo mbalimbali. Nawaambia, msifanye kitu hicho kwa sababu watoto wa shule wa Rombo ni watoto wetu na tunataka tuwalee vizuri, wasome kama sisi, wafanye kazi, wafanye biashara na wahudumie Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulisema ni kuhusu kesi za TAKUKURU zinazokwenda kwa DPP. Kuna wakati ulizuka mjadala katika Bunge hili kwamba TAKUKURU wanapofanya upelelezi wa mashauri yao, iletwe sheria ambayo itawaruhusu TAKUKURU kwenda Mahakamani moja kwa moja bila kupita kwa DPP. Matokeo yake ni kwamba tuhuma nyingi ambazo zinawakabili wananchi zinaweza zikapatiwa ufumbuzi kwa muda mfupi na matokeo yake yakaonekana na TAKUKURU ikaonekana kwamba inafanya kazi yake sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kupita kwa DPP unasababisha kesi nyingi za TAKUKURU kuchelewa na wakati mwingine hata kesi nyingine kuachwa kwa sababu tu ambazo hazijulikani na kwa sababu hiyo kuleta picha kwamba kazi inayofanywa na TAKUKURU siyo kazi nzuri. Naomba sana kusema kwamba umefika wakati sasa TAKUKURU ipewe mamlaka na uwezo wa kupeleleza kesi zake na kuzipeleka Mahakamani moja kwa moja bila kupitia kwenye taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kuzungumza kidogo kuhusu mchakato wa Katiba. Wakati tunatengeneza Katiba hapa, ilitokea sintofahamu ambayo ilisababisha baadhi ya Wajumbe wa Bunge la Katiba wakatoka. Ninachotaka kuzungumza ni kauli ambazo zimekuwa zinatolewa na viongozi wetu wa dini. Wote tunaelewa nguvu ya viongozi wa dini zote, Wakristo na Waislam. Ziko kauli zilitolewa nyingi sana hapa ndani kuwabeza viongozi wa dini.

MBUNGE FULANI: Aaah!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nasikia kuna Mbunge nyuma yangu anasema aaah! Kama tunataka amani katika Taifa hili, tusibezane katika mambo ambayo wengine tunazungumza tukiwa na mwelekeo huo huo wa kuiombea nchi yetu amani. Huwezi ukabeza kundi la viongozi wa dini ambalo ndilo lililokamata karibu Watanzania wote kwa pamoja, ukakataa kuwasikiliza, ukafikiria utakuwa salama. Kwa hiyo, bado naendelea kuiomba Serikali katika mchakato huu, tafadhalini sana, angalieni uwezekano wa kuhakikisha kwamba tunamaliza salama mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Assumpter Mshama, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipata nafasi ili na mimi nichangie katika hoja iliyoko mbele yetu. Ninayo shukrani mbele za Mungu na mbele ya Bunge lako Tukufu kupata nafasi hii na

nianze tu kwa kuwapa pole wale Wanakakunyu waliopigwa juzi na nataka kuwaambia asubuhi, Mheshimiwa Mhagama, bado amesisitiza kwamba hilo jambo analishughulikia na litakwisha kabla hatujamaliza Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumkatalia msemaji aliyemaliza kuongea saa hivi. Hakuna mtu ambaye hafahamu nguvu iliyopo katika viongozi wetu wa dini, hakuna mtu ambaye hafahamu kwamba hata hivi tulivyo, tumekuwa hivi, unyenyekevu au kwa namna yoyote kwa ajili ya viongozi wetu wa dini. Bado Serikali yetu inawaheshimu na inachukua hata wakati mwingine mawaidha kutoka kwao ili kuweza kuendesha nchi hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali yetu na Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete bado Mwenyekiti wetu anaamini pasipo kuambatana au kuwa pamoja nao, Taifa hili haliwezi kuendeshwa. Kwa hiyo, napenda tu niwajulishe Watanzania, bado tunaheshimu vyombo vya dini vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaenda moja kwa moja kwenye mchakato wa Katiba. Naomba nianze tu kwa kusema hivi, wakati mimi nagombea kuwa Mbunge, ndiyo wakati huo Chama cha CHADEMA kilipokuwa kinatafuta kura ya kuweza kupewa nafasi ya kuendesha nchi hii. Walikuja wanasema, wao kama watapewa nchi hii siku 100 watakuwa wametupa Katiba. Nami nikawa najiuliza, kwa mchakato wote tuliotumia hata kutengeneza Kanuni, zilipita siku 100, hivi wao wangukuja namna gani? Leo hatujafika hata mwisho, siku mia ngapi zimeshapita, napenda kuwauliza na wakija wangukuwa na uwezo wa kujibu, wangetueleza hizo siku 100 wanguzitemia namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Watanzania nataka niwaambie, katika ile Katiba tuliyokaa na kuiandaa ina mambo mazuri, imeainisha tunu za Taifa, imetoa nafasi 50 kwa 50 kwa wanawake na wanaume, imetoa haki ya kurithi hata mwanamke atakuwa anaweza kuwa na urithi wa ardhi, imetoa nafasi ya mamlaka ya maamuzi....

TAARIFA

MHE. ESTHER N. MATIKO; Taarifa Mheshimiwa Spika.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:..mamlaka ya maamuzi kwamba tutakwenda kuamua nusu kwa nusu, imeachilia nafasi kwa walemavu, imetoa nafasi kwa vijana na kwa wazee. Mimi nashangaa, ni namna gani unaweza ukabeza ile Katiba Pendekezwa. Kama Mungu akitujalia, labda tunachokiomba Mheshimiwa Waziri, wakati huo atakapokuwa anajibu atatueleza ni lini tutaweza kuipigia kura ya 'Ndiyo' ili iweze kuja kwa wakati muafaka tukaweza kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa sheria na utoaji haki. Kwanza nawapongeza viongozi wa Mahakama ambao wamefanya kazi kwenye mazingira magumu, mazingira ambayo kwa kweli ile bajeti yao inakuwa haitoshi. Mimi naomba niseme tukisimamia haki, dawa hospitalini zitakuwepo, barabara zitapitika, mambo mengi mengi yamesimama katika haki, ina maana rushwa haitakuwepo kama tutakuwa tumesimama kwenye haki. Kwa hiyo, mimi ningeomba kwa kidogo hicho walichonacho, japo hakitoshi, maana siyo wao tu, Wizara nyingi hakitoshi, basi kitumieni tu hichocho kwa ajili ya kuleta haki na haki ipatikane kwa wakati. Kwa hiyo, hilo ndilo napenda kuliona linatokea katika masuala ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika maeneo yangu kule Misenyi, hatuna hata Mahakama ya Mwanzo, watu wanatembea kutoka kule Kakunyu, Kashenye, Minziro kuelekea Bukoba kwa ajili ya kesi zao na hiyo yote ni kwa sababu hata ofisi pale Wilayani hamna. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja ku-*windup*, mimi huwa nakupenda sana maana najua wewe ni mchapakazi, hebu jaribu na sisi wana Misenyi kutupatia Mahakama ya Mwanzo ili tuisumbuke. Mtu ana kesi ya kuku fedha zinaishia kwenye nauli badala angebaki hata kuku ziende, inabidi sasa aende kila siku, kesi inazidi kumnyonya kuliko lile kosa ambalo alikuwa anafuatilia.

Mheshimiwa Spika, nina tatizo na *Commercial Court*, maana ya kuwa na *Commercial Court* ni ili tuweze kuharakisha kesi zingine. Nimeshindwa kuelewa, unakuwa na Mahakama ambayo inalipiwa fedha nyingi na nadhani hiyo ilikuwa ni mojawapo ya kuchangia ili Mahakimu wa *Commercial Court* waweze kuwepo kwa wakati na kuhukumu kesi hizi lakini nimeona kesi hizo nazo zinachukua miaka mitatu, minne, sasa maana ya *Commercial Court* inakuwa haipo. Kwa hiyo, naomba yale mazingira yaliyokusudiwa yaweze kuwekwa ili tuweze kuona kweli mlichokusudia kinakamilika. Sioni sababu ya mtu kulipia kesi shilingi milioni saba au milioni kumi halafu kesi ikakaa miaka mitatu, kisingizio kwamba hamna Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea Sheria ya Uchaguzi. Kwa namna hii tunavyokwenda au sasa hivi tulivyo, watu wanapita kwenye Majimbo wanahonga fedha hata hadharani, lakini huyo mtu kesho kutwa anaweza yamkini akafanikiwa akapita. Je, atakapokuwa amepita, hiyo sheria itasemaje wakati amehonga fedha na watu wanaona na ni hadharani na matokeo yake anakuja kupata ushindi. Mimi napenda kujua, hii Sheria ya Uchaguzi inachukua kasi yake namna gani?

Mheshimiwa Spika, naomba TAKUKURU, mnaomba mtu alete video, hivi yule Mwanankaka anayo simu ya kurekodi hizo taarifa anapoona watu wanatoa fedha. Zamani watu walikuwa wanakamatwaje? Kama mmepata ushahidi kwa wananchi, hebu tuondoe yale mambo ya video na rekodi ili watu

wapate haki zao. Hatuwezi kuingiza watu waliotoa rushwa halafu tukapiga kelele ya kusema kwamba eti tutashindana na ufidiaji. Mtu ametoa shilingi milioni mia, shilingi milioni hamsini, unategemea atakapoingia humu ndani si lazima awe fidiaji ili aweze kurudisha fedha zake? Kwa hiyo, ni vyema tuangalie hii Sheria za Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ofisi za Mahakama kama ile niliyokuwa nimeizungumzia, inavuja. Kwa mfano, ile ambayo ipo kama ya kutumia wanakaa nje kwenye kibaraza, kibaraza chenyewe mvua ikinyesha na unajua kwetu mvua inanyesha saa 24, yaani kipindi cha mvua ni kingi kuliko cha jua. Mimi namwomba atusaidie, akakarabati hiyo iliyopo ili angalau watu waweze kupata mahali pa kufanyia hata lile Baraza la Wazee wakaweza kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo mimi ningeomba sana mnisaidie, niombe au nisisitize tu kwamba katika hali hii tuliyo nayo ambapo kila mmoja akisimama anaongelea rushwa, hivi kwa nini tusije na kitu kizito au tukaja na sheria nzito ya mtu akila rushwa na akipatikana adhabu yake ikawa ya kutosha kwa ajili ya wale wengine ili watu waanza kuzuiliwa kuchukua rushwa. Mtu anakuwa kwenye ofisi fulani, anapokula rushwa anahamishwa anakwenda ofisi nyingine au anaharibu hapa anakwenda mahali pengine na huko huko anatenda yaleyale.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mtendaji wetu mmoja amekula mahali shilingi milioni sita akahamishiwa kata nyingine, akala shilingi milioni nane akahamishiwa kata nyingine, akala shilingi milioni kumi, sasa najjuliza ni lini tutakapopata maendeleo. Mtu kama amekula rushwa ionekane kama dhambi ya kuua, huyu mtu akamatwe, afungwe na ikibidi afitiwe na tukifanya hivyo tutaipata haki.

Mheshimiwa Spika, mimi hakna kitu kinaniuma kama ukiona mtu wa kawaida akienda Mahakamani kupata haki yake inakuwa ngumu kama hana chochote, inakuwa tofauti na yule aliye nacho, ndiyo maana zile kesi zinaahirishwa kila siku. Mimi niombe Watanzania mwenye nacho na asiye nacho sheria isimame wote wapatiwe haki kwa usawa. Tukiliweza hilo, barabara zitatengenezwa, tukiliweza hilo hospitalini kutakuwepo madawa, tukiweza hilo hakuna mtu ambaye atashindwa kwenda shule. Watoto wengine baba zao wamefungwa wakati mwingine pasipo haki kwa sababu ambaye anacho ndiye anapatiwa haki. Kwa hiyo, tukiliweza hili nchi yetu itakaa kwa amani.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii, ahsante kwa kunisikiliza. (Makofi)

TAARIFA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilikuwa nataka nimpe taarifa tu mzungumzaji aliyemaliza kwamba CHADEMA tulisema ndani ya siku mia tutaanza mchakato wa Katiba na siku ndani ya siku mia tutamaliza mchakato wa Katiba.

MBUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Hiyo iko kwenye Ilani yetu. Namshauri Mheshimiwa Assumpter akaisome maana kile cha kampeni ulikuwa ume-*panic* husikilizi mambo vizuri. Ndani ya siku 100 tunaanza mchakato, usome vitabu uelewe vizuri, kasome Ilani yetu ya CHADEMA utaelewa zaidi na wengine wote mkaisome ili msindelee kupotoshwa. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, tunaendelea haina uzito. Mheshimiwa Nyambari Nyangwine atafuataiwa na Mheshimiwa Rosweeter Kasikila.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuweka mambo sawa kutoka kwenye taarifa ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu, asiendeleo kuwapotosha Watanzania kwamba walioshiriki katika Bunge la Katiba ni watuhumiwa au wanaohusika na *EPA, Richmond, Tegeta Escrow, Operesheni Tokomeza*, wafugaji na mambo mengine. Huu ni wendawazimu ambao mimi nafikiri Watanzania wasidanganywe. Hapa walishiriki wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyakazi na hata viongozi wa vyama vya siasa. Sasa wakulima kule vijijini au wanafunzi vyuoni walihusika vipi na *EPA*, huo ni udanganyifu. *(Makofi)*

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nataka kulizungumzia ni la udini. Inaonekana kwamba suala la udini linashika kasi sana hasa kwa vyama dhaifu ambavyo havina dira wala sera, vinataka kuegemea kwa viongozi wa dini kuwachonganisha Watanzania. Nitumie nafasi hii kuwaambia Watanzania kwamba wawe makini sana na siasa rahisi ambazo kwa kweli hazina mtaji katika maendeleo au mustakabali wa nchi hii. *(Makofi)*

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba niende moja kwa moja kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Mimi ni mjumbe katika Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala na nimejifunza mambo mengi sana katika Kamati hii.

Jambo la kwanza, napendekeza kwamba lugha rasmi katika kuandika sheria zetu na katika Mahakama zetu iwe Kiswahili na Mheshimiwa Waziri leo amesema, naomba huo mchakato uendelee haraka sana, sheria zetu za nchi hii zitafsiriwe katika lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la rushwa katika Mahakama zetu hasa Mahakama ya Mwanzo na ya Wilaya, rushwa imekithiri sana. Ni jukumu la Watanzania wote kwa pamoja tuungane kukemea rushwa. Rushwa imekithiri kwa sababu baadhi ya watu wamekuwa wapotoshaji au wanataka kufanikisha mambo yao kirahisi wanatoa na kupokea rushwa.

Nasisitiza kwamba ni vizuri sheria kali itungwe ambayo itawabaini wala rushwa na wachukuliwe hatua kama Wabunge wanavyopendekeza kwamba wala rushwa wote wachunguzwe, wakishabainika wakamatwe na wakishakamatwa wapelekwe Mahakamani wahukumiwe na wafilisiwe. Mwisho, Tume ya Kurekebisha Sheria ilete mabadiliko ya Katiba hapa, hata ikiwezekana wanyongwe, hapo ndipo haki itaweza kutendeka katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la ujenzi wa Mahakama hasa katika Mahakama za Mwanzo, Wilaya, Mikoa na Rufaa. Naamini kabisa kwamba tukiamua tunaweza, kwa sababu tumeanzisha Mfuko wa Mahakama tuutumie kuhakikisha Mahakama hizo zinajengwa. Ukimkuta Hakimku katika Mahakama ya Mwanzo, anakokaa, nafasi anayotumia kutoa haki kwa kweli inasikitisha sana. Mimi nashauri kwamba Serikali yetu ijitahidi na wananchi wote washirikishwe ili kuweza kujenga Mahakama katika ngazi za Mwanzo, Wilaya na Mikoa hasa ile mipya. Kwa Mahakama ya Rufaa kuna kiwanja kiko pale Posta, tutenge bajeti ya kujenga Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Spika, niongelee Tume ya Kurekebisha Sheria. Tume hii ina kazi kubwa ya kufanya tafiti mbalimbali ndani na nje ya nchi. Tume hii ndiyo inayoweza ikarekebisha sheria ambazo zimepitwa na wakati na sheria ambazo zinaweza zikaendana na wakati hata kubashiri mambo yanayoweza kuja ni yapi na kuyatungia sheria. Tume hii naomba iwezeshe na ifanye kazi kwa uaminifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu juzi tulisafiri kwenda Afrika Kusini kujifunza, tuliangalia namna kule Afrika Kusini wanavyoweza kufanya kazi kupitia Tume ya

Kurekebisha Sheria. Mimi nashauri hata hapa Tanzania Tume hii ifanye kazi. Ndiyo maana nasema kwamba ilete mabadiliko ya sheria mbalimbali hata wanaosema uwongo katika vyombo mbalimbali kama hapa Bungeni waweze kuchukuliwa hatua. Naamini kwamba Tume hii itafanya kazi kulingana na utafiti utakaokuwa umefanywa na itarekebisha sheria.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la mikataba. Suala la mikataba katika nchi yetu ni tatizo kwa sababu imekuwa na usiri mkubwa hata baadhi ya wananchi wa kawaida kuipata mikataba inayohusiana na rasilimali zao inakuwa ni shida. Napendekeza kwamba mikataba hii iandikwe katika lugha ya Kiswahili, lugha rahisi na lugha ambayo inaeleweka na vilevile isiwe siri sana kwa sababu mikataba hii inawahusu Watanzania, kwa hiyo ni vizuri mikataba hii ikaeleweka. Mfano wa mikataba hiyo ni ya gesi, madini, mikataba inayohusu mafuta na rasilimali nyingine za Taifa. Hali kadhalika, wale wanaoandika mikataba au wanaoingia katika mikataba hii wajengewe uwezo hasa Wanasheria katika Halmashauri zetu hawana uwezo kabisa, hawawezi kufanya uamuzi wowote ule, inakuwa ni shida. Napendekeza Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yake waangalie namna gani ya kuwajengea uwezo wale wanaohusika katika kuandaa mikataba mbalimbali toka ngazi ya Halmashauri mpaka ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie nafasi hii kukosoa sheria iliyopo kwamba katika Halmashauri zetu mkataba ukizidi shilingi milioni hamsini au katika Mashirika ya Umma mkataba ukizidi shilingi milioni hamsini lazima uende kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ukifika huko unachukua muda mrefu sana. Hili ni tatizo kubwa sana katika kufanikisha mambo ya maendeleo katika Mashirika ya Umma na katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba ni vizuri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikawepo katika kila Kanda na katika kila Mkoa ili kufanikisha suala hili lisilete matatizo au lisilete malumbano katika kufanikisha masuala haya yanayohusiana na mikataba, hasa mikataba inayohusiana na wakandarasi na wazabuni ni tatizo kubwa sana katika nchi hii. Kwa hiyo, napendekeza kwamba tuangalie utaratibu wa kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, wakati tulipokuwa katika Kamati ilionekana kwamba Wizara hii au Mahakama haijapewa shilingi bilioni arobaini. Mheshimiwa Waziri naomba atakapokuwa anahitimisha atuambie hizo shilingi bilioni arobaini kama zimeshapatikana. Kama hazijapatikana ana mkakati gani wa kuzipata hizo shilingi bilioni arobaini ili Mahakama ziweze kuendesha vizuri kazi zake. Hali kadhalika atueleze, tangu tulipoanzisha huu Mfuko wa Mahakama mwaka jana, kwa kipindi cha muda wa mwaka mmoja umeleta mafanikio yapi au umekabiliwa na changamoto zipi na ni kwa vipi changamoto hizo tunaweza tukazitatia au tumeanzisha lakini hauna manufaa yoyote yale? Kwa hiyo,

naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja kuhitimisha aweze kulitolea ufafanuzi suala hili.

Mheshimiwa Spika, vilevile ilionekana kwamba taasisi nyingi zilizo chini ya Wizara hii zinatumiya majengo ya kukodi au kwa maana nyingine ya kupanga. Kwa hiyo, nashauri uwepo utaratibu maalum wa kujenga ofisi au majengo katika taasisi hizi. Kwa mfano, kama *RITA* ilivyofanikisha kujenga jengo lake ni vizuri zaidi kwa sababu itasaidia kupunguza gharama za kupanga ambazo ni kubwa sana hata ukilinganisha kwamba ndani ya miaka miwili zile gharama za kupanga tukiamua kujenga majengo yetu yatasaidia na hizo gharama za kupanga zenyewe zinaweza zikafanikisha kujenga majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kuwasisitiza Watanzania kwamba mambo yote yanawezekana na Mahakama ndicho chombo cha kutoa haki, ndicho chombo cha kutafsiri sheria, lakini Watanzania wote haya mambo hayatawezekana kama hatutazingatia sheria, ni vizuri tukazingatia na kuheshimu sheria za nchi. Kokote kule duniani sheria za nchi zinaheshimika sasa unapokuja kubishana na sheria za nchi inakuwa ni ngumu sana kutendewa haki. Unaweza ukatendewa haki au ukasema kwamba umenyimwa haki endapo umevunja sheria za nchi kwa makusudi. Mara nyingi sana watu wengi wanafanya hivyo kwa kuvunja sheria za nchi makusudi ili baadaye waje kusema kwamba Serikali imechoka, sasa ikianza kuwashughulikia ndiyo wanaanza kulalamika sana. Nashauri Serikali iendeleo kusimamia sheria za nchi, sheria za nchi ziheshimike sana na ziheshimiwe kokote kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mkosamali unachangia hakuna cha taarifa hapa, uvumilivu unatakiwa maana ninyi mmesema wenzenu wakanyamaza na ninyi sikilizeni. Sasa naomba uchangie hakuna cha taarifa hapa. *(Kicheko)*

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nataka niendeleo kuchangia lakini niseme tu kwamba kwanza neno wendawazimu si neno la Kibunge. Hata hivyo, kusema kwamba wahusika wa *ESCROW*, *EPA* na kadhalika walikuwa kwenye Bunge la Katiba ni jambo ambalo ni la kweli. Chenge ndiye aliandika hii Katiba Inayopendekezwa, kwa hiyo ni jambo la kweli. Mwandishi alikuwa kwenye *ESCROW* na wala siyo mambo ya uongo, ni mambo ya kweli na kila mtu anajua. Watu wa *EPA* na wengine wote walikuwepo kwenye Bunge hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichangie kama ifuatavyo. Moja, nchi yetu ina historia nzuri na sisi kwenye baadhi ya mambo huwa tunawapongeza sana. Miaka ya nyuma nchi nyingine kama Zimbabwe, Afrika Kusini, Malawi walikuwa wanakuja kujifunza nchini kwetu namna ambavyo tunaendesha

mambo yetu. Leo ni ajabu, ni aibu, nchi kama Zimbabwe inatunga Katiba vizuri mwaka 2013, inashirikisha vyama vyote vya upinzani vinasaini, taasisi za dini zinaridhika, sasa leo tunavyokwenda kwa *trend* hii Zimbabwe watakuja kujifunza kitu gani kwenye mchakato wa Katiba wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, Malawi walikuwa wanafanya hivyo hivyo, wametunga Katiba vizuri, ni shirikishi. Afrika Kusini walikuwa hapa, tunawasaidia, leo wao wanatunga Katiba wanaelewana na vyama vyao, sisi tunapigana, tunafukuzana na kubezana na watu wanasimama hapa wakidanganya watu kwamba Katiba hii itakuwa Katiba ya miaka hamsini, itakuwaje Katiba ya miaka hamsini mmetunga chama kimoja? Hayo mabilioni ya fedha mnayotumia mkijua kabisa kwamba *document* hii haina maridhiano, chama hiki mmepata shida kubwa sana. Mnasikia kabisa viongozi wote wa dini wanasema waumini wao wapigie kura ya “Hapana” hii Katiba Inayopendekezwa, ninyi mnalazimisha, halafu mnajigamba oooh, tumeshinda vitongoji asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, mimi niwape tu taarifa. Mwaka huu mwezi wa kumi hiyo asilimia 81 ya Serikali za Mitaa ndiyo itakuwa asilimia themanini na moja ya Wabunge wa Upinzani. Hakuna uwiano wa mtu kushinda vijiji, kwanza mmefuta wagombea kwenye maeneo mengi, hizo takwimu mnazitoa wapi, mnasema wamepita bila kupingwa wakati Kanuni za Uchaguzi hazisemi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Machali ameshinda Ubunge, Jimbo lake likiwa na mitaa minne tu lakini ni Mbunge. Sasa wewe Mheshimiwa Ngeleja sasa hivi Jimbo lako asilimia 17 iko Upinzani, jiulize kwamba hiyo asilimia 17 imetokaje, mwaka 2010 ulikuwa nayo? Sisi tumeshinda tulikuwa na vijiji?

MBUNGE FULANI: Hapana.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Hatukuwa navyo! Kwa hiyo, suala la Uchaguzi Mkuu na *issue* ya vijiji havihusiani. Wananchi wametuelewa sana hii miaka mitano, *mme-prove failure*. Mahakama hamuwapi bajeti yao, mnategemea hawa Majaji wetu, Mahakimu watafanyaje kazi, miaka yote mnawadanganya na mnatoa habari za uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tutaendelea na *trend* hii ya kutumia Jeshi la Polisi, uchaguzi wa mwaka huu utakuwa na vurugu sana, mtaua wananchi wengi sana. Nchi hii watu wanawashangaa, sisi viongozi wa vyama vya siasa mnatu-*treat* kama ambavyo wakoloni walivyokuwa wanam-*treat* Mwalimu Nyerere na watu wengine waliokuwa wanapigania uhuru wa nchi hii. Sisi wote hapa mnatulaza vyooni, mnatulaza ndani kwa mambo ambayo ni ya kupigania haki za wananchi. Sisi ni Watanzania wenzenu, hamuwezi kupindisha sheria. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukija Jimboni kwangu baadhi ya vijiji wananchi wamechagua upinzani lakini viongozi wale mpaka miradi ya maendeleo, yale maeneo ambayo mmelazimisha kwamba watu lazima watawale bila kuchaguliwa, shughuli za maendeleo hazifanyiki. TASAF wamekwenda kijiji kinaitwa Kumsenga na Kigina wamefukuzwa, wanasema hatutaki hivyo vitu vyenu mpaka tuchague viongozi wetu. Kwa hiyo, kuna migogoro mingi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuna wananchi wangu kwenye kijiji cha Nduta, wamezuiwa kupiga kura watu zaidi ya 2,000. Sasa hivi Daftari la Wapiga Kura limekwenda kule lakini hawajapeleka kituo, mnachotafuta ni nini? Mnazuia watu wasipate haki zao za Kikatiba. Hivi nchi hii mnaipeleka wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama mmekubali vyama vya siasa viwepo msifikirie kutumia nguvu, msifikirie kutumia Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi lingekuwa linaweza kufanya *enforcement* ya sheria, *Legal and Human Rights Centre* wametoa takwimu zao mara kadhaa, sheria zinazotekelezwa kwenye nchi hii ni asilimia thelathini tu, mambo mengine yanaendeshwa kiholela lakini inapofika muda wa kushughulika na vyama vya siasa, kupiga Wabunge, Mheshimiwa Waziri, kweli wewe Profesa wa Sheria unaona Wabunge kupigwa na wananchi ni sahihi? Sasa hivi kasi ya watu kujichukulia sheria mkononi imeongezeka. Mwendesha bodaboda akigongwa wanaamua kuchukua sheria mikono, watu wakiiba ni kuchoma tu, inaongezeka kwa sababu watu hawaiamini hii Serikali, hawaiamini Jeshi la Polisi. Kesi nyingi wanazozifanya Jeshi la Polisi ni za kutuhumu watu mambo ya uwongo. Kwa hiyo, mambo ya haki za binadamu kwenye nchi hii mme-*fail* kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, tunakokwenda kwenye Uchaguzi Mkuu kama mnafikiri mtaweza kutumia nguvu, nawaambia hamtaweza kufanya jambo hilo, hamtaweza! Kwanza hamna Polisi wa kutosha, Wilaya ya Kibondo kwa mfano mna Polisi 100, sasa Polisi 100 watapambana na wananchi 300,000? Kwa hiyo, kama Polisi itaacha kufuata utaratibu watu watachukua sheria mkononi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumekuja kwenye *issue* ya Kura ya Maoni, ni aibu. Uliagiza Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ya Katiba na Sheria iende Njombe wakati wa mkutano uliopita. Mimi ni mmoja wa watu tuliokwenda Njombe, Tume ilituletea ripoti ikasema Sheria ya Kura ya Maoni haitekelezeki, haiwezekani kwa mazingira, ratiba na jinsi mambo yalivyo. Nashangaa hotuba ya Waziri inasema kutakuwa na Kura ya Maoni. Ni nchi gani duniani inaweza kuendesha jambo kubwa kama hili la Kura ya Maoni bila kuwa na uhakika nalo, bila kuwa na ratiba na bila kuwa na sheria ambayo inaeleweka, nchi gani? Waziri anasisitiza Sheria ya Kura ya Maoni akijua viongozi wote wa dini

wamesema Katiba Mpya ipigiwe kura ya "Hapana", anaongozaje Wizara yake? Waziri gani anayepingana na viongozi wa dini? Waziri wa namna gani anapingana na Maaskofu na Mashekhe? Anadhani akilazimisha hiyo Katiba ikapigiwa kura, ikashinda, hao viongozi wa dini unatengeneza nao mahusiano ya namna gani? *This is a failure government*, hii ni Serikali ambayo ime-fail. Ndiyo maana tangu mwanzo nimesema kwamba mchakato wa Katiba ni mchakato ambao kwa kweli ukiutafakari unashangaza, CCM ambao mlikuwa mnashauriana na vyama vingine vimewapita mbali.

Mheshimiwa Spika, haya mambo nilisema hata wakati fulani, sasa hivi dunia tunavyokwenda hatuko kwenye Rais kushika kila kitu, imebaki ni Tanzania, Burundi, Congo na Uganda, basi! Nchi nyingine Rais alishapunguziwa madaraka. Angalia Katiba za *South Africa*, Kenya na nchi za *West Africa* na nchi ndogondogo kama Malawi na kadhalika, wote wamebadilika wanakwenda na jinsi ambavyo dunia inakwenda. Ninyi bado mnang'ang'ania yaleyale. Watu wanapita wanasema ooh hii Katiba imejali mambo ya wafugaji kwenye hii Katiba mfugaji akikosa haki atakwenda wapi? Kuna kifungu cha kwenda Mahakamani mfugaji akikosa haki yake? Kuna kifungu cha kwenda Mahakamani mvuvi akikosa haki? Hakuna kifungu hicho, ni maelezo tu, *remedy* iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, soma Katiba ya Afrika Kusini, mwanafunzi akikosa mkopo Chuo Kikuu kuna haki ya kwenda Mahakamani, watu wanakwenda Mahakamani wakikosa huduma ya afya, Serikali ije *i-prove* Mahakamani kwamba ilikuwa haina uwezo wa kufanya kile kitu, *i-prove* kwamba huyu hakutakiwa kupata mkopo, ninyi mmeyaweka kwenye hii Katiba? Hamjaweka, *mme-fail*, mnapitisha Katiba kwa ubabe, haya ni maridhiano, mmeua nchi, sasa hivi Zanzibar ina Katiba inayotofautiana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Serikali gani hii? Watanzania sisi hatuongeti na hawa hapa Bungeni, kwanza hata tukiwashauri hawasikii, *they can't listen*, ni watu ambao wamechoka na wanalishangaza Taifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru!

SPIKA: Hivi wewe wangetaka kukutolea taarifa si wangeweza, lakini wamenyamaza. (*Kicheko*)

Sasa namwita Mheshimiwa Rosweeter, Mheshimiwa Lucy Nkya muda hautoshi.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ili na mimi nichangie machache katika Wizara ya hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri lakini pia na watendaji wengine katika Wizara hii ambao usiku na mchana wanafanya kazi ngumu pamoja na kuwa na upungufu mkubwa wa watumishi na ufinyu wa bajeti. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na mengi sana ya kuzungumza kwa sababu mengi kuhusu Wizara hii nimekuwa nikiyazungumzia kwenye maswali niliyokuwa nikiuliza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 24 amezungumzia changamoto nyingi anazozipata kwenye Wizara yake lakini moja ya changamoto alizozitungumzia ni upungufu mkubwa wa watumishi. Nami pia nasema kweli Wizara hii ina upungufu mkubwa sana wa watumishi kwa maana utakuta Halmashauri zetu nyingi hazina wanasheria kinyume na wenzao wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya na Wizara ya Kilimo ambazo zina watumishi mpaka kwenye ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikitoa ushauri kwamba ingekuwa ni vizuri Wizara hii ya Katiba na Sheria wakafikiria kuajiri Wanasheria hadi kufikia ngazi ya Kata. Kwa sababu kwenye ngazi ya Kata kama tutakuwa na Mwanasheria ataweza kufanya kazi ya kuelimisha wananchi katika vijiji vyote vilivyo katika Kata yake na anaweza akawa ni Mjumbe wa WDC akawa anawaelekeza hata Wajumbe wa WDC mambo mengi yanayohusiana na sheria.

Mheshimiwa Spika, pia, tukiwa na Mwanasheria kwenye ngazi ya Kata anaweza akashirikiana na Watendaji wa Vijiji, anaweza kuwa anaomba hata mikutano ya hadhara kwa Mtendaji wa Kijiji na katika mikutano hiyo ya hadhara akaenda kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria mbalimbali kwa sababu kuna sheria nyingi sana ambazo wananchi wanahitaji kuzifahamu kwa mfano, Sheria ya Ardhi, Sheria ya Ndoa na nyingine nyingi sana.

Sasa wananchi wanapokuwa hawazifahamu hizi sheria ndiyo inaleteleza kuwa na kesi nyingi sana zinazorundikana Mahakamani na ukienda Mahakamani utakuta kuna kesi ambazo pengine wala hazikuhitajika kwenda huko. Mfano mdogo tu, mtu anaweza akapita mbele ya Mahakama wakati kesi zinaendelea akapiga kelele, kisheria ni kosa kubwa sana lakini mwananchi huyu angekuwa ameelimishwa asingeweza kupiga kelele mbele ya Mahakama na pengine asingekamatwa na kuwekwa ndani hata kama ni kwa mwezi mmoja.

Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametaja Chuo cha Uongozi wa Mahakama (*IJA*) kilichopo Lushoto na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo.

Kwa maono yangu naona kwamba Wizara ina upungufu wa vyuo. *IJA* na hii taasisi nyingine haiwezi kutoa watumishi wanaotosheleza. Kwa hiyo, natoa ushauri kwamba wangejitahidi basi hata kama katika mwaka mmoja wawe wanajenga chuo kimoja au vyuo viwili ili hatimaye wawe na vyuo vingi. Kwa mfano, ukichukulia Wizara ya Afya ina jumla wa vyuo 77 na vyote vinatoa watumishi ambao wanakwenda mpaka vijijini. Ukiangalia Wizara ya Kilimo ina vyuo kama nane vinatoa cheti na diploma, ukiangalia Maendeleo ya Jamii wana *FDCs* kama 55 na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii nane.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara ingefanya jitihada ili kupata watumishi kwa wingi kwa sababu ukiangalia kila Wizara inatakiwa iwe na Mwanasheria angalau kila Mkoa na kila Wilaya iwe na Mwanasheria kwa maana ya Halmashauri. Kwenye Kata kama nilivyozungumzia, tuna Kata nyingi sana na huko kote kunahitajika Wanasheria maana tunasema utii wa sheria bila shuruti, lakini wengine hawawezi kutii sheria bila shuruti wakati hawajui kwamba jambo hili linakatazwa. Mfano mdogo tu, kuna mwananchi alimkuta mwenzake shambani anang'oa muhogo, kwa sababu alimkuta *red-handed* akasema hii ni haki yangu kwa hiyo akamkata sime. Kumbé yeye angejua kwamba kinachotakiwa ni kumkamata na kumpeleka kwenye vyombo vya dola ingemsaidia zaidi lakini aliishia kukamatwa na kupelekwa Mahakamani na kufungwa kwa sababu alijichukulia sheria mkononi.

Mheshimiwa Spika, tunasema kinga ni bora kuliko tiba, najua kabisa wananchi wakifundishwa hizi sheria mbalimbali mpaka kwenye *grassroot level* itasaidia sana. Kuna wakati, niliwahi kuuliza swali hapa kwamba kwa nini wananchi hawafundishwi sheria mpaka vijijini, lakini nikajibiwa kwamba wanaweza kwenda kwenye maktaba wakasoma vipeperushi na kadhalika. Ukiangalia kuna mwananchi hajui kama duniani kuna kitu kinaitwa maktaba. Kama watakusanywa kwa Watendaji wa Vijiji mpaka Vitongojini na Afisa wa Sheria ambaye ameajiriwa kwenye Kata basi watafundishwa mambo mengi na Afisa wa Sheria (*Legal Officer*) atakuwa *consultant* katika mambo mengi sana, hata kwenye Mabaraza ya Kata. Kwa hiyo, naishauri Wizara ifikirie pia kuongeza vyuo kama Wizara nyingine zinavyokuwa na vyuo vingi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Mahakimu. Mahakimu wanaozalishwa na *IJA* lakini sasa hivi tuna vyuo vingi sana vinavyotoa wahitimu wa sheria wa jinsia zote. Tuna vyuo vya UDOM, Mzumbe, Iringa, *RUCO*, Tumaini na vyuo vikuu vingine na vyote vinafundisha sheria na kama vinafundisha sheria wanachuo wao wanahitimu kama Wanasheria wa kawaida hawawezi kuwa Mahakimu mpaka wamepitia *Law School*. Mheshimiwa Waziri katika taarifa

yake amesema kwamba kuna Mahakama za Wilaya na za Mwanzo nyingi tu zinajengwa lakini Mahakimu ni wachache sana. Kwa uelewa wangu nashauri kwamba pengine hii *Law School curriculum* yake kwa nini isitumbukizwe kwenye hivi vyuo vingine vinavyotoa wahitimu wa sharia ili wanapotoka vuyoni wawe tayari wanaweza kuajiriwa kama Mahakamu na kwa hali hiyo hatutakuwa na upungufu mkubwa wa Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia Magereza zetu nchini. Magereza hizi zinafurika sana wafungwa, wengine ni wale wanaokaa miaka mingi kwamba upelelezi unaendelea ili kesi zao zianze kusikilizwa. Utakuta mtu yuko mahabusu miaka miwili au mitatu mpaka minne na siku anapofikishwa Mahakamani anahukumiwa miaka mitano au nane mingine. Ni kwa nini *procedures* za upelelezi zisifanyike haraka iwezekanavyo ili hawa watu wasiendeleo kuishi kwenye magereza na kwa sababu wakiishi huko kwa upande mwingine bajeti kubwa sana inatumika kwa sababu itabidi wapate chakula, matibabu na mambo mengine ambayo wanahitaji.

Kwa hiyo, nashauri kesi zao zingekuwa zinasikilizwa kwa uharaka ili wapate hukumu, wanaofungwa wafungwe lakini wanaotoka watoke ili wakaendeleo na ujenzi wa Taifa. Mara nyingi utakuta mahabusu wanalalamika kwamba wamebambikiziwa kesi labda ya mauaji au kesi nyingine. Naomba haya mambo yaangaliwe ili kusiwe na kubambikiziana kesi. Utakuta kesi nyingi zilizopo Mahakamani pengine ni mtu ameiba kuku, mbuzi, kampiga au kumtukana mwenzake, anajikuta mahabusu kwa muda mrefu sana kitu ambacho ni *unnecessary*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tumekuwa tukiongelea sana Mfuko wa Mahakama pengine Mheshimiwa Waziri katika *winding up* yake angetuambia huu Mfumo una *function* namna gani, kama unaendelea vizuri au hauendelei vizuri.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni hayo machache, nilitaka kuhimiza uanzishwaji wa vyuo vinavyotoa cheti au diploma kwa wingi ili watu waajiriwe mpaka ngazi ya Kata na hata hawa Wanasheria wengine waajiriwe kwenye Halmahauri zetu. Nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya hawezi kuongea kwani zimebakia dakika kama nne tu. Kwa hiyo, tukirudi watakaoanza ni Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed na Mheshimiwa Muhammad Chomboh majina mengine yatatolewa wakati ukifika.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Waheshimiwa Wabunge, msidhani sioni kama watu wanataka kutoa taarifa, wengine wakisema wenzao wamenyamaza basi na wao wakisema nao watanyamaza hivyo.

Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

(Saa 7.55 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Kidawa Hamid Saleh) Alikalia Kiti

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji wetu wa kwanza kwa jioni hii atakuwa Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, atafuatiwa na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed na Mheshimiwa Muhammad Chomboh ajiandae.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha sisi sote kuwepo hapa tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, napenda kutoa pongezi zangu kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri na Watendaji Wakuu wote pamoja na watumishi wa Mahakama kwa hotuba nzuri na pia kwa kujaribu na kuendelea kuwapa Watanzania haki katika mazingira magumu kwa sababu hata bajeti yao imekuwa inalalamikiwa ni finyu na inaonekana hivyo. Nawatakiwa utekelezaji mwema wa bajeti hii ya 2015/2016 ambayo itakuwa na mafanikio na itaendelea kuwapa Watanzania haki ili kuendelea kudumisha amani iliyopo siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue fursa hii kwa niaba yangu na wananchi wangu wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kuongeza idadi ya Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ili Watanzania waendeleo kupata haki yao kwa muda muafaka siyo kama ilivyokuwa zamani unakwenda Mahakama Kuu kwa muda wa miaka 10 kabla hujajua hatima ya haki yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze tena zaidi Mheshimiwa Rais kwamba ameongeza wanawake katika kada hii kuu ya Mahakama, hii inaonyesha wanawake wanaweza na tunajua kwamba wataendelea kusimamia kidete kuhakikisha wanawake na Watanzania wote tutaendelea

kupata haki. Tunamuomba afya njema na baraka za Mwenyezi Mungu ili aendelee kuwaenzi wanawake na wanyonge wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nisisitize jambo moja kwamba hii nchi ni yetu sote. Bunge hili limepewa dhamana na heshima ya kutunga sheria. Sasa unapotunga sheria halafu huzitii, huzienzi na kuziheshimu inakuwa kama unafanya mchezo wa makida kama wanavyosema watoto wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limekuwa matamshi mengi kutoka kwa wenzetu ambayo yanadharau viongozi wakuu wa nchi hii na Serikali lakini mbaya zaidi ni pale ambapo wanachochea wananchi waache kutii sheria na waendelee kupambana na polisi na pia kudharua viongozi wao. Mimi hainiingii akilini pale ambapo unamkuta mtunga sheria ambaye anafahamu kabisa Katiba ya nchi hii na anafahamu sheria zipo zinazotuelekeza sisi raia tutii mamlaka. Nikienda mbali zaidi unakuta hata Misahafu ya dini zote na maadili kwa wale wote ambao hawana dini yoyote inayotamkwa kwenye vitabu wanasema kwamba tutii mamlaka au tutii wakubwa zetu.

Sasa haiingii akilini kiongozi ambaye yuko hapa mwenye dhamana ya kutunga sheria, naomba ninukuu kutoka kwenye hotuba ya Upinzani, anasema; "...kwenye signature issue ya utawala wake, yaani Katiba Mpya, huyu ni Rais aliyeshindwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Rais ameshindwa nini kama tunaendelea kuishi kwenye amani? Huyu Rais ameshindwa nini kama hii nchi imepata maendeleo, tunatembea kwenye barabara zenye lami? Huyu Rais ameshindwa nini kama anaendelea kutu- *maintain* hapa na kuhakikisha sisi kama Wabunge tunapata haki na maslahi yetu kama inavyostahili? Kama ameshindwa basi usingekuwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaendelea kusema kwamba Serikali imeshindwa. Serikali iliyoshindwa ni ile ambayo haina utawala wa sheria, wala hakuna amani katika nchi. Serikali hii haijashindwa, tuna amani na kuna utawala wa sheria katika nchi yetu ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, sisi viongozi tunaotunga sheria tunatakuwa kuwa *role models*. Unapozungumza lugha ya kudharau tu, huyu kijana ambaye unasema afundishwe uraia ajue maana ya Serikali, maana ya kutii mamlaka na namna ya kutunza amani na kutii wale wote ambao wanalinda amani katika nchi hi, unamtaka afanye nini kama wewe unashindwa kuwa mfano wa kuigwa? Hii nchi ni yetu sote, wote tunawajibika kutunza amani, kuwalea vijana wetu kwenye maadili mema ili tuendelee kuwa na viongozi wenye maadili watakaolinda amani na ninaamini

kwamba kwenye amani ndiko kuna maendeleo na mafanikio ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, napenda sasa kwenda kwenye mada yetu ya leo. Katika mada yetu ya leo kitu ambacho nimekiona ni muhimu kukizungumzia na nimefurahishwa nacho ni pale ambapo Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametambua kwamba msaada wa kisheria ni muhimu kwa Watanzania hususan wale ambao ni maskini na wasiojiweza. Kumekuwepo na msaada wa namna hiyo lakini kwa kiwango kikubwa unaenda kwa wale ambao wana kesi za mauaji. Naomba Waziri ajue kwamba kuna Watanzania walio wengi wanaotoka vijijini wanakwenda kwenye Mahakama za Wilaya, Mkoa na Mahakama Kuu mara nyingine unakuta kwamba Mawakili na Hakimu wanazungumza Kingereza wala hawajui *procedures* za kuendelea na kesi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hivi, kwa sababu kuna mashirika machache sana yenye kutoa msaada wa kisheria na mashirika haya yanategemea sana misaada ya wafadhili, Serikali iangalie namna ambavyo hawa watakuwa ni *partners* wa Wizara hii katika kulinda na kuwasaidia wananchi ili waweze kupata haki. Kuna vijana wengi mitaani ambao wamesoma sharia, tunaomba wasaidiwe ili waweze kutumika katika kutoa elimu ya sheria na kuwasaidia wananchi ambao wanahitaji msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuzungumza ni kuhusu RITA. RITA ina wajibu wa kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata vyeti vya kuzaliwa, vifo na vyeti vingine. Napenda niongelee vyeti vya kuzaliwa. Kuna mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa yanasaidia wanafunzi vijijini kupata vyeti vya kuzaliwa lakini sehemu nyingine unakuta ofisi za RITA kwenye Wilaya hazitoi ushirikiano. Mimi naomba hili liangaliwe ili RITA ishirikiane na haya mashirika na zaidi ishirikiane na Serikali za Vijiji kuhakikisha kwamba watoto wanaozaliwa wanapata vyeti vya kuzaliwa. Hii itatusaidia pia kulinda Utanzania wetu ikiwa tutahakikisha watoto wote wanapata vyeti, wahamiaji haramu hawatapa *loophole* ya kujipatia vyeti na kujiita Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie Mahakama za Mwanzo. Mahakama hizi nyingi zimekuwa kwenye hali mbaya, Mahakama yangu ya Ngerengere inawadondokea Ma-assessors vichwani vipande vipande, tumeiwekea *support* ya miti na mbao lakini sijaona *effort* yoyote ya kusema kwamba tunajenga pale. Hakimu ni mmoja, anashughulikia Tarafa za Ngerengere na Mvuha. Sasa kwa njia hii kesi zinarundikana na Watanzania wanakosa haki zao, pia ma-assessors wanalalamikia posho zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuzungumzia ni Mahakama ya Ardhi. Mahakama hii inaanzia kwenye ngazi ya kijiji, inakwenda

kwenye Kata halafu Wilaya. Hawa wa kwenye ngazi ya kijiji wengi hawajui hata Sheria ya Ardhi inazungumzia nini. Naomba Wizara iangalie namna ambavyo watashirikiana na TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ardhi kusudi hawa wanapochaguliwa na ile Kamati yao wapate mafunzo ambayo yatawaongoza kidogo ili waweze kutoa haki kupunguza mrundikano wa kesi katika Baraza la Ardhi la Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni wafungwa. Wafungwa wengi hawajui kwamba wana haki ya kuomba rufaa na wana haki ya kusaidiwa ili waweze kuomba rufaa. Tunaomba wasaidiwe ili mrundikano wa kesi upungue.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naitakia Wizara kila la kheri katika kutekeleza bajeti yao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuita Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed na Mheshimiwa Chomboh jiandae.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ili niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii yenyewe ya Katiba na Sheria imeshindwa kusimamia sheria katika nchi hii. Hii ni kusema kwamba Mheshimiwa Waziri huyu amefeli. Nasema haya kwa ushahidi, kwa sababu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda katika Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2013 walisema kwamba, alivunja sheria pale aliposema kwamba, watu wapigwe tu yaani piga tu. Kauli hii ilivunja haki za binadamu na Wizara hii imeshindwa kumkemea hadi hii leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maneno haya aliyoyatoa ya 'piga tu' yalizalisha Operesheni Kimbuga na Operesheni Tokomeza jambo ambalo liliathiri sana kwani watu walipigwa, waliharibiwa mali zao na wengine walibakwa. Kwa mujibu wa ripoti hii inaonyesha watu 1,669 walikufa katika operesheni hii na mambo haya yote yalizalishwa na kauli hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, Mheshimiwa Waziri ilikuwaje mpaka leo mkashindwa kukemea jambo hili ambalo limetoka hata katika Ripoti ya Haki za Binadamu? Kwa hiyo, ni kusema kwamba, Mheshimiwa Waziri mmefeli katika kusimamia haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuna sheria kandamizi zilizotolewa na ripoti ya Jaji Nyalali lakini mpaka leo Serikali imeshindwa kuzifuta na Wizara hii inahusika. Ni kwa nini mpaka leo jambo hili halijachukuliwa hatua kwa kuzifuta sheria hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nataka Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi wa hali ya juu kwa sababu jambo hili limetuathiri Wazanzibari wote, tena siyo watu wa vyama fulani ndiyo walioathirika, ni vyama vyote na kwa kweli limetuumiza Wazanzibar wote kwa ujumla. Zanzibar kuna Mahakama ya Mwanzo, Wilaya, Mkoa na Mahakama Kuu, ilikuwaje mpaka Mashekhe wakachukuliwa wakaletwa Bara? Tunaomba ufafanuzi, Waziri atuambie ilikuwaje Mashekhe wakachukuliwa wakaletwa katika Mahakama ya Bara? Ni kwa nini wakati Zanzibar Mahakama zipo? Jambo hili limetuathiri kwa kiasi kikubwa na mimi nawaambia kama hamkulishughulikia hili ndiyo kaburi la CCM mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashekhe ni watu ambao wanasikilizwa na kukubalika katika jamii. Leo wameletwa Bara wanadhaliwa, wanalawitiwa, wananajisiwa, nyie mmekaa kimya hakuna kinachoendelea ambacho tunakijua, hatujui kesi yao itasikilizwa lini. Hivi kweli utawala bora uko wapi katika nchi hii? Waziri wa Wizara hii anatuambiaje kuhusiana na jambo hili hata kama liko Mahakamani, Zanzibar hakuna Mahakama? Inakuwaje mpaka ifikie stage hii? Kwa kweli jambo hili narudia kuwaambia ndiyo kaburi la CCM mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitakwenda kwenye Mahakama ya Kadhi. Namshangaa sana Mheshimiwa Waziri katika ripoti yake hakusema chochote kuhusu Mahakama ya Kadhi, jambo ambalo amesota nalo katika vipindi viwili akijaribu kulileta katika Bunge hili lakini limeshindikana. Waisalamu wote Tanzania wamekaa wanasikiliza kulikoni, ameshindwa kutoa kauli yoyote katika ripoti yake ni kitu gani kilichosababisha suala la Mahakama ya Kadhi halikuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitaka niwaambie Waislam wote Tanzania wajue sababu ya kutokuja kwa Mahakama ya Kadhi ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuchakachua maoni yote yalitotolewa na taasisi za Kiislam 11 zilizokwenda kuonana nao. Wameshindwa kutofautisha kati ya taasisi moja iliyolikubalia jambo lile ambalo lilikuwa ni kama danganya toto. Taasisi 11 zilikataa na zilikataa kwa misingi gani? Mbona Mheshimiwa Waziri ameshindwa kusema au wanasaburi wakati wa uchaguzi waje watoe propaganda kwa Waislam Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niwaambie Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imechakachua maoni ya taasisi 11 na imechakachua kwa sababu tu ya

kulinda maslahi ya kisiasa. Waliosababisha jambo hili kufeli ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu. Waziri Mkuu katika hili hata kama hapa leo si mahali pake, lakini kwa sababu Wizara hii imeshindwa kuleta Muswada wa Mahakama ya Kadhi hapa Bungeni katika mfumo ambao umekubalika kwa taasisi zote mie nataka niliweke wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda timu ya kuzisikiliza zile taasisi 11 lakini badala ya kuwasikiliza na akajua maoni yao yako vipi, walifikia mahali mpaka wakaunda muundo ambao unakubalika kwa taasisi zote pamoja na BAKWATA. Hata hivyo, kwa sababu tu walitaka jambo hili walikabidhi kwa BAKWATA ili wao wawe wamelichukua katika mfumo wa kisiasa na waweze kuzidhibiti zile taasisi nyingine, alipoona mchezo umeenda hivyo akaweza yeye kuchakachua yale maoni ya taasisi 11 na badala yake akasikiliza BAKWATA peke yake na akawapa mamlaka ya kwenda kutangaza Makadhi. Jambo ambalo halikubaliki, ni kuwachonganisha Waisalam kwa Waislam, jambo ambalo lingelela mtafaruku mkubwa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aseme bayana kwamba walioshindwa kuleta Mahakama ya Kadhi hapa ni Wizara yake baada ya kuona kwamba katika mfumo zilizotaka taasisi 11 hautawezekana na Serikali mlitaka jambo hili muwakabidhi BAKWATA ambayo ni taasisi ndogo tu, ilisajiliwa RITA, taasisi ambayo haina hata wanachama. Mimi nasema kwamba taasisi hii ni ya kufutwa, taasisi isiyo na wanachama haiwezi kukubalika katika jamii. Kwa sababu wameshindwa kusema ni sababu zipi zilizotokea wamenyamaza kimya na Mheshimiwa Waziri amenyamaza, kwa nini hawatuambii kwamba wameshindwa mara tatu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mie nasema na Waisalam wanatusikia na wajue tatizo kubwa lililosababisha kutopatikana kwa Mahakama ya Kadhi ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Waziri Mkuu, Mizengo Kayanza Peter Pinda. Wangelileta jambo hili pale ambapo Wabunge tungelegea tukasinzia na mkawakabidhi BAKWATA, lakini baada ya sisi kukataa na tukakazana kwelikweli kulipinga jambo hili ndiyo maana hata Kura ya Maoni haikuletwa kwa sababu jambo hili walikuwa wanalileta kiasiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema hivi, kutopatikana Mahakama ya Kadhi nchi hii, Waislam wote pamoja na watu wanaoitakia amani nchi hii waihukumu CCM mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kukaa kitako. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo atakuwa Mheshimiwa Chomboh.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama jioni hii lakini nakushukuru na wewe kunipa nafasi ya kuchangia kidogo katika Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawapa hongera na naunga mkono bajeti hii. Pia naitaka Serikali izidishe bajeti yake kwa sababu kama tunavyojua Wizara hii ndiyo ambayo ndani yake umo mhimili mmoja wa uongozi wa nchi kwa maana ya Mahakama, jambo ambalo linamgusa kila mtu kwa maana kwamba ndiyo kwenye muktadha wa kutoa haki lakini pia kusimamia mambo mengi ambayo yamezungumzwa na Wabunge waliopita kuhusu haki za binadamu. Basi bila kuwa na nyezo mahsusi au nzuri kwa maana ya bajeti nzuri, haitaweza kufanikisha mambo yake hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ambayo Mwenyezi Mungu alimpa fursa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuthubutu kuweza kuanzisha mchakato wa kupata Katiba Mpya ni jambo la kumsifu, kumpa pongezi lakini pia la kujivunia katika uhai wa kipindi chake hiki cha miaka kumi kwa maana ya Serikali ya Awamu ya Nne, nampongeza sana. Wizara ya Katiba na Sheria imejitahidi kusimamia jambo hili na likafanikisha mpaka leo kuna Katiba Iliyopendekezwa. Tulioshiriki tumeshiriki, tuliotoa maoni tumetoa maoni na tumefika mahali ambapo theluthi mbili za Zanzibar zikapatikana na za Bara zikapatikana. Kwa taarifa yenu kule Zanzibar sisi tunangoja tu siku yoyote kwa sababu sisi uzoefu wa kupiga Kura ya Maoni tunao. Kiufupi kwa Zanzibar Katiba hii imeshapita tunawasubiri ninyi wenzetu tu huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya Katiba ile, Mheshimiwa aliyepita namuita mama yangu kwa sababu namheshimu kwa sababu kachukua jina la mama yangu. Mama yangu mzazi anaitwa Rukia na namheshimu sana lakini leo nitamuelekeza akiwa kama Mbunge na siyo kama mama.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi kaizungumzia kwa kirefu sana. Kuna siku kwenye semina alisimama kwa nguvu akakataa kabisa Mahakama ya Kadhi isije. Akatoa maoni yake mengi tu akasema Mahakama ya Kadhi isije leo namshangaa anageuka. Mama kauli yako Mwenyezi Mungu anaiona na ukizingatia kuwa wewe ni mwanamke Muislamu ulikataa kabisa, umekataa katakata, nikashangaa huyu ni mama yang ninayemtegemea kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa taarifa tu ya Waislam na waliokuwa sio Waislam nataka mjue kwamba kwa Mahakama kwetu sisi Waislam Hakimu ni mmoja peke yake Mwenyezi Mungu na hukumu zake tayari ameshaziweka, zipo tayari. Mahakama za Kadhi hivi sasa jamani zinafanya kazi. Hivi tunavyongea

kila Taasisi ya Kiislam wana Mahakama zao za Kadhi na zinakwenda na wanatoa hukumu zao, wanaozesha, wanatoa talaka na mirathi pia. Kinachotakiwa na tunacholilia kwamba hukumu zile zitambulike kisheria tu lakini kwa hukumu za Kiislam na kwa wale waumini wa Kiislam zinafuata sheria zao. Tunahitaji tunapokwenda kwenye vyombo vya kisheria mfano kwenye *banking* au kwenye mambo mengine, zile haki au hukumu zitambulike. Hukumu ile hatoi Kadhi kichwani mwake hukumu ziko tayari ndani ya Kitabu Kitakatifu, yule mtu anayezisoma hukumu zile ndiyo anaitwa Kadhi kwa maana ya kwamba yeye ndiye anaweza kutafsiri siyo kila mtu anaweza kutafsiri.

TAARIFA

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Rukia.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa baba yangu, mwanagu hizo Mahakama za Kadhi zilizopo hazipo kisheria, ni sawasawa na mdomo usiokuwa na meno. Namuuliza baba yangu anatafuna hata andazi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chomboh umepokea taarifa?

MHE. ALLY K. MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy, naomba ukae.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Taarifa nimepewa mimi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chomboh endelea.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi Waislam Mahakama ya Kadhi zinafanya kazi vizuri sana na kama nilivyotangulia kusema Kadhi hatafasiri kutoka kichwani mwake anatafasiri kutokana na Quran ilivyoandikwa. Kama yeye ana jina Tukufu la Rukia, anawajibika kujua hilo na hasa akijua kwamba yeye ni mwanamke. Mama yangu sitaki kusema sana nisije nikakosa radhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nachotaka kuwaambia Ndugu zangu Waislam hukumu zetu sisi ziko ndani ya Qurani na hazibadiliki na hakuna mtu anayeweza kubadilisha. Anayekwenda kinyume na hukumu hizo basi yeye siyo Muislam kwa sababu anaikataa hukumu iliyotolewa na Hakim ambaye kwetu

ni mmoja tu, hawa Makadhi wanatafsiri tu hukumu ambayo Hakimu ameshatoa, ni Mwenyezi Mungu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mahakama hizi tunazungumza sisi, nataka Ndugu zangu Waislam wajue kwamba hatutaki Mahakama ya Kadhi kwa maana ya jengo au kwa maana ya kwamba ni lazima zilipiwe, wala hatutaki hata *single cent* ya Serikali itumike kwenye Mahakama hii, *no way*. Mpaka sasa niwaambieni Waislam wanatoa hukumu zao ndani ya taasisi za dini, Washia, Ibadhi na Answar Sunna wanahukumiana wenyewe yaani kila Taasisi ya Kiislam wana Mashekhe wao kwa maana ya wale wanaotafsiri na ndiyo wanaitwa Makadhi na wanatoa hukumu zao na zinakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachozungumzwa hapa ni kwamba wanachokitaka Waislam miongoni mwao nikiwemo na mimi kama Muislam ni kwamba ukiona *document* ambayo ni talaka, karatasi ya ndoa au mirathi itambulike kisheria kwa zile taasisi za Kiserikali lakini kwa sababu mambo yale yanatokana na dini ni wajibu wa kila mmoja. Kwa sababu sisi Waislam tulionywa kwanza na tulionywa mambo matatu kwamba enyi watu mtahadhari sana na mali, wanawake na watoto. Kwa misingi hiyo, Mwenyezi Mungu alisema kwa sababu watoto wanakuja kutokana na ndoa na mirathi inakuja kutokana na mali na wanawake ndiyo kiungo cha kuweza kufanyika yote hayo, kwa hiyo, vitu hivi ni muhimu sana. Ndiyo nikasema kwamba mama yangu pale ni mmoja katika watu tuliotahadharishwa nao. Sisemi mimi wanawake ni watu wa kukaa nao kwa tahadhari kwa sababu ni *very sensitive* hayo ni maumbile ya Mwenyezi Mungu tutake tusikatake ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachotaka kumwambia mama yangu kwamba Mahakama ya Kadhi ni yeye na wapinzani wenzake wote ndiyo waliokuja kidete kusema kwamba Mahakama ya Kadhi isije. Siyo Ofisi ya Waziri Mkuu na wala siyo Ofisi ya Sheria ni Wapinzani mkakaa kidete na mka-lobby mambo haya yakawa hivyo. Mjue hivyo ninyi Waislam mlioko katika Vyama vya Upinzani hawa watu ndiyo waliokataa Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hiyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Chomboh, huyu ndiye mchangiaji wa mwisho kwa leo lakini nitamuita Mheshimiwa Naibu Waziri kwa dakika ishirini ili naye achange hoja.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niruhusu nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi na wanawake wa Mkoa wa Tanga kwa kuniwezesha kuwa Mbunge katika Bunge hili la Kumi. Nawashukuru pia kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Napenda kuwahidi wanawake wa Mkoa wa Tanga kupitia UWT, Mkoa wa Tanga kwamba tutaendelea kufanya kazi pamoja katika kuhakikisha kwamba tunaijenga Tanga yetu na niwaombe waendeleo kukiamini Chama cha Mapinduzi kwa sababu katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopita Mkoa wa Tanga ulishika nafasi ya pili. Kwa hiyo, naamini tutatoa fundisho katika Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba. Tunasema kura zaidi kwa Chama cha Mapinduzi, viti zaidi kwa ajili ya Wabunge wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia kwa heshima na unyeyekevu mkubwa, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniamini. Aliniibua kama Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto nikahamia Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na sasa hivi ni Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. Hakika nimejifunza mengi na nimepata uzoefu mkubwa katika kuitumikia nchi yangu katika ngazi hii ya uongozi. Namtakia kila kheri Mheshimiwa Rais na familia yake atakapopumzika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Waziri wa Katiba na Sheria, Mwalimu wangu Dkt. Asha-Rose Migiro kwa kuniongoza vema na amenipa ushirikiano mzuri sana toka nimeingia kwenye Wizara ya Katiba na Sheria. Pia niwashukuru Watendaji wa Wizara na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, napenda pia kuishukuru sana familia yangu, kama unavyofahamu kazi zetu kila siku uko barabarani. Napenda kumshukuru sana mume wangu mpenzi, Pascal Richard, kwa uvumilivu wake mkubwa lakini pia kwa mchango wake katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hayo, sasa napenda nianze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2015/2016 kwa kujibu baadhi ya hoja za Wabunge na hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Mchango wangu utajikita katika eneo linalohusu Mahakama na kama muda utatosha basi nitagusia mambo mengine mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikiliza kwa makini taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyosomwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Jasson Rweikiza na Waheshimiwa Wabunge pia wamechangia

michango mbalimbali. Kamati imeainisha changamoto mbalimbali au changamoto kadhaa ambazo Mahakama inakabiliana nazo. Changamoto kubwa ambayo Kamati imeainisha ni suala la ufinyu wa bajeti ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niweke vizuri kuwa mfumo wa utoaji haki na uhuru wa Mahakama ni kipaumbele cha Serikali ya CCM. Haya siyo maneno ya kutaka kusoma Bungeni lakini utashi huu wa kutaka mhimili wa Mahakama uweze kupata rasilimali fedha za kutosha umethibitishwa na kitendo cha Serikali kuleta katika Bunge lako Tukufu Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011. Bunge lako lilipitisha sheria hii ambayo pamoja na mambo mengine lilianzisha Mfuko wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2013 mpaka 2014, bajeti ya Mahakama imekuwa ikiongozeka kila mwaka. Waheshimiwa Wabunge nitawaomba muende katika kile Kitabu cha Matumizi *Volume II* mtaona mwaka 2013/2014, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama ilikuwa ni shilingi bilioni 102. Mwaka 2014/2015, bajeti ikafikia shilingi bilioni 121 na mwaka 2015/2016, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama ni shilingi bilioni 136. Kwa hiyo, tunakubaliana na maoni ya Kamati ya Bunge kwamba Serikali imechukua hatua za makusudi za kuhakikisha kwamba Mahakama inapewa rasilimali fedha za kutosha ili iweze kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishangaa sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani amesema amefanya utafiti, *research* gani amefanya kama wote tumepewa kitabu humu ndani ambacho kinaonyesha mwenendo wa utoaji wa fedha katika Mfuko wa Mahakama. Wengine wanataka tu kufanya siasa lakini Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete imechukua hatua za makusudi kuhakikisha Mahakama inayo rasilimali fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa takwimu zaidi. Tukienda katika bajeti ya maendeleo mwaka 2012/2013, bajeti ya Mahakama ilikuwa ni shilingi bilioni 10 tu sasa hivi tunazungumzia shilingi bilioni 40. Huu ni utashi wa dhati wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi wa kuhakikisha kwamba upo uhuru wa Mahakama katika nchi yetu lakini pia mfumo wa utoaji haki katika nchi yetu unaboreshwa na unafanya kazi kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kuongezeka kwa bajeti ya Mahakama ya kila mwaka kumechangia kitu gani? Kumeboresha miundombinu ya Mahakama na kumesaidia uharakishaji wa usikilizaji wa mashauri na hivyo kuimarisha mfumo wa utoaji haki. Ukitazama mwenendo wa utoaji fedha katika Mfuko wa Mahakama na Wizara nyingine wao bajeti yao imetolewa kwa zaidi ya 66%, Wizara nyingine tulikuwa tunasema wamepata 22%, 23%. Kwa hiyo, hilo nilitaka tu kuweka vizuri. Changamoto ambayo tunayo ni suala la kutoa fedha kwa ajili ya maendeleo lakini wenzetu wa Wizara ya

Fedha wametuhidi kwamba fedha hizi zitapatikana kabla ya mwaka kuisha. Siku 45 bado ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo Kamati imeliongelea na Waheshimiwa Wabunge pia ni suala la majengo au miundombinu ya Mahakama, nakubali maana tusipokubali hatuasema ukweli. Ni kweli kuwa tunazo changamoto katika baadhi ya maeneo yanayohusiana na uchakavu wa miundombinu ya Mahakama hasa majengo ya Mahakama za Mwanzo, za Wilaya na katika baadhi za Wilaya hasa Wilaya mpya hazina Mahakama kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliochangia suala hili ni Kamati ya Bunge na Mheshimiwa Ritta Kabati, Dada yangu wa Kilindi, Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, Mheshimiwa Keissy umezungumzia suala la ukarabati wa Mahakama ya Nkasi, Mheshimiwa Paul Lwanji umezungumzia kuhusu Manyoni, Mheshimiwa Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Suzan Kiwanga na Mheshimiwa Dunstan Kitandula napenda niwathibitishie kwamba tayari tunao mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali katika mwaka huu wa fedha 2015/2016. Katika kipindi hiki tumeonyesha ni Mahakama ngapi za mwanzo tutajenga na kukarabati, Mahakama ngapi za Wilaya tutakazojenga na kukarabati, ninao hapa mpango na kuonyesha Mahakama Kuu ambazo tutajenga. Nataka kuwathibitishia kwa kweli tutatoa kipaumbele katika zile Wilaya mpya ambazo hazina kabisa Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wameliongelea sana ni kuhusu suala la watumishi, tulikuwa tuna upungufu wa watumishi katika Mahakama lakini kutokana na ongezeko la rasilimali fedha tumeweza kutatua tatizo hili kwa kiasi kikubwa. Serikali inatambua kuwa ni changamoto kama nilivyosema lakini katika mwaka huu wa fedha ambao tunao jumla ya watumishi 760 wanatarajiwa kuajiriwa. Katika ajira hizo tumeonyesha Maafisa Tawala, Maafisa Utumishi lakini pia tumeshalitua tatizo hili, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake alionyesha katika mwaka huu wa Fedha Mheshimiwa Rais ameteua Majaji 20 wa Mahakama Kuu kwa ajili ya kupunguza changamoto hiyo ya watumishi wa Mahakama. Nikuthibitishie pia katika mwaka huu wa fedha mpango wa ajira ya watumishi wapya wa Mahakama, tunatarajia kutangaza tena nafasi 295 za Mahakimu. Kwa hiyo, suala hili tutaweza kulipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nimshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo siku zote amekuwa akipigania maslahi ya watumishi wa Mahakama wakiwemo Majaji na Mahakimu suala hilo tumelifanyia kazi na niwaambie wanawake wa Singida kuwa waendeleo kumchagua Diana Chilolo na kukichagua Chama cha Mapinduzi ili aweze kuwapigania na kuwasemea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani anasema kwamba Mahakama inadaiwa na Majaji. Sasa nataka kumthibitisha au kumueleza Msemaji wa Kambi ya Upinzani, bahati mbaya hayupo lakini salamu zimfikie kwamba Mahakama haina deni lolote la nyumba, mishahara, posho wala samani za nyumba na vitendea kazi. Yeye amesema anafanya utafiti, Waheshimiwa Majaji wale pale aende akawaulize kama kuna Jaji anaidai Mahakama hela yoyote. Maneno mengine ni kutaka tu kufurahisha genge lakini kwa kweli sisi kama Wizara ambao tunasimamia mhimili huu wa dola tunashukuru sana jitihada ambazo Serikali ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete imechukua katika kuimarisha mhimili huu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tumelifanya kwa kutekeleza Sheria ya Malipo na Mafao ya Majaji ya mwaka 2007 na tumefanya kwa 100%. Kwa hiyo, huyo Msemaji aende akamuulize Jaji yeyote kama anadaiwa kitu chochote. Anasema amefanya *research* lakini kama yeye ni Mwanasheria anashindwa hata kuongea na Jaji mmoja tu wa Mahakama Kuu, sasa huyo ni Mwanasheria gani ambaye hana hata mahusiano mazuri na Majaji? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie eneo lingine la mwisho latika suala hili la Mahakama ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge, ni suala la nidhamu na maadili. Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala lakini pia na Waheshimiwa Wabunge wakiwemo Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Mendrad wamezungumzia suala hili kwamba upo ukiukwaji wa maadili kwa Mahakakimu. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania kwamba tumeweka utaratibu mzuri wa kushughulikia nidhamu au ukiukwaji wa maadili kwa watumishi wa Mahakama na utaratibu huu umewekwa chini ya Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na.4 ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitu ambacho Bunge lako hili la Kumi linatakiwa kujipongeza katika kuimarisha mhimili huu wa Mahakama ni kupitishwa kwa sheria hii. Sheria hii ya *Judicial Administration Act* inaaazisha Kamati za Maadili za Mahakama katika ngazi za Wilaya na ngazi za Mikoa na imeonyesha Kamati hizi Mwenyekiti wake katika ngazi ya Wilaya atakuwa ni Mkuu wa Wilaya na katika ngazi ya Mkoa atakuwa ni Mkuu wa Mkoa. Pia wameonyeshwa Wajumbe ambao wanatakiwa kuwa katika Kamati hizo. Kwa hiyo, Tume ya Utumishi wa Mahakama imejitahidi kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba tunazijengea uwezo Kamati hizi za Maadili za Wilaya na Kamati za Maadili za Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu ambacho naomba uniruhusu nikiseme kidogo. Ukisoma *Judicial Administration Act*, kifungu cha 51, kimeweka utaratibu kwa mfano ile Kamati ya Wilaya Mwenyekiti wake atakuwa *District Commissioner*, Hakimu wa Wilaya, *DAS*, watu wawili ambao watateuliwa kutoka

katika mashirika ya dini na watu wawili ambao wanafanya kazi katika Mahakama. Kwa hiyo, nachotaka kusema hapa Kamati hizo zipo katika Wilaya zetu na Mikoa yetu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tunapokaa katika vikao vya DCC na RCC kama kweli utoaji haki ni changamoto ya wananchi wetu, ya wapiga kura, ni lazima tuhakikishe Kamati hizi zinafanya kazi. Hivi kweli ni Wabunge wangapi wanamuuliza DC, katika bajeti yako ya mwaka wa fedha umeweka shilingi ngapi au ni *activity* gani umeziweka kwa ajili ya Kamati za Maadili za Wilaya au Mkoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hili tulizungumze, kaka yangu Machali, Hakimu pale Kasulu anapokunywa pombe wakati wa kuendesha kesi, hutegemei Jaji Mkuu atoke Dar-es-Salaam ndiyo amuone! Palepale Kamati ya Maadili ya Wilaya ndiyo ina kazi hiyo ya kuhakikisha inakutana mara nne kwa mwaka na kujadili changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hii ya Mahakama. Kwa hiyo, hata kama wakati mwingine hamna makosa lakini mnaweza mkakutana DC, RAS na Mheshimiwa Hakimu kwa ajili ya ku-*network* na kubadilishana uzoefu.

Kwa hiyo, mimi narudisha mzigo huu kwenu Waheshimiwa Wabunge. Tunapokaa katika DCC, tunapokaa katika RCC tuhakikishe mojawapo ya ajenda zetu za kila siku za kudumu tusijadili tu barabara na maji lakini hata utoaji haki ni changamoto na mmeonyesha wenyewe ni changamoto, kwa hiyo, ni lazima iwe ni ajenda ya kudumu katika vikao vyetu. Nitumie Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kwamba watambue ni wajibu wao. Sisi Wizara ya Katiba na Sheria kupitia Mahakama, tutatimiza wajibu wetu wa kuwapa elimu na kuwajengea uwezo ili waweze kutambua wajibu wao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo hili nachotaka kusema ni kwamba hatua kadhaa zinazohusiana na ukiukwaji wa nidhamu ya watumishi wa Mahakama zimechukuliwa kwa sababu hizi Kamati zikishakutana zinatoa mapendekezo kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama. Kwa mfano, katika mwaka 2010 mpaka 2014, mashauri ya nidhamu ya Mahakimu 21 yalipelekwa katika Tume ya Utumishi wa Mahakama na kati ya hayo Mahakimu sita walifukuzwa kazi na kumi na tano walipewa onyo. Kwa hiyo, nataka kuonyesha Bunge lako Tukufu kwamba hatua zinachukuliwa lakini tujjulize katika ngazi ya Wilaya na Mkoa ni hatua gani tumechukua katika kutatua changamoto hii.

Napenda sana kulieleza eneo hili lakini kutokana na muda naomba niende katika eneo lingine ambalo limeongelewa sana na Waheshimiwa Wabunge nalo ni suala la ucheleweshaji wa hukumu au mlundikano wa kesi. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameonyesha kwamba katika mwaka

huu wa fedha unaoisha kesho kutwa ni kesi ngapi ambazo zilikuwa Mahakamani katika ngazi zote, Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu na Mahakama za Wilaya, Mahakama za Mwanzo na ni ngapi zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkisoma taarifa ya Mheshimiwa Waziri ni zaidi ya asilimia 72 ya mashauri yamekamilishwa katika kipindi hiki cha mwaka mmoja. Kwa hiyo, yapo malengo ambayo sasa hivi wamejiwekea kila Jaji na Hakimu amepewa idadi maalum ya mashauri kwa muda maalum ambapo wanatakiwa kuyasikiliza.

Kwa hiyo, vilevile idadi ya vikao vya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa vimeongezwa. Kwa hiyo, hii imetusaidia sana kutatua tatizo la ucheleweshaji wa hukumu na mlundikano wa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo ameliongea Mama Lucy Nkya ni suala la lugha inayotumika Mahakamani kwamba ni kikwazo. Serikali inatambua umuhimu wa Mahakama kuendesha mashauri kwa lugha ya Kiswahili na hii ndiyo lugha yetu ya Taifa. Nakiri kwamba lugha ya Kiingereza ni changamoto katika kufikia haki lakini kama Wizara tumeshachukua hatua. Zipo changamoto kwamba sheria zetu nyingi zinaandikwa katika lugha ya Kiingereza lakini pia kuna tatizo la istilahi yaani tunakosa istilahi za kisheria ambazo zinatumika katika Kiswahili. Hata hivyo, tumeshafanya mashauriano na Taasisi ya Utafiti ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam TUKI ili tuweze kutengeneza istilahi ambayo itasaidia kuja na misamiati ambayo itaweza kutumika katika Mahakama zetu. Pia tumeshafanya mawasiliano na Baraza la Kiswahili la Tanzania, tunaendelea kushauriana nao kuhakikisha kwamba mashauri yanaendeshwa kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo tumelifanya kama Serikali, Miswada yote ambayo inakuja katika Bunge lako Tukufu sasa hivi inakuja katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa hiyo, kuna hatua ambazo tumeshaanza kuzichukua na niwathibitishie Watanzania kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kuhakikisha inachukua kila hatua ili haki iweze kupatikana mapema na kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nilitaka kulimalizia ni suala la Mahakama ya Ardhi. Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya ameshauri kwamba tuboreshe mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi ili tuweze kulinganisha na mfumo wa Mahakama. Tumepokea mapendekezo hayo kwa sababu hata Tume ya Kurekebisha Sheria, haya yalikuwa pia ni mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge kwamba tumepokea mapendekezo, Wizara ya Katiba na Sheria itakaa pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya TAMISEMI kuona ni jinsi gani tutaweza kuangalia suala hili. Kwa sababu haya Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji (*Ward Tribunals*) yameanzishwa chini

ya Sheria na Utatuzi wa Migogoro ya mwaka 2002. Kwa hiyo, hili tatizo hili tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie suala moja ameliongelea Mheshimiwa Mary Chatanda na Kamati ya Bunge ya Katiba na Utawala la kuhakikisha kwamba tunakuja na mpango maalum wa kuongeza usajili wa watoto. Naomba niseme, mimi binafsi suala hili nalichukulia kama ni kipaumbele. Kwa sababu ukilinganisha Tanzania, watu ambao wamesajiliwa ni asilimia kumi na sita tu lakini Kenya wenzetu wanazungumzia asilimia 60 watu wenye vyetu vya kuzaliwa, Rwanda wamefikia asilimia 80 na Uganda usajili upo katika asilimia 20. Kwa hiyo, nataka kurudisha tena mzigo kwa Waheshimiwa Wabunge, wote tunarudi Majimboni kuomba kura mwezi ujao, kama kweli suala hili ni kipaumbele chenu, nitawaomba Waheshimiwa Wabunge tunaposimama kuomba kura tuhamasishe Watanzania, wazazi na walezi kuhakikisha wanasajili watoto wao wa chini ya umri wa miaka mitano. Kwa sababu, upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa sasa hivi tumeondoa pia gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mary Chatanda na Kamati ya Bunge kwa kuliongelea suala hili kwa sababu ni suala muhimu sana. Naamini kwamba hata wanawake na wanaume wa Korogwe Mjini utaenda kuwahamasisha kuhakikisha kwamba wanasajili watoto wao ili kuweza kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Nakushukuru sana kwa kuliongelea suala la miundombinu ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nilitaka tu kujibu hizo hoja zilizoletwa kwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge, lakini tunazo pia hoja za Waheshimiwa mbalimbali na Mheshimiwa Waziri atajibu lakini na Waheshimiwa Wabunge wanaweza kupata majibu, kwa mfano Mheshimiwa Assumpter Mshana alizungumzia suala la kutomalizika haraka mashauri katika Mahakama ya Biashara. Nataka kumthibitishia Mheshimiwa Assumpter kwamba Mahakama ya Tanzania imeshachukua hatua ya kuanzisha kanuni maalum kwa Mahakama Kuu, Divisheni ya Biashara katika kukabiliana na changamoto hii. Pia kushushwa kwa viwango vya ada kumpelekea kuongezeka kwa usajili wa mashauri mapya ambayo mara nyingi huambatana na maombi. Vilevile Mahakama ya Biashara katika kukabiliana na suala la mrundikano imeandaa utaratibu maalum wa usikilizaji wa kesi zenye umri mrefu. Aidha, Mahakama ya Biashara imeongezewa Majaji, sasa hivi tunao Majaji wanne badala ya Majaji watatu wa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Diana Chilolo ameongelea Majaji wapatiwe walinzi muda wote. Ni agizo la Serikali kuwa Majaji wapatiwe ulinzi na utekelezaji umeshaanza. Kwa hiyo, tunakushukuru sana na suala hili limeshafanyiwa kazi. Nilikuwa nasema tangu nimeingia Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Diana Chilolo siku zote amekuwa akiongelea maslahi ya

Majaji na Mahakimu. Ningekuwa na uwezo ningeiambia Mahakama ikupe angalau kombe kwa kuwa *champion* wa haki za Mahakimu na naamini wanawake wa Singida watamrudisha tena mwezi Novemba, 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mendrad amezungumzia kesi kuchukua muda mrefu. Nimesema sasa hivi tuna mkakati wa kuhakikisha mashauri yote yenye umri wa miaka miwili yanamalizika. Nimesema sasa hivi takwimu zetu zinaonyesha ni zaidi ya asilimia sabini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine wamezungumzia Kiswahili kutumika Mahakamani, hilo nimeshajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amezungumzia suala la Mahakama za Mwanzo za Igowole, Mgololo, Kibao na Mlangali, naomba niseme kwamba tunao mpango wa ujenzi wa Mahakama.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa fursa hii lakini niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Nina hakika kabisa tukishirikiana pamoja basi kuimarisha mfumo bora wa utoaji haki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namuita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu naye achangie hoja.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Naibu Waziri, Majaji wote na Mahakimu, Watendaji na viongozi wote wa taasisi zilizoko katika Wizara ya Katiba na Sheria ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wote ikiwemo na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa ambao mmekuwa mkinipatia wakati nikishirikiana nanyi hapa katika kutekeleza majukumu yangu. Bila kumsahau Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote ambao wameendelea kutupatia ushirikiano wakati tunapotekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri asilimia mia moja kwa mia moja. Naomba nichangie tu kwa kutoa ufafanuzi

kwenye maeneo haya ambayo yamezungumzwa hapa na ambayo nadhani tu labda Waheshimiwa Wabunge wanahitaji tu ufafanuzi. Zaidi nianze na hizo hoja mbili ambazo zimeletwa na Mheshimiwa Rukia Ahmed. Moja inahusiana na kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Pinda almaarufu kwa hicho kinachoitwa piga tu! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kauli hii siyo iliyopelekea kuwepo kwa Operesheni Kimbunga wala iliyopelekea kuwepo kwa kitu chochote ambacho kimetamkwa na Mheshimiwa Mbunge. Kuliundwa Tume Teule ya Bunge ambayo ilifanya uchunguzi lakini Tume ile haikusema kwamba yaliyojiri kutokana na Operesheni ya Tokomeza Ujangili ilitokana na kauli ya Mheshimiwa Pinda. Kwa hiyo, naomba kushauri Waheshimiwa Wabunge kwamba ni vyema tukawa waangalifu tunapotoa matamko kama haya na hasa yanayowahusu viongozi wakubwa wa Taifa hili ambao wanafanya kazi kubwa sana kwa maslahi ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi kulikuwa na kesi Mahakamani. Hii habari ya kwamba kuna chombo kilisema kwamba ile kauli ilivunja haki za binadamu, hiyo ni kauli ambayo siyo rasmi. Kulikuwa na shauri Mahakamani linalohusiana na suala hili la kauli ya 'piga tu' na kama mtakavyokumbuka niliendesha ile kesi, hakuna wakati wowote ambapo Mahakama ilitamka kwamba kauli ile ilikuwa ni uvunjifu wa Katiba. Kwa hiyo, niliona hili nalo niliweke wazi ili Waheshimiwa Wabunge na wananchi wengine walielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili linalohusiana na mchakato wa Mahakama ya Kadhi. Sisi wote ni mashahidi, tunatambua Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali juhudi kubwa ambazo imefanya katika kuhakikisha kwamba Mahakama hii inakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua yaliyojiri tulipofanya semina pale kwenye ukumbi wa Msekwa, jinsi ambavyo hata kupokea mchango na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliposimama kuhitimisha na kusema kwamba ameyazingatia hayo na anapowasilisha Muswada kesho yake, tarehe 1 Aprili, angeyalingiza hayo ambayo pia yalikuwa yachukua fursa na hata hao Waislam wengine ambao siyo BAKWATA wapate nao ushiriki kwenye hii Mahakama lakini Waheshimiwa Wabunge mnafahamu, hayo mlkataa. Zaidi ya hapo kulikuwa na kesi Mahakamani ilifunguliwa na baadhi Waislam. Kwa hiyo, si kweli kwamba mchakato wa Muswada wa kutambuliwa kwa Mahakama ya Kadhi kwamba umehujumiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Ofisi ya Waziri Mkuu. Nadhani tu hatujafikia hatua sisi wenyewe tukaelewana tuwe na hii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo ninapomshukuru Mheshimiwa Chomboh kwa ufafanuzi ulioutoa kuhusiana na hii hoja, ni nini hasa kilitokea na

mpaka sasa hiyo Mahakama maamuzi yake kutatambuliwa kama ambavyo Serikali ilikuwa imekusudia kwenye Muswada ule. Kwa hiyo, tunachukua hatua sasa hivi kuvifikia hivi vyombo vyote vya Waislam wakubaliane, wakishakubaliana, Muswada utakuja tu hapa na Wabunge mtapata fursa ya kutoa uamuzi huu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili la Mashekhe wanaodaiwa kutoka Zanzibar wakashtakiwa Bara. Ni Mashekhe hawa lakini pia wanatuhumiwa kwa kesi ya ugaidi. Shauri hili linasikilizwa Mahakama za Tanzania Bara kwa sababu lina mlolongo wa jinsi uhalifu ule unadaiwa umetendeka. Mengine yametendeka Zanzibar na mengine Bara.

Kwa hiyo, katika mazingira kama hayo ni sahihi tu kisheria shauri la aina hiyo badala ya kusikilizwa Zanzibar likasikilizwa Bara. Niliomba nitoe ufafanuzi huu ili Waheshimiwa Wabunge wapate kuelewa kitu gani hasa ambacho kimetokea kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rashid Ali na Mheshimiwa Selasini wamezungumza juu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kupewa mamlaka ya kuendesha kesi yenyewe. Taasisi hii mpaka sasa wanayo mamlaka ya kuendesha mashauri yanayotendwa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007. Inaitwa *corrupt transactions*, mtu anaomba, kupokea na kushawishi, mamlaka hayo wanayo. Zaidi ya hayo Mkurugenzi wa Mashtaka anakaimisha mamlaka yake kwa watendaji wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ambao ni Wanasheria kuendesha mashtaka haya Mahakamani na wamekuwa wakifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni la Kikatiba pia. Hata kama tungetaka sasa kwamba PCCB waanze kuendesha mashauri yote kwa mfumo wa Katiba tulionao sasa haiwezekani labda mpaka twende tubadilishe kwanza Katiba kwa sababu Ibara ya 59B(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka kwamba; *“Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini”*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala la ‘mashtaka yote nchini’. Kama kungekuwa na upenyo, kwa sababu ninyi ni wawakilishi wa wananchi kwangu isingekuwa na tatizo. Kwa hiyo, labda katika muktadha wa Katiba inayokuja au kama mpo radhi Katiba hii muibadilishe, hii ndiyo hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnakumbuka mwaka 2008 ilitungwa sheria inaitwa *The National Prosecution Service Act* ambayo ilikusudia kuvifanya hivi vyombo vinavyopeleleza visishiriki pia kuendesha mashtaka, kwamba wewe huwezi kuwa Hakimu katika kesi inayokuhusu wewe mwenyewe. Sasa kama katika hili suala la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mnasema

kwamba hiyo itoke humo tubaki na Polisi, hayo yatakuja kuamuliwa baadaye na watu wa kuamua ndiyo ninyi wenyewe. Kwa hiyo, hili na lenyewe niliona nilitolee ufafanuzi Waheshimiwa Wabunge walifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mikataba kupitiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Makao Makuu. Tunatambua na tunakubaliana kwamba, kwa sasa kipindi hiki ambacho Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imefikia Mikoa yote, masuala ya mikataba kama hii inayoangukia chini ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya thamani inayoishia milioni hamsini, hakuna sababu ya lazima ya kuleta pale. Kama mtakumbuka kwenye Mkutano wa Kumi na Nane, mwezi wa pili nilisema hapa. Tunachokifanya sasa ni kwamba Ofisi zetu hizi za Mikoa zenyewe zimekuwa zikijihusisha sana na mashauri ya jinai na ya madai, wamekuwa hawajishughulishi na masuala ya mikataba. Kwa hiyo, tumepata fedha, tunataka tuwape semina kama ya wiki mbili waanze wao wenyewe kushughulika na mikataba hukohuko Mikoani. Kwa kweli huoni mantiki mtu atoke Nkasi aje Dar-es-Salaam halafu asubirie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ucheleweshaji mwingine unatokana na Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu na sisi pia tunachelewa kuileta mikataba pale. Sheria inasema ukishaleta ile mikataba pale, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana kipindi cha siku 14 cha kuipitia na kutoa maamuzi. Sasa mwingine kwa sababu anatoka mbali labda tuseme Rombo, anakuja pale na mkataba ule zimebaki siku chache anasema anataka kwenda kusainiwa, lakini unakuta kuna rundo kubwa sana la mikataba mingine inayotaka kufanyiwa kazi na Watendaji nao ni wachache.

Naomba kuchukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inafanya kazi kwa umakini sana, Watendaji wale ni wachache na wanajitahidi sana na ni watu wazalendo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama siyo ofisi hiyo, basi mambo mengine yasingekuwa mazuri sana. Kuna haki nadhani ya kuwashukuru na kutambua kazi kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nyangwine amezungumza juu ya kuandikwa kwa sheria. Suala hili amelizungumza Naibu Waziri sitaki kulizungumzia tena. Amezungumza pia kuandika mikataba kwa lugha ya Kiswahili tunakubali. Kama pande zote mbili mnakubaliana, maana mkataba ni makubaliano ya watu wawili, kama mmoja hajui Kiswahili mtapata shida, mnaenda kwenye lugha ambayo inawaunganisha wote; lakini kwa mikataba inayofanyika kwenye kiwango cha Halmashauri kule mnaweza mkaamua mkakubaliana ninyi wenyewe na kule mnaweza mkajiwekea utaratibu wa uwazi sana kwa sababu Wabunge nafahamu kuwa ni Madiwani mnaingia kule ndani, mnaweza mkawa na

msukumo mkubwa kuhakikisha mikataba inayoingiwa kule inaingiwa kwa uwazi sana.

Mheshimiwa Nyangwine vilevile amezungumzia juu ya usiri wa mikataba isiyo ya siri sana. Mikataba mingine ni ya siri kwa sababu za kimsingi, inakuwa na kile tunachoita *commercially sensitive information*, yaani inakuwa na taarifa nyeti za kibiashara ambazo huyu hataki zijulikane kwa watu wengine. Mikataba mingine inaweza ikawa na hizi *intellectual property* na vitu kama hivyo. Kama tulivyokwisha kusema, Mikataba mnaingia watu wawili, mkiweza kukubaliana *well and good* sisi hatuoni shida, lakini mikataba hiyo siyo ya siri sana.

Ukiangalia vizuri Sheria ya TRA au Sheria ya Madini na sheria nyingine, zinatoa maeneo ambapo vitu mnavyovitaka mnaweza mkaviona. Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, kifungu cha 10 kinampa fursa Mbunge, akitaka kuona ile. Bunge lako hili Tukufu limeweka utaratibu wa namna gani Mbunge akitaka kuona mkataba wowote ule, anaenda kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge anaweza akaiona. Sasa wakishaiona mikataba hiyo waitumie kwa sababu hizo wanazotaka kuziona, isije ikatuletea tena shida nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala ambalo limezungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na mamlaka ya Mkuu wa Wilaya kuzuia Mikutano ya Vyama vya Siasa. Kama mnaisoma Sheria ya Tawala za Mikoa (*Regional Administration Act*), ukisoma kifungu cha 14(2), unaona mamlaka haya ya Mkuu ya Wilaya. Imeelezwa vizuri kabisa kwamba, Mkuu wa Wilaya ana wajibu wa kutunza amani katika Wilaya anayoiongoza na kutoa maelekezo ya jumla na mahususi katika kutekeleza Sera za Serikali. Sheria hiyo pia uisome sambamba na Sheria ya Baraza la Taifa la Usalama, uone mamlaka ya Kamati za Usalama na Ulinzi za Wilaya, ziko na za Mikoa. Kwa hiyo, ukishaiona ile unaona ni kwa nini na kwenye hili la Iramba bahati nzuri ambacho kimejiri hapa, hakufunga mikutano ya chama kimoja tu cha Upinzani, alifunga mikutano ya vyama vyote na hawa wanakuwa na taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mngejua ni watu gani wanaunda zile Kamati za Ulinzi na Usalama, mngejua kwamba ni watu ambao tayari wanakuwa na taarifa. Taarifa hizi siyo lazima zitoke kwa kila mtu, ndiyo maana kuna kitu kinaitwa Serikali (*sirikali*). Tofauti na Bunge, Bunge shughuli zake ni za hadharani, Mahakama shughuli zake ni za hadharani, Serikali ziko nyingine ambazo ni za hadharani na nyingine siyo za hadharani. Vinginevyo, kama mambo yanayohusiana na amani na utengamano, ukifanya kila kitu hadharani utaharibu kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, sisi Wabunge na Wananchi wote wa Tanzania, wanasiasa na wasio wanasiasa kama mimi, tuzingatie matakwa ya Katiba. Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, inamtaka kila mtu kuheshimu na kuitii Katiba ile na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inatoa fursa pia kwa mtu yeyote kuchukua hatua kuhakikisha Katiba na Sheria zake zinalindwa na kuhifadhiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu hii pia nizungumzie juu ya tuhuma zinazozungumzwa juu ya Jeshi la Polisi. Polisi hawa wana mamlaka sasa ya kutekeleza wajibu huo, kwa sababu Serikali na ndiyo maana Polisi unakuta wako chini ya Mhimili wa *Executive* (Utawala au Utendaji). Mhimili huu kazi yake ni kusimamia utekelezaji wa sheria zilizotungwa na Bunge na maamuzi ya Mahakama. Kama kuna hawa ndiyo kazi yao kufanya hiyo kazi na ipo sheria inaitwa *The Police Force and Auxiliary Act*, kwa hiyo, wao kama kuna uvunjifu wa amani au kunakusudiwa kuwepo kwa uvunjifu wa amani lazima wachukue hatua. Ila sasa wachukue hatua ndani ya taratibu zilizowekwa kwenye sheria zao wasiende *to the extend* na wale wanaokosea tumekuwa tukiwachukulia hatua, wengine wanafukuzwa lakini wengine wanashitakiwa mahakamani na hii ni pamoja na hata hii mliyozungumza hapa ya mauaji ya Ndugu Mwangosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo niliona pia niliseme ili litusaidie. Polisi hawa hawa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Ibara ya (11), ndiyo wamepewa jukumu la kusimamia ulinzi, amani na usalama wakati mnapoendesha mikutano yenu ya kisiasa. Polisi hawa hawa chini ya Sheria ya Uchaguzi ambayo wamepewa jukumu la kusimamia ulinzi, amani na usalama wakati wa mikutano ya kampeni ya vyama vya siasa wakati wa uchaguzi. Vilevile ni Polisi hawa hawa ambao pia ndiyo wamepewa jukumu la ulinzi na amani wakati wa kura za maoni. Kwa hiyo, hatuna namna tunayoweza kuwakwepa na ni mtu wa ajabu sana ambaye hatataka kuwa na urafiki na Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa sababu kengele imegonga ni hili lililozungumzwa juu ya Katiba Inayopendekezwa kwamba, haina kifungu ambacho kinaiwajibisha Serikali kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu. Niseme tu kwamba, katika Katiba hii ni Sura ya Tano na haki hizi zimetolewa kuanzia Ibara ya 32 zinaenda mpaka Ibara ya 48. Ningekuwa na muda ningeziorodhesha, lakini unaanza na Ibara ya 64, Ibara ya 65(2) inasema, mtu anayeamini kuwa masharti yaliyomo katika Sura hii yamekiukwa au yanaelekea kukiukwa na mamlaka, chombo cha uamuzi, sheria au sera yoyote dhidi yake, anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu kwa hati maalum ya maombi kwa mujibu wa sheria za nchi ili kupata nafuu inayohitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ndogo ya kwanza, Makahama inaweza kutoa maelekezo itakayoona yanafaa kuweka zuio, katazo, kuamuru jambo lisifanyike ambalo lilikuwa limezuiwa. Ibara ndogo ya (4) inatoa fursa kwa kila mtu ambaye ameathirika na kile kitendo, kufungua shauri, wametajwa wale watu pale. Ningekuwa na muda ningezitaja hizi haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, mimi kama mtu ambaye ni Mtaalam wa masuala ya Sheria za Katiba na ndiye Mshauri wa Masuala ya Kikatiba, niseme tu kwamba, hii ni *document* ya Kikatiba ya muhimu sana. Watanzania tusije tukafikia hatua tukaiacha hii, kama tutaiacha hii Katiba, Taifa hili litabaki kuwa tegemezi. Ni Katiba ambayo inaweka *legal framework constitutional* ya kutufanya sisi Serikali iwajibike. Ni Katiba ambayo ina-address maadui watatu wakubwa ambao Mwalimu aliwasema tangu wanzo; ujinga, umaskini na maradhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa zipo haki za wafungwa, wafugaji, wakulima na wavuvi. Hapa kuna haki za afya na uzazi salama, kuna haki za maji safi na salama. Kuna haki ya kila aina; haki ya uhuru wa habari na kadhalika. Ningeweza kuyasema lakini siku za karibuni tutatafuta fursa tuyaseme haya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena, nikushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia. Kwa mara nyingine tena niseme ninaishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa inayofanya. Miaka hii mitano imefanya mambo makubwa sana na kwa ujumla miaka yote kumi imefanya mambo makubwa sana. Niseme tu kwamba, hatuna sababu ya kuitilia mashaka, kwa sababu kazi zake zinaonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa AG. Sasa ninamwita Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Katiba na Sheria. Karibu Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena nashukuru kwa kupata fursa hii ili niweze kujibu hoja mbalimbali zilizojitokeza kama hatua ya kuelekea kwenye kuhitimisha hoja yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, wakiongozwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, kwa maoni na ushauri waliotupatia na maelekezo yao ambayo nitayatolea kauli hivi karibuni. Pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuchangia hoja mbalimbali kwa umahiri mkubwa, zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Vilevile nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kujibu kwa umahiri kabisa na kwa usahihi hoja zilizoibuliwa kama ambavyo amekamilisha kusema hivi karibuni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuzungumzia hoja za Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Mojawapo ya hoja zilizotolewa na Kamati ni kwamba, Wizara iandae Muswada wa Sheria na kuunda chombo mahususi

kuratibu utoaji wa huduma za msaada wa kisheria. Naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, hilo ndilo ambalo Serikali inafanya kupitia Wizara yetu; hivi sasa tumeandaa Waraka ambao upo katika ngazi mbalimbali za maamuzi kama nilivyokwishasema kwenye Hotuba yangu aya ya 57, ambapo tumeeleza kwamba katika mwaka ujao wa fedha tunakusudia kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hicho kitakachoundwa kitakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za msaada wa kisheria na kuzifanya kuwa huduma ya uhakika na haki kwa wale wanaohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imetuagiza tuendelee kuratibu na kusimamia kikamilifu taasisi zilizo chini yetu na kuhakikisha zinatekeleza kikamilifu majukumu yake. Sisi Wizara tumekuwa karibu sana na taasisi zilizo chini yetu na tumekuwa tukifanya hivyo na kama tulivyosema, tumeshachukua hatua mbalimbali kuongeza bajeti, kuongeza uwezo wa kiutendaji na pia kuufahamisha umma kuwepo kwa taasisi hizi ili waweze kunufaika na huduma zinazotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa tutenge fedha za kutosha na kwa wakati ili kuunga mkono au kutia nguvu mfumo wa sheria nchini, hilo tunaendelea kulifanya na kwa kushirikiana na wadau wengine ndani ya Serikali na nje ya Serikali, tutafanya hivyo na tunakusudia kutenga bajeti ya kutosha kuwezesha taasisi za Wizara kujenga majengo yake na hivyo kupunguza gharama kwa kutumia majengo ya kupanga. Hili ni suala ambalo Waheshimiwa Wabunge kadhaa wamelizungumzia na Mheshimiwa Ummy amewataja baadhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata ushauri kwamba, tuangalie masuala ya madeni ya Watumishi wa Wizara na wazabuni na kuyalipa kwa wakati kwa lengo la kuimarisha ari kwa watumishi na wazabuni. Kwa upande wa Watumishi, sisi tunaamini kwamba, rasilimali kuu ya Wizara yetu ni Watumishi na kwa maana hiyo tunayo mipango mbalimbali ambayo tumeshajieleza, lakini tunazingatia ushauri wa Kamati na tutafanya hivyo bila ya kusita kwa sababu wao ndiyo msingi wa kazi tunazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja iliyohusu ufaulu wa wanafunzi wa taasisi ya mafunzo ya washeria kwa vitendo. Waheshimiwa Wabunge baadhi yao na Kamati pia imesema inashauri tusimamie kwa kikamilifu taasisi hii kwa kufanya utafiti hasa kutokana na hoja iliyotolewa kuhusu ufaulu wa wanafunzi. Ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, ufaulu wa wanafunzi wa taasisi ni wastani wa asilimia 20 mpaka 30 kwa kikao cha kwanza cha mtihani. Asilimia 60 mpaka 70 hutakiwa kufanya mitihani ya marudio na

wanafunzi wanaoshindwa kwa takwimu tulizonazo na utafiti tuliofanya ni asilimia 10 tu na hivyo hawa ndiyo wanaotakiwa kurudia mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaribu kutazama yale yanayojiri katika nchi zinazofanana na sisi hasa ndani ya Afrika Mashariki na tumeona kwamba, viwango hivi vya ufaulu vinafanana na za taasisi nyinginezo zinazofana na ya kwetu katika nchi za Afrika Mashariki hususan Kenya na Uganda. Hata hivyo, Bodi ya Uendeshaji wa Taasisi iliunda Kamati Maalum ya kutathmini mambo yanayosababisha viwango vya sasa vya ufaulu kuonekana viko chini na kupendekeza namna bora ya kuboresha mafunzo ya mtihani. Kamati hiyo iko katika hatua za mwisho za kukamilisha kazi hiyo na pindi taarifa hiyo itakapopatikana, basi sisi kwa kushirikiana na bodi ya uendeshaji wa taasisi, tutahakikisha kuwa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na vilevile Waheshimiwa Wabunge mbalimbali yanatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeulizwa ni lini wanafunzi wa Taasisi ya mafunzo ya Wanasheria Tanzania watapata posho ya kujikimu. Kama nilivyosema kwenye Hotuba yangu, tulifanya mashauriano na wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tukakubaliana marekebisho ya sheria yafanywe na yakafanywa. Katika mwaka 2014/15, Serikali ilitenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo. Tayari Serikali imeshatoa fedha za awali ambazo ni shilingi 827,516,124. Shilingi bilioni 1.8 zipo kwenye hatua ya mwisho na tunategemea wiki ijayo zitaweza kutolewa. Fedha hizi zitaweza kumaliza kabisa mahitaji ya wanafunzi kwa mwaka 2014/15.

Kuanzia Mwaka wa Fedha 2015/16 na kuendelea, wanafunzi wa taasisi hii wataweza kupata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, kwa sababu uamuzi ule ulipopitishwa tulikuwa tayari tupo katikati ya mwaka wa fedha. Kuanzia mwaka 2015/16 suala hili litaingia kwenye utaratibu wa kawaida wa mikopo na nichukue fursa hii kuwashukuru Wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo kwa kustahamili na kuweza kuelewa jitihada ambazo Serikali ilikuwa inazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata ushauri kwamba, Mitaala ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo iingizwe kwenye mitaala ya Vyuo Vikuu ili wahitimu wa sheria kutoka vyuo hivyo waweze kuajiriwa moja kwa moja ili kuondoa upungufu wa wanasheria. Kwanza, tunapenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge Rosweeter Kasikila, kwa kuweza kufuatilia kwa karibu jinsi ambavyo taasisi hii inaendeshwa. Tunapenda kusema kwamba, mafunzo ya wanasheria kwa vitendo yanaendeshwa kwa utaratibu wa mtaala mahususi. Azma ya taasisi ni kuwanoa vijana wetu wa kike na wa kiume ambao wameshamaliza masomo yao ya sheria wameshapata shahada. Kwa hiyo, kwa utaratibu uliopo sasa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, viko Vyuo vingi

ambavyo vinatoa mafunzo, vinatoa wanasheria na kwa hiyo taasisi hii pamoja na taasisi ile ya Lushoto, kazi zao ni kutoa mafunzo endelevu ya Makarani, Mahakimu, Majaji wakati taasisi ya wanasheria kwa vitendo inawanao wanafunzi baada ya kumaliza shahada yao na kuwatayarisha waingie katika soko la kujijiri wao wenyewe au la kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauriwa pia tumeelekezwa kwamba, tuiimarisha Tume ya Kurekebisha Sheria. Ni kweli kabisa tunakubaliana na Kamati na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Tume ya Kurekebisha Sheria inafanya kazi kubwa na ina mchango mkubwa. Tunapenda kusema kwamba, Serikali itaongeza kasi ya kufanyia kazi mapendekezo yanayohusu maboresho ya sheria yanayotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria ili kuhakikisha kuwa sheria zinakidhi mahitaji na matakwa ya wakati uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara imetakiwa iweke mfumo wa namna Wizara na taasisi zinazofanya utafiti kuhusu sheria mbalimbali kusimamia Tume ya Kurekebisha Sheria kwani ndiyo yenye jukumu kisheria la kufanya utafiti. Hilo ni jambo linaloendelea na Tume hii imekuwa ikiisaidia sana Serikali katika kufanyia mapitio ya sheria au kutunga sheria mpya na hilo lisingewezekana kama wasingefanya utafiti, nasi tutaungana nao kuhakikisha wanapata nyenzo za kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kuwashukuru Wabunge katika eneo hilo. Niende sasa kwenye eneo linalohusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kwanza, niseme kwamba, asubuhi hapa kulikuwa na baadhi ya Wabunge waliochangia akiwemo Mheshimiwa Tundu Lissu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, Serikali inajisikiaje Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inapotoa ripoti ikionesha kuna upungufu wa hapa na pale.

Mheshimiwa Stella Manyanya ametueleza vizuri sana kwamba, kwa kweli Tume hii imeonesha udhaifu pale palipo na udhaifu na tusingetegemea kitu kingine chochote kutoka kwenye Tume Huru ambayo imepewa mamlaka yote ya kufanya uchuguzi na kutoa Taarifa yao. Tunachokisema ni kwamba, kama kuna askari mmoja, wawili, watatu, wamefanya vitendo vinavyoonekana kukiuka haki za binadamu au utawala bora, hilo ni suala la hao na Serikali iko tayari kabisa kufanyia kazi mapendekezo haya. Ninadhani ingekuwa ni jambo la kujivunia kwamba, Tanzania tumeingia katika ramani ya dunia kuwa na Taasisi ambazo zinaundwa, zinapewa uhuru na zinafanya kazi bila ya uwoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imetolewa hoja na tunaichukua hoja hiyo na tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kuweza kuliona hilo kwamba, bado Tume inakabiliwa na changamoto za fedha. Hizi ni Taasisi, kama tulivyosema, Taasisi hii ni ya kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu. Kwa hiyo, Serikali inathamini sana kazi ya Tume hii, hasa kwa kuzingatia

kwamba, yale ambayo Tume hii inayasimamia ndiyo msingo wa Katiba ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge tumeipitisha katika Bunge hili. Kwa hiyo, ni vyema kazi za Tume hii zikapewa usaidizi, zikapewa nyenzo na zikapewa hamasa ya kufanya kazi ambazo inategemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Tume ina uhaba wa vitendea kazi, lakini Serikali inafanya jitihada za dhati kuhakikisha Tume inawezeshwa, ili iweze kupata vifaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na magari, *computer* na kadhalika. Katika Mwaka wa Fedha 2015/16 Tume inategemea kununua japo gari moja jipya na kadiri fedha zitakavyopatikana, Serikali itaendelea kuhakikisha Tume inawezeshwa ipasavyo. Hizo ni jitihada ambazo tutaendelea nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunatambua umuhimu wa kusogeza huduma za Tume karibu zaidi na wananchi. Hadi kufikia Mwaka wa Fedha 2014/15 Tume iliweza kufungua jumla ya ofisi tano. Waheshimiwa Wabunge wameeleza na sisi tunakubaliana nao kwamba, ipo haja ya kusogeza huduma hizi kwa wananchi. Hivi sasa tumefanikiwa kufungua kupitia Tume hii, ofisi tano kwa nchi nzima; Dar es Salaam, Zanzibar kwa maana ya Ofisi zinazoongozwa na Kamishna Mkazi kwa mfano kule Unguja ipo, Ofisi ya Tawi Pemba, Ofisi ya Tawi Lindi kwa ajili ya kutoa huduma kwa Wananchi wa Mikoa ya Kusini. Vilevile tunayo Ofisi ya Mwanza kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa Wananchi kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Tutaendelea ili huduma za Tume hii ziweze kuwafikia wananchi wengi kwa kadiri inavyowezekana na hali itakapokuwa nzuri, tayari tumeshaweka mpango ambapo tunakusudia kufungua Ofisi au Matawi ya Tume hii katika Mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia baadhi ya hoja hizo, ningependa sasa nijielekeze kwenye hoja zilizotolewa na Wabunge mmoja mmoja. Ninajua kwamba, wenzangu Naibu Waziri na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wamejibu, kwa hiyo, kazi yangu itakuwa ni kutoa majibu ya ziada au pale ambapo hayakutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza kwa kujielekeza kwenye hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Aliko Kibona, Mbunge wa Ileje, ambaye amezungumzia kwa uchungu kabisa suala la usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyokiri yeye mwenyewe gari lilipelekwa, lakini kwa taratibu za kiuendeshaji gari lile likawa nje ya Ileje. Mara baada ya kuahirishwa Bunge, nimetoa maelekezo na gari hilo sasa litakwenda Ileje kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia Mheshimiwa Aliko suala la umbali wa Mahakama. Suala hili limezungumziwa pia na Wabunge Kadhaa. Kuna Mheshimiwa Esther Matiko alizungumzia suala hili, Mheshimiwa Susan Kiwanga amezungumzia suala la umbali wa Mahakama, Mheshimiwa Lwanji amezungumzia kutokukamilika kwa ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo, Mheshimiwa Chilolo vilevile amezungumzia suala la ukarabati na Waheshimiwa wengine pia, wamezungumzia suala la ukarabati na umbali akiwemo Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Hawa wote wamezungumzia suala la umbali wa Mahakama na kutokuwepo kwa Mahakama ambazo zinatoshleza utoaji wa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo Naibu Waziri amesema kwamba, tutatoa mpango utakaoonesha ni lini tunakwenda katika maeneo gani ambayo yanahitaji ukarabati au kujengwa majengo ya Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumekuwa na swali au hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Magreth Agness Mkanga, ambaye amezungumzia suala la hukumu za watu waliohusika kufanya mauaji ya watu wenye u-*albino*. Ni lini hukumu hizi zitatekelezwa?

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwamba, Serikali inachukulia kwa uzito sana suala hili la mauaji ya watu wenye u-*albino* na hata suala la viungo vyao kukatwa. Ningependa kusema kuhusiana na suala la hukumu, ni kweli wapo ambao wameshahukumiwa, lakini tuhamu pia kwamba, kuna utaratibu wa Kisheria hata pale ambapo hukumu imeshatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo hukumu imetolewa na Mahakama Kuu, Sheria inataka suala lile likatiwe rufaa. Ni fursa ya kukata rufaa kwa yule aliyehukumiwa na hayo ni matakwa ya Kisheria. Endapo Mahakama ya Rufani itathibitisha adhabu ile iliyotolewa na Mahakama Kuu, basi vilevile kuna mchakato mwingine wa Kisheria; kuna Kamati ambayo inaundwa kwa mujibu wa Sheria, Sheria inayohusika ni Sheria inayohusu masuala ya Rais (*Presidential Affairs Act*) ambayo inataka kwanza, Mheshimiwa Rais aweze kushauriwa na Kamati ya Msamaha au Kamati ya Huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii inatakiwa kuitazama tena ile hukumu na siyo hukumu peke yake, kutazama mazingira, kwa sababu kama mnavyofahamu hukumu ya kifo inataka ifanywe kwa uangalifu sana. Baada ya kupitia hapo ndipo ambapo Mheshimiwa Rais anashauriwa na yeye anaweza akatoa adhabu. Hii haimaanishi kwamba, nia ni kuchelewesha, kwa upande wa Serikali tutafanya kila linalowezezana tufikishe pale ambapo hukumu hizi

zinatakiwa kufikishwa na kuachia mchakato wa Sheria uweze kuchukua mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulisemwa hapa suala la Mahakama kuendeshwa Kisiasa. Hili ni suala ambalo tungependa kushauri kwamba, liangaliwe kwa karibu sana. Mahakama ni chombo kilicho huru na kama ambavyo tuliona hapa asubuhi kwamba, Tume ile japokuwa Mwenyekiti wake anateuliwa na Rais, ina uhuru wote ambao inahitaji kuendesha shughuli zake. Vilevile kwa Mahakama, wakati mwingine kumekuwa na hoja kwamba, Mahakama hizi haziko huru kwa sababu zinateuliwa na Rais. Sasa pale tunaposema kwamba, Mahakama zinaendeshwa kisiasa kwa kweli ni kama tunataka kuingilia utendaji wao kwa kuwafanya waingie hofu au waingie uwoga kwa kuonekana kwamba, wakiamua aina moja wanaweza wakaambiwa wanafanya kisiasa. Mimi ningependa tuheshimu uhuru wa Mahakama, tuheshimu kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliulizwa suala la msaada wa kisheria, kwa maana ya sheria; hiyo nimeshajibu. Kulikuwa na maelekezo kwamba, tutambue Wasaidizi wa Sheria, wale wanaoitwa *Paralegals*. Kama nilivyosema, tumetayarisha Waraka ambao utawezesha hii Sheria kuweza kutungwa. Ndani ya Sheria hii kuna suala la kuwatambua Wasaidizi wa Sheria na kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na suala la Mahakama ya Kadhi. Napenda nimshukuru *Atorney General*...

MWENYEKITI: Waheshimiwa minong'ono imezidi!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Atorney General* amelijibu suala hili vizuri, lakini yale yaliyotokea hayakuwa siri, inafahamika vizuri ni hoja gani zilijitokeza na nini kimefanya mashauriano yaendeleo kama ambavyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema. Hakukuwa na sababu yoyote ambayo ingemfanya Waziri ashindwe kuzungumzia Mahakama ya Kadhi, ila ni kuheshimu yale yaliyojiri na kutoa fursa kwa mashauriano kama ambavyo *Atorney General* ameeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia suala la TAKUKURU na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa *Atorney General* amezungumzia kwa ufasaha kabisa namshukuru. Suala hilo liko ndani ya Katiba, lakini ningependa pia kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, Sheria tuliyoipitisha sisi wenyewe hapa, Sheria ya Kuanzisha TAKUKURU sinayo hapa, lakini inazungumzia wazi mashauri yote ambayo yanahitaji kupelekwa Mahakamani yatafanyiwa hivyo baada ya kupata Kibali cha Mwendesha Mashitaka Mkuu. Ninapenda kuwahakikishia Wabunge kwamba, hakuna msugvano wowote kati ya Taasisi hizi mbili, zinafanya kazi kwa ushirikiano na

Kifungu cha 15 cha Sheria iliyoanzisha TAKUKURU, kinatamka wazi kwamba, TAKUKURU inayo mamlaka ya kufungua baadhi ya mashauri bila ya kupata ridhaa ya Mwendesha Mashitaka Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwahakikishia kwamba, Taasisi hizi zinafanya kazi vizuri. Pale ambapo kuna upungufu, basi itakuwa ni suala la kuingalia tena Sheria na Katiba, kama ambavyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia suala ambalo Mheshimiwa Chilolo amelizungumzia. Amelisema vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri na mimi ningependa kuungana nae. Ningependa kuungana na Mheshimiwa Chatanda, wote hawa wamekuwa wakitufuatilia kwa karibu kuhusu masuala yanayohusu Mahakama na uendeshaji wa shughuli za Mahakama zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuushukuru mchango wa Mheshimiwa William Ngeleja, ambapo ametumia muda wake kunukuu yale ambayo yametusaidia sana tunapochambua mambo haya. Lazima tufahamu kwamba, hatima ya nchi yetu iko mikononi mwetu; endapo tutatumia jazba, siasa na mambo ambayo hayako sahihi ili kuweza kuvuta hisia za wananchi, kwa kweli tutakuwa hatujitendei haki sisi wenyewe. Tukumbuke kwamba, endapo kutakuwa na mtetereko wowote wa amani na utulivu wa nchi yetu, basi hakuna atakayesalimika.

Napenda kutoa ombi kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunapozungumzia masuala haya yanayohusu utoaji haki, kwa kweli tuyachukulie kwa uzito wake.

Vilevile wapo Waheshimiwa ambao wamezungumzia suala la mtazamo wa baadhi ya Viongozi wa Dini; ningependa kuwathibitishia kuwa sisi kama Serikali hatuna mgogoro wowote, tunaheshimu sana Viongozi wa Dini. Kila fursa ilipojitokeza, tumeweza kuzungumza nao kwa sababu sisi sote tunajua nafasi yao na mchango wao ndani ya jamii na hata katika sheria zetu, Viongozi hawa wanatazamwa kwa jicho tofauti na ambavyo mtu mmoja mmoja anatazamwa. Kwa hiyo, napenda kuwahakikishia kwamba, sisi hatuna lolote ambalo tunaweza tukasema ni tofauti na Viongozi wa Dini na tupo tayari kushirikiana nao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa kuzungumzia suala ambalo lilijitokeza kwenye Hotuba ya Kambi ya Upinzani. Mojawapo ya mambo yaliyojitokeza na hili linalohusu suala la Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kueleza kwamba, suala la Kura ya Maoni ni suala la matakwa ya kisheria. Kama Waheshimiwa Wabunge tutakumbuka, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Ibara ya 28(b) inasema kwamba, masharti ya Katiba Inayopendekezwa yatakamilishwa kwa Kura ya Maoni. Sheria ya Kura ya Maoni inaweka utaratibu kupitia Kifungu cha 4(1) na (2), ambavyo vinaweka utaratibu utakaomtaka Rais aiaturu Tume kupitia amri itakayokuwa imetolewa, kuelekeza Tume kuendesha Kura ya Maoni. Amri hiyo, inatakiwa kwa mujibu wa Sheria kuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kura ya Maoni. Hilo lilifanyika tarehe 20 Oktoba 2014 baada ya kufanyiwa marekebisho tarehe 16 Oktoba.

Marekebisho ya utaratibu wa Jedwali hili yalifanyika chini ya Kifungu cha 51 cha Kura ya Maoni, marekebisho ambayo hayakuhitaji Muswada wowote Bungeni. Ni marekebisho ambayo yanafanywa na Mawaziri wenye dhamana za uchaguzi, ambao ni Waziri Mkuu, akishauriana na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria zetu, endapo mamlaka yametolewa kwa mtu au mamlaka fulani kutekeleza wajibu fulani, wajibu huo unaweza kutekelezwa mara kwa mara kwa kadiri mazingira yatakavyohitaji. Hivyo, Jedwali hili lilifanyiwa marekebisho ili kuruhusu Kura ya Maoni ifanywe na kwa amri aliyotoa Mheshimiwa Rais, ilitajwa muda wa kampeni na kupiga Kura ya Maoni. Kwa maana hiyo, hakuna ambacho kipo nje ya sheria na kinachoendelea kufanyika sasa ni matakwa ya sheria kwamba, Daftali la Mpiga Kura linahitaji kuboreshwa na ndiyo kazi inayoendelea sasa. Itakapokuwa limeboreshwa ndipo hatua nyingine zitaweza kufikiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kulihakikishia Bunge lako kwamba, Sheria zote zimefuatwa baada ya kukamilika kwa utaratibu huo wa kupata Katiba Inayopendekezwa, hatua inayofuata inatawaliwa na Sheria ya Kura ya Maoni na hadi hivi sasa hakuna ambalo limetoka nje ya utaratibu wa Sheria.

Ningependa kuhitimisha majibu haya kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge. Ninapitia orodha yangu hapa ninaona yote tumeyajibu, kama sikuyajibu mimi walijibu wenzangu, lakini labda nizungumze moja ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Lucy Nkya. Naungana nae, mimi ni mmojawapo wa wadau wakubwa sana wa Lugha yetu ya Taifa na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tunachukua hatua mbalimbali. Vilevile tutaimarisha suala zima la Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia vyeti vitolewe kwa ajili ya usajili; hiyo ndiyo kazi ambayo tunaifanya. Kama tulivyosema, tumeweka mkakati mahususi wa kuandikisha. Tutaendelea kufanya hivyo na kupitia kwenu Wabunge, tutawaomba tukae sambamba na wananchi katika kuhimizana suala la uandikishaji wa vizazi na matukio mengine muhimu ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikamilishe kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge. Nakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kutuongoza vyema katika mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nawashukuru wote waliochangia kwa maandishi na kwa kauli ambao walikuwa takribani 27. Ninataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumepokea hoja ambazo mmetupatia, tutazifanyia kazi na zile ambazo hatukuweza kuzijibu hapa, tutazijibu kutokana na Mipango ambayo tumeiweka kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tutazijibu kwa njia ya maandishi na kuwagawia Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

Kif. 1001 – *Administration and HR*

ManagementSh. 2,673,242,000/=

Kif. 1002 – *Finance and Accounts*.....Sh. 157,908,000/=

Kif. 1003 – *Procurement Management Unit*...Sh. 61,925,000/=

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*.....Sh. 6,100,000/=

Kif. 1005 – *Recruitment, Appointment and*

Confirmation.....Sh. 896,061,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 – *Ethics and Discipline Section*.....Sh. 208,220,000/=

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub-Vote 210300 - Personnel Allowance (Non-Discretionary) Optional*, naona kuna zero, nilikuwa najjuliza ni kitu gani ambacho kimetokea hapo kwa sababu naona mwaka jana walikuwa wana pesa ambazo ni nyingi kidogo, shilingi milioni 797,700,000. Naomba ufafanuzi kutoka Serikali ni kitu ambacho kinaendelea hapo?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru sana Mheshimiwa Machali kwa kulionyesha hili. Katika majibu yangu tulisema kwamba, kifungu hiki kinahusu Kamati za Maadili za Wilaya na Mkoa, ambapo sasa tunataka tuzirudishe; yaani sheria inazianzisha kwamba, Mwenyekiti ni Mkuu wa Wilaya kwa ngazi ya Wilaya na Mwenyekiti ni Mkuu wa Mkoa kwa ngazi ya Mkoa. Kwa hiyo, tunataka fedha za

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuendesha vikao hivi ziwe katika Bajeti za Wilaya na Bajeti za Mikoa. Kwa hiyo, sisi Wizara kazi yetu kubwa itakuwa ni kutoa mafunzo kwa Kamati hizi kuhusu majukumu yake na kuzifanyia ukaguzi wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Machali anazidi kuthibitisha hoja yangu kwamba, tutakaporudia katika Vikao vya ushauri vya DCC na RCC, tuwaulize DAS na RAS hela za kuendesha Kamati za Ushauri za Wilaya na Mikoa ziko wapi. Nakushukuru. (Makofi)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu – 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1001 – Administration and HR

Management.....Sh. 2,919,707,000/=

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye Sub-Vote 220700 - Rental Expenses. Nina swali moja, naona wametenga kiasi cha shilingi milioni 229,800,000. Swali langu ni moja; nimekuwa kwa nyakati tofauti nikichangia kwenye michango yangu miaka tofauti juu ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Wilaya ya Kasulu na hasa Ofisi ya Mwendesha Mashitaka, AG. Naomba kujua, je, katika fedha hizi ambazo ni za rental expenses, tena pale kulikuwa kuna jengo la Serikali ambalo pengine mngelitumia lilikuwa inatumiwa na TRA zamani; kutakuwa kuna fedha kwa ajili ya kuanzisha Ofisi hii katika Wilaya ya Kasulu kwa sababu tunaona mambo hayaendi sawasawa?

Naomba ufafanuzi wa Serikali kama kwa kutumia fedha hizi tunaweza tukapata fedha za kuanzisha Ofisi hii katika Wilaya ya Kasulu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi, hela hizi zitumika pia Kasulu?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu ni kwamba, katika mwaka huu wa fedha tumepanga kuajiri Mawakili wa Serikali 332. Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake alionyesha kwamba tutaanza, tumeanza Temeke na Monduli, Kasulu bado haiko katika Mpango.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – Finance and Accounts Unit.....Sh. 876,209,000/=

Kif. 1003 – Planning Division.....Sh. 840,574,000/=

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 1004 – Internal Audit Unit.....	Sh. 533,963,000/=
Kif. 1005 – Government Communication Unit	Sh. 235,297,000/=
Kif. 1006 – Legal Registry Unit.....	Sh. 324,930,000/=
Kif. 1007 – Procurement Management Unit..	Sh. 480,685,000/=
Kif. 1008 – Research and Library Service Unit	Sh. 223,038,000/=
Kif. 1009 – Information and Comm. Technology Unit.....	Sh. 423,608,000/=
Kif. 2003 – Legislative Drafting.....	Sh. 1,346,838,000/=
Kif. 3001 – Civil Litigation and Arbitration Division.....	Sh. 1,310,774,000/=
Kif. 3002 – Treaties and Contracts Division..	Sh. 1,279,204,000/=
Kif. 4001 – Constitutional Affairs and Human Rights.....	Sh. 946,056,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu – 35 – Divisheni ya Mashitaka

Kif. 2002 – Public Prosecutions Division.....	Sh. 7,874,319,000/=
Kif. 2004 – Zonal Office Arusha.....	Sh. 1,190,585,000/=
Kif. 2005 – Zonal Office Dodoma.....	Sh. 618,562,000/=
Kif. 2006 – Zonal Office Dar es Salaam.....	Sh. 2,216,293,000/=
Kif. 2007 – Zonal Office Iringa.....	Sh. 467,143,000/=
Kif. 2008 – Zonal Office Moshi.....	Sh. 515,292,000/=
Kif. 2009 – Zonal Office Kagera.....	Sh. 447,749,000/=
Kif. 2010 – Zonal Office Mbeya.....	Sh. 619,587,000/=
Kif. 2011 – Zonal Office Mtwara.....	Sh. 421,850,000/=
Kif. 2012 – Zonal Office Mwanza.....	Sh. 955,789,000/=
Kif. 2013 – Zonal Office Ruvuma.....	Sh. 375,468,000/=
Kif. 2014 – Zonal Office Sumbawanga.....	Sh. 369,765,000/=
Kif. 2015 – Zonal Office Tabora.....	Sh. 600,113,000/=
Kif. 2016 – Zonal Office Tanga.....	Sh. 640,518,000/=
Kif. 2017 – Zonal Office Shinyanga.....	Sh. 552,552,000/=
Kif. 2018 – Zonal Office Singida.....	Sh. 300,433,000/=
Kif. 2019 – Zonal Office Lindi.....	Sh. 266,273,000/=
Kif. 2020 – Zonal Office Mara.....	Sh. 353,253,000/=
Kif. 2021 – Zonal Office Manyar.....	Sh. 288,497,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2022 – Zonal Office Kigoma.....	Sh. 325,262,000/=
--------------------------------------	-------------------

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza kwenye *item 220700 - Rental Expenses*. Nafikir suala ambalo nimeliuliza pale hapa ni mahali pake. Naomba kauli ya Serikali na hapa mmetenga pesa tena shilingi milioni 24; zimeongezeka vipi mnaweza mkatufikiria Kasulu pengine kuwa na Ofisi hii pale; kwa sababu kumekuwa na ahadi za Serikali tangu mwaka juzi nimehoji hata mwaka jana nimehoji; mkatupa matumaini mtafanya?

Sasa kidogo nimekuwa *disappointed* na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba ufafanuzi; ni lini sasa utekelezaji wa ahadi za tangu mwaka juzi utafanyika maana nimekuwa najaribu kuhoji na kufuatilia mpaka Ofisi ya Mwendesha Mashika, DPP, lakini hakuna kitu ambacho kimefanyika mpaka leo hii, tangu mwaka juzi na mliahidi; itaanza au haianzi mwaka huu?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Moses Machali. Nakubali umuhimu wa kuwa na Ofisi ya DPP katika Wilaya ya Kasulu, lakini katika mwaka huu wa fedha bado tutajikita katika Mkoa wa Kigoma, kwa sababu tunaenda katika Wilaya awamu kwa awamu. Naomba nikuthibitishie na Mheshimiwa Waziri yuko hapa, tutajitahidi katika mwaka wa fedha ujao kutoa kipaumbele. Kubwa, tunatazama pia na wingi wa kesi katika eneo husika, siyo kwamba tunafungua tu Ofisi ya Mwendesha Mashitaka katika Wilaya, lakini tunaangalia na wingi wa kesi. Mpango ni kufika katika Wilaya zote za Tanzania. Mheshimiwa Machali naomba utukubalie.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2023 – Zonal Office Pwani.....Sh. 430,795,000/=
Kif. 2024 – Zonal Office Njombe.....Sh. 292,451,000/=
Kif. 2025 – Morogoro.....Sh. 332,709,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2026 – Zonal Office Geita Sh. 295,041,000/=

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *Sub-Vote 2026, Item 210100 - Basic Salaries - Pensionable Posts*. Mwaka 2014/2015 ilikuwa ni shilingi 51,032,000, lakini hapa imekuwa shilingi 95,041,000. Mbona imezidi sana kuna nini hapa? Naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kuna nini hapa ufafanuzi?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rukia. Katika Hotuba yetu tulionyesha kwamba, mojawapo ya kazi kubwa tutakayoifanya katika mwaka huu wa fedha ni kuongeza watumishi katika Ofisi ya Mwendesha Mashitaka wa Serikali, DPP. Kwa hiyo, kutakuwa na ongezeko la Watumishi lakini pia na ongezeko la mishahara.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2017 – Zonal Office Simiyu.....Sh. 218,600,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2018 – Zonal Office Katavi.....Sh. 233,722,000/=

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kwenye Sub-Vote 2018, Kifungu Namba 221000 - Travel in Country. Kifungu hiki mwaka 2013/2014 hakikuwa hata na shilingi moja, 2014/2015 kuna milioni 23, lakini mwaka 2015/2016 kuna milioni 53,400,000. Kumezidi nini hizi safari mpaka ikafikia hivi? Naomba ufafanuzi.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rukia. Katika michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wanazungumzia suala la ucheleweshaji wa kesi, ikiwemo na masuala ya upelelezi, kwa hiyo, hela imeongezeka kwa ajili ya kuwawezesha Ofisi ya DPP katika Mkoa wa Katavi kuhakikisha wanatembelea Wilaya zote za Mkoa huu. (Makofi)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama

Kif. 2002 – Court of Appeal

Dar es Salaam.....Sh.138,085,699,000/=

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mahakama za Mwanzo Maji ya Chai iliyoko Halmashauri ya Meru, Enaboisho, Emaoi na Nduruma zilizoko Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, majengo yake yamechoka sana kwa sababu yamejengwa siku nyingi sana na hayajafanyiwa ukarabati.

Ningeomba kauli ya Waziri kama katika fungu hili moja ya kazi zitakazofanyika ni marekebisho ya Mahakama hizo au hapana?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Ole-Medeye, lakini naomba asubiri tutakapojadili Bajeti ya *Development* nitaweza kumjibu kama kazi hiyo ya kukarabati Mahakama zilizo katika Jimbo lake zimo au hapana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu – 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kif.1001 – *Administration and HR*

Management.....Sh. 6,721,203,000/=

MWENYEKITI: Okay, sasa kutokana Kanuni, vyama vimeleta majina ya wachangiaji au wanaoomba ufafanuzi. Nyote mnatakiwa mkae chini tafadhalini. Naanza na Mheshimiwa Moses Machali na ni masuala mahususi ya Kisera tafadhalini.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja ambalo kimsingi ningeomba Waziri anisikilize vizuri. Napenda kuiuliza Serikali kupitia Wizara hii ambayo ni *custodian* wa masuala ya kisheria hapa nchini. Hivi Serikali inaona fahari gani kutaka kutugawa Watanzania kupitia suala la kuruhusu baadhi ya madhehebu ya dini kuanzisha mahakama zao na katika hili ni kwamba siyo Sera ya Serikali ije *itu-separate* wananchi bali itulete wananchi pamoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetokea hapa mtafaruku wa jambo moja, suala la Mahakama ya Kadhi, ambayo liliibua *tension* kidogo. Ukisoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 19(2) na (3), imetamka bayana kwamba, mambo haya yatakuwa ni masuala binafsi na watu pamoja na madhehebu yao watakuwa na uhuru wa kuweza kuendesha mambo yao pasipo kuvunja sheria za nchi yetu.

Sasa hali ambayo ilijitokeza majuzi hapa na nimesikia kwenye majibu bado Serikali haiko straight. Leo mkiruhusu dhehebu fulani kuanzisha mahakama yao, mtakuwa mnataka na madhehebu mengine pia yaweze kuanzisha mahakama hizo. Kwa mfano, Kanisa Katoliki wana *Church Tribunal*, ambayo inaongozwa kwa mujibu wa *Cannon Laws*. Waislam wenzetu wana hicho chombo chao ambacho kinaitwa Mahakama ya Kadhi, lakini miaka michache iliyopita miaka ya 2008/2007 tulipata kusikia baada ya kuwa umeibuka mjadala huu mzito, dhehebu la Walutheri Tanzania walipata kusema nao kama

itaruhusiwa kuanzishwa Mahakama hiyo ya Kadhi, nao watataka waruhusiwe kuanzishwa kwa Mahakama ya Utekelezaji wa Amri Kumi za Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sikupata ufafanuzi nakusudia kutoa shilingi, natangaza hivyo. Swali langu ni moja; Serikali mtakuwa tayari kuruhusu tuue mfumo wa Mahakama za sasa ambazo zinatuhudumia wote kwa misingi ya usawa pasipo kujali itikadi zetu za kidini na badala yake mruhusu kuanzishwa kwa Mahakama za Kidini, kila dhahebu lianzishe dhehebu lake? Naomba ufafanuzi wa Serikali kuhusiana na masuala haya kwa sababu yameibua utata katika nchi yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mfupi uliopita, Bunge lako Tukufu lilimsikiliza Mheshimiwa Mbunge Rukia Ahmed hapa, juu ya kutokuwepo kwa Muswada wa hiyo Mahakama katika Bunge hili na akaituhumu sana Ofisi ya Mwanasheria Serikali na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mimi ushauri wangu ni kwamba, mwenzetu hili suala ameliwahisha maana siyo mjadala wake, haliko kwenye mjadala, la Kiseri si Sera, subiri Muswada uje hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya ambayo ni so *much sensitive*, tuliangalia sisi wenyewe ilivyokuwa siku ile kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa. Sasa mnataka tulilete tena sasa hivi? Labda kama hata lingekuja kwenye *plenary* mara ya kwanza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala litaanzisha kitu ambacho kwa sasa siyo lazima wakati yenyewe hii siyo hoja iliyoko mbele yetu. Mimi ndiyo ushauri wangu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninachotaka kusema, Serikali isikwepe maswali. Katika maelezo yangu nimesema kwamba, siyo Sera ya Serikali na nafikiri hata AG atakubaliana na mimi kwamba, Serikali inaweza ikawa na dhamira ya kutaka kutugawa Watanzania kwa sababu ya itikadi za kidini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ibara ya 19(2) imeeleza bayana na hili suala linahusu nchi nzima, liliibua utata hapa. Naiuliza tena Serikali, nataka mtueleze; kwa kuwa Katiba imeeleza bayana kwamba, masuala ya kidini ni mambo binafsi na Muswada ambao pengine mlikuwa mmekusudia kuuleta ni kuruhusu dhehebu moja kutaka kuanzisha Mahakama yake itambuliwe Kiserikali

na kweli wanaitaka na imeonekana suala hili mmewaahidi watu uongo miaka mingi. Tunataka Serikali itoe *position* yake iko wapi?

Kwa sababu nimesema, kuruhusu dhehebu moja kuanzisha Mahakama ya Kidini kutapalekea pia hata madhehebu mengine yatake kuanzishwa kwa mahakama zao. Jambo hili pia litakuja kupelekea pengine Serikali ifikirie kufuta Mfumo wa Mahakama tulionao, jambo ambalo ninaamini litakuwa ni baya zaidi.

Ninaomba kauli ya Serikali, tuelezeni leo mnapata msukumo gani na mnapata uwoga gani kusimamia misingi ya Kikatiba ambayo iko hapa?

Serikali naomba mtoe *position*, msikwepe maswali hapa. Hebu tuelezeni ni kitu gani ambacho kinawasukuma mtake kuleta mambo ambayo yanatugawa?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Machali, AG amezungumza hapa kuwa huo Muswada haujaletwa, leo tunazungumzia bajeti. Tusubiri mpaka ule Muswada utakapoletwa halafu utakuja kutoa hoja yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina Sera wala haitakuwa na Sera ya kuwagawa wananchi wake kwa msingi wowote ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Machali amefanya rejea kwenye Ibara ya 19(2); kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari la mtu binafsi na shughuli ya uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi. Ibara ndogo ya (3) inasema; hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa kitaifa. Kwa hiyo, upo wajibu wa kuweka utaratibu wa kisheria.

Kitu ambacho kimeombwa na wale wanaotaka Mahakama ya Kadhi ni kwamba, maamuzi yao ndiyo yatambuliwe, kwa sababu Mahakama hizo zipo kama tunavyofahamu na zinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Katiba inatutaka tuweke utaratibu wa sheria na utaratibu ule ulipoanza kumekuwa na mashauriano mbalimbali, ikiwa ni pamoja na semina ya Waheshimwa Wabunge iliyofanyika, ikiwa pamoja na michango ambayo ilitaka wajumuishe wadau wengi zaidi, siyo tu Waislamu wenyewe kwa wenyewe bali pia na wenzao wa imani nyingine.

Hicho ndicho ambacho Serikali inataka kukifanya kwa maana ya kuhakikisha utaratibu wowote wa kisheria utakaowekwa, utazingatia usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja kitaifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hakuna Sera ya Serikali ya kuwagawa wananchi. Tungemuomba Mheshimiwa Machali na wale wengine, wavute subira, hoja hiyo haijaja, lakini kama tunavyofahamu ni hoja ambayo inahitaji umakini mkubwa, tusiingize siasa mle, sisi ni Taifa moja, ni watu tuliowana, ni watu tuliokuwa marafiki. Kwa hiyo, ningeuomba kutoa mwito kwamba, sisi Wabunge tusiwe chanzo cha kuchokona. Nitumie pia fursa hii kuomba wale wanaotusikiliza kwamba, tusitumie kalamu zetu kubomoa, tutumie kalamu na kauli zetu kujenga. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Lwanji!

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumza kwenye *development*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aliko Kibona!

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Hoja yangu imejibiwa kifasaha, nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rukia Ahmed!

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu niligusia kuhusu Mashehe. Kwa kuwa wale ni Watanzania wenzetu na tuliwasikia katika vyombo vya habari wakisema wanahitaji kupatiwa matibabu afya zao siyo nzuri.

Mheshimiwa Waziri, naomba unipatie ufafanuzi mzuri juu ya matibabu wa Mashehe wale na kama hukunipa ufafanuzi, ukinitafunia maneno nazuia shilingi.

Je, ni kwa nini mpaka leo hawajapatiwa matibabu mpaka imefika mahali wamegoma wameshindwa wengine hata kufika Mahakamani kwenye kesi zao?

Mheshimiwa Waziri, wale ni Watuhumiwa bado hawajatiwa hatiani; nini hatma ya matibabu ya Mashehe wale?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri! Mheshimiwa AG!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza linao utaratibu mzuri tu kwa ajili ya tiba ya wafungwa na mahabusu wanaokuwa magerezani. Mimi ndiyo ninalisikia hili hapa kwa Mheshimiwa Rukia na kama tatizo limekuwa kubwa sana hawawezi kutibiwa hata kwenye *dispensary* za magereza, kwa sababu magereza haya yana *dispensary* mle ndani, basi huwa kuna utaratibu wanapelekwa kwenye hospitali za nje ya magereza. Kwa kesi kama hiyo wanaweza wakaenda hata Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili ndiyo tumelipata hapa, tutashauriana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani tujue kulikoni halafu Watanzania hawa wapate tiba. Hiki ndicho ambacho ninaweza kushauri hapa Mheshimiwa.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Bado sijaridhika kwa sababu hawa watu tuliwasikia wakiwa Mahakamani, wamesema maneno haya wakiwa Mahakamani na ni uhakika. Mimi nataka jibu. Wamepatiwa matibabu au hawajatiwa? Endapo hawajapatiwa naondoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rukia, leo asubuhi Mheshimiwa Waziri Mkuu aliulizwa swali hili na akaji-*commit* kuwa atalifuatilia.

(Hapa Wabunge fulani walipiga kelele kuonesha kutokubaliana na maelezo ya Mwenyekiti)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rukia endelea na hoja yako!

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ni binadamu kama binadamu wengine na ni Watanzania kama tulivyo sisi humu ndani. Bado ni watuhumiwa hawajatiwa hatiani, naomba watu hawa wapatiwe matibabu na jibu ninalitaka kutoka kwa Mwanasheria Mkuu kwa sababu Mkurugenzi wa Mashitaka yuko chini yake; wamepatiwa au hawajapatiwa? Na mimi nasema natoa shilingi.

WABUNGE FULANI: Toa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Rukia kwamba, haki ya kupata matibabu ni haki ya watuhumiwa na hata wale ambao watakuwa wametiwa hatiani pia wana haki ya kupata matibabu. Napenda kumwambia Mheshimiwa Rukia kwamba,

tumelipokea suala hili, tutalifuatilia kama alivyosema Mwanasheria Mkuu kwa sababu tumelisikia leo na umesema wapatiwe matibabu. Toka umeliibua suala hili, kusingekuwa na muda wa kuhakikishia kwamba sasa hivi wamepatiwa matibabu, lakini tutalifuatilia na tutakuarifu nini kimejiri katika kuhakikisha Watuhumiwa hawa wanapata matibabu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja kwa kumalizia!

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitoa shilingi na nimeitoa naomba watu wachangie, hawa watu wameshindwa kufika Mahakamani kutokana na hali zao kuwa mbaya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rukia, watu hawakunyanyuka kutaka kuchangia. Mmenyanyuka sasa hivi mara ya pili? *(Makofi)*

(Hapa Wabunge fulani walipiga kelele kuonesha kutoridhishwa na maelezo ya Mwenyekiti)

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika, nimetoa shilingi kwa sababu hawa watu hali zao siyo nzuri wameshindwa kufika Mahakamani. Wawili wako pale wameshindwa kupanda kwenye gari, hawa ni binadamu kama binadamu wengine. Mgeni wa leo mwenyeji wa kesho, tatizo kama hili linaweza likampata yeyote miongoni mwetu, lazima hili tulisimamie.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Rukia. Natoa nafasi kwa watu watatu ambao nimewaona. Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Hatibu na Mheshimiwa Kibona. Nimetoa nafasi kwa watatu, wote walisimama mara ya pili. Tuendelee Mheshimiwa.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalazamika kusema pamoja na sauti yangu kuwa dhaifu. Nasema kwa uchungu kwa sababu ya madhila yanayowapata Mashehe hawa. Siyo mara ya kwanza kulisema hili, Serikali inajitia uzio masikioni haitaki kusikia, baadhi ya madhila yamesababishwa na askari wa magereza na askari katika kuwanyanyasa watu wale. Watanzania wote wanajua, tumelalamika sana, lakini Serikali inajitia uziwi. Waziri wa Mambo ya Ndani anayajua wanayofanyiwa watu wale, wamedhalilishwa kijinsia, wamedhalilishwa watu hawa wameona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza tukasema haya, wenzetu wanaona kama sisi tuna udini ndani yake, siyo udini ni kupigania kila Mtanzania anafaa apate haki yake. *(Makofi)*

Leo imefikia watu wale wanafikiria kugoma, katika historia ya nchi hii haijatokea. Kwa nini yametokea haya wanagoma kula? Wanafikiria...

(Hapa Waheshimiwa fulani walipiga kelele)

MWENYEKITI: *Order, oder!*

MHE. KHATIB SAIDI HAJI: Nyamaza kimya!

MWENYEKITI: Ongea na Kiti.

MHE. KHATIB SAIDI HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika historia ya nchi hii haijawahi kutokea mahabusu wakatishia kugoma kula. Haya yanatokea, ni kwa nini Watanzania wale wanafikia kugoma kula? Yote ni kwa sababu ya udhalilishaji wanaofanyiwa watu wale kwa sababu tu ya maamuzi ya kukataa yale ambayo Serikali ya CCM wanayapenda wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale hakuna ugaidi, hakuna chochote, pale ni uonevu kwa Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiomba, watu wale pamoja na kwamba mmewashikilia, bado wapeni haki yao ya msingi ya kwenda hospitali, ya kukutana na watu wao na kufanya yote ambayo ni wajibu kwa mshitakiwa haki zake azipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuko tayari kuona udhalilishaji ule wa kunyimwa matibabu na kunyanyaswa watu wetu yanaendelea. Wazanzibari wote, Wazanzibari wote...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Selasini!

MHE. KHATIB SAIDI HAJI: Naunga mkono hoja ya Rukia, watu wale wapatiwe matibabu hakuna lingine.

MWENYEKITI: Muda umeisha. Mheshimiwa Selasini nimekuita.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi ya Marekani ndiyo kiongozi wa kupambana na ugaidi hapa Duniani, mpaka ilifikia mahali ikawashikilia magaidi katika Gereza la Guantanamo. Hoja hii tangu asubuhi inazungumzwa kwa kuvungwa vungwa, haiwekwi wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme, dini yangu inaniambia kwamba, watu wote ni Taifa la Mungu na ninao wajibu kama mtu wa imani

kutetea watu wote bila kuwabagua. Kinachosemwa hapa ni kwamba, watu hawa wanalalamika kuingiliwa kinyume na maumbile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo halijaanza kusemwa leo. Mimi siwezi kama Mkristo au kama Mwanachama wa Chama chochote cha Siasa, kushabikia mwanadamu mwenzagu kuingiliwa kinyume na maumbile. Kwa hivyo, mimi ninachokiomba, kwa heshima na taadhima na kwa heshima ya Taifa hili letu la Tanzania na nimeanza kusema habari ya Marekani, hatujasikia Wamarekani waliwashika Magaidi wakawaingilia kinyume na maumbile. Leo hapa Tanzania kuna watu wako Gerezani Segerea, waliletwa Mahakama ya Kisutu wanachechemea hawawezi kusimama na madai yao ni kwamba, wameingiliwa kinyume na maumbile na wakamwomba Mheshimiwa Hakimu lete daktari ututazame tumeingiliwa kinyume na maumbile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja ni hii; kama wameingiliwa kinyume na maumbile na Serikali inaona kabisa kwamba hawa watu wako Mahakamani; tuseme nini sasa; tuseme ni askari magereza waliwaingilia au ni watu gani?

Serikali haioni kwamba inadhalilishwa? Kwa nini Serikali isichukue hatua? Wewe utasema ni mimi, lakini Serikali hapa inapata aibu. Nanyi kama mnafikiria jambo hili ni la kushabikia, Serikali inapata aibu, hatuwezi tukaruhusu kitu kama hiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini ahsante sana. Msemaji wa mwisho Mheshimiwa Kibona!

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimewasikiliza wenzangu kuanzia mtoa hoja, lakini hapa naona kuna mambo mawili yanataka kuibuka kwa ghafla na kwa wakati mmoja. Mtoa hoja alikuwa anazungumza habari za watuhumiwa kukataliwa kwenda kutibiwa hospitalini. Jambo hili tukaanza kulifuatilia sisi wengine ambao tunaona huruma kwa ajili ya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utashangaa kwamba ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Selesani anakuja tena na jambo jipya lingine ambalo pia linagusa hisia za watu wengi. Mimi nilidhani kwa sababu nchi yetu tumeridhia Mkataba wa Utawala Bora ni jambo la kuridhia na kuridhia siyo kitu kidogo, maadam tumeridhia habari ya Utawala Bora, Mheshimiwa Waziri amesema jambo hili amelisikia hapa *official*.

Mimi nadhani, mimi nadhani ni bora, ni vizuri, ni hekima na busara, sisi wote hata wewe hata nani upande wowote, ukiwa na ndugu yako anafanyiwa vitendo kama vinavyosemwa pale huwezi kufurahi. Sasa hatua nzuri ya kiungwana ni kumkubalia Waziri kama alivyofanya kwenye mambo mengine.

Mimi nimeonyesha *grievance* zangu hapa, unyanyasaji uliotokea kwenye Wilaya yangu, amechukua hatua. Kwa nini tusimkubalie Waziri wetu achukue hatua zinazostahili atulettee majibu kwa wakati unaofaa, halafu mwisho wa yote tukumbuke kwamba, tunazungumza habari ya Mahakama. *(Makofi)*

Tukisema Waziri aseme hapa maana yake aiamrishe Mahakama. Pengine hapa napo ndugu zangu pamoja na uchungu huo, hebu tuwe na subira, tumsubiri Waziri aliangalie kiutawala, litatulettee umoja wetu. Tuache kusema Serikali ya CCM ninyi na huku upande huu tuache kusema ninyi waongo. Jambo hili ni letu wote, nchi hii ni yetu sote, hebu tuwe na busara, hebu tuwe na subira, Mheshimiwa Waziri tumpe nafasi aweze kulimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wabunge wote waliochangia na napenda kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Rukia alituambia ni matibabu na kwa kweli niliamini ni matibabu katika maradhi ya kawaida. Mheshimiwa Selasini amekwenda hatua ya pili akizungumzia suala la watuhumiwa hawa kulatiwa. Napenda kusema kwamba, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, kulawiti ni kosa la jinai na ni kosa la jinai hata pale ambapo yule anayelawiti au anayelawitiwa ametoa ridhaa yake mwenyewe ni makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, napenda vilevile kusema kwamba, utu na heshima ya binadamu havigawanyiki. Hakuna utu ulio mzuri kwa mtu mmoja na ukawa mbaya kwa mtu mwingine. Ninapenda niseme tunasikitika kama hilo limetokea. Tusingependa litokee siyo tu kwa watuhumiwa, hata kwa watu wasio watuhumiwa, ni kitu ambacho hatukichukulii kwa wepesi kabisa. Sisi sote ni binadamu na tunaona jambo kama hili halifai kabisa kutokea katika mazingira yoyote na kama nilivyosema, hata kama katika mazingira ya ridhaa ni kosa la jinai. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba nimwombe Mheshimiwa Rukia na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameguswa na wameongea kwa hisia kali, watupe fursa tuliangalie. Tunaheshimu haki za binadamu; aliyeko jela, aliyeko mahabusu leo ni mtu mwingine, kesho hata mimi ninaweza nikawa mahabusu au mtu anayenihusu. Kwa hiyo, kwa kweli hatufanyi mchezo kwa jambo hili, ningepomba ridha yao Waheshimiwa, watupe fursa tulifanyie kazi suala hili na tuje tutoe taarifa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Rukia!

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimefarijika kidogo kwa maneno ya Mheshimiwa Waziri, lakini atoe ahadi hapa ni lini...

MBUNGE FULANI: Ahadi gani?

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Wewe ukome!

MWENYEKITI: *Order, order* na lugha za nasaha hakuna ukome, hakuna kurushiana maneno hapa, tuko kwenye kikao muhimu cha Bunge, tuheshimiame.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba ulete kikao na huyu mama akome kama alivyokoma kusota.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rukia, nimeshatoa msisitizo unarudia tena kosa, endelea.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata kidogo faraja kutokana na hisia alizoonyesha Mheshimiwa Waziri. Naomba aahidi katika Bunge hili ni lini ataleta taarifa rasmi kutueleza kuhusu watu hawa kama wamepelekwa hospitali na wamepatiwa matibabu. Akikubali hilo, mimi nitaachia shilingi yake, lakini na pia atupe taarifa rasmi kwa haya niliyomwambia. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rukia kwa kutuelewa na ningeomba tupate fursa ya kupeleka taarifa kwa Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala hili linahusu siyo tu Wizara yetu, bali Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jeshi la Magereza na hata pia utaratibu wa tiba. Kwa hiyo, tungeomba Mheshimiwa Rukia, atuamini tuweze kufanya kazi hiyo na kuhakikisha mahabusu, watuhumiwa na hata waliohukumiwa, wanaishi kwa staha na utu kama ambavyo Katiba yetu inaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri amekubali ataungana na Wizara zinazohusika na wote wanaohusika walifuatilie hili jambo. Baada ya ufafanuzi huo na maelezo, sasa namwita Mheshimiwa Kilufi!

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri ambazo zimeonekana hapa, pamoja na Wataalam wote waliohusika.

Pamoja na michango mingi ambayo imetolewa, nilikuwa naangalia ukurasa wa 31, bajeti ambayo imeombwa, nilitaka kujua kwa sababu Wazee wa Mahakama, wamekuwa wakisaidia sana mahakama zetu, pamoja na kufikiria sana masilahi ya Majaji na Mahakimu, lakini vilevile hawa Wazee wa Mahakama wamekuwa ni msaada mkubwa sana.

Nilitaka kujua katika bajeti hii ni pamoja na malipo ya Wazee wa Mahakama au ni kwa ajili ya shughuli nyingine tu; kwa sababu wao wengi wamekuwa wakilalamika kwamba hawalipwi kwa wakati na wengine wanakaa hata miezi mitatu, minne, wakiwezo Wazee wa Mahakama wa Mbarari, ambao mimi mwenyewe nimeshuhudia kutokulipwa kwao masilahi yao kwa wakati? Nilitaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Kilufi na ningependa kumthibitishia kwamba, posho za Wazee wa Mahakama ni sehemu ya Fungu 40. Tumepokea pia maoni yaliyotolewa katika mjadala wa leo kwamba, zisiwe tu zinatolewa baada ya kesi kuisha. Kwa hiyo, tumepokea ushauri ambao ameutoa Mheshimiwa Diana Chilolo, tutajitahidi sasa hivi kuzitoa, siyo kila mwezi lakini siyo lazima kesi iishe, lakini tutaboresha mfumo wa upatikanaji wa posho za Wazee wa Mahakama.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Kilufi nataka kukuthibitishia kwamba, ni eneo ambalo tunalithamini sana na ni eneo ambalo tutaliboresha katika mwaka huu wa fedha, kuhakikisha tunaimarisha mifumo ya utoaji haki nchini kwetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Esther Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia athari ya kuwa na msongamano kwenye magereza yetu na kikubwa nikasema kuna kesi ambazo zingeweza kupewa dhamana. Kuna kesi ambazo ni ndogo za madai zingeweza kupewa dhamana. Nikaomba kujua ni kwa nini wasitoe kama ni tamko au laa, kulingana na sheria kwamba, kesi ambazo ni za madai ndogondogo ziweze kupewa dhamana kuepusha msongamano kwenye magereza yetu. Kwa mfano, leo hii ukienda Gereza la Tarime, linapokea watu mara mbili ya uwezo wake na ni gereza la zamani, halijakarabatiwa, kuna msongamano mwingi unaopelekea hata maambukizi ya magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa pia inatoa ushawishi, yaani polisi akimkamata mtu kama ni mzururaji au ana kosa lingine dogo tu, anajua kabisa

huyu ataenda mahabusu, anaweza akakaa hata miezi kwa sababu hapewi dhamana, anaona ni bora hata atoe hongo aachiwe asifikishwe kwenye ngazi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepusha hayo yote, kwanza, kuepusha hizi rushwa ndogondogo baina ya aliyekamatwa na polisi. Kingine pia ku-serve gharama za Serikali kuwahudumia watu ambao kesi zao zingeweza kupewa dhamana na wakawa wanakuja mahakamani mpaka hapo itakapochukuliwa hatua.

Sasa nilitaka nijue na tumekuwa tukiongea hili, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu kwenye hizi kesi ambazo zinadhaminika kuweza kutoa dhamana ili kupunguza msongamano wa watu magerezani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kuna ile Sheria ya *Parole*; kwa nini wafungwa wanaoonekana mienendo yao ni mizuri wasipewe kifungo cha nje kuweza kupunguza msongamano magerezani?

Ningependa kujua ni nini mkakati mbadala wa Serikali kuweza kupunguza mahabusu magerezani au wale wafungwa ambao kama nilivyosema kwa Sheria ya *Parole*; ngingependa kujua ni nini mpango mkakati wa Serikali?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, makakati wa Serikali wa kupunguza msongamano!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nifafanue kwamba, kuna aina mbili ya kesi; kesi za jinai na kesi za daawa. Kwa kesi za daawa hakuna watu wanaowekwa mahabusu, lakini kwa kesi za jinai Mheshimiwa Matiko, inawezekana watu wakawekwa mahabusu au wakawekwa gereza.

Sasa tunachosema ni kwamba, kwa upande wa Wizara, tumeona haja ya kupunguza msongamano wa magereza na hivyo tunaanda Waraka wa Dhana (*Concept Paper*) kuhusu suala la kuangalia utaratibu wa kutoa adhabu mbadala ambazo siyo za kizuizi au siyo za kifungo, ili kupunguza msongamano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunafahamu kwamba, mahakama zetu katika kutoa haki huwa zinaangalia uzito wa kosa na kwa yale makosa ambayo siyo makubwa sana, wanapewa adhabu kama kifungo cha nje au kutumikia jamii.

Amezungumzia vilevile suala la *Parole*; *Parole Board* inakuja baada ya mtu ameshahukumiwa. Kwa hiyo, utaratibu unafanywa kumwomba msamaha

na ni utaratibu mrefu kidogo, kwa sababu unaangalia kosa lenyewe na unaangalia kama jamii husika iko tayari kumpokea mtu ambaye anatakiwa kupata msamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Serikali ni kuhakikisha magereza yanabeba watu ambao magereza yale yana uwezo wa kuwabeba kupunguza msogamano, kwa sababu hayo pia yanahusiana na misingi ya Katiba yetu ya Haki za Binadamu na Utu wa Mtu bila ya kujali kama ni mtumiwa au ni mfungwa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kabla sijasema ninachotaka kusema, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyotoa maelezo kuhusu suala ambalo Mheshimiwa Rukia alilibua hapa.

Mheshimiwa Waziri, wakati nikitoka mchango wangu, nilisema kuna kesi nyingi sana za Viongozi wa Kisiasa mahakamani. Karibu Viongozi wote wa Kisiasa, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Slaa, Mheshimiwa Lipumba, baadhi ya Wabunge na baadhi ya Madiwani, wana kesi mahakamani ambazo haziishi. Kesi nyingine zimechukua miaka mitano, zingine minne na kadhalika.

Mheshimiwa Waziri, mahakama ina msemu unaosema, haki siyo tu inatendeka bali ionekane inatendeka. Sasa hizi kesi zinahusiana kwa mfano na maandamano, hizi kesi ushahidi wake ni kibali kutoka kwa OCD au kibali ambacho kinaruhusu yale maandamano yawepo. Sasa polisi kila wakienda mahakamani wanadai ushahidi haujakamilika! Hivi ushahidi wa kesi ya maandamano unakamilika kweli kwa miaka mitano au ni mbinu tu ya Jeshi la Polisi kuifanya mahakama ionekane haifanyi kazi yao na hivyo kujenga chuki kati ya wanasiasa na mahakama? (Makofi)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sababu nyingi zinazoweza kupelekea kuwepo na ucheleweshaji wa kumalizika kwa mashauri mahakamani. Moja, inaweza ikawa ni watuhumiwa wenyewe hawafiki mahakamani au mawakili wao hawafiki. Pili, inaweza ikawa mahakimu wana udhuru au pengine inawezekana kukawa na ucheleweshaji wa kukamilika kwa upelelezi.

Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, kesi hizi zinapaswa ziwe zinamalizika mapema, ili hatima ya kila anayeshitakiwa si kwa Mwanasiasa tu kwa kila Mtanzania na ndiyo maana Dira ya Wizara au ya Serikali ni haki inayopatikana kwa wote mapema ipasavyo, *timely delivery of justice for all*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, concern hii ya Waheshimiwa Wabunge ni ya muhimu. Mimi nadhani tumelisikia hili, baada ya hapa twende tukakae sisi, kama tatizo liko kwa upande wetu sisi tunaoendesha mashitaka yale tuone,

lakini kama tatizo liko kwa upande wa upelelezi nako tujue. Kama tatizo liko kwa upande wa watuhumiwa nako tujue na kama liko kwa upande wa mahakama tujue, lakini tupate mwafaka hizi kesi zishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu pia kwamba, ni kweli haki iliyocheleweshwa ni haki iliyonyimwa, lakini pia haki iliyoharakishwa ni haki iliyokataliwa, *the justice hurried is justice barred.*

Kwa hiyo, vitu hivi vyote ni lazima viwe *harmonized*. Nakubaliana na Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge mtuamini tunaposema haya, tunayasimamia kwa dhati kabisa. Hata mimi yananikera sitaki, Waheshimiwa Wabunge wengi wamenifuata wakiniuliza kwamba bwana kuna kesi hizi na hizi na mimi nawauliza tatizo ni nini; kwa nini hizi kesi haziishi!

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tupeni fursa twende tukajue ni nini, halafu kama ni kesi hazina ushahidi tuziondoe na kama ni *issue* ya kuharakishwa upelelezi uharakishwe kesi zisikilizwe mapema zishe, kila mmoja ajue hatima yake hasa kwenye kipindi hiki muhimu sana kwa maisha ya wanasiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Ole-Medeye!

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ina Mahakama za Mwanzo tatu, ambayo ni moja kwa kila tarafa. Kwa bahati mbaya, polisi wamefanya mahakama hizi zisifanye kazi zake kama inavyopaswa na badala yake wamekuwa wakichukua watu wanaowatuhumu; kwa mfano, Mkazi wa Kata ya Oldonyosambu, kwenye mpaka wa Monduli, Arumeru na Longido, ambayo ni takribani kilomita zaidi ya thelathini kutoka Arusha Mjini, anatuhumiwa anaenda kukamatwa kule, badala ya kumuweka mahabusu pale Oldonyosambu ambapo kuna kituo cha polisi, anapelekwa Usa. Akifikishwa Usa, badala ya kuletwa kwenye Mahakama ya Mwanzo Emawei, ambayo inahudumia Tarafa ya Mukrati, anapelekwa Mahakama ya Mwanzo Maji ya Chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo umekuwa mtindo kwamba yeyote anayekosa katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, polisi wanawachukua badala ya kuwapeleka kwenye mahakama zilizo kwenye Halmashauri hiyo au Mahakama ya Wilaya ambayo iko ndani ya Halmashauri hiyo, anapelekwa Mahakama ya Mwanzo Maji ya Chai!

Ningeomba Mheshimiwa Waziri atujulishe hadhi iliyonayo Mahakama ya Mwanzo Maji ya Chai ikilinganishwa na Mahakama za Mwanzo za Emawei, Enaboishu na Nduruma pamoja na Mahakama ya Wilaya, ambazo zote ziko katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Ole-Medeye, mara kwa mara anatumulisha yanayojiri katika utoaji wa haki. Katika suala hili pia ameweza kututanabahisha kwamba, kuna tatizo katika maeneo aliyoyataja.

Napenda kumuahidi Mheshimiwa Ole-Medeye kwamba, tutalichukua suala hili, kwa kweli huo siyo utaratibu; utaratibu ni kwamba, shauri lifunguliwe kwenye mahakama iliyo karibu na alipo mtuhumiwa au alipo mdaiwa. Kama hilo linafanyika siyo utaratibu na naomba atupe fursa tulifuatilie na tulitafutie ufumbuzi. Mimi niko tayari kukaa naye ili kwa pamoja tuone tunashughulikia vipi tatizo hili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri. Nimekuona Mheshimiwa Lekule Laizer; una hoja gani?

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilitaka kuzungumzia kuhusu Mahakama ya Mwanzo na Mahakama ya Wilaya. Tangu Mheshimiwa Mwapachu alipokuwa Waziri wa Katiba na Sheria, tukiwa katika Jengo la Pius Msekwa, Serikali ilikuwa inahidi kila mwaka kwamba, watajenga Mahakama ya Wilaya ya Longido. Hatuna Mahakama ya Mwanzo wala hatuna Mahakama ya Wilaya.

Sasa nataka kuiuliza Serikali; kwa vile wametoa ahadi kwa muda mrefu na kila mwaka wanajenga katika maeneo mengine; je, ni lini Mahakama ya Wilaya ya Longido itajengwa?

Kwa kuwa ni wilaya ya pembezoni ndiyo maana nadhani wanajenga mahakama nyingine na kuiacha mahakama hii. Kwa hivi sasa Mahakama ya Wilaya wako kwenye jengo ambalo mimi mwenyewe nimelijenga kama ofisi yangu, nimewapa wafanye Mahakama ya Wilaya. *(Makofi)*

Sasa ni ajabu kama jengo lililojengwa na Mbunge...

MWENYEKITI: Mheshimiwa umeelewewa na Mheshimiwa Waziri, kengele imegongwa hapo.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Naomba nipate jibu ni lini mahakama hiyo itajengwa?

NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Laizer Lekule, kwa kuuliza suala hili. Suala la ujenzi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Mahakama ya Wilaya ya Longido, lipo kwenye Mpango wa Ujenzi wa Mahakama kwa Mwaka 2014/15. Tulieleza kwamba, hadi leo Mahakama haijapata fedha kwa ajili ya maendeleo. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa, kwa sababu mpaka dakika hii hatujui tutapata shilingi ngapi, pale tutakapopata fedha basi tutatoa kipaumbele kama Longido ipo katika hali mbaya sana.

Tatizo zipo wilaya ambazo hazina hata yale majengo ya muda na wananchi wanateseka sana katika kuitafuta haki. Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba tu nikuahidi kwamba, tutakupa kipaumbele pale ambapo rasilimali fedha itapatikana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh. 406,126,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Information Services* ...Sh. 632,698,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*...Sh. 220,701,000/=
Kif. 1005 - *Government Communication*
UnitSh. 218,692,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit* .Sh. 311,119,000/=
Kif. 1007 - *Management Information System*
Unit.....Sh. 210,750,000/=
Kif. 2004 - *Public Legal Services Unit*.....Sh. 735,189,000/=
Kif. 4001 - *Cositutional Affairs* Sh. 2,725,628,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kif. 1001 – *Administration and HR*
Management Sh. 3,137,879,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* Sh. 190,892,000/=
Kif. 1003 – *Internal Audit*..... Sh. 85,113,000/=
Kif. 1004 – *Legal Services* Sh. 384, 985,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Unit* Sh. 143,382,000/=
Kif. 1006 – *Management Information System*
Unit Sh. 155,589,000/=
Kif. 2001 – *Administrative Justice* Sh. 769,604,000/=
Kif. 2002 – *Human Rights* Sh. 615,749,000/=
Kif. 2003 – *Research and Documentation*..... Sh. 267,797,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2004 – *Public Education and Training* .. Sh. 264,470,000/=

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza pale kwenye *Item 221400 – Hospitality, Supplies and Services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kufuatilia *trend* kuanzia tulikotoka na mpaka kufikia hapa, nimegundua kwamba, kuna kupungua kwa pesa hizi katika baadhi ya maeneo. Jambo ambalo mimi binafsi naliona ni jema, kwa sababu tumekuwa tuna-*complain* kwamba, unakuta hizi pesa baadhi ya Mawaziri wame-*respond* wanasema ni kwa ajili ya chai, sijui wageni wamekuja, hata ninyi Waheshimiwa Wabunge na kadhalika.

Ukienda kwenye *component ya Development* pesa zimekuwa kidogo. Sasa naiomba Serikali inisaidie na hasa niwapongeze hawa watu wa Wizara ya Katiba na Sheria; wao wamewezaje kuzipunguza pesa hizi za *hospitality, supplies and services* kwenye maeneo mengine hata ukiangalia kwenye *Sub-Vote 1002* wamepunguza fedha kutoka milioni 10 kuja milioni 5.3? Wao wanawezaje na inakuwaje Wizara nyingine wanashindwa wamekuwa *too defensive* kwamba aaah bwana matumizi ni makubwa wageni ni wengi?

Kama wameweza *why not* wengine wasiweze kuzipunguza hizi pesa tukazipeleka kwenye maendeleo wakati huo huo tunalia pesa za maendeleo ni kidogo! Naomba watusaidie wao wamewezaje na wawasaidie wenzao kuweza kufanya kama ambavyo wamefanya wao. Naomba kauli ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri zungumzia Wizara yako umewezaje.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Machali kwa kutambua jitihada za Wizara yetu kupunguza matumizi katika eneo hili. Sisi tumejiwekea utaratibu wa ndani kwamba, tuwe na tija zaidi kwa fedha kidogo.

Vilevile tunawahamasisha watumishi wenzetu na sisi wenyewe kwa kuleta vinywaji na vitafunwa kutoka nyumbani ili rasilimali chache zilizopo ziweze kuelekezwa kuwahudumia wananchi. Kwa utaratibu huo, Mheshimiwa Machali akifika Ofisini kwa Waziri wa Katiba na Sheria, sana sana atakuta Maji ya Uhai au Kilimanjaro. (*Kicheko/Makofi*)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 - Zanzibar Office Sh. 246,720,000/=
Kif. 3002 - Mwanza Office..... Sh. 105,439,000/=
Kif. 3003 - Lindi Office Sh. 92,128,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

Kif. 1001 - Administration and HR
ManagementSh. 4,132,261,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1003 - Planning DivisionSh. 1,300,000,000/=
Kif. 3002 - Treaties and Contracts Division..... Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 35 – Divisheni ya Mashitaka

Kif. 2002 - Public Prosecution DivisionSh. 342,884,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama

Kif. 1001 - Administration and HR Management Sh. 0

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - Planning and Coordination
DivisionSh. 20,401,814,000/=

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu 1003, Kifungu Kidogo 6310 - *Construction and rehabilitation of District Court Buildings*. Wakati nachangia nilionesha ni kwa kiasi gani Wilaya ya Rorya haina Mahakama ya Wilaya. Wilaya ile ina takribani miaka sita au zaidi. Nikaonesha ni jinsi gani Wananchi wa Rorya wanapata shida kuja kwenye Mahakama ya Wilaya ya Tarime, kwa sababu wengi wao wanatembea kwa miguu na wengine usafiri mkubwa pale ni baiskeli. Nikaainisha pia licha ya kwamba, hawana Mahakama ya Wilaya, vilevile Mahakama za Mwanzo ni mbili tu zinazofanya kazi. Mahakama ya Nyabulongo yenyewe Hakimu wake anaenda Siku ya Alhamisi tu.

Nataka kujua katika hizi bilioni tatu zilizotengwa hapa Mahakama ya Wilaya ya Rorya ipo katika ujenzi wa hii; maana mmeainisha ni *construction and rehabilitation of district court buildings*? Nataka nijue kama Mahakama ya Wilaya ya Rorya nayo ipo katika fungu hili kwenye kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Esther Matiko, kwa kuona haja na umuhimu wa kuwa na Mahakama ya Wilaya katika Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, katika Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama za Wilaya wa 2014/15, tulikuwa na mahakama zaidi ya 20 ambazo tumeziweka. Bunge lako linafahamu kwamba, sasa hivi tumetoka katika utegemezi wa fedha za nje.

Kwa hiyo, bajeti ile ya bilioni arobaini imepungua sasa hivi ni bilioni ishirini. Sasa Wataalam hapa kutoka zile Mahakama zaidi ya 20 wametuletea ujenzi wa mahakama 10.

Naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tukisema Rorya haimo, watuachie baada ya bajeti kupita, tuangalie Mpango wa 2014/15 na huu ambao wameupendekeza sasa hivi, tuzichambue sasa badala ya kujenga mahakama 40 za Wilaya, tuchague 10 zipi ziko katika hali mbaya sana. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Matiko unikubalie na ninaomba upitishie kifungu hiki kusudi tuweze kuendelea mbele.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza kwenye *Item 6312*, lakini pia nitakuwa na maelezo ya nyongeza kwenye ile *Item 6310* kwa sababu naona vinaendana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia ukurasa wa 40 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri juu ya ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma, Mara na kwingineko. Ukienda kwenye sehemu ya pili anasema kwamba, Mshauri Mwelekezi *MS Hub Consult Ltd*, amekamilisha na kuwasilisha rasimu ya michoro (*architectural drawings*) na makisio. Huku mwisho michoro ya mwisho, *detailed architectural and structural and service drawings* inakamilishwa sambamba na kuandaa makisio ya rasimu ya makabrasha.

Swali la kwanza hapo nataka Serikali itueleze hii michoro mnatarajia itakamilika ndani ya muda gani ili kazi ziweze kuanza?

Historia ya huko nyuma, nimekuwa nikifuatilia sana na nimshukuru aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Angella Kairuki; Kasulu hivi sasa tunapozungumza hakuna jengo la mahakama. Utaratibu wa kusikiliza mashauri umekuwa unafanyika ofisini kwa Mheshimiwa Hakim wa Wilaya. Ningeomba pia niweze kupata ufafanuzi ndiyo maana nimesema nitahusisha na *item* ambayo Mheshimiwa Matiko alimalizia. Suala la kujenga hizi mahakama na ambayo pia imeinishwa hapa kwenye ukurasa wa 39 Mahakama ya Wilaya ya Kasulu utakamilika lini sambamba na Mahakama Kuu ya Mkoa wa Kigoma kwa sababu tunapata usumbufu mkubwa kutoka Kasulu kwenda Tabora? Ningeomba kujua pengine mambo haya yatakamilika lini hasa? Nakushukuru.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme katika ile kasma 614, Mheshimiwa Machali inabidi utupongeze, kwa sababu licha ya uhaba wa fedha, katika zile Mahakama Kuu ambazo tutazipa kipaumbele kwa mwaka huu ni Kigoma na Mara. Kwa hiyo, hizo zinapita bila hata kupingwa. Katika Mahakama ya Wilaya ni kama vile nilivyomjibu Mheshimiwa Esther Matiko kwamba, kumekuwa na uhaba wa fedha, kwa hiyo inabidi sasa tuangalie. Kwenye Mahakama Kuu tumeshaamua kabisa, Mara na Kigoma, mwaka huu tutajenga haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Naomba niamue kuhusu Longido; Longido nayo ipo katika Mpango kwa ajili ya Mahakama ya Mwanzo, lakini Mahakama ya Wilaya haipo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lekule Leizer, naomba nikutoe hofu kwamba, Mahakama ya Mwanzo ya Longido ipo katika kipaumbele.

MHE. GOODLUCK J. OLE – MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye Kasma 6312 - *Construction and Rehabilitation of Primary Court*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema katika Wilaya ya Arumeru tuna Mahakama ya Mwanzo Emawei, Mahakama ya Mwanzo Enaboishu, Nduruma na Maji ya Chai. Mahakama hizi zilijengwa zamani sana na kwa bahati mbaya

hakujakuwa na utaratibu wa kuzikarabati mara kwa mara ili walau wanadamu waweze kufanyia shughuli pale.

Tarehe 22 Aprili, nilikwenda pale Mahakama ya Mwanzo Maji ya Chai, kuna wapiga kura wangu wanawake, wanaume na watoto, walituhumiwa na wakachukuliwa wakapelekwa kule. Nilipofika nikakuta wameshafikishwa pale kwenye mahakama wamepelekwa rumande. Nikaenda, kwa sababu masharti waliyowekewa ya dhamana ni magumu kwa ndugu zao kuweza kumudu, kwa hiyo, nikaenda kuwasaidia kwamba mimi niwadhamini. Nilipofika pale, kama ningefika pale bila wanadamu kuwepo, nisingethubutu kuingia kwenye majengo yale, maana naogopa huenda kuna chatu mle ndani kwa jinsi yalivyochanika chanika, yamekwisha yale majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachooomba, Waziri atuhakikishie kama Mahakama hizi za Mwanzo katika Wilaya ya Arumeru ni sehemu ya mahakama zitakazokarabatiwa katika mwaka 2014/2015?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, tunamshukuru Mheshimiwa Ole-Medeye, kwa kufuatilia kwa karibu. Alifuatilia vizuri na katika Mipango ya Ukarabati, Mkoa wa Arusha upo, lakini kwa Mahakama ya Mwanzo, naomba nilichukue suala hili ili mpango mzima wa ukarabati, tuone uwezekano ukoje. Siyo kwa mahakama zote nne, lakini japo moja au mbili. Kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, ilibidi tufanye mabadiliko baada ya kuwa tumeamua kwamba, Serikali tujitegemee zaidi kuliko kutegemea wafadhili.

Naomba nimwombe Mheshimiwa Ole Medeye, atukubalie tukae na wenzetu Watendaji wa Mahakama, tuone pamoja na ukarabati wa Mahakama Kuu kama tutapata fursa ya kuona Mahakama za Mwanzo chache kama ambavyo amekuwa akitoa kilio chake katika Bunge hili.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali nilichangia kwa maandishi kuhusu Mahakama za Mwanzo tatu zilizoko Jimboni; Mahakama ya Mwamagembe, Mahakama ya Kayui na Mahakama ya Ifigi. Mbili, katika utekelezaji zilitengewa fedha kwa ajili ya ukarabati, ile ya Mwamagembe na ile ya Kayui. Ya Mwamagembe imekamilishwa vizuri sana na inapendeza, lakini hii ya Kayui mkandarasi ameitelekeza, pamoja na kupewa fedha. Nilipenda kujua hatua gani imechukuliwa ili kukamilisha jengo hili?

Ningependa pia kujua wataanza lini ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo ya Ifigi? Maeneo haya yako katika Wilaya ya Manyoni Mkoa wa Singida. Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru sana Mheshimiwa Lwanji kwa kuzungumzia suala hilo. Sisi tumesikia leo kuhusu mkandarasi ambaye yuko kule na Mtendaji Mkuu wa Mahakama yuko hapa na tayari ameshaanza kulifanyia kazi. Kwa hiyo, ndani ya wiki moja tutakujibu kwamba, tumechukua hatua gani; kama tunamsimamisha, tunavunja mkataba au tutaendelea vipi.

La pili, nataka kumpa moyo Mheshimiwa Lwanji sambamba na wale wengine, yeye angalau Mahakama ya Itigi iko katika Mpango wa Ujenzi kwa mwaka 2015/16. Kwa hiyo, wewe ya kwako haitatoka, itabaki pale pale, naomba niahidi hivyo kwamba tunaahidi ya Itigi itaendelea kubaki katika Mpango wa Ujenzi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* Sh. 0

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – *Policy and Information Services* Sh. 3,959,719,000/=

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Item namba 6517 - Unicef Support to Multisectoral.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nipatiwe ufafanuzi kutoka Serikalini, hizi pesa haziko *direct* mtu akajua kwamba hii ni *support* ya kutoka *Unicef* kwa ajili ku-*support* maeneo mbalimbali.

Pili, kama haziko *specified* kwamba pesa hizi zinakwenda kutumika wapi *specifically* labda wataangalia kulingana na mahitaji yao, naomba kujua kama Serikali ipo tayari kutumia pesa hizi ili tuanze ujenzi kwenye Mahakama ya Wilaya ya Kasulu ambayo inaonekana iko kwenye Programu?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hela ambazo zipo katika kasma hii ya 6517, ambazo baadhi zinatoka *Unicef* ni kwa ajili ya kuimarisha shughuli za usajili wa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano na watoto kati ya miaka sita mpaka miaka kumi na nane. Kwa hiyo, hatuwezi kuzitumia kwa ajili ya kujenga Mahakama ya Wilaya ya Kasulu, zina kazi maalum.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kif. 1001 – Administration and HR Management Sh. 0
Kif. 2001 – Administrative Justice..... Sh. 0
Kif. 2002 – Human Rights Sh. 0
Kif. 2003 – Research and Documentations ... Sh. 57,909,000/=
Kif. 2004 – Public Education and Training Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/16 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila marekebisho. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2015/2016 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa vile sina matangazo yoyote, naomba nikushukuruni sana kwa michango yenu na hoja zenu nzuri za kujenga mlizozitoa kwa Wizara. Ahadi ya Wizara au Serikali iliyoitoa hapa ya kuwa mengi watayafanyia kazi, watayachukua na yale ya kufuatilia watayafuatilia na wataleta majibu. Nawashukuruni sana kwa hilo.

Kwa vile sina matangazo, naomba sasa niahirishe kikao chetu cha leo hadi kesho saa tatu asubuhi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Saa 1.00 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 22 Mei, 2015 Saa Tatu Asubuhi)